JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI
**TUME YA TAIFA YA MIPANGO**

# MAPENDEKEZO YA SERIKALI YA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA WA MWAKA 2026/2027



MACHI, 2026

# ORODHA YA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| **ADC** | Aquaculture Development Centres |
| **ADEM** | Agency for the Development of Educational Management |
| **AFCON** | Africa Cup of Nations |
| **AFDP** | Agriculture and Fisheries Development Programme |
| **AHSP** | Annual Health Sector Performance Report |
| **AMIS** | Airport Management Information |
| **ASDP II** | Agricultural Sector Development Programme II |
| **ATCL** | Air Tanzania Company Limited |
| **ATE** | Association of Tanzania Employers |
| **AU** | African Union |
| **BAKITA** | Baraza la Kiswahili Tanzania |
| **BBT** | Building Better Tomorrow |
| **BEVAC** | Beekeeping Value Chain |
| **CAMARTEC** | Centre for Agricultural Mechanization and Rural Technology |
| **CBE** | College of Business Education |
| **CBR** | Central Bank Rate |
| **CNG** | Compressed Natural Gas |
| **COSTECH** | Commission for Science and Technology |
| **DAWASA** | Dar es Salaam Water and Sewarage Authority |
| **DIT** | Dar es Salaam Institute of Technology |
| **DMDPII** | Dar es Salaam Metropolitan Development Project II |
| **DMGP** | Dar es Salaam Maritime Gateway Program |
| **DMI** | Dar es Salaam Maritime Institute |
| **DRC** | Democratic Republic of the Congo |
| **EAC** | East African Community |
| **EACOP** | East African Crude Oil Pipeline |
| **EASTRIP** | East Africa Skills for Transformation and Regional Integration Project |
| **EIA** | Environmental Impact Assessment |
| **EOCC** | Emergency Operations and Communication Centre |
| **EP4R** | Education Programme for Results |
| **EPZA** | Export Processing Zones Authority |

| | |
|---|---|
| **ETF** | Enhanced Transparency Framework |
| **FCC** | Fair Competition Commission |
| **FCT** | Fair Competition Tribunal |
| **FDCs** | Folk Development Colleges |
| **FOLUR** | Food Systems, Land Use and Restoration |
| **FORLAND** | Forestry, Land Use and Value Chains Development |
| **FYDP IV** | Fourth Five Year Development Plan |
| **FYDP III** | Third Five Year Development Plan |
| **GAVI** | Global Alliance for Vaccines and Immunization |
| **GPE** | Global Partnership for Education |
| **Ha** | Hectare |
| **HBF** | Health Basket Fund |
| **HEET** | Higher Education for Economic Transformation |
| **HEP** | Hamlet Electrification Project |
| **ICHF** | Improved Community Health Fund |
| **IJCs** | Intergrated Justice Centers |
| **ILFS** | Integrated Labour Force Survey |
| **IMF** | International Monetary Fund |
| **IWT** | Illegal Wildlife Trade |
| **JNHPP** | Julius Nyerere Hydropower Plant |
| **JNIA** | Julius Nyerere International Airport |
| **JPM** | John Pombe Magufuli |
| **KIA** | Kilimanjaro International Airport |
| **KM** | Kilometer |
| **KPI** | Key Performance Indicator |
| **KWh** | Kilowatt Hour |
| **LGAs** | Local Government Authorities |
| **LNG** | Liquefied Natural Gas |
| **LPG** | Liquefied Petroleum Gas |
| **LVD** | Lake Victoria to Dodoma |
| **MDAs** | Ministries, Departments and Agencies |
| **MICE** | Meetings, Incentives, Conferences and Exhibition |
| **MIT** | Ministry of Industry and Trade |

| | |
|---|---|
| **MoCU** | Moshi Co-operative University |
| **MW** | Megawatt |
| **NACTE** | National Council for Technical Education |
| **NCAA** | Ngorongoro Conservation Area Authority |
| **NCT** | National college of Tourism |
| **NDC** | National Development Corporation |
| **NEMC** | National Environment Managament Council |
| **NHC** | National Housing Corporation |
| **NHIF** | National Health Insuarance Fund |
| **NIDA** | National Identification Authority |
| **NIT** | National Institute of Transport |
| **NMT** | National Museum of Tanzania |
| **NPMIS** | National Project Management Information System |
| **NPS** | National Prosecution Service |
| **NRW** | Non-Revenue Water |
| **PAMOJA** | Project for Advancing Gender Equality in Tanzania |
| **PCP** | Programme for Country Partnership |
| **PFMRP** | Public Finance Management Reform Programme |
| **PIM-OM** | Public Investment Management Operational Manual |
| **PPP** | Public-Private Partnership |
| **PPPC** | Public-Private Partnership Centre |
| **PSRP** | Public Service Reform Programme |
| **PSRS** | Public Service Recruitment Secretariat |
| **PSSN** | Productive Social Safetynet |
| **SADC** | Southern African Development Community |
| **SDGs** | Sustainable Development Goals |
| **SDL** | Skills Development Levy |
| **SEZ** | Special Economic Zones |
| **SGR** | Standard Gauge Railway |
| **SIDO** | Small Industries Development Organisation |
| **SMMRP** | Sustainable Management of Mineral Resources Project |
| **SPV** | Special Purpose Vehicle |
| **SRWSSP** | Sustainable Rural Water Supply and Sanitation Programme |
| **TaESA** | Tanzania Employment Services Agency |

| | |
|---|---|
| **TAFICO** | Tanzania Fishing Corporation |
| **TAISP** | Tanzania Agricultural Input Support Project |
| **TAKUKURU** | Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa |
| **TANAPA** | Tanzania National Parks |
| **TANIPAC** | Tanzania Initiative for Preventing Aflatoxin Contamination |
| **TANROADS** | Tanzania National Road Agency |
| **TANTRADE** | Tanzania Trade Development Authority |
| **TANZIS** | Tanzania Innovation Systems |
| **TASAF** | Tanzania Social Action Fund |
| **TaSUBa** | Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo |
| **TATC** | Tanzania Automotive Technology Centre |
| **TAWA** | Tanzania Wildlife Management Authority |
| **TAWIRI** | Tanzania Wildlife Research Institute |
| **TAZAMA** | Tanzania Zambia Mafuta |
| **TAZARA** | Tanzania - Zambia Railway Authority |
| **TBC** | Tanzania Broadcasting Cooperation |
| **TBS** | Tanzania Bureau of Standards |
| **TDHS-MIS** | Tanzania Demographic and Health Survey and Malaria Indicator Survey |
| **TEA** | Tanzania Education Authority |
| **TEHAMA** | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| **TEMDO** | Tanzania Engineering and Manufacturing Design Organization |
| **TFSRP** | Tanzania Food Systems Resilience Program |
| **TGC** | Tanzania Gemmological Centre |
| **TIC** | Tanzania Investment Centre |
| **TIRDO** | Tanzania Industrial Research and Development Organisation. |
| **TIRP II** | Tanzania Intermodal Railway Project II |
| **TMCHIP** | Tanzania Maternal and Child Health Program |
| **TPSF** | Tanzania Private Sector Foundation |
| **TUCTA** | Trade Union Congress of Tanzania |
| **U&T** | Ufuatiliaji na Tathmini |
| **UDSM** | University of Dar es Salaam |
| **UNFPA** | United Nations Population Fund |
| **UNICEF** | United Nations Children’s Fund |

| | |
|---|---|
| **USD** | United States Dollar |
| **UVIKO – 19** | Ugonjwa wa Virusi vya Korona – 2019 |
| **VHF** | Very High Frequency |
| **VVU** | Virusi Vya Ukimwi |
| **WMA** | Weight and Measurement Agency |
| **WRRB** | Warehouse Receipt Regulatory Board |
| **WSDP** | Water Sector Development Programme |

# YALIYOMO


ORODHA YA VIFUPISHO ..... i
YALIYOMO ..... vi

SURA YA KWANZA ..... 1
UTANGULIZI ..... 1
1.1 Usuli ..... 1
1.2 Malengo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2026/27 ..... 1
1.3 Ugharamiaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2026/27 ..... 2
1.4 Mfumo wa Utekelezaji ..... 2
1.5 Mawanda ya Mpango ..... 2
1.6 Mbinu na Njia Zilizotumika Kuandaa Mpango ..... 3
1.7 Mpangilio wa Kitabu ..... 3

SURA YA PILI ..... 4
HALI YA UCHUMI ..... 4
2.1 Utangulizi ..... 4
2.2 Mapitio ya Hali ya Uchumi wa Dunia na Kikanda ..... 4
2.2.1 Uchumi wa Dunia ..... 4
2.2.2 Uchumi wa Kikanda ..... 5
2.2.3 Mfumuko wa Bei wa Dunia ..... 6
2.2.4 Mfumuko wa Bei wa Nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika na Nchi za Afrika zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara ..... 6
2.2.5 Mfumuko wa Bei kwa Nchi za Ukanda wa Afrika Mashariki ..... 7
2.3 Mapitio ya Hali ya Uchumi wa Taifa ..... 8
2.3.1 Uchumi wa Taifa ..... 8
2.3.2 Mfumuko wa Bei Nchini ..... 10
2.3.3 Sekta ya Nje ..... 11
2.3.4 Sekta ya Fedha ..... 13
2.3.5 Deni la Serikali ..... 16
2.3.6 Demografia na Maendeleo ya Watu ..... 18
2.3.6.1 Demografia ..... 18
2.3.6.2 Maendeleo ya Watu ..... 19
2.4 Mwenendo wa Sekta Binafsi ..... 20
2.4.1 Ukuzaji wa Mitaji ..... 20
2.4.2 Mitaji kutoka Nje ..... 20
2.4.3 Uwekezaji wa Moja kwa Moja kutoka Nje kwa Shughuli za Kiuchumi ..... 21
2.5 Mwelekeo wa Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2026/27 ..... 21
2.5.1 Malengo na Shabaha za Ukuaji wa Uchumi Jumla ..... 21
2.5.2 Misingi ya Mpango kwa Mwaka 2026/27 ..... 22

SURA YA TATU ..... 23
MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO ..... 23

3.1 Utangulizi ..... 23
3.2. Miradi ya Kielelezo ..... 24
3.2.1. Miundombinu ya Usafirishaji ..... 24
3.2.2 Miradi ya Miundombinu ya Nishati ..... 26
3.2.3 Miradi ya Kuongeza Uzalishaji Viwandani ..... 27
3.3 Mapitio ya Utekelezaji Kisekta ..... 29
3.3.1 Sekta ya Ujenzi ..... 29
3.3.2 Sekta ya Uchukuzi ..... 31
3.3.3 Sekta ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari ..... 32
3.3.4 Sekta ya Nishati ..... 33
3.3.5 Sekta ya Kilimo ..... 35
3.3.6 Sekta ya Mifugo ..... 36
3.3.7 Sekta ya Uvuvi ..... 38
3.3.8 Sekta ya Uzalishaji Bidhaa Viwandani ..... 40
3.3.9 Sekta ya Madini ..... 41
3.3.10 Sekta ya Mazingira na Maliasili ..... 43
3.3.11 Sekta ya Utalii ..... 44
3.3.13 Sekta ya Kukuza Uwekezaji na Biashara ..... 47
3.3.14 Uwekezaji wa Umma na Sekta Binafsi ..... 47
3.3.15 Sekta ya Mahusiano ya Kimataifa na Diplomasia ya Uchumi ..... 49
3.3.16 Sekta ya Elimu na Maendeleo ya Ujuzi ..... 50
3.3.17 Sekta ya Afya ..... 55
3.3.18 Sekta ya Huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira ..... 56
3.3.19 Sekta ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi ..... 56
3.3.20 Sekta ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii ..... 58
3.3.21 Kuendeleza Ujuzi ..... 59
3.3.22 Maendeleo ya Vijana ..... 59
3.3.23 Utawala Bora na Utawala wa Sheria ..... 60

SURA YA NNE ..... 64
VIPAUMBELE KWA MWAKA 2026/27 ..... 64
4.1 Utangulizi ..... 64
4.2 Maeneo ya Kipaumbele ya Mpango ..... 64
4.2.1 Utawala, Amani, Usalama na Utulivu ..... 64
4.2.2 Uchumi Imara, Jumuishi na Shindani ..... 68
4.2.2.1 Uchumi Jumla Tulivu na Unaotabirika ..... 68
4.2.2.2 Sera za Bajeti Endelevu ..... 69
4.2.2.3 Sekta ya Nje Iliyohimilivu na Mseto ..... 69
4.2.2.4 Sekta Muhimu za Mageuzi ..... 70
4.2.2.4.1 Sekta ya Kilimo (Mazao, Mifugo, Uvuvi na Misitu) ..... 70
4.2.2.4.2 Sekta ya Uzalishaji Bidhaa Viwandani ..... 73
4.2.2.4.3 Sekta ya Ujenzi ..... 74
4.2.2.4.4 Sekta ya Madini na Uchimbaji wa Mawe ..... 76
4.2.2.4.5 Sekta ya Utalii ..... 77

4.2.2.4.6 Sekta ya Michezo na Ubunifu ... 78
4.2.2.4.7 Sekta ya Uwekezaji na Biashara ... 79
4.2.2.4.8 Sekta binafsi ... 81
4.2.2.4.9 Uhusiano wa Kimataifa na Diplomasia ya Uchumi ... 82
4.2.3 Kujenga Uwezo wa Watu na Maendeleo ya Jamii. ... 83
4.2.3.1 Jamii Iliyoelimika, yenye Ujuzi na inayopenda Kujifunza ... 83
4.2.3.2 Nguvu Kazi yenye Ari na Uwezo wa Kufanya Kazi ... 87
4.2.3.3 Ajira na Soko la Ajira ... 88
4.2.3.4 Jamii Jumuishi na inayolindwa ... 90
4.2.3.5 Afya Bora kwa Wote ... 91
4.2.3.6 Upatikanaji na Uunganishwaji wa huduma za maji safi na Usafi wa Mazingira ... 93
4.2.4 Uhifadhi wa mazingira na ustahimilivu wa mabadiliko ya tabianchi ... 94
4.2.4.1 Ustahimilivu wa Mazingira ... 95
4.2.4.2 Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ... 96
4.2.5 Vichocheo vya Maendeleo ... 97
4.2.5.1 Nishati ... 97
4.2.5.2 TEHAMA ... 99
4.2.5.3 Uchukuzi ... 101
4.3 Programu za Kielelezo ... 102
4.4. Mwelekeo wa Kimkakati na Mageuzi kwa mwaka 2026/27 ... 104

SURA YA TANO ... 105
UGHARAMIAJI WA MPANGO ... 105
5.1 Utangulizi ... 105
5.2 Mahitaji ya fedha kwa mwaka 2026/27 ... 105
5.2.1 Vyanzo vya Mapato kwa Mwaka 2026/27 ... 105
5.2.2 Mwelekeo wa Sera ya Fedha na Bajeti kwa 2026/27 ... 105
5.2.3 Uboreshaji wa Matumizi na Nidhamu ya Kifedha ... 106
5.3 Ushiriki wa Mashirika ya Umma (PSCs) ... 106
5.4 Uwekezaji wa Sekta Binafsi ... 107

SURA YA SITA ... 110
UFUATILIAJI NA TATHMINI ... 110
6.1 Utangulizi ... 110
6.2 Malengo ya Mfumo wa Ufuatiliaji, Tathmini na Utoaji wa Taarifa ... 110
6.3 Mfumo wa Matokeo ... 110
6.4 Mfumo wa Ufuatiliaji ... 111
6.4.1 Njia za Ufuatiliaji ... 111
6.4.2 Ngazi za Ufuatiliaji ... 111
6.5 Mfumo wa Tathmini ... 111
6.5.1 Aina za Tathmini ... 112
6.6 Mfumo wa Utoaji Taarifa ... 112
6.7 Ratiba ya Ufuatiliaji na Tathmini ... 112

6.8 Taarifa za utekelezaji wa miradi, ufuatiliaji, na tathmini ..... 113
6.9 Mgawanyo wa Majukumu ..... 113

SURA YA SABA ..... 115
VIHATARISHI VYA MPANGO KWA MWAKA 2026/27 ..... 115
7.1 Utangulizi ..... 115
7.2 Maeneo ya Vihatarishi na Mikakati ya Kudhibiti ..... 115
7.3 Usimamizi wa Vihatarishi ..... 118

Kiambatisho Na. 1: Mwenendo wa Viashiria vilivyotumika katika Upimaji wa Utekelezaji Wa Mpango kwa kipindi cha Miaka Mitano. ..... 119
Kiambatisho Na. 2: Orodha ya Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka 2026/27 ..... 128

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.1 Usuli

Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2026/27 unaandaliwa wakati Taifa linaanza rasmi Utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 (Dira 2050) huku mkazo ukiwekwa katika kufanya mabadiliko na mageuzi makubwa ya kimfumo na mitazamo ili kujiletea maendeleo. Mpango wa 2026/27 ni mpango wa kwanza ukiwa nyenzo muhimu ya utekelezaji wa Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2026/27 - 2030/31) unaotekeleza Dira 2050 (FYDP IV) ambao una dhima ya "**Mageuzi kwa ajili ya Ukuaji Jumuishi wa Uchumi na Uzalishaji Ajira**". Mpango wa 2026/27 unalenga kuwa na utekelezaji wenye matokeo na hivyo kuwezesha: Kubainisha vipaumbele vya mwaka mmoja kutoka vile vya miaka Mitano; kurahisisha utengaji wa rasilimali fedha; ufuatiliaji na upimaji wa matokeo ya muda mfupi; na kuwezesha mfumo mabadiliko ya kimkakati kutoka katika Malengo makubwa yaliyobainishwa.

Utekelezaji wa Mpango wa 2026/27 utakuwa ni muendelezo wa utaratibu bora wa kujipanga kimkakati katika kuelekea maendeleo endelevu ambayo kwa miongo miwili na nusu nchi yetu imeweza kuyafikia. Mpango utabainisha vipaumbele vitakavyotekelezwa kwa mwaka mmoja kupitia miradi ya kielelezo na ya kimkakati katika sekta mbalimbali. Vipaumbele hivyo ni pamoja na: Uchumi imara, jumuishi na shindani; kuimarisha tija na kuleta mageuzi ya kiuchumi kwenye sekta za kimkakati; uwezo wa watu na maendeleo ya jamii; uhifadhi wa mazingira na uhimilivu wa mabadiliko ya tabianchi; kutumia kikamilifu vichocheo vya maendeleo; kuimarisha misingi endelevu ya taifa; ujumuishaji wa mabadiliko na kuwekeza kwenye maeneo yanayoleta mageuzi.

## 1.2 Malengo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2026/27

Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2026/27 umebainisha kwa kipaumbele miradi na programu za maendeleo pamoja na afua muhimu ambazo utekelezaji wake utasaidia kuleta matokeo katika kipindi cha mwaka mmoja. Kwa ujumla, miradi na programu hizi zinaendana na mwelekeo wa vipaumbele vya FYDP IV na matumizi bora ya rasilimali ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Hivyo, vipaumbele vya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2026/27 vimetafsiri na kuweka mfumo wa matokeo kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa FYDP IV kwa kuweka malengo, matokeo na viashiria vinavyopimika ili kuhakikisha kunakuwa na utekelezaji. Aidha, Mpango wa 2026/27 utahusisha wadau ikiwemo sekta binafsi katika utekelezaji huku wakiwa washirika muhimu katika hatua zote

kuanzia uanzishaji hadi kukamilika kwa miradi na programu zitakazoanzishwa na Serikali pamoja na ufuatiliaji kwa maeneo ambayo wao watawekeza.

### 1.3 Ugharamiaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2026/27

Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2026/27 utagharamiwa kutoka vyanzo vya mapato vinavyohusisha rasilimali za ndani na nje ya nchi. Serikali itatenga jumla ya shilingi bilioni 20,744.7 sawa na asilimia 33.3 ya Bajeti Kuu ya Serikali ya shilingi bilioni 62,334.2 kwa mwaka 2026/27 ili kugharamia programu na miradi ya maendeleo. Vilevile, Serikali inalenga kutekeleza vipaumbele vilivyoainishwa na kuwa na nidhamu ya matumizi pamoja na kuongeza ushirikiano na mchango wa sekta binafsi katika kufanikisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Sekta binafsi itakuwa na mchango mkubwa katika utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2026/27 huku maboresho yakifanyika katika Sheria na Kanuni zinazokwamisha kubainika kwa mchango wake katika bajeti ya Serikali kupitia njia bunifu na mbadala za kugharamia miradi hiyo.

### 1.4 Mfumo wa Utekelezaji

Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2026/27 utakuwa na mwelekeo jumuishi ambapo Tume ya Taifa ya Mipango itasimamia kwa karibu miradi ya kielelezo na kushirikiana na Taasisi za Serikali zinazohusika na Sekta binafsi. Usimamizi huu utazingatia mwelekeo wa Dira 2050 wa kufanya utekelezaji kwa utofauti na kuzingatia matokeo. Aidha, Wizara za Uratibu zitakuwa na jukumu la kusimamia utekelezaji wa miradi kwa kushirikiana na Wizara za kisekta na taasisi za Serikali huku zikiweka mazingira wezeshi ya kiutendaji na utekelezaji. Vile vile, Sekta binafsi itakuwa na nafasi ya kushirikiana na watendaji wa Serikali kutokana na uwazi na maboresho ya kiutendaji yanayotarajiwa kujitokeza katika mwaka wa kwanza wa utekelezaji.

### 1.5 Mawanda ya Mpango

Mwanda ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2026/27 yamejikita katika maeneo ya kipaumbele yaliyobainishwa katika FYDP IV. Mwelekeo wa Utekelezaji wa Mpango wa 2026 utajikita katika kufanya mageuzi na kuendeleza masuala ambayo hayajakamilika katika Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2025/26 pamoja na kujenga msingi wa Utekelezaji wa Mipango mingine minne itakayofuata. Aidha, Utekelezaji wa miradi saba (7) ya kielelezo imepewa msukumo kwa kubainisha maeneo yanayoweza kuleta matokeo makubwa katika mwaka wa kwanza wa utekelezaji. Vile vile, kwa kushirikiana na sekta binafsi taasisi za Serikali zimeainisha miradi mahsusi itakayotekelezwa kwa kuzingatia mfumo wa upimaji kwa matokeo.

### 1.6 Mbinu na Njia Zilizotumika Kuandaa Mpango

Mbinu na njia za kuhusisha wadau mbalimbali kutoka Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Sekretariati za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Taasisi na Mashirika ya Umma na Sekta Binafsi pamoja na Asasi za Kiraia zimetumika wakati wa maandalizi ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2026/27. Majadiliano yamefanyika katika ngazi za wataalamu na viongozi ili kujenga uelewa wa pamoja wa mwelekeo wa Mpango na mahitaji ya kufanya mambo kitofauti na ilivyozoeleka ili kutekeleza FYDP IV.

Kwa ujumla, Mpango wa 2026/27 umezingatia Mipango ya Maendeleo ya Kitaifa pamoja na Ajenda za Kikanda na Kimataifa ikijumuisha Dira 2050, Mpango Elekezi wa Maendeleo wa Muda Mrefu 2026/27 – 2050/51, Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2026/27 – 2030/31, Ajenda 2030 ya Malengo ya Maendeleo Endelevu, Ajenda 2063 ya Umoja wa Afrika, na Dira ya Jumuiya ya Afrika Mashariki 2050 (Vision 2050) na Dira ya Jumuiya ya Maendeleo Nchi za Kusini mwa Afrika (Vision 2050). Mpango pia umezingatia masuala mtambuka katika maeneo yote ya kipaumbele yakiwemo usawa wa kijinsia na uwezeshaji wa wanawake, ajira kwa vijana, mabadiliko ya tabianchi na utunzaji wa mazingira, mabadiliko ya kidigitali, sayansi, teknolojia na ubunifu, utawala bora, pamoja na usawa katika upatikanaji wa fursa.

### 1.7 Mpangilio wa Kitabu

Kitabu cha Mpango kimegawanyika katika sura saba (7): Sura ya Kwanza: utangulizi ambao unajumuisha usuli, malengo ya mapendekezo, mawanda na maandalizi; Sura ya Pili: inaelezea mapitio ya hali ya uchumi; Sura ya Tatu: inatoa uchambuzi wa mapitio ya utekelezaji wa Mipango iliyopita katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (FYDP III); Sura ya Nne: inaelezea vipaumbele kwa mwaka 2026/27; Sura ya Tano: inaelezea ugharamiaji wa Mpango; Sura ya Sita: inaainisha ufuatiliaji na tathmini; na Sura ya saba: Vihatarishi vya Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2026/27. Pia kitabu hiki cha Mpango kina viambatisho viwili ambavyo ni **Kiambatisho Na.1:** Mwenendo wa Viashiria vilivyotumika katika Upimaji wa Utekelezaji wa Mpango kwa kipindi cha Miaka Mitano na **Kiambatisho Na. 2:** Orodha ya Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka 2026/27.

# SURA YA PILI

# HALI YA UCHUMI

## 2.1 Utangulizi

Sura hii inatoa tathmini ya mwenendo wa viashiria vya kiuchumi na kijamii katika ngazi ya dunia, kikanda, na kitaifa kwa mwaka 2024 na 2025, pamoja na matarajio kwa mwaka 2026. Uchambuzi huu ni sehemu muhimu ya mapitio ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka uliopita, kwa madhumuni ya kubaini mafanikio na changamoto, na kutumia mafunzo yake katika maandalizi ya Mpango unaofuata.

Uchambuzi wa viashiria hivi una umuhimu mkubwa katika kupanga maendeleo ya Taifa kwa kuwa unawezesha: Kufanya tathmini ya ufanisi wa sera za uchumi na kijamii; Kulinganisha mwenendo wa uchumi wa ndani na mazingira ya dunia na kikanda; Kubaini maeneo yenye changamoto na fursa; na Kutoa mapendekezo mahususi kwa ajili ya kupanga sera, mipango na mikakati. Viashiria vilivyofanyiwa uchambuzi ni pamoja na: Pato la Taifa; mfumuko wa bei; mwenendo wa sekta ya nje; sekta ya fedha; deni la Serikali; na demografia na maendeleo ya watu.

## 2.2 Mapitio ya Hali ya Uchumi wa Dunia na Kikanda

### 2.2.1 Uchumi wa Dunia

Uchumi wa Dunia umeendelea kuimarika licha ya changamoto mbalimbali, ikiwemo migogoro ya kikanda na kutokutabirika kwa sera za biashara. Kwa mujibu wa taarifa ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) ya Januari 2026, uchumi wa dunia umeendelea kukua kwa wastani wa asilimia 3.3 mwaka 2025 kama ilivokua kwa mwaka 2024 ikilinganishwa na asilimia 3.5 mwaka 2023. Kasi ya ukuaji wa uchumi wa dunia inatarajia kuendelea kubaki wastani wa asilimia 3.3 mwaka 2026 na kupungua hadi asilimia 3.2 mwaka 2027. Mwenendo huu unatokana na uwiano kati ya nguvu kinzani zenye msukumo hasi na chanya ambapo msukumo hasi unaotokana na mabadiliko ya sera za biashara unafidiwa na msukumo chanya unaotokana na kuongezeka kwa uwekezaji katika teknolojia, hususan teknolojia ya akili mnemba (AI), hasa katika Amerika Kaskazini na Asia kuliko maeneo mengine. Aidha, matarajio ya utekelezaji wa sera za bajeti na fedha zinazolenga kuongeza fedha katika uchumi na kupungua kwa athari zitokanazo na utekelezaji wa sera za bajeti zinazolenga kuongeza ushuru kwa mataifa yaliyoendelea hususan nchi ya Marekani. Vilevile, uwezo wa sekta binafsi kuhimili na kuendana na mabadiliko, vimechangia kukua kwa uchumi. Kwa upande wa Tanzania, maoteo ya kushuka kwa uchumi wa dunia yanaweza sababisha kupungua kwa uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje, kushuka kwa bei za bidhaa katika soko la dunia, na kupungua kwa misaada na mikopo nafuu. Ili kukabiliana na athari hizo, Serikali itaendelea

kuimarisha vyanzo vya ndani vya ukuaji wa uchumi, kuongeza wigo wa masoko ya bidhaa, na kukuza uwekezaji wa ndani hususan kupitia sekta binafsi.

### 2.2.2 Uchumi wa Kikanda

Kasi ya ukuaji wa uchumi kwa nchi za Afrika zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara uliongezeka na kufikia wastani wa asilimia 4.4 mwaka 2025 ikilinganishwa na asilimia 4.1 na 3.7 mwaka 2024 na 2023 mtawalia. Kuongezeka kwa ukuaji kulichangiwa na kupungua kwa athari za majanga yanayokabili uchumi wa dunia, kuimarika kwa shughuli za kiuchumi kufuatia ongezeko la uwekezaji katika sekta ya umma, kuimarika kwa mauzo ya bidhaa nje na utekelezaji mzuri wa sera za kupunguza mfumuko wa bei. Ukuaji wa uchumi unatarajiwa kuongezeka hadi kufikia asilimia 4.6 mwaka 2026 na 2027, kutokana na juhudi za kuimarisha uchumi jumla na mageuzi ya sera za kiuchumi katika nchi za eneo hili.

Uchumi wa nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika - SADC ulikua kwa wastani wa asilimia 3.0 mwaka 2024 ikilinganishwa na asilimia 3.8 mwaka 2023 na unatarajiwa kukua kwa asilimia 3.4 na asilimia 3.7 mwaka 2025 na 2026, mtawalia. Katika ukanda wa uchumi wa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki ukuaji wa Pato la Taifa ulikua kwa wastani wa asilimia 1.7 mwaka 2024 ikilinganishwa na asilimia 5.3 mwaka 2023. Kasi ndogo ya ukuaji wa uchumi wa ukanda wa EAC ilichangiwa na kuporomoka kwa uchumi wa nchi ya Sudani Kusini ambao ulikuwa na ukuaji hasi wa asilimia 26.1 mwaka 2024. Uchumi wa nchi za EAC unakadiriwa kukua kwa wastani wa asilimia 7.7 mwaka 2025 na mwaka 2026.

**Kielelezo Na. 2.1: Ukuaji wa Uchumi kwa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) Mwaka 2023 - 2024 na Matarajio mwaka 2025**




***Chanzo:*** Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF)

**Kielelezo Na. 2.2: Ukuaji wa Uchumi kwa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), 2023 – 2024 na matarajio 2025**




***Chanzo:*** Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF)

### 2.2.3 Mfumuko wa Bei wa Dunia

Kwa mujibu wa taarifa ya Shirika la Fedha la Kimataifa toleo la Januari 2026, mfumuko wa bei uliendelea kupungua katika nchi nyingi kutokana na utekelezaji wa sera za fedha zilizolenga kuwa na utulivu wa mfumuko wa bei. Mfumuko wa bei wa dunia unatarajiwa kupungua kutoka wastani wa asilimia 5.6 na 4.1 kwa mwaka 2024 na 2025 mtawalia hadi asilimia 3.8 mwaka 2026 na 3.4 mwaka 2027. Mwenendo huu unaonesha imani ya kufikia malengo ya kudhibiti mfumuko wa bei kwa nchi ya Marekani na nchi nyingine zilizoendelea.

Kwa upande wa makundi ya nchi, mfumuko wa bei kwa nchi zenye kipato cha chini uliongezeka na kufikia wastani wa asilimia 4.1 mwaka 2024, sawa na wastani wa mwaka 2023; kwa nchi zinazoibukia na zinazoendelea kiuchumi ulipungua hadi asilimia 7.8 mwaka 2024 kutoka asilimia 8.1 mwaka 2023; na kwa nchi zilizoendelea ulipungua zaidi, kufikia wastani wa asilimia 2.6 mwaka 2024 ikilinganishwa na asilimia 4.6 mwaka 2023.

### 2.2.4 Mfumuko wa Bei wa Nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika na Nchi za Afrika zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara

Kwa mujibu wa taarifa ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) ya Oktoba 2025, nchi zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara, mfumuko wa bei ulifikia wastani wa asilimia 20.3 mwaka 2024, ikilinganishwa na asilimia 19.4 mwaka 2023. Ongezeko la mfumuko wa bei lilitokana na sababu mbalimbali ikiwemo athari za kushuka kwa

thamani ya fedha pamoja na uzalishaji usioridhisha katika shughuli za kilimo. Nchi zilizokuwa na mfumuko wa bei wa juu ni pamoja na Zimbwabwe (asilimia 736.1), Sudan Kusini (asilimia 99.8), Nigeria (asilimia 31.4), Malawi (asilimia 32.2) na Angola (asilimia 28.2).

Aidha, Mfumuko wa bei kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) umefikia wastani wa asilimia 54.5 mwaka 2024 ikilinganishwa na asilimia 50.3 mwaka 2023 (Jedwali Na. 2.1) .

**Jedwali Na. 2.1 : Mwenendo wa Mfumuko wa Bei kwa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).**

| Nchi/ Miaka | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 | 2026 (Moteo) |
|---|---|---|---|---|---|
| Angola | 21.4 | 13.6 | 28.2 | 21.6 | 16.3 |
| Botswana | 12.2 | 5.1 | 2.8 | 3.4 | 4.7 |
| Comoros | 12.4 | 8.5 | 5.0 | 3.3 | 1.9 |
| DRC* | 9.3 | 19.9 | 17.7 | 8.8 | 7.1 |
| Eswatini | 4.8 | 4.9 | 4.0 | 3.5 | 4.0 |
| Lesotho | 8.2 | 6.5 | 5.2 | 4.5 | 4.8 |
| Madagascar | 8.2 | 9.9 | 7.6 | 8.4 | 7.2 |
| Malawi | 20.8 | 28.8 | 32.2 | 28.2 | 42.1 |
| Mauritius | 10.8 | 7.0 | 3.6 | 3.9 | 3.6 |
| Mozambique | 10.4 | 7.0 | 3.2 | 4.9 | 5.4 |
| Namibia | 6.1 | 5.9 | 4.2 | 3.7 | 3.6 |
| Seychelles | 2.6 | -0.9 | 0.3 | 0.4 | 1.1 |
| South Africa | 6.9 | 5.9 | 4.4 | 3.4 | 3.7 |
| Tanzania | 4.4 | 3.8 | 3.1 | 3.3 | 3.5 |
| Zambia | 11.0 | 10.9 | 15.0 | 14.2 | 9.2 |
| Zimbabwe | 193.4 | 667.4 | 736.1 | 89.0 | 18.2 |
| Wastani wa Ujumla | **21.4** | **50.3** | **54.5** | **12.8** | **8.5** |
| Wastani (bila Zimbabwe) | **10.0** | **9.1** | **9.1** | **7.7** | **7.9** |

***Jamhuri ya kidemokrasia ya Kongo**
***Chanzo:*** Ofisi za Taifa za Takwimu za Nchi husika na Taarifa ya IMF.

### 2.2.5 Mfumuko wa Bei kwa Nchi za Ukanda wa Afrika Mashariki

Kwa upande wa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), mfumuko wa bei umeendelea kutofautiana kati ya wanachama, ambapo Sudan Kusini na Burundi zilirekodi viwango vya juu zaidi vya wastani wa asilimia 99.8 na 29.2 mwaka 2024, ikilinganishwa na asilimia 39.7.0 na 27.1 mwaka 2023 mtawalia. Nchi nyingine kama Kenya ikifikia asilimia 4.5, Uganda asilimia 3.3 na Rwanda asilimia 4.8 mwaka 2024. Tanzania imeendelea kudumisha utulivu wa bei, ambapo mwaka 2024 mfumuko wa bei umefikia wastani wa asilimia 3.1. Hii imetokana na utekelezaji wa sera thabiti za fedha, utulivu wa soko la chakula na kupungua kwa bei za bidhaa za kimataifa. Hali hii inaonesha tofauti kubwa za kiuchumi ndani ya ukanda wa EAC, ambapo baadhi

ya nchi zinakabiliwa na shinikizo kubwa la bei huku nyingine zikidumisha uthabiti wa kiuchumi.

**Jedwali Na. 2.2: Mfumuko wa Bei katika Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa Mwaka 2022 - 2024 na Matarajio mwaka 2025**

| Nchi/ Miaka | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 | 2026 (Moteo) |
|---|---|---|---|---|---|
| Burundi | 18.9 | 27.1 | 29.2 | 37.3 | 26.3 |
| DRC* | 9.3 | 19.9 | 17.7 | 8.8 | 7.1 |
| Kenya | 7.6 | 7.7 | 4.5 | 4.0 | 5.2 |
| Rwanda | 13.9 | 14 | 4.8 | 7.0 | 4.7 |
| Sudani Kusini | -3.2 | 39.7 | 99.8 | 97.5 | 15.8 |
| Tanzania | 4.4 | 3.8 | 3.1 | 3.3 | 3.5 |
| Uganda | 7.2 | 5.4 | 3.3 | 3.8 | 4.3 |
| Wastani wa Ujumla | **8.3** | **16.8** | **23.2** | **23.1** | **9.6** |

**Jamhuri ya kidemokrasia ya Kongo*

***Chanzo:*** Ofisi za Taifa za Takwimu za Nchi husika na IMF

## 2.3 Mapitio ya Hali ya Uchumi wa Taifa

### 2.3.1 Uchumi wa Taifa

Uchumi umeendelea kukua kwa kasi ambapo, Pato halisi la Taifa lilikua kwa wastani wa asilimia 5.5 mwaka 2024 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 5.1 mwaka 2023. Ukuaji huo ulichangiwa na: uwekezaji wa Serikali kwenye miradi ya kimkakati na ya kielelezo inayohusisha miundombinu ya nishati na usafirishaji; kuanza kwa uzalishaji wa umeme katika Bwawa la Kufua Umeme wa Maji la Julius Nyerere; kuongezeka kwa mikopo kwa sekta binafsi; usimamizi madhubuti wa sera za fedha; kuimarika kwa uzalishaji wa mazao ya kilimo; kuimarika kwa huduma za fedha na bima; pamoja na uwekezaji wa Serikali katika huduma za jamii ikiwemo elimu, afya, maji na hifadhi ya jamii.

Katika kipindi cha Januari hadi Septemba 2025, ukuaji wa Pato la Taifa kwa bei za mwaka wa kizio wa 2015 ulifikia wastani wa asilimia 6.0 ikilinganishwa na asilimia 5.5 katika kipindi kama hicho mwaka 2024 **(Kielelezo 2.3).** Ukuaji huo ulitokana na: uwekezaji wa Serikali katika miradi ya kimkakati ya miundombinu ya nishati, maji, na usafirishaji; kuongezeka kwa shughuli za uzalishaji hususan kilimo, viwanda na uchimbaji wa madini na mawe; pamoja na kuendelea kuimarika kwa sekta ya fedha na shughuli za usafirishaji nchini.

**Kielelezo 2.3: Ukuaji wa Uchumi kwa Robo Mwaka**




***Mwaka 2025 unajumisha takwimu za Januari hadi Septemba***
***Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS)*

Aidha, Sekta zilizokuwa na kiwango kikubwa cha ukuaji katika kipindi cha marejeo ni pamoja na shughuli za uzalishaji umeme zilizokuwa na ukuaji wa asilimia 15.5, shughuli za fedha na bima (asilimia 14.8) pamoja na uchimbaji madini na mawe (asilimia 13.7). Shughuli za kilimo ziliongoza kwa kuwa na mchango mkubwa katika katika Pato la Taifa kwa kuchangia asilimia 24.5, ikifuatiwa na shughuli za ujenzi (asilimia 12.7), madini (11.9), biashara na matengenezo (asilimia 8.5) na usafiri na usafirishaji (asilimia 7.7) **(Kielelezo 2.4)**.

**Kielelezo 2.4: Mchango wa Baadhi ya Shughuli za Kiuchumi Katika Pato la Taifa**




**mwaka 2025 unajumisha takwimu za Januari hadi Septemba*
***Chanzo:*** Ofisi ya taifa ya Takwimu

Kwa kuzingatia mwenendo wa viashiria mbalimbali ikiwemo ukuaji halisi wa Pato la Taifa katika robo tatu ya mwaka 2025 (Julai – Septemba), uchumi umekua kwa asilimia 6.4 na unatarajiwa kukua kwa asilimia 5.9 mwaka 2025 na kuongezeka hadi asilimia 6.3 mwaka 2026. Aidha, katika kipindi cha muda wa kati (2025 – 2029) uchumi unatarajiwa kukua kwa wastani wa asilimia 6.9. Ukuaji huu utategemea utekelezaji endelevu wa miradi mikubwa ya kimkakati inayohusisha miundombinu ya nishati na usafirishaji, jitihada za Serikali kuboresha mazingira ya uwekezaji, utekelezaji wa Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili – ASDP II na Mpango Kabambe wa Sekta ya Kilimo 2050, utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Maendeleo ya Sekta ya Fedha pamoja na uwekezaji wa Serikali katika sekta ya huduma za kijamii. Mwelekeo wa uchumi katika kipindi cha muda wa kati ni kama unavyoonekana katika **Kielelezo Na. 2.5.**

**Kielelezo Na. 2.5: Mwelekeo wa Uchumi wa Tanzania**




**Mwaka 2025 – 2030 maoteo*
***Chanzo:** Wizara ya Fedha*

### 2.3.2 Mfumuko wa Bei Nchini

Mwaka 2025, mfumuko wa bei ulikuwa wastani wa asilimia 3.3 ikilinganishwa na asilimia 3.1 mwaka 2024 (**Kielelezo Na. 2.6**). Mwenendo wa mfumuko wa bei ulichangiwa na kuongezeka kwa bei ya vyakula na mabadiliko katika makundi ya bidhaa na huduma. Aidha, kiwango hicho cha mfumuko wa bei kipo ndani ya lengo la nchi la muda wa kati la asilimia 3.0 hadi 5.0, vigezo vya mtengamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (usiozidi asilimia 8.0) na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (wigo wa asilimia 3.0 hadi 7.0).

**Kielelezo 2.6: Mwenendo wa Mfumuko wa Bei Nchini kwa mwaka 2021 hadi 2025.**




***Chanzo:*** Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS)

### 2.3.3 Sekta ya Nje

Sekta ya nje iliendelea kuimarika mwaka 2025, hali iliyoakisi kupungua kwa nakisi ya urari wa malipo ya kawaida hadi dola za Marekani milioni 2,015.5 kutoka dola za Marekani milioni 2,379.8 zilizorekodiwa mwaka 2024. Kuimarika huku kulichangiwa zaidi na ongezeko la mauzo ya nje ya bidhaa na huduma ikilinganishwa na uagizaji, ambapo kwa kiasi kikubwa kimechangiwa na uagizaji wa bidhaa za kati na bidhaa mtaji zinazohusiana na shughuli za uzalishaji na uwekezaji. Mwaka 2025, mauzo ya nje ya bidhaa na huduma yaliongezeka kwa asilimia 10.2 na kufikia dola za Marekani milioni 17,599.2 kutoka dola za Marekani milioni 15,968.4 mwaka 2024.

Mwaka 2025/26 na katika kipindi cha muda wa kati, urari wa malipo ya kawaida unatarajiwa kupungua kutoka asilimia 2.5 ya pato la Taifa mwaka 2024/25 hadi wastani wa asilimia 2.0 katika kipindi cha muda wa kati. Hii ni kutokana na matarajio ya kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa na huduma nje na kupungua kwa uagizaji wa bidhaa na huduma. Ongezeko la mauzo ya bidhaa na huduma ni kutokana na matarajio ya kuendelea kuimarika kwa sekta ya utalii, uuzaji wa bidhaa za asili na zisizo asilia ikiwemo dhahabu na bidhaa za maua na mbogamboga. Aidha, uagizaji wa bidhaa na huduma unatarajiwa kupungua kutokana na kukamilika kwa baadhi ya miradi inayotekelezwa na Serikali.

#### a) Mwenendo wa Mauzo ya Bidhaa Nje na Mapato ya Huduma

Mwaka 2025, mauzo ya nje ya bidhaa na huduma yaliongezeka kwa asilimia 10.2 na kufikia dola za Marekani milioni 17,599.2 kutoka dola za Marekani milioni 15,968.4

mwaka 2024. Mauzo ya nje ya bidhaa yaliongezeka hadi dola za Marekani milioni 10,282.4 mwaka 2025, kutoka dola za Marekani milioni 9,121.6 zilizorekodiwa mwaka 2024. Ongezeko hili lilitokana zaidi na mauzo ya dhahabu, bidhaa za viwandani, tumbaku, na kahawa. Mauzo ya dhahabu, ambayo yalichangia asilimia 45.7 ya jumla ya mauzo ya nje ya bidhaa, yaliongezeka kwa asilimia 37.4 na kufikia dola za Marekani milioni 4,697.6, kutokana na bei nzuri katika soko la dunia Pamoja na kuongezeka kwa uzalishaji. Mauzo ya nje ya bidhaa za viwandani yaliongezeka na kufikia dola za Marekani milioni 1,548.6 kutoka dola za Marekani milioni 1,341.3 mwaka 2024.

Mauzo ya bidhaa asilia yaliongezeka hadi dola za Marekani milioni 1,512.2 mwaka 2025, kutoka dola za Marekani milioni 1,473.3 mwaka 2024. Ukuaji huu ulitokana zaidi na kuongezeka kwa mauzo ya tumbaku na kahawa, yaliyochochewa na kuongezeka kwa bei na kiwango cha mauzo. Mauzo ya nje ya bidhaa kwa mwezi yalifikia dola za Marekani milioni 1,059.8 mwezi Desemba 2025, ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 951.5 mwezi Desemba 2024, kutokana na kuongezeka kwa mauzo ya nje ya dhahabu na bidhaa za viwandani.

Mapato yatokanayo na huduma yaliongezeka kwa kiasi kikubwa hadi kufikia dola za Marekani milioni 7,316.8 mwaka 2025 kutoka dola za Marekani milioni 6,846.8 mwaka 2024. Ongezeko hili lilitokana zaidi na kuongezeka kwa mapato ya huduma za utalii na usafirishaji. Mapato ya huduma za utalii yaliongezeka hadi dola za Marekani milioni 3,948.2 mwaka 2025 kutoka dola za Marekani milioni 3,903.1 mwaka 2024, ikiwa ni sambamba na ongezeko la asilimia 7.1 la idadi ya watalii waliofikia 2,294,495. Mapato ya huduma za usafirishaji yaliongezeka hadi dola za Marekani milioni 2,796.5 mwaka 2025 kutoka dola za Marekani milioni 2,353.4 mwaka 2024, yakichangiwa zaidi na ongezeko la mapato ya usafirishaji wa bidhaa (Kielelezo 2.8.3). Kwa mwezi, mapato ya huduma yalifikia dola za Marekani milioni 626.1 mwezi Desemba 2025, ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 696.7 mwezi Desemba 2024. Mwelekeo huu unatofautiana na mwenendo wa mwaka.

**b) Mwenendo wa Uagizaji wa Bidhaa na Huduma**

Uagizaji wa bidhaa na huduma uliongezeka hadi dola za Marekani milioni 17,826.1 mwaka 2025, ikiwa ni ongezeko la asilimia 4.9 kutoka dola za Marekani milioni 16,990.7 mwaka 2024. Ongezeko hili lilitokana zaidi na uagizaji wa bidhaa za viwandani, huduma za usafirishaji, vifaa vya usafiri viwandani, pamoja na mashine na mitambo, ambavyo kwa kiasi kikubwa ni bidhaa mtaji na kati. Uagizaji wa mafuta ulipungua kwa asilimia 6.7 hadi dola za Marekani milioni 2,380.1 kutoka dola za Marekani milioni 2,552.3. Hali inaashiria kushuka kwa bei ya mafuta katika soko la dunia. Kwa ulinganifu wa kila mwezi, uagizaji wa bidhaa ulifikia dola za Marekani milioni 1,379.1 mwezi Desemba 2025, kutoka dola za Marekani milioni 1,340.2 mwezi Desemba 2024.

Malipo ya huduma yaliongezeka kwa asilimia 12.5 hadi dola za Marekani milioni 3,144.4 mwaka 2025 kutoka dola za Marekani milioni 2,795 mwaka 2024. Ongezeko hili lilitokana na kuongezeka kwa malipo ya usafirishaji, ambayo ni sambamba na mwenendo wa uagizaji bidhaa za nje. Kwa ulinganifu wa kila mwezi, malipo ya huduma yalifikia dola za Marekani milioni 288.8 mwezi Desemba 2025, ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 261 mwezi Desemba 2024.

Nakisi ya urari wa mapato ya vitega uchumi kwa mwaka 2025 iliongezeka hadi dola za Marekani milioni 2,072.1 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 1,887.4 mwaka 2024. Ongezeko hili lilichangiwa na kuongezeka kwa malipo ya mapato yatokanayo na umiliki wa mtaji (hisa) na riba. Kwa ulinganifu wa kila mwezi, nakisi ya mapato ya vitega uchumi yalifikia dola za Marekani milioni 199 mwezi Desemba 2025, ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 181.8 mwezi Desemba 2024.

**c) Akiba ya Fedha za Kigeni**

Hadi kufikia Desemba 2025, akiba ya fedha za kigeni ilikuwa dola za Marekani milioni 6,329.0 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 5,546.9 katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Kiasi hicho kinatosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi kisichopungua miezi 4.9, juu ya lengo la nchi la kutosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma kwa kipindi cha angalau miezi minne (4) na kigezo cha mtangamano kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki cha angalau miezi 4.5. Ongezeko hilo lilichangiwa na utekelezaji thabiti wa programu ya Benki Kuu ya ununuzi wa dhahabu nchini, pamoja na kuongezeka kwa mapato ya fedha za kigeni yatokanayo na mauzo ya dhahabu, korosho na kuimarika kwa shughuli za utalii nchini. Aidha, akiba ya fedha za kigeni inatarajiwa kuendelea kuimarika kutokana na matarajio ya kuendelea kukua kwa mapato ya fedha za kigeni na utekelezaji wa programu ya Benki Kuu ya ununuzi wa dhahabu katika soko la ndani.

### 2.3.4 Sekta ya Fedha

Katika kipindi cha Julai hadi Desemba 2025, utekelezaji wa sera ya fedha ulilenga kuhakikisha kuwa matarajio ya mfumuko wa bei yanabaki ndani ya lengo la asilimia 3 hadi 5 na kuchagiza ukuaji wa uchumi. Kwa muktadha huo, Kamati ya Sera ya Fedha, iliamua kupunguza Riba ya Benki Kuu (CBR) kutoka asilimia 6.00 kwa kipindi cha mwaka 2024/25 hadi asilimia 5.75 kwa kipindi cha Julai hadi Desemba 2025. Uamuzi huu ulilenga kuongeza ukuaji wa mikopo kwenye sekta ya binafsi ili kuchochea zaidi shughuli za kiuchumi, vilevile, kwa kuzingatia mwelekeo wa mfumuko wa bei ambao unatarajiwa kuendelea kuwa chini ya asilimia 5; vihatarishi vinavyotokana na kutotabirika kwa mwenendo wa uchumi wa dunia, na kuendelea kuimarika kwa hali ya uchumi wa ndani. Aidha, Benki Kuu imeendelea kutekeleza sera ya fedha kwa lengo la kuhakikisha kuwa riba ya mikopo ya siku saba katika soko la fedha baina ya benki inakuwa ndani ya wigo wa asilimia 3.75 hadi asilimia 7.75.

### a) Viwango vya Riba

Riba za mikopo zilipungua na kufikia wastani wa asilimia 15.24 mwezi Desemba 2025 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 15.71 Desemba 2024 (**Kielelezo Na. 2.7**). Aidha, katika kipindi cha miezi sita ya kwanza ya mwaka 2025/26 riba za mikopo zilipungua na kufikia wastani wa asilimia 15.19 ikilinganishwa na asilimia 15.52 katika kipindi kama hicho mwaka 2024/25. Mwenendo huu unaakisi utekelezaji wa sera thabiti za kibajeti, pamoja na hatua za kisera zilizochukuliwa na Benki Kuu katika kuhakisha kunakuwa na ukwasi wa kutosheleza shughuli za kiuchumi na kuchochea ongezeko la ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi.

**Kielelezo Na. 2.7: Riba za Mikopo**




***Chanzo:*** Benki Kuu ya Tanzania

Wastani wa riba za amana uliongezeka kidogo kufikia asilimia 8.36 Desemba 2025, ikilinganishwa na asilimia 8.33 Desemba 2024. Ongezeko hilo lilitokana na jitihada za mabenki kuvutia amana kwa kutoa riba shindani. Aidha, katika kipindi cha miezi sita ya kwanza ya mwaka 2025/26 wastani wa riba za amana ulikuwa asilimia 8.53 ikilinganishwa na asilimia 8.18 katika kipindi kama hicho mwaka 2024/25 (**Kielelezo Na. 2.8**). Kwa kuzingatia mwenendo huo, wigo kati ya riba za mikopo na amana za mwaka mmoja (*interest rate spread*) ulipungua hadi asilimia 5.88 Desemba 2025 kutoka asilimia 6.12 mwaka 2024.

**Kielelezo Na. 2.8: Riba za Amana**




***Chanzo:*** *Benki Kuu ya Tanzania*

**b) Mikopo kwa Sekta Binafsi**

Katika kipindi cha Julai hadi Desemba 2025, mikopo kwa sekta binafsi ilikua kwa wastani wa asilimia 17.6, ikilinganishwa na wastani wa asilimia 16.1 katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Hadi kufikia Desemba 2025, ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi ulifikia asilimia 23.5 kwa mwaka, ikilinganishwa na asilimia 12.4 katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Hii ilitokana na utekelezaji wa sera ya fedha inayolenga kuongeza ukwasi kwenye uchumi.

Shughuli za uchimbaji madini zimekuwa na ukuaji wa kasi wa mikopo zikifuatiwa na biashara, kilimo, viwanda, shughuli za usafirishaji pamoja na ujenzi. Aidha, shughuli binafsi zimeendelea kuchukua sehemu kubwa ya mikopo kwa sekta binafsi, ikifuatiwa na biashara, kilimo na uzalishaji viwandani. **Kielelezo Na. 2.9** kimeainisha mchanganuo wa mikopo kwa sekta binafsi.

**Kielelezo Na. 2.9: Mchanganua wa Mikopo kwa Sekta Binafsi**




*Chanzo*: Benki kuu ya Tanzania

### c) Ukwasi na Faida za Biashara katika Benki

Hali ya ukwasi katika sekta ya benki iliendelea kuwa ya kuridhisha, ikiwa juu ya ukomo unaokubalika kisheria. Uwiano kati ya mali inayoweza kubadilishwa kuwa fedha taslimu na amana zinazoweza kuhitajika kwa muda mfupi (*Liquid Assets to Demand Liabilities*) ulikuwa asilimia 27.8 mwezi Desemba 2025 ikilinganishwa na asilimia 28.6 katika kipindi kama hicho mwaka 2024, kiwango ambacho ni zaidi ya uwiano wa chini unaohitajika kisheria wa asilimia 20. Aidha, uwiano wa mtaji wa msingi na rasilimali za benki ilikuwa asilimia 19.3 mwezi Desemba 2025 kama ilivyokuwa Novemba 2024. Uwiano huo ni zaidi ya ukomo wa chini unaokubalika kisheria wa asilimia 10. Hii inaashiria kuwa benki zina ukwasi wa kutosha kwa ajili ya shughuli zake za kila siku ikiwemo kutoa mikopo.

Mapato ya benki yatokanayo na rasilimali (*Returns on Asset - ROA*) yalikuwa asilimia 4.7 mwezi Desemba 2025, ikilinganishwa na asilimia 5.2 mwezi Desemba 2024. Aidha, mapato yatokanayo na mtaji (*Returns on Equity - ROE*) yalifikia wastani wa asilimia 20.6 mwezi Desemba 2025 kutoka asilimia 23.7 kipindi kama hicho mwaka 2024. Hali hii inaashiria sekta ya benki inaendelea kuwa himilivu na yenye kutengeneza faida.

### 2.3.5 Deni la Serikali

Hadi Novemba 2025, Deni la Serikali lilikuwa shilingi bilioni 109,012.72 ikilinganishwa na shilingi bilioni 100,352.49 katika kipindi kama hicho mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 8.63. Kati ya kiasi hicho, deni la ndani lilikuwa shilingi bilioni 38,181.30 (sawa na asilimia 35 ya deni lote) na deni la nje lilikuwa shilingi bilioni 70,831.42. Ongezeko la deni limetokana na Serikali kuendelea kupokea fedha za mikopo kutoka vyanzo mbalimbali kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo

ikiwemo ujenzi wa miundombinu ya barabara, reli, viwanja vya ndege, umeme na maji. **Kielelezo Na. 2.10** kinaonesha mwenendo wa Deni la Serikali.

**Kielelezo Na. 2.10: Mwenendo wa Deni la Serikali hadi kufikia Novemba 2025**




***Chanzo:*** Wizara ya Fedha

Matokeo ya tathmini ya Uhimilivu wa Deni iliyofanyika Oktoba 2025 yalionesha kuwa deni limeendelea kuwa himilivu kwa kipindi cha muda wa kati na mrefu. Tathmini hiyo huzingatia vigezo vya uhimilivu ambavyo ni pamoja na uwiano wa deni halisi kwa Pato la Taifa, uwiano wa deni halisi kwa malipo ya nje na uwiano wa malipo ya deni kwa mapato ya ndani na mapato yatokanayo na mauzo ya nje.

Viashiria vya deni vilionesha kuwa: mwaka 2024/25 thamani ya sasa ya deni la nje kwa Pato la Taifa ni asilimia 24.9 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 40; thamani ya sasa ya deni la nje kwa mauzo ya nje ni asilimia 125.4 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 180; ulipaji wa deni la nje kwa kutumia mapato yatokanayo na mauzo ya nje ni asilimia 11.6 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 15; na ulipaji wa deni la nje kwa kutumia mapato ya ndani ni asilimia 14.7 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 18. Aidha kwa upande wa viashiria vya deni lote (deni la nje na la ndani), thamani ya deni kwa Pato la Taifa ni asilimia 40.7 ukilinganisha na ukomo wa asilimia 55 wa Pato la Taifa na chini ya ukomo wa asilimia 50 unaotumika kama kigezo cha muunganiko wa viashiria vya uchumi jumla kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mwaka 2025, Tanzania ilifanyiwa tathmini ya kukopesheka katika masoko ya mitaji ya kimataifa na kampuni za Moody’s Investors Service na Fitch Ratings. Matokeo ya tathmini hizo yameendelea kuwa yakuridhisha, ambapo tathmini ya Fitch Ratings Services kuweka daraja la B+ na tathmini ya Moody’s ya Februari 2026 imeiweka

Tanzania katika daraja B1 (Stable Outlook). Matokeo mazuri ya tathmini hizo yanaakisi uhimilivu wa deni la serikali kutokana na ukuaji mzuri wa uchumi unaoweza kuhimili majanga ya kimataifa, utekelezaji wa mageuzi ya kimuundo yanayoboresha mazingira ya biashara, ufanisi wa ukusanyaji wa mapato na usimamizi wa fedha za umma.

### 2.3.6 Demografia na Maendeleo ya Watu

#### 2.3.6.1 Demografia

Idadi ya watu wa Tanzania Bara inakadiriwa kufikia takribani watu milioni 66.1 mwaka 2025 na milioni 67.9 mwaka 2026, kwa mujibu wa taarifa zinazotolewa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS). Kasi ya ongezeko la watu inaendelea kutoa fursa chanya kwa maendeleo ya nchi, ikiwemo upatikanaji wa nguvu kazi ya kutosha na uwezekano wa kuchochea mageuzi ya kidijitali katika shughuli mbalimbali za uzalishaji. Fursa hizi zinaimarishwa zaidi na uwiano mkubwa wa kundi la vijana wenye umri wa miaka 15 hadi 35, ambao ni nguzo muhimu katika ustawi wa uchumi wa kisasa.

Pamoja na fursa hizo, ongezeko la idadi ya watu linaashiria pia ongezeko la mahitaji ya huduma za kijamii na mageuzi katika mifumo ya elimu, mafunzo na utendaji kazi. Hivyo, ni muhimu kutekeleza mikakati mahsusi ya kuwawezesha vijana kuongeza tija katika uzalishaji. Hatua hizi zitasaidia kuimarisha ubora wa rasilimali watu, kuongeza ushindani wa Taifa katika soko la kimataifa na kuchochea ukuaji endelevu wa uchumi.

Kwa upande mwingine, kiwango cha utegemezi kinakadiriwa kubaki 0.87 mwaka 2025 na kupungua kidogo hadi 0.86 mwaka 2026. Hali hii inaonesha kuwa mzigo wa utegemezi bado ni mkubwa kwa kundi la watu wanaozalisha, jambo linalohitaji mikakati madhubuti ya kupunguza utegemezi huo kupitia uboreshaji wa uzalishaji na ajira zenye tija.

Aidha, kwa kuzingatia mwenendo wa ongezeko la watu na kasi ya maendeleo ya kiuchumi, ni muhimu kutekeleza mikakati ya kukuza uchumi jumuishi, inayowahusisha wadau wote muhimu katika kuleta maendeleo, hususan katika sekta za huduma za kijamii na miundombinu ya kiuchumi. Kwa muktadha huu, Serikali inatakiwa kuendelea kuwekeza kwa makusudi katika sekta za elimu, mafunzo ya ujuzi, lishe bora, afya, maji safi na salama, miundombinu ya barabara, nishati, mawasiliano na teknolojia pamoja na kuimarisha uhusiano wa kiuchumi kati ya maeneo ya mijini na vijijini. Uwekezaji katika sekta hizi ni nyenzo muhimu za kuongeza tija, kuboresha ustawi wa wananchi na kuchochea ukuaji wa uchumi wa taifa kwa ujumla.

### 2.3.6.2 Maendeleo ya Watu

Serikali imeendelea kutekeleza jitihada mbalimbali za kuboresha maendeleo ya watu kwa lengo la kuimarisha ustawi wa jamii na kufikia malengo yaliyoainishwa katika Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050. Jitihada hizo zimeelekezwa katika kuimarisha upatikanaji wa huduma za kijamii na kiuchumi kwa wananchi wote, mijini na vijijini.

Miongoni mwa hatua zilizotekelezwa ni pamoja na: kuendelea kutoa elimu bila ada ili kuongeza ushiriki na uandikishaji wa wanafunzi; kuimarisha upatikanaji wa huduma za maji safi na salama katika maeneo ya mijini na vijijini; kuboresha ushiriki wa sekta binafsi katika utoaji wa huduma za afya, hususan katika maeneo ya pembezoni; kuendelea na ujenzi na ukamilishaji wa zahanati, vituo vya afya na hospitali; pamoja na ujenzi wa barabara zinazochochea fursa za kiuchumi na kijamii katika maeneo mbalimbali ya nchi.

Utekelezaji wa miradi na programu hizo za maendeleo umechangia matokeo chanya katika viashiria vya maendeleo ya watu, ikiwemo kuboreka kwa huduma za afya, elimu, maji na miundombinu, sambamba na ongezeko la fursa za ajira na shughuli za uzalishaji mali. Baadhi ya viashiria vya maendeleo ya watu ni kama ifuatavyo[1];

i. Kuongezeka kwa wastani wa umri wa kuishi kutoka miaka 66.8 mwaka 2022 hadi miaka 68.3 mwaka 2025. Aidha, wastani wa umri wa kuishi kwa kuzingatia jinsia, umefikia miaka 70.7 kwa wanawake na miaka 65.9 kwa wanaume mwaka 2025; Hii ni kwa mujibu wa makadirio yaliyotakana na Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022;
ii. Kuimarika kwa mwenendo wa vifo vya watoto wa umri chini ya miaka mitano na kufikia vifo 43 kwa vizazi hai 1,000 mwaka 2022 kutoka vifo 81 kwa vizazi hai 1,000 mwaka 2019/20;
iii. Kupungua kwa vifo vitokanavyo na uzazi kutoka vifo 556 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2019/20 hadi vifo 104 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2022;
iv. Kuongezeka kwa kiwango cha uandikishaji wa wanafunzi wa elimu ya sekondari kutoka asilimia 47.4 mwaka 2021/22 hadi asilimia 51.7 mwaka 2024/25;
v. Kuongezeka kwa idadi ya watu wa vijijini wanaopata maji ya bomba kama chanzo kikuu kutoka asilimia 72.3 mwaka 2020/21 hadi asilimia 85.3 mwaka 2024/25;
vi. Kuunganishwa na huduma ya umeme kwa vijiji vyote 12,261 vya Tanzania Bara mwaka 2025/26;
vii. Fahirisi ya maendeleo ya watu imefikia 0.556 mwaka 2024 kutoka 0.529 mwaka 2019, fahirisi hii inaashiria kuimarika kwa upatikanaji wa huduma za

[1] Kutofautina kwa vipindi vya ulinganifu wa takwimu kunatokana na baadhi ya viashira kutumia tafiti kuzalisha takwimu husika.

jamii za muhimu kama vile afya, elimu na maji pamoja na kuimarika kwa kiwango cha maisha. Hii ni kwa mujibu wa taarifa za UNDP.

### 2.4 Mwenendo wa Sekta Binafsi

Malengo ya Tanzania ni kufikia hadhi ya nchi yenye kipato cha kati ngazi ya juu ifikapo mwisho wa utekelezaji wa Dira ya Taifa Maendeleo 2050, kupitia ukuaji endelevu wa uchumi unaochochewa na mageuzi ya kisera yanayotoa kipaumbele kwa ushiriki wa sekta binafsi. Tanzania imejipanga vyema kutumia utulivu wa kisiasa na uwepo wa maliasili ili kuvutia uwekezaji wa ndani na nje ya nchi. Ushiriki wa sekta binafsi umeleta manufaa makubwa, ikiwa ni pamoja na kuongeza fursa za ajira, kuchochea shughuli za kibiashara, na kuboresha urari wa malipo. Manufaa haya yanachangia kufanikisha lengo la kujenga uchumi shindani na wa viwanda, kama ilivyoainishwa katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano.

#### 2.4.1 Ukuzaji wa Mitaji

Mwaka 2024, ukuzaji wa rasilimali kwa bei za mwaka husika ulifikia shilingi bilioni 76,301.64 kutoka shilingi milioni 69,226.05 mwaka 2023. Ongezeko hili lilichangiwa na ujenzi wa majengo, barabara, madaraja, na miradi mingine ya miundombinu. Katika kipindi hicho, uwiano wa ukuzaji rasilimali kwa Pato la Taifa kwa bei za mwaka husika ulikuwa asilimia 37.1 kama ilivyokuwa mwaka 2023. Mwaka 2024, ukuzaji rasilimali za kudumu kwa bei za mwaka husika ulifikia shilingi bilioni 77,126.78 kutoka shilingi bilioni 71,482.46 zilizokuwa mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 7.9.

#### 2.4.2 Mitaji kutoka Nje

Kwa mujibu wa Taarifa ya Uwekezaji Tanzania ya mwaka 2025, uwekezaji wa sekta binafsi kutoka nje uliongezeka kwa asilimia 27.67 na kufikia dola za Marekani milioni 7,216.68 ukilinganisha na miradi iliyosajiliwa kwa kipindi kama hicho kwa mwaka 2024. Uwekezaji huu unatarajia kuzalisha ajira 119,386.

Mwaka 2024, uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje ulikuwa na thamani ya dola za Marekani milioni 5,651.92 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 3,330.52 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 69.70 (**Jedwali Na 2.3)**. Ongezeko hilo lilichangiwa na Serikali kuendelea kuboresha mazingira ya uwekezaji.

**Jedwali Na. 2.3: Mwenendo wa Mitaji kutoka Nje na Ajira**

| Mwaka | Mitaji (dola za Marekani - Milioni) | Ajira |
|---|---|---|
| 2025 | 7,216.68 | 119,386 |
| 2024 | 5,651.92 | 66,560 |
| 2023 | 3330.53 | 25,642 |

***Chanzo:*** TISEZA

### 2.4.3 Uwekezaji wa Moja kwa Moja kutoka Nje kwa Shughuli za Kiuchumi

Mwaka 2025, uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje uliendelea kujikita zaidi katika shughuli za uzalishaji viwandani, majengo ya biashara/ujenzi na kilimo. Shughuli hizo zilichangia wastani wa asilimia 80.68 ya uwekezaji wote wa moja kwa moja kutoka nje. Aidha, shughuli za uzalishaji viwandani zilikuwa na uwekezaji mkubwa zaidi wenye thamani ya dola za Marekani milioni 3,992.19 sawa na asilimia 55.32 ya uwekezaji wote, ikifuatiwa na majengo ya biashara/ujenzi wenye thamani ya Dola za Marekani milioni 1,088.25 (asilimia 15.08) na shughuli za kilimo zenye thamani ya dola za Marekani milioni 741.77 (asilimia 10.28) mwaka 2025. Uchangiaji wa sekta nyingine kama zinavyoonekana kwenye **Jedwali Na 2.4**.

**Jedwali Na 2.4: Uwekezaji wa Moja kwa Moja kutoka Nje kwa Shughuli za Kiuchumi**

| Na. | Sekta | Mitaji (dola za Marekani - Milioni) | Asilimia |
|---|---|---|---|
| 1. | Viwanda | 3,992.19 | 55.32 |
| 2. | Majengo ya Biashara / Ujenzi | 1,088.25 | 15.08 |
| 3. | Kilimo | 741.77 | 10.28 |
| 4. | Miundombinu ya Kiuchumi | 393.81 | 5.46 |
| 5. | Nishati | 354.63 | 4.91 |
| 6. | Utalii | 185.98 | 2.58 |
| 7. | Usafirishaji | 174.75 | 2.42 |
| 8. | Madini na Mafuta (Petroli) | 161.38 | 2.24 |
| 9. | Huduma | 82.36 | 1.14 |
| 10. | Rasilimali Watu | 30.24 | 0.42 |
| 11. | Mawasiliano | 6.73 | 0.09 |
| 12. | Kompyuta | 4.60 | 0.06 |
| | **Jumla** | **7,216.68** | **100.00** |

***Chanzo:*** TISEZA

## 2.5 Mwelekeo wa Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2026/27

Tanzania inatarajiwa kuendelea kukua kiuchumi kwa kasi ya wastani wa asilimia 6.3 mwaka 2026 na wastani wa asilimia 6.6 katika muda wa kati. Ukuaji huu unategemea uwekezaji mkubwa wa Serikali katika sekta za mageuzi na vichocheo vya kufikia malengo ya Dira 2050.

Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2026/27 umejielekeza katika maeneo matano (5) mahsusi: (i) Utawala, amani, usalama na utulivu (ii) Kujenga uchumi imara, jumuishi na shindani kupitia sekta tisa (9) muhimu za mageuzi; (iii) kuimarisha uwezo wa watu na maendeleo ya kijamii; (iv) uhifadhi wa mazingira na ustahimilivu wa mabadiliko ya tabianchi; na (v) kuimarisha vichocheo vya maendeleo.

### 2.5.1 Malengo na Shabaha za Ukuaji wa Uchumi Jumla

Malengo na shabaha za msingi za uchumi jumla ni kama ifuatavyo:

i. Kuongeza kasi ya ukuaji wa Pato Halisi la Taifa kufikia asilimia 6.3 mwaka 2026 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 6.0 kwa mwaka 2025;
ii. Kuimarisha mfumuko wa bei katika wigo wa asilimia 3.0 – 5.0 katika kipindi cha muda wa kati, ili kulinda uwezo wa wananchi kumudu mahitaji muhimu;
iii. Kuongeza mapato ya ndani kufikia asilimia 17.1 ya Pato la Taifa mwaka 2026/27, kutoka asilimia 16.8 mwaka 2025/26;
iv. Kuongeza mapato ya kodi kufikia asilimia 13.7 ya Pato la Taifa mwaka 2026/27, kutoka asilimia 13.3 mwaka 2025/26;
v. Kuwa na nakisi ya bajeti isiyozidi asilimia 3.0 ya Pato la Taifa mwaka 2026;
vi. Kiwango cha akiba ya fedha za kigeni kinachotosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne (4); na
vii. Kuongeza uzalishaji wa ajira kufikia 1,700,000 mwaka 2026 kutoka ajira 981,000 zilizozalishwa mwaka 2024.

### 2.5.2 Misingi ya Mpango kwa Mwaka 2026/27

Ufanisi wa utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2026/27 utajengwa katika misingi ifuatayo:

i. Kuendelea kuwepo kwa demokrasia, amani, usalama na utulivu wa ndani na katika nchi jirani, inayowezesha shughuli za kiuchumi na uwekezaji kustawi;
ii. Kudumisha misingi ya utawala bora na utawala wa sheria, ikiwa ni pamoja na uwajibikaji, uwazi na ufanisi katika matumizi ya rasilimali za umma;
iii. Kuendelezwa kwa miundombinu ya nishati, bandari, barabara na reli kwa mujibu wa dira ya kuwa kitovu cha biashara, viwanda na usafirishaji katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kati;
iv. Kuimarika kwa ubunifu na matumizi ya teknolojia za kidijitali katika huduma za kijamii na uzalishaji;
v. Utekelezaji wa mageuzi ya kitaasisi na kiutawala chini ya falsafa ya 4Rs, unaolenga kuongeza ufanisi, uwazi na uwajibikaji;
vi. Kuimarika kwa mazingira ya uwekezaji kupitia mashirikiano ya sekta binafsi (PPP) na ushirikiano wa kikanda (EAC na SADC);
vii. Kuendelea kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi na majanga ya asili na yasiyo ya asili ikiwemo ukame, mafuriko, vita, milipuko ya magonjwa na misukosuko ya kiuchumi ya kimataifa kupitia mikakati ya kukabiliana na kupunguza athari zake;
viii. Kuendelea kuimarika kwa uchumi wa dunia na utulivu wa bei katika masoko ya fedha na bidhaa;
ix. Kuendelea kuimarika kwa upatikanaji na usalama wa chakula nchini; na
x. Kuweka misingi imara ya utekelezaji thabiti wa mipango iliyopangwa.

# SURA YA TATU

# MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO

### 3.1 Utangulizi

Serikali imeendelea kuchukua jitihada za dhati na mahsusi za kuandaa na kutekeleza mipango ya maendeleo ya muda mfupi, wa kati na mrefu yenye lengo la kuifanya nchi kuwa taifa linalo jitegemea kiuchumi, kisiasa na kijamii. Mipango hii ilijikita katika kuboresha maisha ya wananchi, kupunguza umasikini, kukuza uchumi wa taifa, na kuhakikisha maendeleo endelevu yanayoweza kunufaisha vizazi vya sasa na vijavyo.

Katika utekelezaji wa mipango hiyo, Serikali huibua miradi na programu mbalimbali ambazo huchangia kwa kiasi kikubwa katika maendeleo ya sekta mbalimbali. Mfano kwenye sekta ya kilimo, miradi ya umwagiliaji na ukuzaji wa mazao ya kimkakati kama pamba, korosho, kahawa, na nafaka imewezesha kuongeza uzalishaji, kuboresha usalama wa chakula, na kukuza pato la wakulima. Vilevile, sekta ya umeme ilipata msukumo kupitia miradi ya uzalishaji wa umeme kama vile mradi wa bwawa la Kufua Umeme wa Maji la Julius Nyerere pamoja na miradi ya gesi asilia ya **Kinyerezi I na II**, ambayo imeongeza upatikanaji wa umeme kwa viwanda, biashara, hivyo kuchangia moja kwa moja katika ukuaji wa uchumi.

Kwa upande wa sekta ya elimu, Serikali imehakikisha inaibua miradi mahsusi kwa ajili ya wananchi waliokuwa wamekosa fursa ya kusoma ambapo kupitia miradi hiyo, Serikali imelenga kuongeza wigo wa upatikanaji wa elimu, uboreshaji wa miundombinu ya shule, mafunzo ya walimu, na kuhakikisha kuwa watoto wote wanapata elimu bora ya msingi bure na sekondari. Vilevile, sekta ya maji na usafi wa mazingira imeimarishwa kupitia miradi, ambayo imehakikisha upatikanaji wa maji safi na huduma za usafi vijijini na mijini, kupunguza magonjwa yanayohusiana na maji machafu, na kuleta maendeleo ya kijamii. Katika kukabiliana na umaskini, Serikali iliibua na kutekeleza programu kama vile TASAF, ili kuongeza kipato na hivyo kupunguza umaskini, kukuza ajira, na kuhakikisha kuwa ukuaji wa uchumi unawanufaisha wananchi wote kwa usawa.

Aidha, tathmini ya utekelezaji wa viashiria dhidi ya shabaha zilizowekwa unaonesha matokeo chanya katika sekta mbalimbali. Kwa ujumla, sekta za miundombinu, uchukuzi, nishati, maji, utalii, viwanda, kilimo, mifugo na madini zimeonesha mwelekeo chanya unaoendana na uwekezaji mkubwa wa serikali katika miundombinu ya uzalishaji wa umeme, usafirishaji na programu za kuimarisha uzalishaji. Mafanikio mengine yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa miradi na programu za maendeleo ni pamoja na: kuongezeka kwa abiria wanaosafiri kwa njia ya reli. Hii imewezesha kupungua kwa muda na gharama za usafiri na usafirishaji, kuongezeka kwa ufanisi wa bandari na reli, na kuchochea biashara na utalii. Vilevile, uzalishaji wa umeme umeongezeka. Aidha, vijiji vyote vya Tanzania Bara viliunganishwa na huduma ya

umeme; upatikanaji wa huduma za intaneti umeongezeka; kupungua kwa muda wa makasha kukaa bandarini; na kuzalishwa kwa ajira katika sekta rasmi na isiyo rasmi.

Katika sekta za kijamii ikiwemo elimu, afya, maji, utawala bora na maendeleo ya jamii, kuna mafanikio katika upatikanaji wa huduma. Hali hii inatokana na: kuongezeka kwa miundombinu ya kutolea huduma za afya ambapo hospitali, zahanati na vituo vya afya hivyo kufanya wananchi wanaopata huduma hizi kuongezeka. Vilevile, wastani wa umri wa kuishi umeongezeka. Kwa upande wa elimu mwenendo unaonesha kuwa, kiwango cha uandikishaji rika lengwa katika elimu ya awali kimeongezeka na kiwango cha uandikishaji elimu ya awali. Aidha, idadi ya watu wa vijijini wanaopata maji ya bomba kama chanzo kikuu imeongezeka. Mafanikio katika nyanja mbalimbali za kiuchumi na kijamii yamewezesha kuongezeka kwa fahirisi ya maendeleo ya watu.

Pamoja na kwamba kumekuwa na mwenendo mzuri wa utekelezaji wa viashiria vya mpango, tathmini imeonesha baadhi ya sekta hazikuwa na mwenendo wa kuridhisha kama vile sekta ya michezo, sanaa na utamaduni. Hali hii imetokana na kukosekana kwa takwimu zinazojitosheleza kufanya tathmini.

Kwa ujumla, asilimia kubwa ya viashiria vinaonesha ongezeko, jambo linalodhihirisha kuwa utekelezaji wa Mpango umeleta matokeo chanya katika maeneo mengi ya kiuchumi na kijamii. Hata hivyo, mwendelezo wa mageuzi, uwekezaji katika rasilimali watu, ubunifu na maboresho ya mifumo ya usimamizi ni muhimu ili kuongeza uthabiti na ubora wa huduma, pamoja na kufikia shabaha za 2025/26 kikamilifu. Maelezo ya kina ya utekelezaji wa kisekta pamoja na mwenendo wa utekelezaji wa viashiria na shabaha umeainishwa kwa kina katika **Sehemu ya 3.3** na **Kiambatisho Na I**.

Mpango uliainisha miradi katika makundi mawili yaani miradi ya kielelezo na miradi ya kimkakati ambapo miradi ya kielelezo ilipewa kipaumbele kwa sababu ni miradi yenye matokeo mkubwa kiuchumi na kijamii endapo itatekelezwa kama ilivyopangwa. Miradi ya kimkakati ni ile ambayo utekelezaji wake una mchango wa kai kijamii na kiuchumi. Utekelezaji wa miradi hiyo ni kama ifuatavyo.

## 3.2. Miradi ya Kielelezo

Mpango ulijumuisha miradi 17 ya kielelezo, ambapo hadi Desemba, 2025 utekelezaji wa miradi hiyo ulikuwa katika hatua mbalimbali kama ifuatavyo.

### 3.2.1. Miundombinu ya Usafirishaji

Katika eneo hili Serikali imetekeleza miradi ifuatayo:

#### i. Ujenzi wa Madaraja ya Makubwa

Katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (FYDPIII), Serikali imetekeleza miradi ya ujenzi wa madaraja makubwa ambayo ujenzi wake utachochea shughuli za kiuchumi na kurahisisha usafiri na usafirishaji na hivyo kupunguza msongamano wa magari mijini.

Madaraja makubwa yaliyokamilika katika kipindi cha mpango ni Kigongo – Busisi (JPM), na Tanzanite. Vilevile, Serikali imekamilisha Ujenzi wa barabara za juu (Flyovers) katika maeneo ya Uhasibu na Chang'ombe. Kuanza kutumika kwa miundombinu hii kutachochea ukuaji wa uchumi kwa Ukanda wa Ziwa na nchi jirani kama Uganda, Rwanda na Burundi, hivyo kurahisisha usafirishaji wa mizigo na kukuza biashara ya kikanda, kupungua kwa msongamano wa magari na kurahisisha usafiri na usafirishaji wa malighafi kwenda viwandani na bidhaa kutoka viwandani pamoja na watu.

Aidha, Serikali inaendelea na ujenzi wa daraja la Jangwani jijini Dar es Salaam, ikiwa ni sehemu ya mkakati wa kudumu wa kupunguza foleni na kuondoa changamoto ya mafuriko ya mara kwa mara yanayoathiri jiji la Dar es salaam. Daraja hilo lina urefu wa mita 390, ambapo hadi kufikia Februari, 2026 utekelezaji ulikuwa asilimia 26. Hivyo, kukamilika kwa daraja hili kutachangia kuimarisha usafiri na usafirishaji katika maeneo ya Ilala, Buguruni, pamoja na sehemu nyingine zinazotegemea barabara ya Morogoro.

**ii. Ujenzi wa Reli ya Kati kwa Kiwango cha Kimataifa**

Serikali imeendelea na utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha kimataifa ili kuinua na kuimarisha huduma za usafirishaji. Katika kipindi cha kufikia Desemba 2025, utandazaji wa reli ya kati kwa kiwango cha kimataifa (Standard Gauge Railway – SGR) umefikia km 747 ambapo ujenzi wa kipande cha Dar es Salaam – Morogoro (km 300) umefikia asilimia 99.93; Morogoro – Makutupora (km 422) umefikia asilimia 98.60; Makutupora – Tabora (km 368) umefikia asilimia 14.54; Tabora – Isaka (km 165) umefikia asilimia 8.95, Mwanza – Isaka (km 341) umefikia asilimia 67.85 na Tabora – Kigoma (km 506) umefikia asilimia 9.06.

Kuanza kwa huduma za usafirishaji wa abiria kutoka Dar es Saalam hadi Dodoma kumepunguza muda wa safari kutoka saa 10 – 12 kwa mabasi hadi saa 3 – 4 kwa treni. Vilevile, jumla ya abiria 4,665,004 wamesafirishwa na mizigo tani 52,305 imesafirishwa, na watanzania wapatao 207,468 wamepata ajira katika utekelezaji wa mradi huu. Kati ya ajira hizo, watanzania 1,304 wameajiriwa katika kutoa huduma kwenye vituo vya SGR, watanzania 55,284 wamepata ajira za moja kwa moja na watanzania 150,880 ajira zisizo za moja kwa moja katika ujenzi wa reli ya SGR. Vilevile, safari za treni ya SGR zimeongeza tija katika uchumi na biashara kwa ujumla.

**iii. Ununuzi wa Meli na Ujenzi wa Bandari ya Uvuvi**

Ujenzi wa Bandari ya Uvuvi katika eneo la Kilwa - Masoko umeendelea, ambapo ujenzi huo umefikia asilimia 90. Ujenzi wa bandari hii ukikamilika utawezesha meli kubwa nne, ndogo 30 za kutoa huduma na meli mbili za doria. Shughuli zilizotekelezwa ni; kukamilika kwa uongezaji wa eneo kutoka baharini ili kuwezesha ujenzi wa miundombinu nchi kavu na baharini; na kuendelea na ujenzi wa majengo ya utawala, jengo la kupoza na kusambaza umeme, jengo la nitrojeni, jengo la soko, jengo la kuhifadhia na kuchambulia samaki, chelezo, ghala la kuhifadhia zana na jengo la karakana ya meli.

Kukamilika kwa mradi huu kutaboresha upatikanaji wa huduma zinazotolewa kwa meli za uvuvi; kuongezeka kwa uzalishaji na tija ya mazao ya uvuvi, katika Bahari Kuu; kuwezesha meli za uvuvi kushusha samaki wasiolengwa na kufanyika kwa shughuli ya kuaulisha (transhipment) mazao ya uvuvi; kuongeza fursa za ajira na kipato; na kuongeza uwekezaji katika viwanda vya kuchakata samaki katika mnyororo wa uongezaji thamani ya mazao ya uvuvi pamoja na kuongeza mapato ya fedha za nje yatakayotokana na mauzo nje ya mazao ya uvuvi.

**iv. Kuboresha Shirika la Ndege la Taifa**

Serikali imeendelea na utekelezaji wa mradi wa kuboresha Kampuni ya Ndege ya Taifa (ATCL), ambapo jumla ya ndege 15 zimenunuliwa na hivyo kuiwezesha Kampuni kuwa na jumla ya ndege 16 sawa na asilimia 84.2 ya lengo la ndege 19 ifikapo 2025/26. Idadi ya abiria imefikia 1,178,025 kwa mwaka 2024/2025 sawa na asilimia 49 ya lengo la kuhudumia wasafiri 1,549,764. Aidha, katika kipindi cha nusu mwaka (Julai-Desemba 2025) Kampuni ilisafirisha abiria 709, 432. Vile vile, usafirishaji wa mizigo ulikuwa tani 6,919 mwaka 2024/2025 na tani 2,779.05 Julai hadi Desemba 2025. Mtandao wa safari umefikia vituo 33 ikiwemo Kituo cha Lagos (Nigeria) na Accra (Ghana) kilichofunguliwa mwezi Januari 2026. Hivyo kuwezesha kuwa na huduma ya uhakika ya usafiri wa anga, kuongezeka kwa watalii wa ndani na nje ya nchi, na usafirishaji wa mazao na bidhaa za kilimo na mifugo na sekta ndogo ya mbogamboga na matunda.

### 3.2.2 Miradi ya Miundombinu ya Nishati

Katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, Serikali ilipanga kutekeleza miradi Saba (7) ya kielelezo ya nishati inayojumuisha uzalishaji umeme wa maji, utafutaji mafuta, gesi asilia, na bomba la kusafirisha mafuta ghafi kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga (Tanzania). Miradi hii ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

**i. Miradi ya Uzalishaji Umeme wa Maji**

Miradi ya kuzalisha umeme kwa njia ya maji inayotekelezwa ni pamoja na Mradi wa Kufua Umeme wa Julius Nyerere (MW 2,115), ambapo mitambo yote tisa (9) imekamilika na umeme umeunganishwa kwenye Gridi ya Taifa.

Aidha, miradi miwili ya Ruhudji (MW 358) na Rumakali (MW 222) ipo katika hatua za maandalizi. Kukamilika kwa miradi hii kutaimarisha upatikanaji wa umeme wa uhakika kwa ajili ya uzalishaji wa viwandani, kuongeza ajira kutokana na kuongezeka kwa shughuli za uzalishaji, kuchochea uwekezaji nchini, kupunguza utegemezi wa mafuta katika uzalishaji wa umeme ambao hutumia fedha nyingi za kigeni, na kukuza uchumi shindani na jumuishi.

**ii. Miradi ya Usindikaji Gesi Asilia na Utafutaji Mafuta**

Serikali imetekeleza miradi ya utafutaji wa mafuta na gesi asilia katika vitalu vya Eyasi – Wembere na Mnazi Bay, pamoja na mradi wa Kusindika Gesi Asilia kuwa Kimiminika (LNG). Miradi hiyo ipo katika hatua za awali za utafiti ambapo kwa upande wa utafutaji mafuta, shughuli za ukusanyaji wa taarifa za *seismic* za 2D zinaendelea

na hali ya utekelezaji kwa ujumla imefikia asilimia 40. Aidha, kwa upande wa mradi wa LNG, majadiliano baina ya Serikali na wawekezaji yapo katika hatua za ukamilishaji.

Kukamilika kwa miradi hii kutaongeza uzalishaji wa gesi asilia nchini kwa ajili ya matumizi ya ndani ikiwemo viwandani pamoja na kuuza gesi hiyo katika nchi jirani za Kenya, Uganda, Zambia na Malawi. Hatua hiyo itachangia katika ukuaji wa uchumi, ongezeko la fedha za kigeni, fursa za ajira na huduma za ugavi na biashara kwa Watanzania. Aidha, itachochea uchumi shindani na jumuishi, uwekezaji, kuongezeka kwa uzalishaji viwandani, kuchangia maendeleo ya watu na ujuzi.

**iii. Mradi wa bomba la kusafirisha mafuta ghafi kutoka Uganda hadi Tanzania (EACOP)**

Serikali inaendelea na utekelezaji wa mradi wa Ujenzi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Ghafi lenye urefu wa km 1,443 kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga (Tanzania) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 79. Kukamilika kwa mradi huu kutaongeza ajira za kudumu na za muda mfupi; kukuza mapato ya Serikali; kuhamasisha shughuli za utafutaji wa mafuta na gesi asilia nchini; kuongeza wigo wa shughuli za uwekezaji na biashara; kuchangia maendeleo ya rasilimali watu na ujuzi; na kuchochea ukuaji wa uchumi shindani na endelevu.

**iv. Mradi wa makaa ya mawe Mchuchuma na Chuma Liganga**

Mgodi wa makaa ya mawe unatarajiwa kuzalisha tani milioni tatu za makaa ya mawe kwa mwaka na kuzalisha umeme MW 600. Aidha, uzalishaji wa chuma unatarjiwa kuwa tani milioni 2.9 kwa mwaka, kiwanda cha kuzalisha bidhaa za chuma tani 1.1 kwa mwaka. Serikali imefanikiwa kulipa fidia ya shilingi bilioni 15.4 kwa wananchi 1,142 wanaopisha utekelezaji wa mradi huo sawa na asilimia 99.8. Mafanikio mengine ni pamoja na kuandaliwa kwa rasimu za mikataba ya ubia (JVAs) na mikataba ya wanahisa (SHAs) kwa miradi ya uchimbaji na kiwanda cha kutengeneza bidhaa za chuma. Majadiliano na mwekezaji yanaendelea.

Matokeo ya mradi huu utakapoanza kutekelezwa ni pamoja na kupatikana kwa malighafi ya chuma na makaa ya mawe kwa ajili ya matumizi ya viwanda vya ndani na nje ya nchi; kupunguza matumizi ya fedha za kigeni kuagiza chuma nje; kuimarisha maendeleo ya watu kupitia ajira zitakazozalishwa; na kuongeza upatikanaji wa fedha za kigeni kwa kuongeza mauzo chuma, makaa ya mawe na saruji nje. Mradi huu unatarajiwa kuchochea uchumi shindani na jumuishi, uwekezaji na biashara na kuongeza uzalishaji bidhaa viwandani.

### 3.2.3 Miradi ya Kuongeza Uzalishaji Viwandani

Serikali kupitia Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano iliainisha miradi mitatu ya kielelezo yenye kujielekeza moja kwa moja kwenye kuongeza uzalishaji viwandani. Miradi hiyo ni Magadi soda (Engaruka), kiwanda cha sukari Mkulazi na Kanda maalum za uchumi na uwekezaji.

**i. Mradi wa Magadi Soda ya Engaruka**

Zoezi la uthamini kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi wa Magadi Soda katika eneo la Engaruka lilifanyika mwaka 2017 na kuidhinishwa rasmi na Mthamini Mkuu wa Serikali mwaka 2022. Hadi Februari 2025, kiasi cha Shilingi 5,821,993,050.28 kimelipwa kama fidia kwa wanufaika 508.

Matokeo ya kukamilika kwa mradi huu ni pamoja na: kuongeza ajira; kupunguza matumizi ya fedha za kigeni kwa ajili ya kuagiza magadi soda kutoka nchi za nje; na kuongeza mauzo nje ya nchi. Mradi utasaidia upatikanaji wa malighafi za magadi soda na kuanzishwa kwa viwanda vinavyotumia malighafi hizo.

**ii. Kiwanda cha Sukari Mkulazi**

Mradi wa Kiwanda cha Sukari Mkulazi ni moja kati ya uwekezaji wa kimkakati wa Serikali kupitia ubia kati ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) unaomiliki asilimia 96 na Jeshi la Magereza kupitia Shirika la Uzalishaji Mali linalomiliki asilimia 4. Utekelezaji wa mradi unajumuisha uendelezaji wa shamba la miwa lenye ukubwa wa hekari 3600, pamoja na ujenzi wa kiwanda cha kuzalisha sukari katika eneo la Mbigiri wilaya ya Kilosa, Morogoro kwa gharama ya shilingi bilioni 354. Aidha, uendelezaji wa shamba la miwa ulianza tarehe 20 Septemba, 2016 na kukamilika 10 Septemba, 2025. Ujenzi wa kiwanda cha kuzalisha sukari ulianza tarehe 9 Julai, 2021 na kukamilika 31 Agosti, 2024.

Utekelezaji wa mradi umekamilika na jumla ya shilingi bilioni 354 zimetumika, ambapo usimikaji wa mitambo ya kuzalisha sukari ya matumizi ya majumbani (brown sugar) umekamilika. Uzalishaji rasmi wa sukari ya majumbani ulioanza msimu wa 2024/25 ulizalisha tani 19,124 za sukari sawa na asilimia 96 ya lengo la tani 20,000 na tani 10,773 za molasi sawa na asilimia 118 ya lengo la tani 9,115. Aidha, uzalishaji wa msimu wa pili wa 2025/26 ulizalisha tani 26,470 za sukari sawa na asilimia 97.5 ya lengo la tani 27,139, pamoja na tani 9,197 za molasi sawa na asilimia 99.7 ya lengo la tani 9,227.

Usimikaji wa mitambo ya kuzalisha sukari ya viwandani (refined sugar) umekamilika na katika kipindi cha majaribio tani 256 za sukari ya viwandani zilizalishwa, hatua inayoifanya nchi na kuwa na kiwanda chenye uwezo wa kuzalisha sukari ya viwandani. Kuanza kwa uzalishaji wa sukari kumepunguza upungufu wa sukari nchini. Aidha, uzalishaji huu umepunguza uagizaji sukari nje na hivyo kusaidia Serikali kupunguza matumizi ya fedha za kigeni za uagizaji wa sukari.

Kwa upande wa mashamba ya miwa, uendelezaji umefikia asilimia 97 ambapo kati ya hekta 3,600, hekta 3,500 za shamba zimelimwa na kupandwa; kukamilika kwa ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika hekta 2,730 kati ya hekta 3,600 pamoja na kukamilika kwa mabwawa mawili (2) yenye uwezo wa mita za ujazo milioni 1.6 na mita za ujazo 3.5. Vilevile, uendelezaji wa mashamba ya wakulima wadogo wadogo umefikia asilimia 80 ambapo hekta 1,384 kati ya 1,717 zimeendelezwa; usimikaji wa mitambo ya kuzalisha megawati 15 za umeme umekamilika, ambapo megawati 8 zinatumika kiwandani na megawati 7 zinatarajiwa kuuzwa TANESCO; na kukamilika kwa njia ya usafirishaji wa umeme wa megawati 15 yenye urefu wa kilometa 56.439.

Kukamilika kwa mradi huu kutaongeza uzalishaji wa sukari ndani ya nchi kwa kufikia tani 50,000 ifikapo Juni 2028, hivyo kupunguza pengo la mahitaji ya sukari kutoka nje na kuchochea maendeleo ya kijamii na kiuchumi kupitia ongezeko la thamani kwenye mazao ya kilimo. Aidha, mradi huu umesaidia kuimarisha ushirikiano na wakulima wadogo 304 wanaozalisha miwa kwa ajili ya kiwanda. Ushirikiano huo umechangia kuongeza kipato cha kaya, kukuza ajira za moja kwa moja kwa takribani wafanyakazi 2,000, pamoja na ajira zisizo za moja kwa moja zinazokadiriwa kuwa 8,000.

**iii. Maeneo Maalum ya Kichumi**

Serikali ililenga kuendelea kuimarisha miundombinu katika Maeneo Maalum ya Kiuchumi pamoja na kuanzisha maeneo mapya katika mikoa ya Singida (Manyoni), Pwani, Kigoma, Tanga, Manyara, Mara, na Ruvuma. Aidha, maeneo ya Benjamin William Mkapa SEZ, Bagamoyo SEZ na Mtwara SEZ yanaendelea na uzalishaji.

Utekelezaji wa miradi katika maeneo maalum ya kiuchumi umeongeza idadi ya miradi ya uwekezaji iliyosajiliwa ilikuwa 157 mwaka 2024/25. Miradi hii ipo katika hatua mbalimbali za uibuaji na utekelezaji ambayo ilikuwa na thamani ya uwekezaji dola za marekani milioni 8,813 mwaka 2024/25 na dola za marekani milioni 8,500 kwa kipindi cha nusu mwaka 2025/26. Aidha, kongani za uwekezaji zimefikia 32 Desemba 2025, na kutengeneza ajira 280,000 mwaka 2024/25 na ajira 250,000 Desemba 2025. Kutekelezwa kwa miradi ya maeneo maalum ya uchumi na uwekezaji kumeongeza ushindani katika soko la ndani na nje, uzalishaji viwandani pamoja na kuvutia uwekezaji nchini.

## 3.3 Mapitio ya Utekelezaji Kisekta

Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano uliweka shabaha za utekelezaji zilizotakiwa kupimwa kupitia viashiria vya kisekta. Ufikiwaji wa shabaha zilizowekwa unategemea utekelezaji wa miradi na programu mbalimbali za maendeleo ambazo zinachangia katika maendeleo ya sekta. Aidha, ili kuwa na tathmini mathubuti ya utekelezaji wa Mpango na kujenga msingi wa kuweka vipaumbele vya Mpango kwa mwaka 2026/27, sehemu hii imeainisha uchambuzi wa kila sekta na kuonesha hatua zilizochukuliwa, mafanikio yaliyopatikana na matarajio ya sekta ili kuimarisha utekelezaji. Mwendendo wa viashiria na shabaha za Mpango ni kama ifuatavyo**:**

### 3.3.1 Sekta ya Ujenzi

Ujenzi wa mtandao wa barabara ulifikia urefu wa kilometa 37,734. Mtandao huo, unawezesha kuifungua nchi na kurahisisha usafiri na usafirishaji wa bidhaa kwenda kwenye maeneo mbalimbali. Vilevile,ulilenga kujenga miundombinu imara ambayo ni kichocheo kikuu cha ukuaji wa uchumi, biashara na kuongeza ajira hasa ikizingatiwa kuwa Tanzania ni lango kuu la biashara kwa nchi za Zambia, Malawi, DRC, Burundi, Rwanda na Uganda. Mpango ulilenga kushirikisha Sekta binafsi katika utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa barabara, madaraja na majengo inayotekelezwa ambayo itachochea maendeleo ya sekta nyingine kama viwanda, huduma na maendeleo ya miji.

Utekelezaji wa afua umechangia: mtandao wa barabara zinazopitika wakati wote za kitaifa na za mikoa umefikia km 37,734.41 Desemba, 2025 kutoka km 37,435 mwaka 2024/25; mchango wa kampuni za ndani katika soko la Ujenzi ulikuwa asilimia 40 ya jumla ya thamani ya miradi yote mwaka 2024/25; Nafasi katika mpangilio, kati ya nchi 189 kimataifa ulikuwa nafasi ya 50 mwaka 2024/25; na wastani wa ukuaji sekta ulikuwa 4.1 mwaka 2024/25; ajira kwa makandarasi, washauri elekezi, mafundi na wafanyabiashara wa vifaa vya ujenzi zilikuwa 21,527 Desemba 2024 ilikinganishwa na ajira 18,988 Desemba 2025. Aidha, Sekta ya Ujenzi imekuwa na mchango mkubwa katika pato la taifa ambapo katika mwaka 2024/25 imechangia kwa asilimia 12.8 na kukamilika kwa miradi 40 kati ya miradi 81 ya ujenzi wa madaraja ya dharura na kuwezesha mawasiliano ya barabara kurejea haraka baada ya kukatika.

**Kielelezo Na. 3.1: Mwenendo wa Mchango wa Kampuni za Ndani katika Soko la Ujenzi (Asilimia)**




***Chanzo:*** Wizara ya Ujenzi

Mafanikio ya yaliyopatikana ni pamoja na: kupunguza gharama na muda wa usafirishaji, kuongeza mzunguko wa bidhaa na huduma, na kukuza ushindani wa uzalishaji katika sekta za kilimo, viwanda, biashara na utalii. Aidha, barabara bora huvutia uwekezaji wa ndani na nje kwa kuweka mazingira rafiki ya biashara, kuongeza ajira na kipato kwa wananchi kupitia shughuli mbalimbali za kiuchumi, na kuboresha upatikanaji wa huduma za kijamii kama afya, elimu na huduma za dharura. Vilevile, huimarisha muunganiko wa kitaifa na kukuza biashara ya kikanda kwa kuunganisha maeneo ya uzalishaji na masoko, hivyo kuchangia kwa kiasi kikubwa katika kupunguza umaskini na kuinua ustawi wa jamii kwa ujumla.

Matarajio ya Sekta ya Ujenzi ni kuhakikisha inaongeza kasi ya kujenga miundombinu kwa njia ya ubia baina ya Serikali na Sekta Binafsi na kuondoa dhana ya miradi ya ujenzi wa miundombinu kutekelezwa na Serikali pekee. Sekta binafsi na mashirika ya kimataifa yanayo nafasi muhimu sana, siyo tu kwenye kufadhili bali pia kwenye utaalamu wa kiufundi, ubunifu wa kiteknolojia na usimamizi. Sekta ya Ujenzi

itahakikisha inajenga mazingira wezeshi ili wakandarasi, wawekezaji na washauri binafsi waone fursa katika kila hatua kuanzia usanifu hadi uendeshaji wa mradi.

**Kielelezo Na. 3.2**: **Mchango katika Pato la Taifa, Wastani wa Ukuaji wa Sekta ya Ujenzi kuanzia mwaka 2019/20 hadi mwaka 2025/26**




***Chanzo:*** Wizara ya Ujenzi

### 3.3.2 Sekta ya Uchukuzi

Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ulilenga kuboresha miundombinu ya usafiri na usafirishaji kwa njia ya reli, anga, maji na huduma za hali ya hewa; kuendeleza na kuboresha viwanja vya ndege; na kuimarisha huduma za mawasiliano katika viwanja vya ndege.

Utekelezaji wa afua zilizowekwa umechangia kuongezeka kwa mchango wa sekta ya uchukuzi katika pato la taifa kufikia asilimia 7.5 mwaka 2024; idadi ya abiria waliosafirishwa kwa reli ilikuwa 7,851,127 kwa mwaka 2024/25 na kipindi cha Julai hadi Desemba 2025 ni 2,893,457; kuongezeka kwa wanaanga waliopatiwa mafunzo kufikia wanaanga 1,204 mwaka 2024/25; kuongezeka kwa idadi ya meli zilizohudumiwa na bandari zote nchini kufikia 4,888 kwa mwaka 2024/25 Aidha, kwa kipindi cha Julai hadi Desemba 2025 idadi ya meli zilizohudumiwa zilifikia 1,761; na kupungua kwa muda wa makasha kukaa bandarini kufikia wastani wa siku nne na nusu (4.5) mwaka 2025/26.

Mafanikio yaliyopatikana kutokana utekelezaji wa afua: kuimarika kwa huduma za reli kwa kupunguza muda na gharama za safari, kuongeza usafirishaji wa abiria na shehena, na kuchochea uzalishaji mali katika mikoa inayounganishwa na SGR; kuongezeka kwa wigo wa safari za ndege ndani na nje ya nchi, kumechochea utalii na kuongeza mapato yatokanayo na bidhaa za kilimo kupitia usafirishaji wa mazao yanayoharibika haraka kwa ndege maalumu ya mizigo; na kuongezeka kwa ufanisi wa kuhudumia meli hivyo, kupunguza muda wa meli kukaa bandarini na kuongeza ushindani wa Bandari ya Dar es Salaam katika ukanda wa Afrika Mashariki.

**Kielelezo Na. 3.3: Idadi ya Abiria wanaosafirishwa na Reli**




***Chanzo:*** Wizara ya Uchukuzi

Utekelezaji wa afua za Uchukuzi unaonesha mafanikio kupitia kuimarika kwa ufanisi wa usafiri wa reli, huduma za usafiri wa barabara (usafiri wa mabasi kwa saa 24), anga na bandari, na hivyo kupungua kwa gharama na muda wa usafiri na usafirishaji. Uwekezaji katika miundombinu ya usafiri na usafirishaji umeongeza tija, kukuza biashara, utalii, na kuongeza ushindani wa kimataifa sambamba na kuimarisha ujuzi wa wataalamu wa ndani kupitia uhawilishaji teknolojia. Aidha, matarajio ya mwenendo wa sekta ni kukamilisha sehemu zilizobaki za SGR na kuongeza usafirishaji wa mizigo; kuongeza idadi ya ndege na kuongeza mtandao wa safari kimataifa; kuimarisha usalama wa usafiri majini; kuimarisha miundombinu na rada za hali ya hewa; na kuendelea kuimarisha ufanisi wa bandari.

### 3.3.3 Sekta ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari

Sekta Mawasiliano na Teknolojia ya Habari imeendelea kuwa kichocheo muhimu cha shughuli za kiuchumi na kijamii kupitia matumizi ya mtandao wa intaneti, hivyo kuchangia katika kufanikisha vipaumbele vya kuchochea ushindani, kuongeza uzalishaji viwandani, pamoja na kuimarisha uwekezaji na biashara, kama ilivyobainishwa katika Mpango wa mwaka 2025/26.

Serikali imechukua hatua mbalimbali ili kuboresha mawasiliano, upatikanaji na utumiaji wa intaneti nchini ikiwemo: Kuongeza urefu wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano (NICTBB) hadi kufikia kilomita 15,066; kuboresha mtandao wa intaneti katika minara 304 ya simu kutoka 2G hadi 2G/3G na 4G; kujenga minara 758; ujenzi na uunganishaji wa mifumo ya TEHAMA; maandalizi ya miongozo mbalimbali inayochochea ukuaji wa shughuli za uchumi wa kidigitali pamoja na matumizi salama ya mitandao; na utekelezaji wa mradi wa Anwani za Makazi ambao umewezesha kusajili jumla ya anwani 13,200,000 kwenye Mfumo wa Anwani za Makazi (NaPA) mwaka 2024/25.

Utekelezaji wa afua zilizowekwa umechangia kuongezeka kwa: Uwiano wa watumiaji wa intaneti nchini kutoka asilimia 74 mwaka 2024 hadi asilimia 85 mwaka 2025;Uwiano wa watu waliofikiwa na mitandao ya simu za mkononi kutoka asilimia 94 mwaka 2024/25 hadi asilimia 98 mwaka 2025/26; na Majengo yenye anwani za makazi kufikia 18,558,268 mwaka 2025/26 kutoka majengo 18,186,0000 mwaka 2024/25;

Mafanikio yaliyopatikana kutokana utekelezaji wa afua hizo ni pamoja na: Kuongezeka kwa Upatikanaji wa Habari; Kuongezeka kwa Fursa za Kiuchumi; Uboreshaji wa Huduma za Serikali (e-Government); Kuchochea ubunifu na uwekezaji; na Kuboresha huduma za afya na kilimo. Pia kuongezeka kwa idadi ya majengo yenye anwani za makazi kumeleta matokeo chanya kwa jamii ikiwemo kumuongoza (Navigation) mtu kutoka eneo moja au anwani ya makazi moja kwenda eneo jingine; kutambua na kuyafikia maeneo ya utalii na vivutio; kuonesha huduma za karibu kama vile ATM, Hospitali, Hoteli na Stendi; na kutoa barua ya utambulisho wa mkazi kidijitali kupitia mfumo wa kidijitali wa NaPA ambapo kwa sasa muda wowote na mahali popote, mwananchi ataweza kuomba na kupata barua ya utambulisho wa mkazi kupitia simu yake ya mkononi au kompyuta bila kufika ofisi ya Mtendaji wa Kata, Mtaa au Kijiji.

Utekelezaji wa afua za Sekta ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari umebainisha kuongezeka kwa Uwiano wa watumiaji wa intaneti nchini, Uwiano wa watu waliofikiwa na mitandao ya simu za mkononi pamoja na kuboresha utoaji huduma wa Serikali. Aidha matarajio ya Sekta ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari ni kuwa na jamii iliyoimarishwa kidijitali inayoendeshwa na uchumi wa kidijitali kwa maendeleo endelevu.

**Kielelezo Na. 3.4: Kiwango cha watu wanaopata na kutumia mtandao wa internet pamoja na simu kuanzia mwaka 2019/20 hadi mwaka 2025/26**




***Chanzo:*** Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari

### 3.3.4 Sekta ya Nishati

Sekta ya Nishati ni sekta wezeshi inayochagiza na kuchochea shughuli mbalimbali za

kiuchumi na kijamii. Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ulilenga kuimarisha upatikanaji wa nishati ya umeme kwa kuongeza uwezo wa uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme nchini; kujenga na kuimarisha miundombinu ya usambazaji wa gesi asilia; kubuni vyanzo vya nishati jadilifu kwa ajili ya kupikia ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi; na kuendeleza shughuli za utafutaji wa mafuta na gesi asilia.

Utekelezaji wa afua umechangia: kuongezeka kwa uwezo wa mitambo ya uzalishaji wa umeme kufikia MW 4,504.54 Desemba 2025 kutoka MW 4,437.53 mwaka 2024/25; kuongezeka kwa urefu wa Gridi ya Taifa kufikia km 8,500.38 mwaka 2024/25 sawa na asilimia 72.22 ya lengo la kufikia urefu wa km 9,351 ifikapo mwaka 2025/26; kupungua kwa upotevu wa umeme kufikia asilimia 13.86 mwaka 2024/25; kuongezeka kwa idadi ya vituo vya CNG *(Compressed Natural Gas)* kufikia vituo 13 mwaka 2025/26; kuongezeka kwa kiwango cha matumizi ya umeme kwa mtu mmoja kufikia kWh 170 mwaka 2024/25; na kuunganishwa umeme vijiji vyote 12,318 mwaka 2024/25. Aidha, hadi Desemba 2025 jumla ya vitongoji 39,003 kati ya vitongoji 64,359 vya Tanzania bara sawa na asilimia 61 vimepewa huduma ya umeme kupitia miradi mbalimbali inayotekelezwa na REA.

**Kielelezo Na. 3.5: Mwenendo wa uzalishaji wa umeme nchini (MW) kuanzia mwaka 2019/20 hadi mwaka 2025/26**




***Chanzo:*** Wizara ya Nishati

Mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa afua ni pamoja na: kuboreshwa kwa upatikanaji wa nishati kwa wananchi, taasisi na viwanda; kuanzishwa kwa viwanda na biashara ndogo ndogo ambazo zinahitaji huduma ya nishati; kuongezeka kwa matumizi ya nishati safi ya kupikia kumechangia kuboresha maisha ya wananchi na kulinda mazingira; kuongezeka kwa ajira, ujuzi, na mapato ya Serikali. Mafanikio haya yameweka msingi thabiti wa uchumi wa viwanda, kuongeza ushindani wa taifa katika masoko ya kikanda na kimataifa, na kuimarisha usalama wa nishati kwa maendeleo endelevu ya Taifa.

Utekelezaji wa afua za sekta ya nishati umebainisha kuwa: uwekezaji katika miradi mikubwa ya kimkakati kama Bwawa la Umeme la Julius Nyerere ni muhimu kwa kuongeza uzalishaji wa umeme na kuimarisha miundombinu ya viwanda; ushirikiano kati ya sekta ya umma na binafsi umethibitisha kuwa ni njia bora ya kufanikisha miradi ya kimataifa kama EACOP; matumizi ya nishati safi kama gesi asilia, jua na upepo yameonekana kuwa na mchango mkubwa katika kulinda mazingira na afya ya jamii; takwimu sahihi na mifumo ya ufuatiliaji wa miradi ni muhimu kwa kuhakikisha utekelezaji bora; maendeleo ya rasilimali watu kupitia mafunzo ya kitaalamu yameongeza ufanisi wa sekta; na upanuzi wa mtandao wa usambazaji umeme vijijini umechangia kwa kiasi kikubwa katika kuharakisha maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Aidha, matarajio ya mwenendo wa sekta ni kuendelea: kuimarisha sekta ya nishati kwa kuongeza uwezo wa uzalishaji wa umeme hadi kufikia megawati 8,000 kupitia vyanzo mbalimbali; kuunganisha vitongoji vyote vilivyobakia, na kuboresha miundombinu ya usafirishaji na usambazaji wa umeme; kukuza matumizi ya nishati safi ya kupikia; na kuendelea na shughuli za utafiti, uchimbaji na usindikaji wa mafuta na gesi asilia. Hatua hizi zote zinalenga kuleta mageuzi ya kiuchumi, kuboresha maisha ya wananchi na kuhakikisha upatikanaji endelevu wa nishati nchini.

### 3.3.5 Sekta ya Kilimo

Mpango wa ulilenga kuboresha mifumo ya umwagiliaji ikiwa ni pamoja na ujenzi wa mabwawa ya maji, kuimarisha Utafiti na maendeleo katika mazao ya kimkakati; kuimarisha mnyororo wa uongezaji thamani ya mazao ya biashara pamoja na kuhimiza matumizi ya TEHAMA katika uendeshaji wa vyama vya ushirika; kuhakikisha upatikanaji wa malighafi za viwandani; uongezaji tija na uzalishaji wa mazao ya kilimo; kuongeza usalama wa chakula na lishe; kuongeza thamani ya mauzo nje ya nchi; na kupunguza upotevu wa mazao baada ya kuvuna.

Utekelezaji wa afua umechangia: eneo la umwagiliaji lilikuwa hekta 983,466.6 mwaka 2024/25; uzalishaji wa mazao ya chakula ilikuwa tani 22,803,316 mwaka 2024/2025; utoshelevu wa chakula nchini umefikia asilimia 128 mwaka 2024/25; uwezo wa miundombinu ya Hifadhi ya Taifa ya Chakula (NFRA) umefikia tani 776,000 mwaka 2024/2025; uzalishaji wa mazao ya bustani ulikuwa tani 7,518,560.84 mwaka 2024/2025; uzalishaji wa mazao asili ya biashara ilikuwa tani 1,451,694.11 mwaka 2024/2025. Vilevile, idadi ya wanachama wa vyama vya ushirika imefikia milioni 8.4 mwaka 2024/25; na kuongezeka kwa idadi ya viwanda vinavyomilikiwa na vyama vya ushirika kufikia 331 mwaka 2024/25.

Mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa afua ni pamoja na: kuongezeka kwa ajira zenye staha na ushiriki wa vijana na wanawake katika kilimo; kuimarika kwa upatikanaji wa pembejeo za kilimo ikiwemo mbegu bora, mbolea, viuatilifu na zana za kilimo; kupungua kwa upotevu wa mazao baada ya kuvunwa; kuimarika kwa usalama wa chakula, kupungua kwa uagizaji wa sukari na mafuta nje ya nchi; kuongezeka kwa upatikanaji wa masoko ya mazao na kupanda thamani ya mauzo ya mazao nje ya nchi; na kuimarika kwa huduma za ugani katika kilimo.

**Kielelezo Na. 3.6**: **Hekta za Kilimo cha Umwagiliaji kwa kipindi cha mwaka 2019/20 hadi mwaka 2025 /26**




***Chanzo:*** Wizara ya Kilimo

**Kielelezo Na. 3.7**: **Uzalishaji wa Mazao asili ya biashara kwa kipindi cha mwaka 2021/22 hadi mwaka 2025/26**




***Chanzo:*** Wizara ya Kilimo

Utekelezaji wa afua za kuendeleza kilimo umebainisha kuwa uwekezaji katika miundombinu ya umwagiliaji ni muhimu ili kuwezesha uzalishaji kufanyika kwa kipindi chote cha mwaka bila kutegemea mvua za msimu. Vilevile, matumizi ya teknolojia bora za kilimo husaidia kupunguza watu mashambani ili wajiajiri katika sekta za viwanda na huduma za ugani na ushauri wa kitaalamu kuhusu matumizi ya mbegu bora, mbolea, udhibiti wa visumbufu vya mazao na kilimo endelevu ni muhimu katika kuongeza uzalishaji na tija. Aidha, matarajio ya mwenendo wa sekta ya kilimo ni kuhakikisha sekta inakua kwa asilimia 10 kwa mwaka ifikapo mwaka 2030, na hivyo kuchangia katika kupunguza umaskini kwa kuongeza pato la mkulima.

### 3.3.6 Sekta ya Mifugo

Mpango ulilenga kuwezesha upatikanaji wa chanjo bora za magonjwa ya mifugo; kuimarisha mifumo ya kufuatilia na kudhibiti magonjwa ya mifugo; kuimarisha ujenzi wa miundombinu ya mifugo ya udhibiti wa vimelea; kutenga, kupima na kuendeleza maeneo ya malisho; kuwezesha utambuzi, usajili na kuhamasisha mauzo ya bidhaa za mifugo nje; na kuongeza idadi na uwezo wa viwanda vya kuchakata mazao ya mifugo.

Utekelezaji wa mwaka 2024/2025 unaonesha kupungua kwa vifo vya mifugo kutoka asilimia 16 Desemba 2024 hadi asilimia 12 Desemba 2025; kupungua kwa magonjwa ya mifugo kutoka asilimia 2.5 Desemba 2024 hadi asilimia 1.8 Desemba 2025; kuimarika kwa kiwango cha uogeshaji wa mifugo kutoka asilimia 82 Desemba 2025 hadi asilimia 85 Desemba 2025; kuimarika kwa kiwango cha utowaji wa chanjo ya mifugo kutoka asilimia 42 Desemba 2025 hadi asilimia 70 Desemba 2025; uzalishaji wa maziwa umeongezeka kutoka lita bilioni 4.1 Desemba 2025 hadi lita bilioni 4.5 Desemba 2025 na mauzo ya nyama nje ya nchi zilikuwa tani 14,900 Desemba 2025.

Mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa afua ni pamoja na; kuongezeka kwa tija na mnyororo wa thamani katika uzalishaji wa bidhaa za mifugo; kupungua kwa vifo na magonjwa ya mifugo; na kuongezeka kwa mauzo ya mazao ya mifugo ndani na nje ya nchi.

Utekelezaji wa afua za Sekta ya Mifugo unaonesha kuongezeka kwa matumizi ya chanjo na mwitikio wa uogeshaji wa mifugo pamoja na uboreshaji wa miundombinu ya malisho, maji na huduma za ugani kulikopelekea ongezeko la uzalishaji wa mifugo na bidhaa za mifugo. Aidha, matarajio ya mwenendo wa sekta ni kuongeza uwekezaji katika ufugaji wa kibiashara; kufanya mageuzi ya miundombinu ya malisho na maji; na kuimarisha teknolojia za udhibiti wa magonjwa ili kupunguza milipuko na kuongeza ubora wa mifugo.

**Kielelezo Na. 3.8: Mlinganisho wa kiwango cha Magonjwa ya Mifugo na Uzalishaji wa Maziwa (Lita Bilioni) kwa kipindi cha mwaka 2021/22 hadi mwaka 2025/26**




***Chanzo:*** Wizara ya Mifugo na Uvuvi

**Kielelezo Na. 3.9: Mlinganisho wa Kiwango cha Vifo vya Mifugo, Uogeshaji Mifugo katika Josho na chanjo ya mifugo kwa kipindi cha mwaka 2021/22 hadi mwaka 2025/26**




***Chanzo:*** Wizara ya Mifugo na Uvuvi

**Kielelezo Na. 3.10**: **Mauzo ya Nyama nje ya nchi (Tani) kwa kipindi cha mwaka 2021/22 hadi mwaka 2025/26**




***Chanzo:*** Wizara ya Mifugo na Uvuvi

### 3.3.7 Sekta ya Uvuvi

Mpango ulilenga kuimarisha ujenzi wa miundombinu na uwezo wa kitaasisi ili kuboresha usimamizi wa sekta ya uvuvi. Miongoni mwa afua zitakazotekelezwa zinajumuisha: ujenzi wa bandari ya uvuvi; kuboresha mazingira ya uwekezaji kwa sekta binafsi; kuanzisha na kukarabati viwanda vya mazao ya uvuvi; ujenzi wa miundombinu ya uvuvi; ununuzi wa zana na vifaa vya uvuvi; na kuhamasisha ukuzaji viumbemaji kibiashara.

Ukuaji wa sekta ya uvuvi ulifikia asilimia 2.3 mwaka 2024/25; mapato ya sekta ya uvuvi yatokanayo na mauzo nje yalikuwa asilimia 3.4 mwaka 2024/25; uzalishaji wa samaki ulikuwa tani 575,000 mwaka 2024/25; na idadai ya viwanda vya uchakataji na usindikaji wa samaki vimefikia 21 mwaka 2024. Uzalishaji wa vifaranga vya samaki ulikuwa 154,846,692 Desemba 2025.

Mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa afua ni pamoja na: kuongeza mchango wa sekta katika usalama wa chakula na lishe; kutoa ajira za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja; na kuchangia upatikanaji wa fedha za kigeni.

Utekelezaji wa afua za sekta ya uvuvi umebainisha kuwa, kuna fursa kubwa za uvuvi katika bahari kuu. Hivyo Serikali itaendelea kuweka mikakati ya kuhakikisha kuwa ujenzi wa bandari ya uvuvi na ununuzi wa meli ya uvuvi vinakamilika ili kuweza kutumia fursa hiyo. Aidha, matarajio ya mwenendo wa sekta ni kuongeza uzalishaji wa mazao ya uvuvi na ukuzaji viumbemaji; kuboresha miundombinu ya uvuvi; na kuimarisha tafiti za uvuvi na kutumia taarifa za tafiti.

**Kielelezo Na. 3.11**: **Uzalishaji wa Samaki kwa kipindi cha mwaka 2021/22 hadi mwaka 2025/26**




***Chanzo:*** Wizara ya Mifugo na Uvuvi

**Kielelezo Na. 3.12: Uwiano wa Kiwango cha Ukuaji wa Sekta ya Uvuvi, mapato yatokanayo na Mauzo Nje, Mchango katika ulaji wa Protini ya Wanyama na Idadi ya Viwanda vya kusindika samaki**




***Chanzo:*** Wizara ya Mifugo na Uvuvi

### 3.3.8 Sekta ya Uzalishaji Bidhaa Viwandani

Sekta ya Viwanda imeendelea kuwa nguzo muhimu katika kuleta matokeo makubwa kwenye sekta mbalimbali za uzalishaji malighafi nchini hususan sekta za kilimo, mifugo na uvuvi. Sekta hii inajenga msingi muhimu katika uongezaji wa tija na thamani ya malighafi mbalimbali zinazozalishwa nchini na imekuwa nguzo katika kuelekea katika kujenga uchumi imara unaoendeshwa na viwanda na hivyo kuweza kufikiwa kwa malengo ya Dira 2050.

Utekelezaji wa afua umechangia: idadi ya viwanda nchini ilifikia 128,032 Desemba 2024, ukuaji wa sekta ya viwanda ulikuwa asilimia 4.8 Desemba 2024; mchango katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 8.5 Desemba 2024; mauzo nje katika soko la Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) yalikuwa dola za Marekani milioni 1,163.8 Desemba 2024; na mauzo katika soko la Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) yalifikia dola za Marekani milioni 2,968 Desemba 2024.

Mafanikio yaliyopatikana kutokana utekelezaji wa afua: Kuongeza kwa uzalishaji wa bidhaa za viwandani; kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa nje hivyo kuchangia kuongezeka kwa fedha za kigeni; kuongezeka kwa nafasi za ajira katika sekta ya viwanda; na kuongezeka kwa masoko kwa bidhaa zinazozalishwa nchini ikiwemo bidhaa za kilimo.

Utekelezaji wa afua za Sekta ya uzalishaji wa bidhaa viwandani unaonesha, Mazingira wezeshi ya uwekezaji ni nyenzo muhimu. Kukamilika na kuanza utekelezaji wa miradi ya kielelezo na miradi ya kimkakati kutaongeza kasi ya ukuaji wa sekta kwa kutoa ajira, kuongeza upatikanaji wa fedha za kigeni na kuongeza uzalishaji bidhaa viwandani. Aidha, matarajio ya mwelekeo wa sekta kwa miaka mitano ijayo ni: kupanua na kuimarisha Masoko ya Kikanda na Kimataifa; kutekeleza mpango maalum wa kukuza viwanda nchini wa Dkt. Samia; kufanya Mageuzi ya Dijitali katika Viwanda na Biashara; kurasimisha shughuli za wajasiriamali wadogo na wa kati; na kuendelea kuweka mazingira wezeshi ya ujenzi wa viwanda na biashara nchini.

**Kielelezo Na. 3.13: Mchango wa Sekta ya Viwanda katika Pato la Taifa na Ajira zote**




***Chanzo:*** Wizara ya Viwanda na Biashara

**Kielelezo Na. 3.14: Mchango na Ukuaji wa Sekta ya Uzalishaji Viwandani kwa teknolojia ya juu na kati katika mauzo yote ya nje**




***Chanzo:*** Wizara ya Viwanda na Biashara

### 3.3.9 Sekta ya Madini

Sekta ya madini ni miongoni mwa sekta zinazokua kwa kasi na zenye mchango mkubwa katika ukuaji wa uchumi nchini. Hali hiyo imechangiwa kwa kiasi kikubwa na utekelezaji wa mikakati ilivyoainishwa katika Mpango wa mwaka 2025/26. Mikakati hiyo imeimarisha usimamizi na udhibiti wa rasilimali za madini kwenye mnyororo wa kuongeza thamani; kuwezesha wachimbaji wadogo na wa kati; kuimarisha taasisi za utafiti wa madini; kuhamasisha uongezaji thamani ndani ya nchi; na kuwezesha

uchimbaji wa madini muhimu na ya kimkakati. Katika utekelezaji wa mikakati yote hii, Sekta binafsi inaendelea kupewa msukumo wa kipekee kama kiungo muhimu katika kufikia malengo hayo.

Utekelezaji wa afua umechangia ukuaji halisi wa sekta ya madini ulikuwa asilimia 8.3 mwaka 2024; mchango wa sekta hii kwenye Pato la Taifa ulifikia asilimia 10.1 mwaka 2024; Mchango katika mapato yote ya fedha za nje yatokanayo na mauzo ya bidhaa nje ulifikia asilimia 57.1 mwaka 2024; na jumla ya mapato ya fedha za nje kutokana na mauzo ya dhahabu yalikuwa dola za Marekani milioni 4,119.9 mwaka 2024.

Mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa afua ni pamoja na: kuongezeka kwa ufanisi  na kusababisha baadhi ya viashiria kuvuka malengo kwa kufikiwa kabla ya muda uliopangwa kukamilika;  kuongeza mapato ya Serikali, hatua inayowezesha utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo na kuboresha huduma za kijamii kwa wananchi; kuongezeka kwa ajira, jambo linalotokana na wingi wa wachimbaji wadogo, wa kati na wakubwa waliojitokeza kushiriki katika shughuli za uchimbaji madini; viwanda vya kusafisha na kuchenjua madini ndani ya nchi, hatua inayosaidia uongezaji thamani wa madini.

Utekelezaji wa afua za Sekta ya madini unaonesha kuwepo kwa ushirikiano kati ya Serikali na sekta binafsi, utekelezaji wa Sera kuhusu "Ushirikishwaji wa Watanzania katika shughuli za madini (Local Content)" na "Wajibu wa Kampuni kwa Jamii (CSR)" pamoja na Sera ya Madini ya Mwaka 2009 ni nguzo muhimu za ukuaji endelevu wa sekta hii. Kufikia asilimia 10.1 mwaka 2024 ya mchango wa sekta katika Pato la Taifa mwaka imethibitisha ufanisi mkubwa uliotokana na mageuzi yaliyofanyika katika Sekta ya Madini.

Matarajio ya mwenendo wa Sekta ya Madini ni kuongeza mapato na mchango wake kwenye Pato la Taifa; kuendelea kudhibiti utoroshaji na biashara haramu ya madini kwa kuimarisha masoko na vituo vya ununuzi; uanzishaji wa migodi mipya ya madini muhimu na madini mkakati ili kuongeza uzalishaji wake; uongezaji thamani madini, sekta itavutia uwekezaji kwenye ujenzi wa *smelters* na *refineries* ili kupunguza mauzo ya madini ghafi nje ya nchi;  kuendeleza minada na maonesho ya madini ya vito ikiwa ni pamoja na kufanya tafiti za kina za madini kutoka asilimia 16 hadi kufikia angalau asilimia 50 ifikapo 2030; kuvutia wawekezaji; kuwarasimisha na kuwapatia maeneo yenye taarifa za jiolojia, leseni na mafunzo ili kuongeza tija na kupunguza uchimbaji holela.

**Kielelezo Na. 3.15: Mchango na Ukuaji wa Sekta ya Madini katika kipindi cha Mwaka 2019/20 hadi mwaka 2025/26**




***Chanzo:*** Wizara ya Madini

### 3.3.10 Sekta ya Mazingira na Maliasili

Sekta ya Mazingira na Maliasili Asilia imeendelea kutekeleza afua za Mpango wa mwaka 2025/26 ikiwemo: kuhamasisha matumizi ya nishati jadidifu; kuimarisha usimamizi wa tathmini ya athari kwa mazingira na jamii; kuimarisha na kuhamasisha matumizi endelevu ya maliasili asilia kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii; kupunguza uchafuzi wa mazingira pamoja na athari zake; na kuimarisha uwezo wa taifa kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Afua nyingine ni pamoja na: kuboresha miundombinu ya taasisi za mafunzo ya misitu na nyuki; kuongeza mchango wa sekta ndogo ya ufugaji nyuki kwenye uchumi; kutekeleza mkakati wa kitaifa wa kupambana na ujangili na usafirishaji haramu wa wanyamapori; na kuendeleza mikakati ya kupambana na ujangili, biashara haramu, uvunaji haramu wa rasilimali za wanyamapori, misitu,nyuki, na malikale nchini. Lengo ni kuimarisha uhifadhi na usimamizi wa mazingira, uhimilivu wa jamii dhidi ya athari za mabadiliko ya tabianchi na matumizi endelevu ya rasilimali asilia.

Utekelezaji wa afua hizo umechangia: idadi ya miti iliyopandwa na kustawi ilikuwa miti 800,660,000 kwa Desemba 2025 kati ya miti hiyo miti 658,943,180 imestawi sawa na asilimia 82.3; idadi ya taasisi zinazotumia nishati safi ya kupikia kwa kulisha watu zaidi ya 100 kwa siku zilifikia 1,136 mwaka 2024; takribani tani 235.62 za taka hatarishi zilisafirishwa nje ya nchi; takribani tani 150,000 za taka za chupa za plastiki zilikusanywa, taka za chupa za plastiki tani 75,000 za taka hizo zilirejelezwa; na kujengwa kwa vituo vya kuchakata na kurejeresha taka ozo katika majiji sita ya Dar es Salaam, Mwanza, Arusha, Tanga, Mbeya na Dodoma ili kupunguza uchafuzi wa mazingira.

Mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa afua ni pamoja na: kuongezeka kwa uelewa na ushiriki wa jamii katika masuala ya hifadhi ya mazingira ambapo zaidi

ya makundi 2,000 ya jamii yanashiriki kwenye upandaji miti; kupungua kwa uharibifu wa ardhi, bionuwai, na kuenea kwa hali ya jangwa kutokana na jitihada za uhifadhi wa misitu na upandaji miti; kupungua kwa athari za kiafya na mazingira kutokana na ongezeko la matumizi ya nishati safi ya kupikia hususani kwa taasisi zinazolisha watu zaidi ya 100 kwa siku na kupelekea kupunguza utegemezi wa kuni na mkaa; na kuongezeka kwa kipato kwa jamii na mapato ya Serikali kupitia utekelezaji wa miradi ya biashara ya kaboni ambapo jumla ya shilingi bilioni 48 zimepatikana mwaka 2024/25.

**Kielelezo Na. 3.16: Miradi Mikubwa inayokidhi Uchambuzi wa Athari kwa Mazingira na Kanuni za Ukaguzi kwa kipindi cha mwaka 2019/20 hadi mwaka 2024/25**




***Chanzo:*** Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira

Utekelezaji wa afua za mazingira na Maliasili Asilia umebainisha kuhamasisha, kusimamia, na kufuatilia utekelezaji wa programu, kuhakikisha azma ya kitaifa ya upandaji miti na hifadhi ya mazingira; kuwekeza katika uhamasishaji wamatumizi ya nishati safi ya kupikia zinazolisha watu zaidi ya 100 kwa siku, ili kupunguza utegemezi wa kuni na mkaa; kuwekeza katika utekelezaji wa miradi na programmu za biashara ya kaboni ili kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi; kutekeleza programu za kurejesha ardhi, misitu, ardhioevu na nyanda za malisho zilizoharibiwa ili kuimarisha mifumo ikolojia na uhifadhi wa bionuwai; kuwekeza katika usimamizi na udhibiti wa taka kwa kushirikiana Sekta binafsi; kuendelea kupanda miti, kulinda vyanzo vya maji na kuhamasisha matumizi endelevu ya misitu; na kuimarisha ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa katika juhudi za kuhifadhi mazingira.

### 3.3.11 Sekta ya Utalii

Sekta ya utalii ni sekta inayotegemea uwepo wa vivutio endelevu vya watalii ikijumuisha misitu yenye eneo la ukubwa takribani hekta milioni 48.1 Hifadhi za Taifa 21 na mapori ya akiba 29, mapori tengefu 23, hifadhi za jamii (WMA) 40 na misitu ya asili 23. Aidha, Mpango umeainisha utekelezaji wa afua ya sekta hii kuwa ni: kutangaza utalii ndani na nje ya nchi; kuibua na kuendeleza mazao ya utalii ya kimkakati; kuboresha miundombinu ya utalii na uhifadhi; na kuimarisha matumizi bora

ya teknolojia za kisasa katika usimamizi wa uhifadhi.

Utekelezaji wa afua zilizowekwa umechangia: idadi ya watalii wa kimataifa ilikuwa 2,294,495 mwaka 2024 na idadi ya watalii wa ndani ilikuwa 3,610,960 mwaka 2024, hivyo kufanya jumla ya watalii wa kimataifa na wa ndani kuwa 5,905,455 mwaka 2024 ikiwa ni zaidi ya lengo la kufikia watalii milioni tano (5) mwaka 2025/26; mapato yatokanayo na watalii wa kimataifa dola za Marekani bilioni 3.9 mwaka 2024. Kwa upande wa utalii wa ndani, mapato yalikuwa shilingi bilioni 209.8 mwaka 2024.

Mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa afua ni pamoja na: Tanzania kuwa kinara Afrika kwa ongezeko kubwa la watalii mwaka 2024; ongezeko la ajira kwa wananchi kutokana na huduma za utalii; kuongezeka kwa idadi ya wanyama waliohatarini kupotea na kuimarika kwa ulinzi na usimamizi wa rasilimali za wanyama pori; na kuimarika kwa biashara ya mazao na misitu na nyuki.

Utekelezaji wa afua za sekta ya utalii umebainisha kuwa kuna ongezeko la kampeni za kuhamasisha utalii wa ndani; ongezeko la bajeti na juhudi za kudhibiti athari za mabadiliko ya tabianchi; ongezeko la ushiriki wa Jamii katika masuala ya uhifadhi; na kuimarika kwa mifumo ya M&E kwa takwimu na taarifa za muda halisi.

Aidha, matarajio ya mwenendo wa sekta ni kuendelea kubuni vyanzo vya kuongeza mapato; kuimarisha mifumo ya kielektroniki ya kukusanya mapato ma utalii wa kidijitali; kuendelea kupanda miti; kulinda vyanzo vya maji na kuhamasisha matumizi endelevu ya misitu; kuimarisha ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa katika juhudi za kuhifadhi mazingira; kukabiliana na changamoto za wanyamapori wakali na waharibifu kwa kutumia vifaa vya kisasa; kuboresha miundombinu (barabara, viwanja vya Ndege, Mawasiliano n.k); na kubuni na kuendeleza mazao mapya ya utalii ya kimkakati ikiwemo utalii wa fukwe na malikale.

**Kielelezo Na. 3.17: Mwenendo na Ulinganifu wa Idadi ya Watalii kwa kipindi cha mwaka 2019/20 hadi mwaka 2024/25**




***Chanzo:*** Wizara ya Maliasili na Utalii

**Kielelezo Na. 3.18: Mchango wa Sekta ya Utalii Katika Pato la Taifa na Mchango Wake Katika Mapato ya Fedha za Kigeni Katika Kipindi cha Mwaka 2019/20 hadi 2025/26**




***Chanzo:*** Wizara ya Maliasili na Utalii

### 3.3.12 Sekta ya Habari, Utamaduni, Sanaa, na Michezo

Sekta ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo imetekeleza afua zilizoainishwa katika Mpango wa mwaka 2025/26. Afua hizo ni pamoja na: kukuza uwekezaji katika sekta ya ubunifu; kuimarisha ulinzi wa kazi za sanaa; kudumisha utamaduni, mila na maadili kwa lengo la kurejesha, kuendeleza na kuhifadhi kwa vizazi vya sasa na vya baadaye; kutambua na kuirejesha historia ya harakati za ukombozi barani Afrika; kukuza na kuendeleza lugha ya Kiswahili kikanda na kimataifa; kujenga viwanja vya mpira vya kisasa, maonyesho ya sanaa na maonesho ya michezo na sanaa za kimataifa; na kuhabarisha, kuelimisha, kuburudisha na kuhakikisha wananchi wanapata taarifa muhimu.

Utekelezaji wa afua umechangia: idadi ya miundombinu ya michezo ilikuwa 174 mwaka 2024/25; idadi ya wasanii waliosajiliwa katika tasnia ya ubunifu ilikuwa 7,310 mwaka 2024/25; na idadi ya wataalamu katika tasnia ya ubunifu waliopata mafunzo ilikuwa wataalamu 11,500 mwaka 2024/25.

Mafanikio yaliyopatikana kutokana utekelezaji wa afua ni pamoja na: kuongezeka kwa fursa za ajira kwa vijana; kuongezeka kwa pato la taifa; kuimarika kwa ushirikiano wa kimataifa kupitia lugha ya kiswahili pamoja na kazi za sanaa na michezo; kutoa mikopo na mafunzo kwa wasanii na wadau wa sanaa; kuongezeka kwa ushindani katika michezo na kazi za sanaa; na kuimarika kwa upatikanaji wa habari kwa umma.

Utekelezaji wa afua za Sekta ya utamaduni, Sanaa na michezo umebainisha kuwa sekta hii licha ya kuwa sekta ya burudani imeendelea kuwa na nguvu ya kuendeleza uchumi, kuongeza pato la taifa na ajira kwa vijana hivyo ni muhimu iendelee kutambulika kama sehemu ya maendeleo ya kiuchumi. Aidha, matarajio ya

mwenendo wa sekta ni: kuendelea kuwekeza katika sekta za michezo kwa kuendeleza miundombinu ya michezo, kukuza vipaji kwa kujenga studio za kisasa na shule za michezo, na kuhakikisha shughuli za michezo na sanaa zinapatikana ngazi ya mikoa na halmashauri; kuendeleza lugha ya Kiswahili ili kiweze kutumika kikanda na kimataifa na kuwa chombo cha utambulisho wa Taifa na utamaduni; na kuboresha miundombinu ya Habari na mawasiliano kwa umma kama sehemu muhimu ya kuboresha ufikikaji wa Habari na utangazaji wa shughuli za Serikali kwa umma.

### 3.3.13 Sekta ya Kukuza Uwekezaji na Biashara

Utekelezaji wa afua umechangia: idadi ya miradi ya uwekezaji iliyosajiliwa ilifikia 3,363 mwaka 2024/25; thamani ya miradi ya uwekezaji iliyosajiliwa ilifikia dola za Marekani milioni 38,297.49 mwaka 2024/25; ardhi ya uwekezaji iliyotengwa ekari 454,035.90 mwaka 2024/25.

Mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa afua husika zimechangia: kuongezeka kwa ushindani katika soko la ndani na nje; kuongeza ushiriki wa sekta binfasi katika shughuli za uzalishaji na huduma; kuongezeka kwa ajira katika sekta ya biashara; na kuongezeka kwa mapato ya Serikali kupitia kodi na tozo mbalimbali zitokanazo na shughuli za kibiashara na uwekezaji.

### 3.3.14 Uwekezaji wa Umma na Sekta Binafsi

#### i. Ubia wa Sekta ya Umma na Sekta Binafsi

Katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango wa mwaka 2025/26, Serikali imeendelea kutekeleza Programu ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (Public-Private Partnership – PPP). Utekelezaji wa Programu ya PPP ni njia mbadala ya kugharamia miradi ya maendeleo kwenye sekta zote za kiuchumi kwa lengo la kuimarisha ushiriki wa sekta binafsi katika kuongeza wigo wa utoaji wa huduma za umma na ujenzi wa miundombinu ya kiuchumi. Aidha, hadi Februari 2026, Serikali imesajili miradi ya PPP yenye jumla ya shilingi trilioni 6.9 sawa na asilimia 32 ya lengo la shilingi trilioni 21.3.

Shughuli zilizotekelezwa katika kufikia malengo ya mpango ni pamoja na: kuanzisha Kituo cha Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP Centre) kwa ajili ya kuratibu na kuhamasisha utekelezaji wa miradi ya PPP kwenye sekta zote; kutoa mafunzo ya weledi kwa Wataalam Elekezi katika masuala ya PPP kwenye Mamlaka za Serikali na Taasisi za Elimu ya Juu; na kufanya uchambuzi wa miradi ya PPP katika hatua zote za utekelezaji wake tangu uibuaji, maandalizi, ununuzi, utekelezaji na usimamizi wa mikataba ya miradi hiyo.

Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na: kuongezeka kwa hamasa ya kutekeleza miradi kwa utaratibu wa PPP miongoni mwa Taasisi za Umma na Mamlaka za Serikali za Mitaa; ambapo idadi ya miradi kwenye orodha ya miradi iliyokidhi vigezo vya kutekelezwa kwa utaratibu wa PPP ambapo miradi iliyofikia hatua ya utekelezaji imeongezeka kutoka miradi mitano (5) mwaka 2024/2025 hadi miradi saba (7) Desemba 2025; miradi mitatu (3) iko hatua ya majadiliano ya mkataba na Wabia; minne (4) iko hatua ya ununuzi wa Wabia; miradi 22 iko hatua ya upembuzi yakinifu; 33 iko hatua ya upembuzi yakinifu wa Awali na 32 iko hatua ya andiko dhana.

Aidha, Kituo cha Ubia kimeendelea na jitihada za kuzijengea uwezo wa kutekeleza miradi kwa utaratibu wa PPP Mamlaka za Serikali za Mitaa, ambapo miradi 410 inayokidhi vigezo vya kutekelezwa kwa utaratibu wa PPP imeibuliwa kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa kwenye mikoa yote 26 ya Tanzania Bara. Matokeo chanya ya utekelezaji wa Programu ya PPP ni pamoja na kuongeza wigo wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kuishirikisha sekta binafsi, kuongeza mapato ya Serikali, kuongeza fursa za ajira, na kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma za umma.

**Jedwali 3.1 Orodha ya Miradi ya PPP katika Hatua za Utekelezaji**

| Na. | Jina la Mradi | Taasisi inayotekeleza | Mratibu | Thamani ya mradi (TZS Bilioni) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Ujenzi wa Jengo la Kisasa la Biashara la Kariakoo One Stop Commercial Complex. | Shirika la Maendeleo la Dar es Salaam (DDC) | OWM-TAMISEMI | 37 |
| 2 | Uendeshaji wa Huduma ya Mabasi Yaendayo Haraka - Dar Rapid Transit, Awamu ya Kwanza | Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART) | OWM - TAMISEMI | 195.45 |
| 3 | Uendeshaji wa Huduma ya Mabasi Yaendayo Haraka - Dar Rapid Transit, Awamu ya Pili, Trunk Road | Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART) | OWM - TAMISEMI | 177.135 |
| 4 | Kuboresha Uendeshaji wa Bandari ya Dar es Salaam kwa Ubia na DPW (Operation and Maintenance Concession) | Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) | Wizara ya Uchukuzi | 2,700 |
| 5 | Kuboresha Uendeshaji wa Bandari ya Dar es Salaam kwaubia na ADANI Group (Operation and Maintenance Concession) | Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) | Wizara ya Uchukuzi | 256.5 |
| 6 | Ukarabati na Kuboresha Uendeshaji wa Reli ya TAZARA (Rehabilitation, Operation and Maintenance Concession) | TAZARA | Wizara ya Uchukuzi | 3,200 |
| 7 | Ujenzi wa Vituo vya Ukaguzi wa Lazima wa Vyombo vya Moto | Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Polisi (TPFCS) | Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi | 313 |

***Chanzo:*** Kituo cha Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi

### ii. Uwekezaji wa Mashirika ya Umma

Serikali kupitia taasisi na mashirika ya umma yanayosimamiwa na Ofisi ya Msajili wa Hazina imeendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo yenye lengo la kuboresha utoaji wa huduma, kuongeza ufanisi wa kiutendaji na kuimarisha uwezo wa kifedha wa taasisi hizo ili kupunguza utegemezi wa ruzuku kutoka Serikalini na kujiendesha kwa tija. Uwekezaji wa mtaji wa Serikali kupitia taasisi na mashirika ya umma 309 (ambapo 253 zinamilikiwa kwa asilimia 100 na Serikali na 56 zina umiliki wa hisa chache za Serikali) ulifikia TZS trilioni 90.6 mwaka 2024/25.

### 3.3.15 Sekta ya Mahusiano ya Kimataifa na Diplomasia ya Uchumi

Mpango wa mwaka 2025/26 ulilenga kuendelea kustawisha utekelezaji wa diplomasia ya siasa na uchumi kupitia ushirikiano wa uwili, kikanda na kimataifa; kuimarisha ushiriki wa Tanzania kwenye mikutano ya jumuiya za kikanda na mashirika ya kimataifa na kushiriki katika jitihada za upatikanaji wa amani, ulinzi na usalama kwa ajili ya maslahi ya Taifa na maendeleo jumuishi.

Utekelezaji wa afua umechangia: kuongezeka kwa uwakilishi wa Tanzania nje ikiwa ni pamoja na kufunguliwa kwa Ubalozi na Uwakilishi wa Kudumu wa Tanzania katika Umoja wa Mataifa Vienna, Austria na Ubalozi wa Tanzania Jarkata, Indonesia. Vilevile, kufunguliwa kwa konseli kuu mbili katika Jiji la Lubumbashi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Guangzhou, Jamhuri ya Watu wa China. Hadi Desemba 2025, Tanzania ilikuwa na jumla ya balozi 45 na konseli kuu tano nje.

Tanzania ilishiriki mikutano 42 ya Tume za Pamoja za Kudumu za Ushirikiano (JPC), Tume za Pamoja za Ushirikiano (JCC) na mashauriano ya kisiasa kwa ajili ya kutetea na kuendeleza maslahi ya Taifa kwenye ushirkiano wa mahusiano wa pande mbili kwa kipindi cha hadi Desemba 2025. Vilevile, ziara 90 zilifanyika za Viongozi Wakuu wa Kitaifa nje na kufanikisha kusainiwa kwa mikataba na hati za makubaliano 161 baina ya Tanzania na nchi mbalimbali. Kwa upande mwingine, ziara 31 zilifanyika za Wakuu wa Nchi na Serikali wa mataifa mengine na wakuu wa mashirika ya kikanda na kimataifa nchini.

Mafanikio ya yaliyopatikana ni pamoja na: Kupata fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika sekta mbalimbali, vibali vya safari za moja kwa moja za kampuni za ndege, kufanya makongamno ya kushawishi Watanzania wanaoishi nje kuchangia maendeleo nchini na kuwezesha Watanzania kupata nafasi za uongozi katika taasisi za kikanda na kimataifa. Vilevile, nchi mbalimbali na jumuiya za kikanda zimekubali ushawishi wa Tanzania kuhusu umuhimu wa kutumia Kiswahili ambapo Uganda, Kenya, Rwanda na Burundi zimeingiza lugha hiyo kwenye mitaala ya shule za msingi na sekondari na nchi za Marekani, Canada, Ujerumani, China, Urusi na Uingereza zimefanya hivyo kwenye mitaala ya vyuo vikuu. Aidha, Umoja wa Afrika, Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika na Jumuiya ya Afrika Mashariki zinatumia Kiswahili kama lugha rasmi ya kazi.

Mafanikio mengine yaliyopatikana katika utekelezaji wa afua hizo ni pamoja na Tanzania kuteuliwa kuwa Mjumbe wa Baraza la Amani na Usalama la Umoja wa Afrika kwa vipindi viwili tofauti, mwaka 2022 na 2024; kushiriki katika operesheni za kulinda amani kikanda na kimataifa. Aidha, Tanzania ilifanikiwa pia kuwa Mwenyeji wa Kituo cha Kupambana na Ugaidi cha Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika chenye Makao Makuu jijini Dar es Salaam.

**Kielelezo Na. 3.19: Mwenendo wa Utiaji Saini Mikataba na Hati za Makubaliano baina ya Tanzania na Nchi Mbalimbali**




***Chanzo:*** Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki

### 3.3.16 Sekta ya Elimu na Maendeleo ya Ujuzi

Serikali katika utekelezaji wa mpango wa 2025/26 ililenga kutekeleza afua zifuatazo: Kuboresha na kuwianisha mazingira jumuishi ya kujifunzia na kufundishia katika ngazi zote za elimu; kuhuisha na kuandaa mitaala kulingana na mahitaji ya soko la ajira; kuimarisha mifumo ya ithibati na uthibiti ubora wa elimu; kuboresha umahiri wa walimu katika masomo ya hisabati na sayansi; kuongeza upatikanaji wa mikopo ya wanafunzi katika elimu ya juu hasa kwa wanafunzi wa masomo ya Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati, kada maalumu na adimu; kujumuisha matumizi ya TEHAMA katika kufundisha na kujifunza katika ngazi zote za elimu; na kukuza na kuwezesha matumizi ya TEHAMA katika kufundisha na kujifunza katika ngazi zote za elimu.

Utekelezaji wa afua hizi umechangia kujenga na kukarabati miundombinu ya Elimu Msingi na Sekondari kwa kipindi cha kutoka mwaka 2024/25 hadi Desemba 2025: ongezeko la idadi ya vyumba vya madarasa kutoka 191,708 hadi 254,393, sawa na asilimia 32.69; idadi ya shule za msingi kutoka shule 16,406 hadi 17,986 sawa na ongezeko la asilimia 9.63; idadi ya shule za sekondari kutoka shule 3,863 hadi 4,894 sawa na asilimia 26.68; ongezeko la idadi ya matundu ya vyoo kutoka 206,670 hadi 278,911 (shule za msingi) sawa na asilimia 34.95; na kutoka matundu 92,724 hadi 120,970 (shule za sekondari) sawa na asilimia 30.43; idadi ya nyumba za walimu kutoka 58,637 hadi 60,429 sawa na ongezeko la asilimia 3.05; idadi ya maktaba kutoka 1,537 hadi 2,665 sawa na ongezeko la asilimia 73.38; idadi ya maabara kutoka 8,072 hadi 8,710 sawa na asilimia 7.90; idadi ya mabweni kutoka 2,245 hadi 3,245 sawa na asilimia 44.54; na idadi ya mabwalo kutoka 871 hadi 1,004 sawa na asilimia 15.26; ajira za walimu 68,279 (Msingi 36,226 na Sekondari 32,053) zimeimarisha uwiano wa mwalimu kwa mwanafunzi; na Ruzuku ya Elimu Bila Ada ilikuwa shilingi bilioni 484.27 mwaka 2024/25.

Aidha, kwa upande wa elimu ya msingi mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na: ufaulu wa darasa la saba umefikia asilimia 81.8 mwaka 2025, uwiano wa idadi ya wanafunzi

kwa mwalimu mwenye sifa uliboreshwa na kufikia 1:55 Desemba 2025, uwiano wa idadi ya wanafunzi kwa darasa kutoka 1:75 mwaka 2020 hadi 1:60, uwiano wa idadi ya wanafunzi wa kike kwa tundu la choo kufikia1:39 Desemba 2025.

Vilevile, katika Elimu ya Sekondari ya chini (Kidato cha I-IV) mafaniko yaliyopatikana ni pamoja na: ufaulu wa kidato cha Nne ulikuwa asilimia 92.37 Desemba 2025; na kiwango cha uandikishaji wa jumla (Gross enrolment rate) ulikuwa asilimia 53.1 Desemba 2025. Aidha, Kiwango cha uandikishaji jumla (% ya wanaostahili) Sekondari ya juu (V-VI) ulikuwa asilimia 9.8 Desemba 2025 ambapo uandikishaji wa wasichana kwa rika lengwa ulikuwa asilimia 3.9. Kuimarika kwa matokeo ya mitihani ya kitaifa Kidato cha sita ufaulu umefikia asilimia 99.62 Desemba 2025.

Aidha, idadi ya vyuo vya elimu ilifikia 512 Desemba 2025, idadi ya vyuo vya mafunzo ya ufundi stadi (VET) vimefikia 905 Desemba 2025. Kwa upande wa elimu ya Juu, Bajeti ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu imefikia shilingi bilioni 916.7 mwaka 2025/26 ambapo kati ya fedha hizi, ufadhili wenye thamani ya Shilingi bilioni 7.29 umetolewa kwa wanafunzi 7,534 wenye ufaulu uliojipambanua katika fani za Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati kupitia SAMIA Skolashipu.

Mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa afua ni pamoja na: kiwango cha uandikishaji rika lengwa (Net enrolment rate-NER) katika elimu ya awali kufikia asilimia 51.2 mwaka mwaka 2024; kiwango cha uandikishaji jumla (Gross enrolment rate - GER) elimu ya awali kufikia asilimia 84.5 Desemba 2025; na uwiano wa idadi ya wanafunzi kwa mwalimu mwenye sifa kufikia 1:151 Desemba mwaka 2025 katika elimu ya awali.

Kwa upande wa elimu ya msingi mafanikio yalijumuisha: ufaulu wa darasa la saba ulikuwa asilimia 80.87 Desemba 2025, uwiano wa idadi ya wanafunzi kwa mwalimu mwenye sifa umefikia 1:56 Desemba 2025, uwiano wa idadi ya wanafunzi kwa darasa umefikia 1:63 Desemba mwaka 2025, uwiano wa idadi ya wanafunzi wa kike kwa tundu la choo kufikia1:43 Desemba 2025.

Aidha, katika Elimu ya Sekondari ya chini (Kidato cha I-IV) mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na: ufaulu wa kidato cha Nne umefikia asilimia 92.37 Desemba 2025; na kiwango cha uandikishaji wa jumla (Gross enrolment rate) umefikia asilimia 51.7 Desemba 2025. Aidha, Kiwango cha uandikishaji jumla (% ya wanaostahili) Sekondari ya juu (V-VI) kimefikia asilimia 9.1 Desemba 2025 ambapo uandikishaji wa wasichana kwa rika lengwa umefikia asilimia 5.2 Desemba 2025. Kuimarika kwa matokeo ya mitihani ya kitaifa Kidato cha sita ambapo ufaulu umefikia asilimia 99.99 Desemba 2025.

Katika vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi (TVET) mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na: kiwango cha udahili jumla (%) kimefikia asilimia 10.4 Desemba 2025, idadi ya wahitimu imefikia wahitimu 129,766 Desemba 2025. Aidha, idadi ya wanafunzi katika vyuo vya mafunzo ya Ufundi Stadi - VET imefikia wanafunzi 58,912 (wanawake 12,022 na wanaume 46,890) ambapo kati yao wanafunzi wa kozi

za muda mrefu 24,670 (wanawake 8,450 na wanaume 16,220) na wa kozi za muda mfupi ni 34,242 (wanawake 3,572 na wanaume 30,670).

Kwa upande wa elimu ya Juu, mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na: udahili katika Vyuo vya Elimu ya Juu umefikia 361,257 mwaka 2024/25, idadi ya wanafunzi walionufaika na mikopo ya elimu ya juu imefikia 248,331 mwaka 2024/25; na idadi ya wahitimu wa vyuo vikuu imefikia 62,570 Desemba 2025.

Aidha, idadi ya vyuo vya elimu ilifikia 512 Desemba 2025, idadi ya vyuo vya mafunzo ya ufundi stadi (VET) vimefikia 905 Desemba 2025. Kwa upande wa elimu ya Juu, Bajeti ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya imefikia shilingi bilioni 916.7 mwaka 2025/26 ambapo kati ya fedha hizi, ufadhili wenye thamani ya Shilingi bilioni 7.29 umetolewa kwa wanafunzi 7,534 wenye ufaulu uliojipambanua katika fani za Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati kupitia SAMIA Skolashipu.

Mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa afua ni pamoja na: kuongezeka kwa kiwango cha uandikishaji rika lengwa (Net enrolment rate-NER) katika elimu ya awali kufikia asilimia 51.2 mwaka mwaka 2024; kiwango cha uandikishaji jumla (Gross enrolment rate - GER) elimu ya awali kufikia asilimia 84.5 Desemba 2025; na kupungua kwa uwiano wa idadi ya wanafunzi kwa mwalimu mwenye sifa kufikia 1:151 Desemba mwaka 2025 katika elimu ya awali.

Aidha, kwa upande wa elimu ya msingi, ufaulu wa darasa la saba ulikuwa asilimia 80.87 Desemba 2025, uwiano wa idadi ya wanafunzi kwa mwalimu mwenye sifa umefikia 1:56 Desemba 2025, uwiano wa idadi ya wanafunzi kwa darasa umefikia 1:63 Desemba mwaka 2025, uwiano wa idadi ya wanafunzi wa kike kwa tundu la choo kufikia1:43 Desemba 2025.

Vilevile, katika Elimu ya Sekondari ya chini (Kidato cha I-IV), ufaulu wa kidato cha Nne umefikia asilimia 92.37 Desemba 2024; na kiwango cha uandikishaji wa jumla (Gross enrolment rate) umefikia asilimia 51.7 Desemba 2024. Aidha, Kiwango cha uandikishaji jumla (% ya wanaostahili) Sekondari ya juu (V-VI) kimefikia asilimia 9.1 Desemba 2024 ambapo uandikishaji wa wasichana kwa rika lengwa umefikia asilimia 5.2 Desemba 2024. Kuimarika kwa matokeo ya mitihani ya kitaifa Kidato cha sita ambapo ufaulu umefikia asilimia 99.99 Desemba 2024.

Katika vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi (TVET), Kiwango cha udahili jumla (%) kimefikia asilimia 10.4 Desemba 2025, idadi ya wahitimu imefikia wahitimu 129,766 Desemba 2025. Aidha, idadi ya wanafunzi katika vyuo vya mafunzo ya Ufundi Stadi - VET imefikia wanafunzi 58,912 (wanawake 12,022 na wanaume 46,890) ambapo kati yao wanafunzi wa kozi za muda mrefu 24,670 (wanawake 8,450 na wanaume 16,220) na wa kozi za muda mfupi ni 34,242 (wanawake 3,572 na wanaume 30,670).

Aidha, kwa upande wa elimu ya Juu, mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na: udahili katika Vyuo vya Elimu ya Juu umefikia wanafunzi 361,257 mwaka 2024/25, idadi ya

wanafunzi walionufaika na mikopo ya elimu ya juu imefikia 248,331 mwaka 2024/25; na idadi ya wahitimu wa vyuo vikuu imefikia 62,570 Desemba 2025.

Vilevile, katika utekelezaji wa Ahadi za Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ndani ya siku 100 baada ya kuchaguliwa, Sekta ya Elimu ilitekeleza hatua mahsusi za kimkakati zikihusisha ukamilishaji na uzinduzi wa Mpango Mkakati wa Kisayansi wa Kujenga Umahiri wa Kusoma, Kuandika na Kuhesabu wenye kauli mbiu ya "Mtoto Asome, Aandike na Kuhesabu bila Shida", uliolenga kuimarisha stadi za msingi katika elimu ya awali na msingi. Kukamilika kwa zoezi la usaili na kuajiri walimu wa Sayansi na Hisabati 7,000 kwa lengo la kupunguza uhaba wa walimu katika masomo hayo muhimu na kuboresha uwiano wa wanafunzi kwa mwalimu mwenye sifa.

Kuzinduliwa kwa mpango wa kuoanisha mafunzo na mahitaji ya soko la ajira kupitia vyuo vya ufundi stadi na vyuo vikuu, ili kuhakikisha mitaala na mafunzo yanayotolewa yanajibu mahitaji halisi ya sekta za uzalishaji na uchumi wa viwanda.

Utekelezaji wa afua za elimu umebainisha: kuongezeka kwa uandikishaji, udahili na ufaulu katika ngazi zote za elimu; kuimarika kwa ushiriki wa wasichana katika masomo ya STEM na vyuo vya ufundi; kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi wenye ulemavu wanaojiunga na elimu; pamoja na kuimarika kwa ushiriki wa sekta binafsi katika uwekezaji wa elimu.

Aidha, matarajio ya mwelekeo wa sekta ni kuendelea kuimarisha miundombinu katika ngazi zote za elimu, hususan katika vyuo vya ufundi na taasisi za mafunzo ya ufundi stadi, ili kuongeza uwezo wa kudahili wanafunzi wengi zaidi na kupanua fursa za elimu. Sambamba na hilo, sekta itaendelea kuimarisha upatikanaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia, hasa vifaa vya mafunzo ya amali na vitabu vya wanafunzi, kwa lengo la kufikia uwiano wa kitabu kimoja kwa mwanafunzi mmoja (1:1). Vilevile, juhudi zitaelekezwa katika kuimarisha matumizi ya TEHAMA na teknolojia za kidijitali katika ufundishaji na ujifunzaji katika ngazi zote za elimu nchini, pamoja na kuimarisha elimu maalum na jumuishi ili kuhakikisha wanafunzi wenye ulemavu wanapata fursa sawa ya kupata elimu bora na yenye ubora unaostahili.

Sekta itaendelea kutoa ruzuku ya ada katika elimu ya msingi na sekondari, pamoja na mikopo na ufadhili kwa wanafunzi, hususan wa jinsia ya kike, ili kuongeza ushiriki wao katika masomo ya Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati (STEM). Aidha, wanafunzi wenye ufaulu wa juu katika masomo ya sayansi katika matokeo ya Kidato cha Sita watawezeshwa kujiunga na vyuo bora vya nje ya nchi kusomea fani za Akili Unde (AI) na Sayansi ya Takwimu (Data Science) kupitia programu ya Samia Extended Scholarship (DS/AI+), pamoja na kuwezeshwa kusoma sayansi na teknolojia ya nyuklia katika ngazi ya shahada ya umahiri. Serikali itaendelea pia kuboresha mitaala katika ngazi za elimu ya ufundi, mafunzo ya ufundi stadi na elimu ya juu ili kuimarisha ujuzi wa wahitimu, kushirikiana na sekta binafsi kuongeza uwekezaji katika elimu, na kuimarisha ushiriki wa sekta ya umma na binafsi katika kukuza utafiti na ubunifu kwa ajili ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

**Kielelezo Na. 3.20: Mwenendo wa uandikishaji rika lengwa na uandikishaji jumla katika Elimu ya Awali kuanzia Mwaka 2021 hadi 2025**




***Chanzo:*** Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

**Kielelezo Na. 3.21: Mwenendo wa Kiwango cha uandikishaji jumla na uandikishaji rika lengwa kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2021 hadi 2025, Elimu ya Sekondari (Kidato cha I-IV)**




***Chanzo:*** Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

**Kielelezo Na. 3.22: Idadi ya Wanafunzi waliopata Mikopo ya Elimu ya Juu katika kipindi cha mwaka 2020/21 hadi mwaka 2024/25**




***Chanzo:*** Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

### 3.3.17 Sekta ya Afya

Serikali ililenga kuimarisha mifumo ya usimamizi, ubora wa huduma za afya, huduma za kinga na tiba ikiwemo upatikanaji wa chanjo, dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi. Afua zilizotekelezwa ni pamoja na: kujenga na kukarabati miundombinu ya kutolea huduma za afya katika ngazi zote; kuajiri na kuendeleza wataalam wa sekta ya afya katika ngazi mbalimbali za utoaji wa huduma za afya nchini; kuhamasisha na kuongeza wigo wa matumizi ya bima ya afya; kuimarisha huduma za tiba za dharura; na kuimarisha huduma za kibingwa na kibingwa bobezi.

Utekelezaji wa afua umechangia: idadi ya vifo vya watoto wachanga kwa kila vizazi hai 1000 imefikia vifo 24 mwaka 2025; na wastani wa umri wa kuishi umefikia miaka 68 Desemba 2025; idadi ya Hospitali imefikia 473 Desemba 2025; idadi ya Vituo vya Afya vya Serikali imefikia 1,351 Desemba 2025; idadi ya Zahanati za Serikali imefikia 8,649 Desemba 2025; idadi ya watumishi katika Sekta ya Afya imefikia 177,711 mwaka 2024/25.

Mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa afua ni pamoja na: kuongezeka kwa upatikanaji wa bidhaa za afya muhimu (382 tracers); huduma za afya kutolewa katika miundombinu bora; kupunguza muda wa mgonjwa kupata huduma; na kutolewa kwa huduma za kibingwa na ubingwa ubobezi. Aidha, Serikali imeendelea kuhamasisha uwekezaji wa viwanda vya dawa nchini na kufanikiwa kuongeza idadi ya Viwanda kutoka 11 hadi kufikia viwanda 12. Kutolea kwa chanjo ya Penta kwa jumla ya watoto 2,361,592 sawa na asilimia 95 ambayo hutumika kama kipimo kikuu cha utoaji wa chanjo nchini kwa watoto wa chini ya mwaka mmoja.

Utekelezaji wa afua za afya umebainisha kuwa uwekezaji mkubwa ambao Serikali imewekeza katika Sekta ya Afya katika kipindi cha mwaka 2024/25 katika maeneo mbalimbali ya utoaji wa huduma za afya nchini ikiwemo miundombinu, upatikanaji wa bidhaa za afya muhimu (Dawa, Vifaa, Vifaa tiba, Vitendanishi pamoja na chanjo), ajira

(Rasiliamali watu) na mafunzo kwa watumishi wa afya kumewezesha kuboreshwa kwa huduma za afya nchini ambapo matokeo yake yamejidhihirisha na kiashiria cha ongezeko la umri wa kuishi kufikia miaka 68. Aidha, matarajio ya mwenendo wa sekta ni kuongeza wigo wa upatikanaji wa huduma ya afya kwa wote kwa kutekeleza Sheria ya Bima ya Afya kwa wote ya mwaka 2023.

**3.3.18 Sekta ya Huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira**

Afua zifuatazo zimetekelezwa: ujenzi na uboreshaji wa miundombinu ya maji; kuimarisha upatikanaji wa huduma za usafi wa mazingira; na kuendesha kampeni za kuhamasisha matumizi bora ya maji na usafi wa mazingira.

Utekelezaji wa afua umechangia: idadi ya watu vijijini wanaopata maji ya bomba kama chanzo kikuu imefikia asilimia 85.2 Desemba 2025; kaya za vijijini zenye miundombinu iliyoboreshwa ya usafi wa mazingira imefikia asilimia 78.5 Desemba 2025; idadi ya watu katika makao makuu ya mikoa wanaopata maji ya bomba imefikia asilimia 92.5 Desemba 2025; na vyanzo vya maji vilivyowekwa mipaka na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali vimefikia vyanzo 80 Desemba 2025 kuwa maeneo tengefu kwa ajili ya ulinzi na uhifadhi.

Mafanikio yaliyopatikana kutokana utekelezaji wa afua ni pamoja na: kupungua kwa milipuko ya magonjwa yatokanayo na maji; kuongezeka kwa tija katika sekta za uzalishaji; na kupunguza muda wa wananchi kutafuta maji kwa ajili ya matumizi ya majumbani kutokana na vituo vya kuchotea maji kupatikana umbali wa wastani usiozidi mita 400. Aidha, katika siku 100 za awamu ya Pili ya Serikali ya Awamu ya Sita mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kukamilika kwa miradi 16 ya maji na wananchi zaidi ya 118,400 wamenufaika na upatikanaji wa huduma ya maji katika maeneo mbalimbali nchini; na kununua Dira 2,271 za malipo kabla na zinazoendelea kufungwa kwa wateja suala litakaloongeza tija kwa Mamlaka za maji na kupunguza malalamiko ya bili za maji za wateja.

Utekelezaji wa afua za sekta ya huduma ya maji na usafi wa mazingira umebainisha umuhimu wa Serikali kuendelea kutekeleza miradi ya maji na usafi wa mazingira kupitia ujenzi wa mabwawa yanayohakikisha upatikanaji wa maji wa uhakika. Aidha, matarajio ya mwenendo wa sekta ni kuandaa gridi ya Taifa ya maji ili kuongeza uhakika wa upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama nchini.

**3.3.19 Sekta ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi**

Afua zifuatazo zimetekelezwa: uwekezaji katika upangaji, upimaji na utoaji wa hatimiliki za ardhi; kuandaa mipango kabambe ya miji, visiwa na fukwe; kuimarisha uwekezaji katika ujenzi wa nyumba za gharama nafuu; kuboresha mfumo wa usimamizi wa taarifa za ardhi; kuwianisha mifumo ya usimamizi wa ardhi na mipango ya sekta nyingine; pamoja na kuhamasisha matumizi ya TEHAMA katika upimaji wa ardhi na utoaji wa hatimiliki.

Utekelezaji wa afua umechangia: viwanja na mashamba yaliyopimwa ulikuwa 3,544,338 Desemba, 2025 ambapo jumla ya Hatimiliki (CROs) 1,288,133 na Hati za

Hakimiliki za Kimila (CCROs) 1,296295 zimetolewa kutokana na kuimarika kwa mfumo wa ILMIS/e-Ardhi; uwiano wa vijiji vyenye mipango ya matumizi bora ya ardhi umefikia asilimia 38.97 Desemba, 2025; makazi yaliyopimwa na kurasimishwa yalikuwa 2,942,661 Desemba, 2025; leseni za makazi zilikuwa 29,478 Desemba, 2025; eneo la ardhi lililotengwa na kulindwa kwa matumizi ya umma limefikia ekari 875,360 Desemba, 2025; Mabaraza ya ardhi na nyumba ya wilaya yanayotoa huduma yamefikia 117 Desemba, 2025; na ujenzi wa nyumba za gharama nafuu kupitia Shirika la Nyumba la Taifa ulifikia nyumba 228 mwaka 2025.

**Kielelezo Na. 3.23: Ulinganifu wa Idadi ya Mali zilizorasimisha, Eneo la Ardhi lililotengwa na Idadi ya Viwanja vilivyotengwa**




***Chanzo:*** Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

**Kielelezo Na. 3.24: Mwenendo wa eneo la ardhi yenye makazi yasiyo rasmi, vijiji vyenye mipango ya matumizi bora ya ardhi na ardhi iliyopimwa katika kipindi cha mwaka 2019/20 hadi mwaka 2025/26**




***Chanzo:*** Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

Mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa afua ni pamoja na: kuongezeka kwa ardhi iliyopangwa na kupimwa kwa matumizi mbalimbali; kuongezeka kwa uwazi

na urahisi wa upatikanaji wa taarifa za ardhi; kupungua kwa makazi holela na kuwezesha urahisi wa ufikiwaji wa huduma za jamii na shughuli za uchumi; kuongezeka kwa makazi bora, salama, na ya gharama nafuu; kupungua kwa migogoro ya matumizi ya ardhi; na kuongezeka kwa uwekezaji na thamani ya ardhi nchini.

Utekelezaji wa afua za Sekta ya ardhi na Maendeleo ya Makazi umebainisha umuhimu wa: kuongeza kasi ya upangaji wa miji na vijiji, upimaji ardhi na kuboresha makazi; kuwa na ramani za msingi zitakazotumika kwa matumizi mbalimbali; kuboresha mifumo ya TEHAMA ya utunzaji wa taarifa za ardhi na umilikishaji katika Ofisi za Ardhi za Mikoa 26 pamoja na Halmashauri 184 nchini na kuimarisha vyombo vya utatuzi wa migogoro ya ardhi. Aidha, matarajio ya mwenendo wa sekta ni: kuwa na miji ya kisasa iliyopangwa na kupimwa, makazi bora na mipango ya matumizi ya ardhi inayokidhi mahitaji ya huduma za kijamii, kuwepo kwa urahisi wa upatikanaji na matumizi ya taarifa sahihi za ardhi, na kupungua kwa migogoro ya ardhi.

### 3.3.20 Sekta ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii

Katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango, sekta ya ustawi na maendeleo ya jamii ililenga: kuwawezesha wanawake kiuchumi kupitia mikopo yenye riba nafuu na majukwaa ya uwezeshaji wanawake kiuchumi; kuimarisha huduma za haki jinai kwa watoto na kuendelea kuwajengea uwezo watoa huduma walio kwenye mfumo wa haki jinai; Kupunguza uwepo wa mila na desturi kandamizi na zenye madhara; kuimarisha matunzo, ulinzi na usalama wa mtoto; na kupunguza matumizi yasiyo sahihi ya teknolojia ikiwemo mitandao yanayosababisha ongezeko la mmomonyoko wa maadili katika jami.

Utekelezaji wa afua umechangia: idadi ya vituo vya kulelea watoto wadogo mchana vilivyosajiliwa vilikuwa 4,723 Desemba, 2025; idadi ya wazee na wasiojiweza wanaopata huduma za bima ya afya bure ilikuwa 1,256,544 mwaka 2024/25; kuwatambua na kuwasajili wafanyabiashara wadogo 119,595 Desemba, 2025.

Mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa afua ni pamoja na: kuongezeka kwa muda kwa wanawake kujishughulisha na shughuli za uzalishaji mali; upatikanaji wa huduma za afya kwa wazee na wasiojiweza; na upatikanaji wa ajira na mitaji kwa wafanyabiashara wadogo ambapo wafanyabiashara 5,208 wamenufaika na mikopo.

Utekelezaji wa afua za ustawi na maendeleo ya jamii umebainisha kuwa idadi ya watoto wanaolelewa baada ya mapatano umeongezeka ikimaanisha watoto kupata huduma za malezi pindi migogoro ya kifamilia inapotokea. Aidha, matarajio ya mwenendo wa sekta ni kuendelea kuimarisha malezi katika ngazi ya familia ili kuwa na jamii inayozingatia misingi ya usawa; kuhamasisha wananchi kuwa kitovu cha maendeleo na kutokomeza mila na desturi hasi ili kuwa na jamii yenye maadili; Kutambua, kusajili na kuwezesha makundi maalum; pamoja na kusimamia mashirika yasiyo ya kiserikali ili kuwa na maendeleo endelevu kwa vizazi vya sasa na vijavyo.

### 3.3.21 Kuendeleza Ujuzi

Mpango ulilenga kuimarisha huduma za kinga ya jamii, kuongeza ushiriki wa vijana na watu wenye ulemavu katika shughuli za jamii na kiuchumi, kuhamasisha ukuaji wa fursa za ajira na kazi za staha kwa vijana na kukuza ujuzi wa nguvu kazi iliyopo kwenye soko la ajira. Sekta ya kazi, vijana, ajira na wenye ulemavu ililenga: kuhamasisha uzalishaji wa fursa za ajira na kazi za staha; kuratibu utekelezaji wa mpango wa kitaifa wa kuendeleza ujuzi kwa vijana walio nje ya mfumo rasmi wa elimu; kuongeza wigo wa huduma za kinga ya jamii katika sekta rasmi na isiyo rasmi; kukuza uwezeshaji wa kiuchumi kwa vijana kupitia mikopo rafiki na mafunzo ya ujasiriamali; na kukuza ujumuishaji na uwezeshaji wa kiuchumi kwa watu wenye ulemavu.

Utekelezaji wa afua umechangia: idadi ya ajira zilizozalishwa zilikuwa 981,000 mwaka 2024/25; wigo wa kinga ya jamii kufikia asilimia 26.9 mwaka 2024/25; watu waliopata mafunzo ya ujuzi ilifikia 157,867 mwaka 2024/25; kuanzishwa kwa mfuko wa kutoa ruzuku kwa vyama vya watu wenye ulemavu; kutoa mafunzo kwa vijana 94,779 kuhusu ujuzi wa stadi za maisha, afya ya uzazi na uzazi wa jinsia, na elimu ya familia; na kutoa mikopo ya masharti nafuu ya jumla ya shilingi bilioni 3.2 kwa vikundi na makampuni 1,241 ya vijana kupitia mfuko wa maendeleo ya vijana.

Mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa afua ni pamoja na: kuongezeka kwa nguvu kazi inayotakiwa kwenye soko la ajira; kuongezeka kwa ushiriki wa watu wenye ulemavu katika shughuli za kijamii na kiuchumi; na kuimarika kwa huduma za malezi, afya ya uzazi, ushauri nasaha na uwezeshaji wa kiuchumi kwa vijana.

Aidha, Serikali itaendelea kutekeleza na kuongeza wigo wa programu ya kitaifa ya kuendeleza ujuzi kwa nguvu kazi ya Taifa kulingana na mahitaji ya soko; kufanya utafiti wa kina wa rasilimali watu; kuongeza wigo wa huduma za kinga ya jamii; kuboresha mfumo wa kielektroniki wa utoaji wa vibali vya ajira kwa wageni; na kuendelea kuwawezesha kijamii na kiuchumi vijana na watu wenye ulemavu.

### 3.3.22 Maendeleo ya Vijana

Utekelezaji wa mpango ulilenga kuongeza ushiriki wa vijana katika shughuli za kijamii, kiuchumi na kuhamasisha ukuaji wa fursa za mitaji kwa vijana. Hii ilijumuisha kukuza uwezeshaji wa kiuchumi kwa vijana kupitia mikopo rafiki na mafunzo ya ujasiriamali.

Utekelezaji wa afua umeleta mafanikio mbalimbali ikiwemo: kutoa mafunzo ya stadi za maisha, afya ya uzazi na elimu ya familia kwa vijana 655,600 mwaka 2024/25; na mikopo ya masharti nafuu yenye thamani ya shiling bililioni 3.1 kwa miradi 148 ya vikundi na makampuni ya vijana kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana umefikia mwaka 2024/25.

Mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa afua hiii ni pamoja na; kuongezeka kwa kipato cha vijana kilikochochewa na upatikanaji wa mikopo nafuu na kuongezeka kwa ushiriki wa vijana katika shughuli za kijamii na kiuchumi.

Aidha, katika kuhakikisha masuala ya vijana yanasimamiwa kikamilifu, Serikali itaendelea kutekeleza programu mbalimbali za maendeleo ya vijana ikiwemo kuanzisha Majukwaa ya Vijana, kuunda Mifumo ya kidigiti ya utoaji na upatikanaji wa taarifa za fursa kwa vijana, kusimamia ustawi na maongozi kwa vijana, kusimamia elimu ya uraia na uzalendo kwa vijana, kukarabati vituo 3 kwa ajili ya kutoa mafunzo kwa vijana pamoja na kuimarisha mfuko wa Maendeleo ya Vijana.

### 3.3.23 Utawala Bora na Utawala wa Sheria

Utawala bora na utawala wa sheria unahusisha utekelezaji wa programu na mikakati ifuatayo: programu ya maboresho katika utumishi wa umma; mkakati wa kitaifa dhidi ya rushwa na mpango wa utekelezaji ambapo awamu ya tatu imekamilika na kuzinduliwa kwa awamu ya nne; programu ya maboresho ya Mahakama; usalama wa raia na mali zao; uendelezaji wa nyumba za viongozi; na uendelezaji wa mji wa Serikali Dodoma.

#### i. Utumishi na Utawala Bora

Mpango ulilenga kuboresha miundombinu mbalimbali ikijumuisha miundombinu ya kuimarisha utawala bora kwa kufanya maboresho katika utumishi wa umma kwa lengo la kuongeza ufanisi na tija katika utoaji wa huduma.

Utekelezaji wa afua umechangia: kutoa mafunzo ya maadili ya utendaji katika utumishi wa umma kwa watumishi 46,500 mwaka 2024/25; kutumia Mfumo wa e-Mrejesho kwa taasisi 408 mwaka 2024/25; na malalamiko yatokanayo na masuala ya utawala bora yalikuwa 138 mwaka 2024/25. Mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa afua ni pamoja na: kuongezeka kwa ari ya watumishi wa umma kutoa huduma bora; pamoja na kuimarika kwa uwezo wa Taasisi za Umma kutoa huduma bora na zenye tija.

Mafanikio yaliyopatikana kutokana utekelezaji wa afua ni pamoja na: kuongezeka kwa ari ya watumishi wa umma kutoa huduma bora; kuimarika kwa uwezo wa Taasisi za Umma kutoa huduma bora na zenye tija. Utekelezaji wa afua za kiutumishi na utawala bora umebainisha kuwa kuna umuhimu wa kuendelea kujengea uwezo watumishi wa Umma pamoja na kuimarisha mifumo ya kielektroniki.

Aidha, matarajio ya mwenendo wa sekta ni: Uwepo wa nafasi ya kuendesha mafunzo ya kujenga uwezo wa watumishi; kutumia teknolojia za kidigitali kuongeza ufanisi, pamoja na ushirikiano wa wadau wa kitaifa na kimataifa zimekuwa ni fursa kubwa katika kuhakikisha uwajibikaji katika utumishi wa umma unaoimarisha utoaji huduma kwa wananchi; uimarishaji wa miundombinu ya kisasa ya kuharakisha mageuzi ya utumishi wa umma; kuwekeza katika mafunzo ya mara kwa mara kwa watumishi ili kuongeza ujuzi hususan katika teknolojia; kupunguza urasimu kwa kutumia mifumo ya kidigitali; kuimarisha uwazi na uwajibikaji kupitia mifumo ya ufuatiliaji na tathmini; kushirikisha wadau kwa karibu; kuhamasisha nidhamu ya kazi serikalini ni hatua muhimu zitakazosaidia utoaji wa huduma bora na kwa ufanisi; kuweka mikakati itakayoongeza uwajibikaji wa Watumishi na Taasisi za Umma katika utoaji wa

huduma ili kuongeza ufanisi na tija katika utoaji huduma; kuondoa mwingiliano wa majukumu na kuongeza ufanisi kwa kufanya mapitio ya kimuundo na mgawanyo wa majukumu katika Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Mashirika na Taasisi za Umma; pamoja na kuendelea kuboresha mifumo ya uwajibikaji ikiwemo mfumo wa utoaji mrejesho (e-Mrejesho) na Mfumo wa Usimamizi wa Utendaji kazi katika Utumishi wa Umma (e-Utendaji) ili kuboresha utendaji kazi katika utumishi wa umma.

**ii. Utawala wa Sheria**

Mpango ulilenga kuboresha mifumo ya utoaji na upatikanaji haki kwa: kuboresha mifumo na miundombinu ya mahakama pamoja na majengo jumuishi ya utoaji haki; kuhamasisha matumizi ya TEHAMA katika utoaji na upatikanaji haki; kuimarisha huduma za usajili wa vizazi na vifo na kuimarisha mifumo ya utunzaji wa taarifa na kumbukumbu za mahakama; na kuimarisha upatikanaji haki kwa Wananchi.

Utekelezaji wa afua umechangia: ujenzi Vituo Jumuisha vya Upatikanaji Haki (*Integrated Justice Centres – IJCs*) 9 mwaka 2024/25; ujenzi wa majengo ya mahakama ya mwanzo 740 mwaka 2024/2025; raia wanaoishi katika mikoa yenye Mahakama Kuu inayofanya kazi imefikia asilimia 83 mwaka 2024/2025. Sheria kuu zilizotafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili zilikuwa sheria 433 Desemba 2025. Idadi ya wananchi waliofikia na kupatiwa huduma za msaada wa kisheria ilikuwa 31,286,215 wakiwemo wanaume 15,443,957 na wanawake 15,842,258 mwaka 2024/2025.

Mafanikio mengine yaliyopatikana ni pamoja na: Mashirika yanayotoa huduma za msaada wa kisheria yalikuwa 377 mwaka 2024/2025; uanzishwaji wa Madawati ya Msaada wa Kisheria katika Mamlaka 184 za Serikali za Mitaa; kutunga na kufanya marekebisho kwa Sheria Kuu 57 na Sheria Ndogo 4,087**;** mrundikano wa mashauri yenye umri mrefu Mahakamani ni 2,780 sawa na asilimia 4 ya mashauri yote yaliyobaki Mahakamani na hivyo kuifanya Tanzania kuwa miongoni mwa nchi chache Barani Afrika zenye mrundikano mdogo wa mashauri Mahakamani; Ofisi za Mashtaka za Wilaya zimefikia 108 mwaka 2024/25. Vilevile, kupungua kwa muda na gharama wanazotumia wananchi kupata huduma za mahakama na msaada wa kisheria; kurahishwa kwa upatikanaji wa huduma za usajili wa Vizazi, Vifo, Ndoa, Talaka na Bodi za Wadhamini kidijitali kupitia eRITA.

**iii. Amani, Utulivu na Usalama**

Mpango ulilenga kuimarisha usalama wa raia na mali zao nchini kwa kupunguza kiwango cha uhalifu; kuongeza utambuzi na usajili wa raia; na kupunguza kiwango cha ajali barabarani.

Utekelezaji wa afua umechangia; idadi ya watu waliosajiliwa na kutambuliwa imefikia 26,374,903 mwaka 2024/25; kiwango cha uhalifu nchini kimefikia asilimia 3.2 mwaka 2024/25; na kuendelea kuimarisha miundombinu ya uangalizi wa usalama barabarani ambapo *Mradi wa Smart Traffic Management Monitoring and Surveillance* wenye lengo la kuboresha mifumo ya usalama kwa kutumia teknolojia ya kamera za kisasa imepangwa kuanza kutekelezwa kwa kupita Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta

Binafsi (PPP). Hatua iliyofikiwa ni kuandaliwa kwa mikataba baada ya kupatikana kwa Mbia Kampuni ya ROM Solution Limited.

**Kielelezo Na. 3.25: Idadi ya watu waliosajiliwa na kutambuliwa na NIDA**




***Chanzo:*** Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi

Mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa afua ni pamoja na: kuimarika kwa hali ya amani, utulivu na usalama kutokana na kudhibitiwa kwa vitendo vya uhalifu; kurahisishwa kwa udhibiti wa uhalifu, utambuzi wa wahalifu, na kupungua kwa matumizi ya vitambulisho feki; na kuongezeka kwa ushiriki wa jamii katika shughuli za usalama.

**iv. Uendelezaji wa Mji wa Serikali Dodoma**

Katika kipindi cha utekelezaji wa mpango, Serikali imeendelea kukamilisha Awamu ya Pili ya ujenzi wa mji wa Serikali Mtumba. Utekelezaji wa afua hii umechangia: jumla ya Wizara 14 kati ya 25 zimehamia katika majengo ya kudumu na wastani wa ujenzi katika mji wa Serikali ni asilimia 92.3 Desemba, 2025; na huduma za Serikali kupatikana katika eneo moja hivyo kuongeza ufanisi katika kuwahudumia wananchi.

**v. Kukabiliana na Maafa**

Serikali imeendelea kuimarisha utoaji wa huduma za kukabiliana na maafa kwa kuendelea na ujenzi wa Kituo cha usimamizi wa Maafa kwa Awamu ya pili katika eneo la Nzuguni B jijini Dodoma ambapo utekelezaji umefikia asilimia 70. Mafanikio yatakayopatikana ni kuboreshwa kwa mazingira ya utoaji huduma katika kituo cha taifa cha menejimenti ya maafa pamoja na kuwezesha kutolewa kwa taarifa za tahadhari za mapema ambazo zitasaidia kupunguza athari zitokanazo na maafa.

### 3.4 Changamoto, Hatua za Kuboresha katika Utekelezaji wa Miradi

Utekelezaji wa mpango umechangia katika kuharakisha mabadiliko ya kiuchumi na kijamii nchini. Aidha, licha ya mafanikio yaliyopatikana, utekelezaji wa miradi unakabiliwa na changamoto mbalimbali ambazo zimeathiri ufanisi katika utekelezaji wa miradi hiyo. **Jedwali Na. 3. 2:** linaelezea changamoto za utekelezaji wa mpango pamoja na hatua za kuboresha.

**Jedwali Na. 3.2: Changamoto, Hatua za Kuboresha katika Utekelezaji wa Miradi**

| No. | Changamoto | Hatua za Kuboresha |
|---|---|---|
| 1. | Kutolipwa kwa wakati kwa madai ya makandarasi kunakotokana na upungufu wa rasilimali fedha. | Kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani na kuweka vipaumbele katika utekelezaji wa programu na miradi |
| 2. | Kuongezeka kwa gharama za utekelezaji wa miradi kunakotokana na kutohusishwa kwa Wadau muhimu wakati wa maandalizi na utekelezaji; | Kuimarisha ushiriki wa wadau muhimu na usimamizi wa miradi kupitia matumizi ya mifumo ya TEHAMA, ikiwemo kuimarisha mfumo wa NPMIS |
| 3. | Athari za mabadiliko ya tabianchi ikiwemo ukame na mvua zisizotabirika zilizoathiri sekta za uzalishaji; | Kuweka mikakati ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi, ikiwemo kuhimiza uhifadhi wa mazingira |
| 4. | Kutofanyika kwa wakati sahihi umilikishaji wa ardhi na fidia katika maeneo ya utekelezaji wa miradi na hivyo kuchelewesha kuanza | Kuharakisha michakato ya fidia na umilikishaji wa ardhi kwa miradi ya maendeleo |
| 5. | Uratibu usioridhisha kati ya Wizara mama na taasisi zilizo chini yake katika utekelezaji wa miradi | Kuimarisha uratibu kati ya wizara mama na taasisi zilizo chini yake |

# SURA YA NNE

# VIPAUMBELE KWA MWAKA 2026/27

## 4.1 Utangulizi

Vipaumbele vya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2026/27 ni vya kwanza katika utekelezaji wa Dira 2050 yenye dhima ya kuifanya Tanzania kuwa **Taifa Jumuishi Lenye Ustawi, Haki na Linalojitegemea** lililojengwa katika misingi ya demokrasia, haki na uhuru, utu, amani na umoja, umiliki kamili wa utajiri na rasilimali asilia pamoja na uhifadhi na uendelezaji chanya wa utamaduni na maadili ya taifa.

Aidha, katika kuifikia ndoto ya Tanzania katika kipindi cha miaka 25 ijayo, vipaumbele vya mpngo vinajenga msingi wa utekelezaji wa malengo makuu ya Dira 2050 ambayo ni: Tanzania kuwa nchi yenye uchumi wa kipato cha kati ngazi ya juu, ulio mseto, himilivu, jumuishi na shindani; maisha bora na ustawi kwa wote; Taifa linalohifadhi na kutumia rasilimali za asili kwa ufanisi, uendelevu na tija, na linalostahimili mabadiliko ya tabianchi; na Jamii yenye umahiri na ujuzi wa kutumia teknolojia za kidijitali katika kuchochea ubunifu na kuongeza ushindani wake kimataifa.

Katika kuyatekeleza malengo makuu ya Dira 2050, vipaumbele vya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2026/27 vimeandaliwa kwa kutohoa maeneo ya vipaumbele, malengo, shabaha, afua na viashiria muhimu vya utendaji vilivyoainishwa katika Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2026/27 – 2030/31 wenye dhima ya “**Mageuzi kwa ajili ya Ukuaji Jumuishi wa Uchumi na Uzalishaji Ajira”** ambao ni wa kwanza katika utekelezaji wa Mpango Elekezi wa Maendeleo wa Muda Mrefu 2026/27 – 2050/51.

## 4.2 Maeneo ya Kipaumbele ya Mpango

Vipaumbele vya Mpango kwa Mwaka 2026/27 vimeandaliwa kwa kuzingatia maeneo yafuatayo: (i) utawala, amani, usalama na utulivu; na (ii) uchumi imara, jumuishi na shindani unaotekelezwa kwa sekta tisa (9) za kimageuzi; (iii) uwezo wa watu na maendeleo ya kijamii; (iv) uhifadhi wa mazingira na ustahimilivu wa mabadiliko ya tabianchi; na (v) sekta tano (5) za vichocheo vya kimageuzi. Vipaumbele hivi vitatekelezwa kupitia programu za kielelezo za kitaifa saba (7) na zinazotekelezwa kupitia miradi shikizi (anchor projects) 38 kwa mwaka 2026/27. Aidha, utekelezaji wa Mpango utajielekeza katika kuhakikisha uendelevu wa utekelezaji wa miradi ya kielelezo na afua za maendeleo ambazo hazikukamilika katika kipindi cha utekelezaji wa Dira 2025.

### 4.2.1 Utawala, Amani, Usalama na Utulivu

Eneo hili limetoa kipaumbele katika eneo la uimarishaji wa utawala bora, demokrasia, ulinzi na utulivu. Msisitizo umewekwa katika kuendeleza utawala bora, kuheshimu na kusimamia utawala wa sheria, pamoja na kudumisha amani, utulivu na usalama kwa wananchi wote. Mikakati, shabaha, afua, viashiria muhimu vya upimaji wa utendaji, miradi na programu za maendeleo katika eneo hili ni kama ifuatavyo:

i. **Utawala Bora**

Sekta ya Utawala Bora itaendelea kuboresha utumishi wa umma kwa kuimarisha mifumo na miundombinu itakayosaidia taasisi za umma kuwa imara, zenye ufanisi na zinazowajibika ili kuongeza ufanisi na tija katika utoaji wa huduma. Maboresho haya yatajumuisha kuimarisha taratibu za kiutendaji, kusasisha kanuni na miongozo ya kazi, pamoja na kuboresha mifumo ya TEHAMA ili kurahisisha utoaji wa huduma na kupunguza urasimu usio wa lazima. Aidha, sekta itaongeza juhudi katika kujenga uwezo wa watumishi kupitia mafunzo endelevu, tathmini za utendaji kazi kwa kuzingatia viwango vya kupimika (performance standards), na kuimarisha maadili ya kazi kwa kuzingatia misingi ya uadilifu na nidhamu. Hatua hizi zitalenga kuongeza tija, kuimarisha uwajibikaji binafsi wa watumishi na wa taasisi, pamoja na kuondoa mianya ya rushwa na matumizi mabaya ya rasilimali za umma.

Utekelezaji wa malengo haya utafanyika kupitia miradi ya maendeleo utakaopelekea kuondoa muingiliano wa majukumu na kuongeza ufanisi kwenye taasisi za umma; kurahisisha ushughulikiaji wa malalamiko ya wananchi kuhusu masuala ya utawala bora; kuongeza ujuzi kwa watumishi wa umma utakaoboresha utoaji wa huduma kwa wananchi; kuwa na Sera, Sheria, taratibu na miongozo ya usimamizi wa rasilimaliwatu na ajira katika utumishi wa umma inayoendana na wakati wa sasa; kuboresha utendaji kazi wa watumishi na taasisi za umma; kuongezeka kwa kiwango cha maadili katika utumishi wa umma; kuongezeka kwa uwazi katika ajira na upandishwaji vyeo; na kuwa na viongozi waandamizi na viongozi wapya wenye maadili ya uongozi. Viashiria na shabaha za sekta kwa mwaka 2026/27 zimeainishwa katika **Jedwali Na. 4.1** na orodha ya miradi itakayotekelezwa kulingana na vipaumbele imeainishwa katika **Kiambatisho Na. 2.**

**Jedwali Na. 4.1: Viashiria na Shabaha katika Eneo la Utawala Bora**

| Na. | Kiashiria | Mwaka wa Kizio (2024/25) | Shabaha (2026/27) | Shabaha (2030/31) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Idadi ya taasisi za Umma zilizofanyiwa ufuatiliaji wa matumizi ya Mfumo wa Usimamizi wa Utendaji Kazi katika Utumishi wa Umma (e-Utendaji). | 571 | 571 | 571 |
| 2. | Idadi ya taasisi za umma zilizofundishwa matumizi ya Mfumo wa e-Mrejesho (ili kuongeza uwajibikaji na mapambano dhidi ya rushwa katika utumishi wa umma na nchi kwa ujumla). | 100 | 100 | 570 |
| 3. | Idadi ya watumishi wa umma waliopatiwa mafunzo ya maadili ya utendaji katika Utumishi wa Umma. | 69,047 | 84,047 | 144,047 |

***Chanzo:*** Ofisi Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora

### ii. Utawala wa Sheria

Serikali itaendelea kuimarisha utawala bora na utawala wa sheria kwa kutekeleza miradi mbalimbali inayolenga kuimairisha utoaji wa huduma kwa wananchi. Miradi hiyo itahusisha Awamu ya Pili ya uendelezaji wa Mji wa Serikali Mtumba – Dodoma, Kuimarisha uwezo wa nchi wa kuzuia, kujiandaa, kukabiliana na kurejesha hali pindi maafa yanapotokea kwa kuendelea na ujenzi wa Kituo cha Usimamizi wa Maafa eneo la Nzuguni B – Dodoma na utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Usimamizi wa Maafa ya Mwaka 2004 Toleo la 2025, kuimarisha huduma za uchapishaji wa Nyaraka za Serikali kwa kukamilisha Kiwanda cha Kisasa cha Uchapishaji wa Nyaraka za Serikali eneo la Kisasa – Dodoma, Kuimarisha udhibiti na mapambano dhidi ya dawa za kulevya kwa kuendelea na utekelezaji wa Sera ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ya Mwaka 2024 pamoja na ujenzi wa Kituo cha Utengamao (Rehabilitation Center) Itega – Dodoma.

Utekelezaji wa miradi na vipaumbele hivi katika sekta utakuwa na matokeo chanya katika kuimarisha utawala bora na utoaji wa huduma kwa wananchi. Aidha, matokeo mengine ni kuimarika kwa uwezo wa nchi katika kuzuia, kujiandaa, kukabiliana na kurejesha hali pindi maafa yanapotokea nchini, kuongeza ufanisi katika udhibiti na mapambano dhidi ya dawa za kulevya na kukaribia dira ya kutokuwa na jamii inayojihusisha na biashara na matumizi ya dawa za kulevya, na kuimarika kwa ulinzi na usalama wa nyaraka za Serikali. Orodha ya miradi itakayotekelezwa imeoneshwa katika **Kiambatisho Na. 2.**

Sekta ya sheria itaendelea kutekeleza miradi ya kipaumble inayolenga Kuimarishwa kwa uwazi, uwajibikaji, maadili na demokrasia, amani na utulivu kwa ajili ya ushiriki wa ufanisi na usawa wa wanajamii wote katika maendeleo ya taifa. Kuimarishwa kwa uadilifu na uaminifu wa taasisi zinazosimamia mahusiano na mausala ya wananchi.

Utekelezaji wa malengo haya utakaofanyika kupitia miradi ya maendeleo utapelekea kuongezeka kwa Kiwango cha Fahirisi ya Ushiriki wa Wananchi na Uwajibikaji *(Voice and Accountability Index)*, Kuimarisha fahirisi ya kiashiria cha Rushwa (Corruption Perception Index), kiwango cha utulivu wa kisiasa, amani na usalama, Kuimarika kwa fahirisi ya utawala wa sheria *(Rule of Law Index),* Kuimarika kwa fahirisi ya kiwango cha uaminifu wa umma. Viashiria na shabaha za sekta kwa mwaka 2026/27 zimeainishwa katika **Jedwali Na. 4.2**.

**Jedwali Na. 4.2: Viashiria na Shabaha katika eneo la Utawala Sheria**

| Na. | Kiashiria | Mwaka wa Kizio | Shabaha (2026/27) | Shabaha (2030/31) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Fahirisi ya Utulivu wa kisiasa, Kutokuwepo kwa Vurugu na Ugaidi. | - 0.05 (2023) | -0.02 | 0.1 |
| 2. | Fahirisi ya Utawala wa Sheria katika Nchi Zenye Kipato cha Chini hadi Kati. | 15/37 (2024) | 13 | Top 10 |
| 3. | Fahirisi ya Kiashiria cha Rushwa Upangaji wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (Nchi Yenye Rushwa | 2nd (2024) | 1.8 | 1st |

| Na. | Kiashiria | Mwaka wa Kizio | Shabaha (2026/27) | Shabaha (2030/31) |
|---|---|---|---|---|
| | kiwango cha Chini Zaidi)) | | | |

***Chanzo:*** Wizara ya Katiba na Sheria

### iii. Amani, Utulivu na Usalama

Sekta ya Amani, Utulivu na Usalama itaendelea kutekeleza miradi ya kipaumbele kwa lengo la kuimarisha usalama wa raia na mali zao kwa kupunguza kiwango cha uhalifu, kuongeza utambuzi na usajili wa raia kupitia Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), na kupunguza ajali za barabarani.

Katika kufanikisha hilo, Serikali inaendelea kutekeleza programu na miradi sita ya kimkakati ili kuboresha utendakazi wa vyombo vya usalama na kudumisha amani, utulivu na usalama nchini, ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano.

Aidha, Serikali imeimarisha usimamizi wa kampuni binafsi za ulinzi ili kuongeza uwajibikaji, kuimarisha usalama wa raia na mali zao, na kuwezesha mazingira bora ya utekelezaji wa shughuli za uchumi na maendeleo. Viashiria na shabaha za sekta kwa mwaka 2026/27 zimeainishwa katika **Jedwali Na. 4.3**, huku orodha ya miradi ya kipaumbele ikiwa katika **Kiambatisho Na. 2.**

**Jedwali Na. 4.3: Viashiria na Shabaha katika Eneo la Amani, Utulivu na Salama**

| No. | Kiashiria | Mwaka wa Kizio | Shabaha (2026/27) | Shabaha (2030/31) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Kupungua kwa kiwango cha ajali za barabara (Asilimia) | 35.0 (2023/24) | 36 | 40.00 |
| 2. | Asilimia ya ongezeko la wigo wa hifadhi ya jamii | 28.4 (2023/24) | 31.24 | 42.60% |
| 3. | Wastani wa alama ya Farihisi ya kiwango cha uhalifu | 53.2 (2025) | 52.12 | 47.8 |
| 4. | Kiwango cha matukio ya ukatili wa kijinsia | 38.9 (2022) | 35.12 | ≤20 |
| 5. | Ukatili dhidi ya watoto (VAC) – Wasichana: Unyanyasaji wa kingono (asilimia) | 11 (2024) | 9.9 | ≤5.50 |
| 6. | Ukatili dhidi ya watoto (VAC) – Wasichana: Unyanyasaji wa kihisia (asilimia) | 22 (2024) | 20.24 | ≤13.20 |
| 7. | Ukatili dhidi ya watoto (VAC) – Wavulana: Unyanyasaji wa kingono (asilimia) | 5 (2024) | 4.54 | ≤2.69 |
| 8. | Kiwango cha uhalifu (asilimia) | 5.2 | 6 | 35 |
| 9. | Idadi ya kampeni za amani zilizofanyika | 50 | 60 | 150 |
| 10. | Kiwango cha ushiriki wa jamii | 30 | 35 | 80 |

| No. | Kiashiria | Mwaka wa Kizio | Shabaha (2026/27) | Shabaha (2030/31) |
|---|---|---|---|---|
| | katika shughuli za usalama (%) | | | |
| 11. | Idadi ya ajira zilizozalishwa katika miradi ya maendeleo | 23,000 | 24,000 | 33,000 |
| 12. | Mchango katika ajira (%) | 14.7 | 15.7 | 18.8 |
| 13. | Kiwango cha kupungua kwa ajali za barabarani (%) | 30.50 | 35.8 | 60 |
| 14. | Idadi ya askari waliopatiwa makazi bora | 11,824 | 15,000 | 20,688 |
| 15. | Kiwango cha matukio ya hatari yaliyotambuliwa na kuripotiwa na jamii (%) | 75 | 80 | 98 |

***Chanzo:*** Wizara ya Mambo ya Ndani

#### 4.2.2 Uchumi Imara, Jumuishi na Shindani

Kwa mwaka 2026/27 mikakati, shabaha, afua, viashiria muhimu vya upimaji wa utendaji, miradi na programu za maendeleo zitajikita katika kuimarisha maeneo manne (4) ambayo ni: Uchumi Jumla tulivu na unaotabirika; Sera za bajeti endelevu; sekta ya nje iliyohimilivu na mseto; na na sekta muhimu za mageuzi. Aidha, miradi na programu za maendeleo zitakazotekelezwa katika eneo hili imelenga kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji; kuimarisha na kuendeleza ushirikiano na nchi mbalimbali na mashirika ya kimataifa ili kukuza fursa za kidiplomasia na kiuchumi:

##### 4.2.2.1 Uchumi Jumla Tulivu na Unaotabirika

Katika eneo hili miradi na programu zitakazotekelezwa zitajielekeza katika kuhakisha viashiria vilivyoainishwa katika **Jedwali Na. 4.4** vinafikiwa.

**Jedwali Na. 4.4: Viashiria Muhimu vya Uchumi Jumla Tulivu na Unaotabirika**

| Na. | Kiashiria | Mwaka wa Kizio | Shabaha (2026/27) | Shabaha (2030/31) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Pato ghafi la taifa la sasa (Bilioni) | 81.537 (2024) | 88.84 | 118.052 |
| 2. | Ukuaji Halisi wa Pato laTaifa (asilimia) | 5.5.% (2024) | 6.3% | 10.5% |
| 3. | Pato la Taifa kwa kila mtu (dola za Marekani) | 1,343.91 (2024) | 1,346.70 | 1,638 |
| 4. | Uwiano wa Deni la Taifa kwa Pato la Taifa (unaopimwa dhidi ya malengo ya DSA). | 48.9% (2025) | 50.12 | <55% |
| 5. | Mfumuko wa Bei wa Walaji (Wastani wa Kipindi) | 3.1% (2024) | 3% - 5% | 3%–5% |
| 6. | Mikopo kwa Sekta Binafsi(Ukua kila mwaka) | 15.9% (2024) | 17.20 | 22.4% |
| 7. | Mikopo ya ndani kwa sekta binafsi (Hisa katika Pato la Taifa) | 16.3% (2025) | 18.04 | 25% |
| 8. | Kiwango cha Mfumuko wa Bei wa Taifa wa Mwaka (mwisho wa kipindi) | 3.1% (2024) | 3% - 5% | 3%–5% |
| 9. | Kiwango cha mfumuko wa bei za msingi kwa mwaka | 3.4% (2024) | 3% - 5% | 3%–5% |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 10. | Mikopo Chechefu (Hisa katika Mikopo Ghafi) | 3.3% (2024) | <5% | <5% |
| 11. | Ujumuishi wa Kifedha (Watu Wazima) | 76% (2023) | 74.65% | 90% |
| 12. | Watu wazima wenye akaunti za miamala | 72% (2023) | 74.60% | 85%% |
| 13. | Watu wazima wanaotumia malipo ya kidijitali | 13% (2023) | 18.40% | 40% |

***Chanzo:*** Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano

#### 4.2.2.2 Sera za Bajeti Endelevu

Katika eneo hili miradi na programu zitakazotekelezwa zitajielekeza katika kuhakisha viashiria vilivyoainishwa katika **Jedwali Na. 4.5** vinafikiwa.

**Jedwali Na. 4.5: Viashiria muhimu vya Sera endelevu za Kibajeti**

| Na. | Kiashiria | Mwaka wa Kizio | Shabaha (2030/31) |
|---|---|---|---|
| 1. | Uwiano wa Mapato ya Ndani kwa Pato la Taifa | 14.9% (2024/25) | 20.0% |
| 2. | Uwiano wa Mapato ya Kodi kwa Pato la Taifa | 13.3% (2024/25) | 18.0% |
| 3. | Uwiano wa Mapato Yasiyo ya Kodi kwa Pato la Taifa | 2.7% (2024/25) | 5.0% |
| 4. | Uwiano wa Deni la Taifa kwa Pato la Taifa (ukilinganishwa na malengo ya Tathmini ya Uimilivu wa Deni - DSA) | 47.0% (2024/25) | <50.0% |
| 5. | Thamani ya Sasa ya Deni la Taifa kwa Pato la Taifa | 40.3 (2024/25) | 19.6 |
| 6. | Thamani ya Sasa ya Huduma ya Deni la Taifa kwa Mapato ya Ndani | 44.3 (2023/24) | 15 |
| 7. | Thamani ya Sasa ya Deni la Nje la Taifa kwa Mauzo ya Nje | 123.8 (2024/25) | 100.3 |
| 8. | Nakisi ya Bajeti (Asilimia ya Pato la Taifa) | -3.1% (2024) | -2.8% |
| 9. | Matumizi ya Maendeleo (Asilimia ya Bajeti Kuu) | 31% (2024/25) | 35%–40% |
| 10. | Uwiano wa Malipo ya Riba kwa Mapato ya Jumla (Kila Mwaka) | 11% (2023) | ≤8% |
| 11. | Mahitaji Ghafi ya Ugharamiaji (Asilimia ya Pato la Taifa) | 35% (2024) | 35% |
| 12. | Wastani wa Muda wa Kuiva kwa Deni (Miaka) | 9 years (2023) | 12 years |
| 13. | Gawio Halisi kutoka Mashirika ya Umma (Asilimia ya Pato la Taifa) | <0.2% (2023) | 0.5–1% |
| 14. | Dhamana za Serikali (Asilimia ya Pato la Taifa) | 2.8% (2023) | ≤3% |

***Chanzo:*** Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano

#### 4.2.2.3 Sekta ya Nje Iliyohimilivu na Mseto

Katika eneo hili miradi na programu zitakazotekelezwa zitajielekeza katika kuhakisha viashiria vilivyoainishwa katika **Jedwali Na. 4.6** vinafikiwa.

**Jedwali Na. 4.6: Viashiria muhimu vya Sekta ya Nje Iliyohimilivu na Mseto**

| Na. | Kiashiria | Mwaka wa Kizio | Shabaha (2030/31) |
|---|---|---|---|
| 1. | Urari wa Akaunti ya Sasa (Asilimia ya Pato la Taifa) | -2.6% (2024) | -2.1% |
| 2. | Akiba ya Fedha za Kigeni (Miezi ya Uagizaji wa Bidhaa na Huduma) | 4.5 (2024) | 5 |
| 3. | Uwekezaji wa Moja kwa Moja wa Kigeni (Dola za Marekani Milioni) | 1,717.6 (2024) | 8,366.28 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 4. | Mchango wa Mauzo ya Mazao ya Asili katika Thamani ya Jumla ya Mauzo ya Nje | 16.2% (2024) | 11.05% |
| 5. | Mchango wa Mauzo ya Bidhaa Zisizo za Asili katika Thamani ya Jumla ya Mauzo ya Nje | 79.2% (2024) | 84.15% |
| 6. | Mchango wa Thamani ya Mauzo ya Bidhaa za Viwandani katika Mauzo ya Nje Zisizo za Asili | 18.6% (2024) | 29.59% |

***Chanzo:*** Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano

#### 4.2.2.4 Sekta Muhimu za Mageuzi

Eneo hili limetoa kipaumbele katika mikakati, shabaha, afua, viashiria muhimu vya upimaji wa utendaji, miradi na programu za maendeleo zitajikita katika kuchochea mageuzi katika sekta tisa (9). Sekta hizo ni: kilimo (mazao, mifugo, uvuvi na misitu); viwanda na uzalishaji; ujenzi; madini na uchimbaji wa mawe; utalii; michezo na ubunifu; Uwekezaji na biashara; sekta binafsi; na Uhusiano wa Kimataifa na Diplomasia ya Uchumi. Hivyo, mikakati, shabaha, afua, viashiria muhimu vya upimaji wa utendaji, programu na miradi ya maendeleo katika eneo hili ni kama ifuatavyo:

##### 4.2.2.4.1 Sekta ya Kilimo (Mazao, Mifugo, Uvuvi na Misitu)

**i. Sekta ya Mazao**

Sekta ya Kilimo itaendelea kutekeleza miradi ya kipaumbele inayolenga kuimarisha kilimo biashara cha mazao himilivu ili kuchochea ukuaji wa uchumi na maisha vijijini; kuimarisha usalama wa chakula na Lishe kwa lengo la kupunguza njaa na kuongeza ubora wa afya ya umma; kuimarisha vyama vya ushirika ili kuchochea maendeleo vijijini na kuwapa nguvu wanachama wa ushirika; kuimarisha Mfuko wa Maendeleo ya Kilimo (ADF) ili kupunguza vihatarishi katika uwekezaji wa muda mrefu wa kilimo kila mwaka; kuanzisha mpango wa kitaifa wa dhamana ya mikopo ili kuwezesha ufadhili wa benki za biashara kwa wakulima vijana na wanawake; kutekeleza mpango mahsusi wa ruzuku kwa pembejeo muhimu za kilimo; kupanua ufadhili (patient finance) kutoka vyanzo vya ndani na kimataifa ili kuboresha upatikanaji wa fedha kwa wakulima wadogo kila mwaka; kuwezesha wakulima binafsi kwa kuwapatia masoko ya uhakika, upatikanaji wa pembejeo bora, msaada wa kiufundi na bei thabiti kupitia makubaliano ya moja kwa moja na wanunuzi kila mwaka; kuandaa mfumo wa kawaida wa kilimo cha mkataba ili kulinda wakulima na wanunuzi kila mwaka; kuimarisha mnyororo wa thamani wa pamba kwa kuzalisha nyuzi (lint/fibre), uzi, vitambaa vilivyofumwa (denim, poplin), bidhaa zenye rangi na zilizokamilika, pamoja na nguo (apparel); na kuanzisha mfumo wa kitaifa wa kidijitali wa ufuatiliaji wa mazao kwa ajili ya mauzo ya mazao makuu nje.

Utekelezaji wa malengo haya utapelekea kuongezeka kwa tija na uzalishaji wa mazao ya kilimo; kuongeza uzalishaji wa mazao ya bustani; kupunguza gharama za uagizaji wa mafuta ya kula, ngano na nafaka nyingine; kuongeza idadi ya wakulima watakaopatiwa pembejeo bora za kilimo; kupunguza upotevu wa mazao baada ya kuvuna; kuhakikisha upatikanaji wa malighafi za viwandani kwa asilimia 100; kutengeneza ajira mpya kwa vijana na wanawake; kuongeza thamani ya mauzo nje; kuongezeka kwa ardhi ya kilimo iliyolimwa kwa kutumia mbinu za kilimo

zinazozingatia mabadiliko ya hali ya hewa hadi asilimia 40 na kuboresha uwiano wa maafisa ugani na wataalamu wa kilimo.

Viashiria na shabaha za sekta ya Kilimo kwa mwaka 2026/27 ni kama vilivyoainishwa katika **Jedwali Na. 4.7** na orodha ya miradi itakayotekelezwa kulingana na vipaumbele imeainishwa katika **Kiambatisho Na. 2**

**Jedwali Na. 4.7 : Viashiria na Shabaha za Sekta ya Kilimo**

| Na. | Kiashiria | Mwaka wa Kizio | Shabaha (2026/27) | Shabaha (2030/31) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Mchango wa sekta ya Kilimo katika pato la Taifa (%) | 26.3 (2024) | 26.16 | 25.60 |
| 2. | Ukuaji wa Sekta ya Kilimo | 4.1 (2024) | 5.28 | 10 |
| 3. | Kiwango cha Utoshelevu wa Chakula (%) | 128 (2024) | 128.4 | 130 |
| 4. | Thamani ya mauzo ya nje ya mazao ya Kilimo (USD in Billions) | 3.54 (2024) | 3.83 | 5 |
| 5. | Kiwango cha Upotevu wa mazao (%) | 35 (2024) | 30 | 10 |
| 6. | Eneo linalomwagiliwa (Hekta) | 983 (2024) | 1,200 | 5,000 |

***Chanzo:*** Wizara ya Kilimo

### ii. Sekta ya Mifugo

Sekta ya Mifugo itaendelea kutekeleza miradi ya kipaumbele inayolenga ukuaji wa uchumi na kuboresha maisha ya jamii kwa kuongeza uzalishaji, masoko na kuongeza thamani ya mazao ya mifugo; kuimarisha ulinzi na usimamizi wa rasilimali za mifugo; kuhamasisha uwekezaji; na kuimarisha utafiti, mafunzo na huduma za ugani.

Utekelezaji wa malengo haya utakaofanyika kupitia miradi ya maendeleo unalenga kuleta ongezeko la thamani ya mazao ya Mifugo, ongezeko la matumizi ya chanjo na mwitikio wa uogeshaji wa mifugo; kuimarika kwa teknolojia za udhibiti wa magonjwa ili kupunguza milipuko na kuongeza ubora wa mifugo; ongezeko la upatikanaji wa mbari bora za mifugo ikiwemo madume na mitamba; uboreshaji wa miundombinu ya malisho, maji, majosho na huduma za ugani ambao kwa pamoja utachochea ongezeko la uzalishaji wa mifugo na bidhaa za mifugo itakayopelekea kuongezeka kwa mauzo ya mifugo na mazao yake ndani na nje ya nchi.

Aidha, viashiria na shabaha za sekta ya Mifugo kwa mwaka 2026/27 ni kama vilivyoainishwa katika **Jedwali 4.8** na orodha ya miradi itakayotekelezwa kulingana na vipaumbele imeainishwa katika **Kiambatisho Na. 2**

**Jedwali Na. 4.8: Viashiria na Shabaha katika Sekta ya Mifugo**

| Na. | Kiashiria | Mwaka wa Kizio (2024/25) | Shabaha (2026/27) | Shabaha (2030/31) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Kiwango cha Vifo vya Mifugo (%) | 16 | 12 | 7 |
| 2. | Kiwango cha Magonjwa ya Mifugo (%) | 2.5 | 1.8 | 1.4 |
| 3. | Kiwango cha Uogeshaji Mifugo | 82 | 84 | 95 |

| Na. | Kiashiria | Mwaka wa Kizio (2024/25) | Shabaha (2026/27) | Shabaha (2030/31) |
|---|---|---|---|---|
| | katika josho (%) | | | |
| 4. | Kiwango cha Chanjo ya Mifugo (%) | 53.01 | 70 | 90 |
| 5. | Uzalishaji wa Nyama (Tani) | 1,124,449 | 1,152,823.40 | 1,250,000 |
| 6. | Mauzo ya nyama nje ya nchi (Tani) | 13,112.44 | 14,745 | 15,500 |
| 7. | Kiasi cha Ardhi kilichotengwa kwa ajili ya malisho (Hekta) | 3,489,701.13 | 3,991,760.93 | 6,000,000 |
| 8. | Kiasi cha Ardhi kilichotangazwa kwenye gazeli la serikali (Hekta) | 1,349,486.29 | 1,777,529.26 | 3,489,701.13 |
| 9. | Idadi ya Mabwawa ya Mifugo | 1,397 | 1,401 | 1,842 |
| 10. | Idadi ya Visima Virefu (Idadi) | 124 | 130 | 225 |
| 11. | Kiasi cha mbegu za malisho (Tani) | 222.54 | 317.3 | 790.98 |

***Chanzo:*** Wizara ya Mifugo na Uvuvi

### iii. Sekta ya Uvuvi

Sekta ya Uvuvi itaendelea kutekeleza miradi ya kipaumbele inayolenga kuifanya sekta hiyo kuongeza uzalishaji, masoko na kuongeza thamani ya mazao ya uvuvi na ukuzaji viumbemaji; kuimarisha ulinzi na usimamizi wa rasilimali za uvuvi; kuhamasisha uwekezaji ikiwemo uvuvi wa bahari kuu; na kuimarisha tafiti za uvuvi, mafunzo na huduma za ugani.

Utekelezaji wa malengo haya utakaofanyika kupitia miradi ya maendeleo unatarajiwa kuleta ongezeko la uvunaji endelevu na mauzo ya mazao ya uvuvi na ukuzaji viumbemaji; upatikanaji wa vifaa vya kisasa vya uvuvi ikiwemo meli, boti na vizimba; ongezeko la uzalishaji wa vifaranga vya samaki na chakula cha samaki; uongezaji wa thamani ya mazao ya uvuvi na ukuzaji viumbemaji; uboreshwaji wa miundombinu ya uvuvi na ukuzaji viumbemaji; na kuimarisha tafiti za uvuvi  na kutumia taarifa za tafiti kuendeleza sekta.

Aidha, viashiria na shabaha za sekta ya Uvuvi kwa mwaka 2026/27 ni kama vilivyoainishwa katika **Jedwali 4.9** na orodha ya miradi itakayotekelezwa kulingana na vipaumbele imeainishwa katika **Kiambatisho Na. 2**

**Jedwali Na. 4.9 :Viashiria na Shabaha katika Sekta ya Uvuvi**

| Na. | Kiashiria | Mwaka wa Kizio (2024/25) | Shabaha (2026/27) | Shabaha (2030/31) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Uzalishaji wa samaki (tani) | 575,000 | 600,000 | 750,000 |
| 2. | Mauzo ya Samaki nje ya nchi (Tani) | 52,565.56 | 54,000 | 60,000 |
| 3. | Uzalishaji wa chakula cha samaki (tani) | 5,879 | 8,000 | 11,000 |
| 4. | Uzalishaji wa vifaranga vya Samaki (Idadi) | 140,018,196 | 174,645,520 | 428,051, 828 |
| 5. | Idadi ya Vizimba (idadi) | 1,636 | 2,045 | 4,992 |
| 6. | Mchango katika Pato la Taifa (%) | 1.7 | 2.0 | 3.5 |

***Chanzo:*** Wizara ya Mifugo na Uvuvi

**iv. Misitu**

Sekta ya Maliasili (Misitu) inalenga kuendelea kuhakikisha usambazaji endelevu wa mazao na huduma za misitu kwa kudumisha eneo la misitu la kutosha chini ya usimamizi madhubuti, na hivyo kuboresha mfumo wa ikolojia, kuimarisha maisha vijijini na uhakika wa usambazaji wa malighafi kwa viwanda vinavyotegemea misitu. Kukuza maendeleo endelevu ya viwanda vinavyotegemea misitu biashara na kuwa na mchango wenye tija katika kuongeza thamani ya bidhaa za misitu, kupanua wigo wa bidhaa, kuongeza mauzo nje na kutumia bidhaa za ndani badala ya kuagiza, kufanya ufugaji wa kisasa na wa kibiashara wa nyuki na uzalishaji wa asali ili kukidhi mahitaji kwa njia endelevu, kukuza biashara inayolinda mazingira, na kuongeza ushindani katika masoko ya nje kupitia uboreshaji wa ujuzi, ukuzaji wa teknolojia, na ujumuishaji wa masoko.

Utekelezaji wa malengo haya utafanyika kupitia miradi ya maendeleo ambayo itawezesha kuongezeka kwa eneo la biashara kwa ajili ya mashamba ya misitu na vitalu vya miti ya jamii kufikia hekta milioni 1.5 ifikapo Juni 2031, kuongeza mchango wa mazao ya misitu katika Pato la Taifa kutoka asilimia 3 hadi asilimia 4 na mauzo nje kufikia dola za Marekani milioni 150 – 200 ifikapo Juni 2031, kuongezeka kwa uzalishaji wa asali na mazao ya nyuki kitaifa kwa asilimia 50 ya kiwango cha sasa ifikapo Juni 2031, kuongeza uwekezaji unaoongozwa na sekta binafsi katika mnyororo wa thamani wa ufugaji nyuki kwa asilimia 50 ya kiwango cha sasa na kuanzisha angalau shughuli 5 kubwa za ufugaji nyuki zinazolenga mauzo ya nje ifikapo Juni 2031. Aidha, viashiria na shabaha za sekta ya Maliasili kwa mwaka 2026/27 ni kama vilivyoainishwa katika **Jedwali Na. 4.10** na orodha ya miradi itakayotekelezwa kulingana na vipaumbele imeainishwa katika **Kiambatisho Na. 2.**

**Jedwali Na. 4.10 : Viashiria na Shabaha katika eneo la Misitu**

| No. | Kiashiria | Mwaka wa Kizio | Shabaha 2026/27 | Shabaha 2030/31 |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Kuongezeka kwa eneo la mashamba ya miti ya jamii, misitu na vitalu vya miti | 190 (2023/24) | 203 | 253 |
| 2. | Asilimia ya rasilimali za kipaumbele za kijenetiki za mimea, wanyama na misitu zimehifadhiwa ipasavyo | 30 (2022) | 34 | 50% |

***Chanzo:*** Wizara ya Maliasili na Utalii

### 4.2.2.4.2 Sekta ya Uzalishaji Bidhaa Viwandani

Sekta ya Viwanda itaendelea kutekeleza miradi ya kipumbele inayolenga kuifanya sekta ya Viwanda Kuwa na misingi ya uchumi wa viwanda shindani, yenye kuleta mapinduzi, endelevu na maendeleo jumuishi huku ikidumisha na kuimarisha minyororo ya thamani ya ndani. Aidha, sekta ya viwanda inalenga: kuwezesha Tanzania kuwa kitovu cha uzalishaji viwandani katika kanda ya Afrika; kuimarisha sekta ya biashara yenye ushindani wa kimataifa, sekta ya biashara ya kidijitali; kuongeza mauzo ya nje; kukuza ukuaji jumuishi wa viwanda vidogo na vya kati na kuimarisha ushirikiano na masoko muhimu ya kikanda na kimataifa; kuongeza uwekezaji binafsi unaochochea ubunifu; kukuza ushindani na ujumuishaji

unaoshughulikia mahitaji ya ndani na kuunganisha Tanzania katika minyororo ya thamani ya kimataifa ili kusaidia ukuaji endelevu wa uchumi. Vilevile, Serikali itaimarisha matumizi ya rasilimali za ndani na kukuza uchumi jumuishi unaolenga biashara ndogo ndogo, na za kati.

Utekelezaji wa malengo haya utakaofanyika kupitia miradi ya maendeleo utapelekea Tanzania kuwa miongoni mwa nchi bora duniani kulingana na Farihisi ya Benki ya Dunia cha Urahisi wa Kufanya Biashara; kuongezeka kwa wigo wa mauzo ya nje yatokanayo na kanda za uzalishaji bidhaa za kuuza nje na maeneo maalumu ya uwekezaji; ongezeko la thamani katika uzalishaji (MVA) kwa biashara ndogo ndogo na za kati; na kuongezeka kwa biashara ya kidijitali. Aidha, viashiria na shabaha za sekta ya Viwanda na Biashara kwa mwaka 2026/27 vimeainishwa katika **Jedwali Na. 4.11** na orodha ya miradi itakayotekelezwa kulingana na vipaumbele imeainishwa katika **Kiambatisho Na. 2**

**Jedwali Na. 4.11: Viashiria na Shabaha katika Sekta ya Uzalishaji bidhaa viwandani**

| Na. | Kiashiria | Mwaka wa Kizio | Shabaha( 2026/27) | Shabaha (2030/31) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Mchango katika Pato la Taifa (Kwa bei za sasa) (%) | 30.4 (2024) | 31.62 | 36.50 |
| 2. | Ukuaji halisi wa Pato la Taifa wa sekta ya viwanda kwa ujumla | 5.5 (2024) | 6 | 8 |
| 3. | Mchango wa Uzalishaji Viwandani kwa Pato la Taifa (%) | 7.3 (2024) | 7.44 | 8 |
| 4. | Kiwango cha ukuaji wa Uzalishaji Viwandani | 4.8 (2024) | 5.82 | 9.90 |
| 5. | Sehemu ya mapato ya mauzo ya nje ya bidhaa zinazotokana na viwanda katika jumla ya mapato ya mauzo ya nje ya bidhaa | 22 (2024) | 23.6 | 30 |
| 6. | Sehemu ya mapato ya mauzo ya nje ya viwanda katika jumla ya mapato ya mauzo ya nje | 9 (2024) | 10.2 | 15 |
| 7. | Thamani ya mauzo ya nje kama sehemu ya asilimia ya Pato la Taifa. | 17 (2023) | 18.6 | 25 |
| 8. | Mchango wa Tanzania katika biashara ya ndani ya Afrika | 13 (2023) | 15.4 | 25 |
| 9. | Asilimia ya biashara ndogo, ndogo za kati na za kati zinazotumia majukwaa ya biashara mtandaoni | 15 (2023) | 24 | 60 |
| 10. | Mchango wa sekta ya Viwanda katika Ajira zote | 9 (2024) | 10.2 | 15% |
| 11. | Mchango wa Uzalishaji Viwandani katika Ajira zote | 6 (2024) | 6.8 | 10% |

***Chanzo:*** Wizara ya Viwanda na Biashara

#### 4.2.2.4.3 Sekta ya Ujenzi

Sekta ya Ujenzi itaendelea kutekeleza miradi ya kipaumbele inayolenga kuifanya sekta kuwa endelevu, jumuishi na shindani kikanda, inayoongozwa na wakandarasi wa ndani, itakayochochea ukuaji wa uchumi, kuendeleza ubiasharishaji, kuboresha

viwango vya maisha, pamoja na kuhimiza maendeleo ya teknolojia na ubunifu nchini. Aidha, sekta ya ujenzi inatarajia kuongeza thamani ya hisa za wakandarasi wa ndani wanaoshiriki katika miradi mikubwa ya ujenzi hadi kufikia asilimia 50, kuongeza utekelezaji wa miradi mikubwa ya ujenzi kupitia Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP) kwa kushirikiana na wakandarasi wa ndani kwa asilimia 60 pamoja na kuhakikisha kampuni za ujenzi za ndani zinatumia teknolojia za kisasa na mbinu endelevu katika miradi mikubwa angalau kwa asilimia 50. Vilevile, Sekta ya Ujenzi inalenga kuhakikisha asilimia 80 ya kazi za kitaalamu na zenye ujuzi zinafanyika na wakandarasi wa ndani ambao watajumuisha miundo yenye ufanisi wa matumizi ya nishati na mbinu rafiki kwa mazingira katika utekelezaji wa miradi.

Vile vile, Sekta ya Ujenzi itaendelea kutekeleza miradi ya kipaumble inayolenga kuimarisha ufanisi na uunganishaji wa miundombinu ya usafiri na usafirishaji kwa kuboresha usafirishaji wa watu, bidhaa na rasilimali ndani ya miji na mikoa ili kuchochea ukuaji endelevu wa uchumi, maendeleo ya viwanda na upatikanaji wa masoko ya kimataifa. Aidha, Serikali inatarajia kuanzisha mfumo jumuishi, endelevu na wa kisasa wa miundombinu ya barabara kwa kuasili viwango vya usanifu vinavyostahimili mabadiliko ya tabianchi na kutumia teknolojia za kidijitali kama AI na GIS katika matengenezo ya barabara, pamoja na kufunga taa za barabarani zinazotumia nishati ya jua na mifumo ya kisasa ya usimamizi wa vyombo vya usafiri. Sekta ya Ujenzi inatarajia kuongeza uwiano wa barabara za lami kutoka asilimia 8.6 hadi asilimia 10.58, ukarabati na matengenezo ya barabara za mikoa na *feeder roads* zinazounganisha maeneo ya kilimo, madini na viwanda, kuongeza mtandao wa Usafiri wa Mabasi Yaendayo Haraka (BRT), kujenga barabara za mchepuo ili kupunguza msongamano wa magari katika miji na majiji na kuboresha barabara za mipakani zinazounganisha Tanzania na nchi jirani za EAC na SADC ili kukuza biashara ya kikanda.

Matokeo ya utekelezaji wa malengo haya yanatarajiwa kuifanya Sekta ya Ujenzi kuwa endelevu, jumuishi na shindani kikanda, huku ikiimarisha nafasi ya wakandarasi wa ndani katika uchumi wa taifa. Vilevile, utekelezaji wa malengo haya unalenga kuwajengea uwezo wa kiufundi, kifedha na kiusimamizi wakandarasi wa ndani ili waweze kushindana kikamilifu katika zabuni za miradi mikubwa na ya kimkakati katika kukuza Uchumi wa nchi kwa kuongeza mzunguko wa fedha ndani ya taifa pamoja na kuchangia ongezeko la thamani ya hisa za makandarasi wa ndani katika miradi yote inayotekelezwa.

Vilevile, utekelezaji wa malengo husika utaifanya Sekta ya Ujenzi kuwa na ufanisi katika usafirishaji wa watu, bidhaa na huduma kati ya miji na vijiji, hali inayochochea ukuaji wa uchumi na kuongeza tija katika sekta za kilimo, viwanda na biashara. Aidha, uboreshaji wa usafiri wa barabara utapunguza muda wa safari na gharama za usafirishaji, hivyo kuongeza ushindani wa bidhaa katika masoko ya ndani na nje ya nchi pamoja na kuboresha viwango vya maisha vya wananchi.

Aidha, viashiria na shabaha za Sekta ya Ujenzi kwa mwaka 2026/27 ni kama vilivyoainishwa katika **Jedwali Na. 4.12** na orodha ya miradi itakayotekelezwa kulingana na vipaumbele imeainishwa katika **Kiambatisho Na. 2.**

**Jedwali Na. 4.12 : Viashiria na Shabaha katika Sekta ya Ujenzi**

| Na. | Kiashiria | Mwaka wa Kizio | Shabaha (2026/27) | Shabaha (2030/31) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Tasnia ya Ujenzi katika pato la Taifa % | 12.8 (2024) | 13.34 | 15.50 |
| 2. | Mchango wa Tasnia ya Ujenzi katika Ukuaji wa Pato la Taifa (%) | 4.1 (2024) | 4.98 | 8.50 |
| 3. | Mchango wa Kampuni za Ndani katika soko la Ujenzi (%) | 40 (2023) | 42 | 50 |
| 4. | Idadi ya Ajira zilizozalishwa katika miradi ya Ujenzi | 21,527 (2024 | 21,800 | 22,100 |
| 5. | Ongezeko la Mtandao wa Barabara za Kitaifa (km) | 37,435 (2024) | 37,734.41 | 38,800.00 |

***Chanzo:*** Wizara ya Ujenzi

#### 4.2.2.4.4 Sekta ya Madini na Uchimbaji wa Mawe

**i. Madini na Uchimbaji wa Mawe**

Sekta ya Madini itaendelea kutekeleza miradi ya kipaumbele inayolenga kuifanya sekta kuwa shindani, jumuishi na inayochochea maendeleo ya viwanda kwa kutumia rasilimali za madini kwa ufanisi, sambamba na kuimarisha mnyororo wa thamani ndani ya nchi. Katika kufikia azma hiyo, juhudi zitaelekezwa katika kuongeza uanzishaji wa miradi mipya ya uchimbaji wa madini pamoja na kufufua miradi ya utafiti na uchimbaji iliyokwama. Serikali itaendelea kuweka mazingira wezeshi na kurahisisha taratibu za uwekezaji kwa wawekezaji wa ndani na wa nje katika shughuli za utafiti na uendelezaji wa madini. Vilevile, msukumo utawekwa katika kuhamasisha uwekezaji kwenye uchenjuaji, uchakataji, usafishaji na uchimbaji wa madini ya viwandani na madini muhimu (critical minerals) ili kuchochea ukuaji wa viwanda na uchumi kwa ujumla. Aidha, jitihada zitaelekezwa katika kuongeza uzalishaji na mauzo ya nje ya dhahabu na vito vya thamani, pamoja na kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha biashara ya madini ya vito barani Afrika.

Utekelezaji wa vipaumbele hivi unatarajiwa kuongeza upatikanaji wa wataalamu wenye ujuzi unaoendana na uongezaji thamani wa madini na uchumi wa viwanda, kuboresha ufanisi katika usimamizi wa sekta ya madini, na kuongeza ushiriki wa wanawake, vijana na watu wenye mahitaji maalum katika shughuli za uchimbaji mkubwa. Pia utaongeza upatikanaji wa huduma za ramani za kijiolojia, kijiofizikia na kijiokemia; kukuza ubia kati ya Serikali na sekta binafsi katika migodi yenye tija; na kuongeza idadi ya miradi ya kimkakati ya uchimbaji na uchenjuaji wa madini. Aidha, mchango wa madini ya viwandani na madini muhimu utaongezeka kupitia uongezaji thamani na uzalishaji wa viwandani, wakati uzalishaji na mauzo ya nje ya dhahabu na vito utaimarishwa kupitia ushirikishwaji wa wachimbaji wakubwa na wadogo (SSM), ikiwemo urasimishaji wa shughuli zao na uboreshaji wa upatikanaji wa mitaji.

Vilevile, utekelezaji wa mikakati hii utaongeza mchango wa sekta ya madini katika mapato ya fedha za kigeni, kuimarisha ushindani na udhibiti wa biashara ya madini ya vito kupitia mifumo madhubuti ya kisheria, na kuongeza urasimishaji wa biashara hizo. Maendeleo ya miundombinu ya uongezaji thamani wa madini ya vito kupitia ukataji, ung'arishaji na uthaminishaji yatawezesha kuongeza thamani ya mauzo ya vito kabla ya kuuzwa nje ya nchi, sambamba na kuanzishwa kwa Kituo cha Biashara ya Madini ya Vito nchini.

Aidha, viashiria na shabaha za Sekta ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 vimeainishwa katika **Jedwali Na. 4.13,** na orodha ya miradi itakayotekelezwa kulingana na vipaumbele imewasilishwa katika **Kiambatisho Na. 2**

**Jedwali Na. 4.13 :Vishiria na Shabaha katika Sekta ya Madini**

| Na. | Kiashiria | Mwaka wa Kizio | Shabaha (2026/27) | Shabaha (2030/31) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Mchango katika Pato la Taifa (%) | 10.1 (2024) | 10.58 | 12.5% |
| 2. | Mchango katika ukuaji wa Pato la taifa (%) | 8.3 (2024) | 8.44 | 9% |
| 3. | Mauzo nje (asilimia mapato katika mauzo jumla ya nje )(%) | 46 (2024) | 47.8 | 55% |
| 4. | Mauzo nje ya madini (asilimia ya mapato yatokanayo na uuzaji wa bidhaa nje (%) | 55 (2024) | 56 | 60% |

***Chanzo:*** Wizara ya Madini

#### 4.2.2.4.5 Sekta ya Utalii

Sekta ya Utalii itaendelea kufungamanisha vivutio vya utalii na kuboresha vyuo vya utalii na ukarimu ili kuongeza idadi ya watoa huduma wenye weledi kwenye fani zote za utalii na ukarimu kwa kutekeleza miradi ya kipaumbele. Vile vile, kuimarisha shughuli, bidhaa, mbinu na uzoefu wa utalii ili kukuza uendelevu, ujumuishi na uimara, sambamba na kupanua fursa za ushiriki kwa jamii za wenyeji na kuhakikisha ukuaji wa muda mrefu wa sekta.

Utekelezaji wa malengo haya utakaofanyika kupitia miradi ya maendeleo ambao utawezesha kuboresha nafasi ya Tanzania katika Usafiri na fahirisi ya maendeleo ya utalii (Travel and Tourism Development Index ) kutoka nafasi ya 81 hadi 60 kati ya nchi 119 duniani ifikapo Juni 2031, kuendelea kwa Maeneo manne (4) maalum ya kiuchumi ya utalii (Tourism SEZs) na kuanza kufanya kazi ifikapo Juni 2031, kuongezeka kwa Ushiriki wa wazawa (local content) katika sekta ya utalii hadi kufikia asilimia 10 ifikapo Juni 2031, kuongezeka zaidi ya asilimia 12 ya maeneo ya vivutio vya utalii yaliyohifadhiwa na kuunganishwa kufikia Juni 2031, kuimarika angalau asilimia 40 ya biashara za utalii wa kidijitali ifikapo Juni 2031, kufikia kiwango cha matumizi ya mfumo jumuishi wa utalii wa kisasa (smart tourism ecosystem) nchini kwa asilimia 33, unaoendeshwa na majukwaa ya kidijitali, miundombinu na uboreshaji wa matumizi ya rasilimali kwa kutumia teknolojia za kidijitali kufikia Juni 2031 na kuifanya Tanzania kuwa kituo kikuu cha utalii wa matukio, utamaduni, na ikolojia kufikia Juni 2031. Aidha, viashiria na shabaha za sekta ya Utalii kwa mwaka 2026/27 ni kama

vilivyoainishwa katika **Jedwali Na. 4.14** na orodha ya miradi itakayotekelezwa kulingana na vipaumbele imeainishwa katika **Kiambatisho Na. 2**

**Jedwali Na. 4.14: Viashiria na Shabaha katika Sekta ya Utalii**

| No. | Kiashiria | Mwaka wa Kizio | Shabaha 2026/27 | Shabaha 2030/31 |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Kiwango cha Kimataifa cha Maendeleo ya Sekta ya Usafiri na Utalii | 81/119 (2021) | 78/119 | 60/119 |
| 2. | Mapato ya Mauzo ya Nje yatokanayo na Utalii (In Billion USD) | 373.8 (2023) | 300 | 4.81 |
| 3. | Mapato ya Mauzo ya Nje yatokanayo na Utalii (% ya jumla ya mapato ya mauzo ya nje) | 27 (2024) | 28.6 | 35 |
| 4. | Asilimia ya mchango wa huduma za Malazi kwa watalii katika Pato la Taifa (GDP) | 1.1 (2024) | 1.16 | 1.40% |
| 5. | Mchango wa huduma ya Malazi katika Ukuaji wa Pato la Taifa | 6 (2024) | 6.54 | 8.70% |

***Chanzo:*** Wizara ya Maliasili na Utalii

#### 4.2.2.4.6 Sekta ya Michezo na Ubunifu

Sekta ya Habari, Utamaduni, Sanaa, na Michezo itaendelea kutekeleza miradi ya kipaumbele inayolenga kuifanya sekta kuimarisha ushindani wa ndani, kikanda na kimataifa wa tasnia ya michezo na ubunifu, kukuza ukuaji, na fursa za uwekezaji.

Utekelezaji wa malengo haya utakaofanyika kupitia miradi ya maendeleo utapelekea ukuaji wa sekta ya Michezo na ubunifu, kwa kuendelea kuboresha miundombinu ya michezo kote nchini kwa kuzingatia viwango vya mashirikisho ya kimataifa; kuvutia watalii zaidi wa michezo kwa kuanzisha mfumo/utaratibu wa biashara ya michezo ili kukuza utalii wa michezo, ikiwa ni pamoja na kuanzisha mfumo/utaratibu wa biashara ya michezo ili kukuza utalii wa michezo; kutambulisha wasanii wa Tanzania kimataifa katika angalau nyanja moja kuu ya ubunifu , kwa kujenga mfumo endelevu wa utengenezaji wa filamu, usambazaji na kurekodi muziki na kuanzisha majukwaa ya kikanda kwa wasanii wa Tanzania kuonesha kazi zao za ndani na nje ya nchi; na kuwezesha wasanii kupokea mirahaba kwa kazi zao kupitia mashirika ya wabunifu na michezo ambapo Mifumo ya Hakimiliki na Hatimiliki (IP) itaimarishwa na kuanzisha mfumo bora wa usajili wa hakimiliki na Hatimiliki ili kulinda wasanii wa ndani dhidi ya matumizi yasiyoidhinishwa na uharamia.

Viashiria na shabaha za sekta ya Habari, Utamaduni, Sanaa, na Michezo kwa mwaka 2026/27 ni kama vilivyoainishwa katika **Jedwali 4.15** na orodha ya miradi itakayotekelezwa kulingana na vipaumbele imeainishwa katika **Kiambatisho Na.2**

**Jedwali Na. 4.15: Viashriia na Shabaha katika Sekta ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo**

| Na. | Kiashiria | Mwaka wa Kizio | Shabaha (2026/27) | Shabaha (2030/31) |
|---|---|---|---|---|

| Na. | Kiashiria | Mwaka wa Kizio | Shabaha (2026/27) | Shabaha (2030/31) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Nafasi ya Tanzania katika Viwango vya FIFA – Wanaume | 112 (2025) | 50 Bora | 80 Bora |
| 2. | Nafasi ya Tanzania katika Viwango vya FIFA – Wanawake | 145 (2025) | 40 Bora | 100 Bora |
| 3. | Nafasi ya Tanzania katika Viwango vya CAF – Wanaume | 25 (2025) | 5 Bora | 15 Bora |
| 4. | Nafasi ya Tanzania katika Viwango vya CAF – Wanawake | 30 (2025) | 10 Bora | 20 Bora |
| 5. | Idadi ya Wachezaji Wanaoshiriki Michezo ya Kitaalamu – Wanaume | 1,200 (2025) | 1,560 | ≥3,000 |
| 6. | Idadi ya Wachezaji Wanaoshiriki Michezo ya Kitaalamu – Wanawake | 250 (2025) | 400 | 1,000 |
| 7. | Idadi ya Wasanii wa Muziki wa Tanzania Wanaopokea Tuzo za Kimataifa | 17 (2024/25) | 20 | ≥15 |
| 8. | Idadi ya Wadau wa Filamu Wanaopokea Tuzo za Kimataifa | 86 (2024) | 95 | 133 |
| 9. | Miradi ya Filamu Iliyopokea Mikopo | 137 (2025) | 183 | 321 |
| 10. | Sekta za Ubunifu na Maudhui ya Kidijitali | 1,211 (2025) | 1,500 | 3,000 |
| 11. | Sehemu ya Maudhui Yanayopatikana Kupitia Majukwaa ya Kidijitali ya Kimataifa (%) | <20 (2024) | — | ≥10% |
| 12. | Asilimia ya Wasanii na Mashirika ya Michezo Yanayopokea Mirabaha (%) | <20% (2024) | 35% | ≥45% |

***Chanzo:*** Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo

#### 4.2.2.4.7 Sekta ya Uwekezaji na Biashara

**i. Sekta ya Uwekezaji**

Sekta ya uwekezaji itaendelea kutekeleza miradi ya kipaumbele inayolenga kuifanya sekta ya uwekezaji kuwa shindani, jumuishi, na yenye tija ya hali ya juu ikitumia maeneo maalum ya kiuchumi (SEZs) kuvutia uwekezaji unaoweza kuhimili mabadiliko ya soko la kimataifa kwa Kukuza Mauzo ya Nje, Kuboresha Mazingira ya Biashara, ikuvutia Uwekezaji wa Moja kwa Moja wa Kigeni (FDI), Uzalishaji wa Ajira za Uhakika na Uhawilishaji wa Teknolojia na Ujuzi huku ikitoa kipaumbele kwa maendeleo ya sekta za kimkakati (k.m., usindikaji wa mazao ya kilimo, nishati) kwa ajili ya mabadiliko ya kimuundo na mwelekeo wa mauzo ya nje, kujadiliana na kuanzisha ushirikiano wa uwekezaji wa nchi na nchi, kikanda na wa kimataifa katika sekta muhimu za kimkakati, kuanzisha vituo vya kitaifa vya ubunifu kwa ajili ya vijana vinavyotoa malezi, ufadhili na maeneo ya kufanyia kazi, kuendeleza maeneo maalum ya kiuchumi, Kutoa vivutio maalum vya kifedha na visivyo vya kifedha ili kuvutia na kushikilia uwekezaji katika sekta zenye thamani ya juu kama vile: teknolojia, viwanda vya dawa, na viwanda vinavyotumia teknolojia ya juu, kuanzisha benki ya kitaifa ya ardhi kwa ajili ya kusimamia na kutenga ardhi kwa matumizi ya kongani za viwanda,

SEZs na shoroba kubwa za usafirishaji,uhakiki wa kina wa kanuni za biashara ili kuboresha urahisi wa kufanya biashara, kuanzisha mwongozo mahsusi unaozingatia vigezo vya kutoa motisha iliyopangwa kwa uwekezaji wa kimkakati na makampuni chipukizi ya teknolojia ya juu.

Utekelezaji wa malengo haya utakaofanyika kupitia miradi ya maendeleo utapelekea: kuongezeka kwa uwekezaji wa mtaji na uwekezaji binafsi kwa kampuni chipukizi; kuanzishwa kwa mashirikiano ya uwekezaji kati ya nchi na nchi, kikanda na kimataifa kwa lengo la kuvutia uwekezaji kutoka nje (FDI's) katika sekta muhim; na kuongezeka kwa uwekezaji katika Maeneo Maalum ya Kiuchumi (SEZs). Aidha, viashiria na shabaha za sekta ya uwekezaji kwa mwaka 2026/27 ni kama vilivyoainishwa katika **Jedwali 4.16** na orodha ya miradi itakayotekelezwa kulingana na vipaumbele imeainishwa katika **Kiambatisho Na.2**.

**Jedwali Na. 4.16: Viashiria na Shabaha katika Sekta ya Uwekezaji**

| Na. | Viashiria | Mwaka wa Kizio | Shabaha (2026/27) | Shabaha( 2030/31) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Uwekezaji wa Moja kwa moja (dola za Marekani “Milioni) | 1,717.6 (2024) | 3,047.34 | 8,366.28 |
| 2. | Idadi ya ajira zitakazozalishwa kupitia shughuli za uwekezaji | 969 | 1,100 | 5,700 |
| 3. | Sehemu ya kilimo katika ajira zote (%) | 46 | 54 | 50% |
| 4. | Sehemu ya sekta ya viwanda katika ajira zote (%) | 18 | 20 | 20% |
| 5. | Sehemu ya sekta ya ujenzi katika ajira zote (%) | 25 | 25 | 25% |

***Chanzo:*** Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji

### ii. Uwekezaji wa Mashirika ya Umma

Serikali inaendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ya kuimarisha usimamizi wa taasisi na mashirika ya umma ili kuongeza tija katika uwekezaji wa Serikali, hususan kwenye miradi ya maendeleo. Mikakati hiyo inajumuisha kufanya maboresho ya Sheria ya Msajili wa Hazina ili kuimarisha uwezo katika kusimamia utendaji na ufanisi wa taasisi za umma, kuingia mikataba ya utendaji kazi na Bodi za Wakurugenzi, kufanya tathmini ya mwaka ya utendaji wa Bodi hizo, kufanya uhakiki wa utendaji katika taasisi na mashirika ya umma, kuendeleza ujenzi wa Mfumo wa Usimamizi wa Uwekezaji wa Umma (Public Investment Management System – PIMS) utakaochangia kuongeza ufanisi katika usimamizi wa uwekezaji wa Serikali kwenye taasisi na mashirika ya umma, kuwajengea uwezo Wajumbe wa Bodi za Wakurugenzi ili kuimarisha uwezo wao katika usimamizi wa Taasisi pamoja na kuandaa jukwaa linalowakutanisha Wenyeviti wa Bodi na Wakurugenzi wa Taasisi na Mashirika ya Umma kwa lengo la kujadili na kuweka mikakati ya kuimarisha usimamizi na utendaji wa mashirika ya umma. Aidha, mashirika ya umma yanayojiendesha kibiashara yanatarajiwa kuwekeza kiasi cha shilingi trilioni 5.5 kutokana na vyanzo vyake vya mapato, faida, na mikopo inayopatikana kwa kutumia mizania za mashirika.

### iii. Mazingira Wezeshi ya Biashara

Katika mwaka wa fedha 2026/27, Serikali itaendelea kuimarisha Mazingira Wezeshi ya Biashara kupitia utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Kuboresha Mazingira ya Biashara (MKUMBI II), unaolenga kuondoa vikwazo vya kisheria, kiutawala na kimfumo vinavyoathiri uwekezaji na ukuaji wa sekta binafsi. Kupitia MKUMBI II, tunatarajia kusimamia kwa karibu utekelezaji wa maboresho katika sekta zote za kipaumbele, kuandaa na kuratibu kutungwa kwa Sheria ya Uwezeshaji wa Mazingira ya Biashara na Uwekezaji (Business Facilitation Act), pamoja na kufanya mapitio ya sheria na kanuni za kisekta ili kupunguza urasimu, gharama na muda unaohitajika kupata vibali na leseni. Aidha, tunakusudia kuanzisha Mfumo wa Kitaifa wa Upimaji wa Hali ya Mazingira ya Biashara na Uwekezaji ili kupima utendaji, ushindani na ufanisi wa taasisi za udhibiti, sambamba na kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa vibali, leseni, usajili na huduma za ukaguzi, kwa lengo la kuongeza uwazi, uwajibikaji na urahisi wa kufanya biashara.

Vilevile, tutaendelea kujenga uwezo wa Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, hususan Idara za Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa kuzipatia vitendea kazi kama komputa ili ziwe na uwezo wa kutoa huduma za haraka, zenye uwazi na urahisi, kusaidia wawekezaji na wafanyabiashara kufanikisha uwekezaji, kupata vibali na leseni, na kushirikiana kwa ufanisi na sekta binafsi. Viashiria na shabaha za Mazingira Wezeshi ya Biashara uwekezaji kwa mwaka 2026/27 ni kama vilivyoainishwa katika **Jedwali 4:17** hapo chini.

**Jedwali Na. 4.17: Viashiria na Shabaha katika Mazingira Wezeshi ya Biashara**

| Na. | Viashiria | Mwaka wa Kizio (2024) | Shabaha (2026/27) | Shabaha (2030/31) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Nafasi ya Tanzania katika Business Enabling Environment (EAC) | Nafasi ya 4 EAC | Ndani ya Nafasi 2 Bora EAC | Ndani ya Nafasi 1 Bora EAC |
| 3. | Jumla ya sheria na kanuni za biashara zilizofanyiwa maboresho ili kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji | 55 | ≥ Sheria 66 | ≥ Sheria 100 |
| 4. | Jumla ya tozo/ada kandamizi zilizofutwa au kupunguzwa | 374 | ≥700 | ≥900 |
| 5. | Asilimia ya huduma za usajili na leseni zilizo kidijitali | 50% | ≥70% | 95% |
| 6. | Wastani wa muda wa kuanzisha biashara (siku) | Siku 7 | ≤4 siku | Siku 1 |
| 7. | Idadi ya mikoa yenye mifumo ya kidijitali ya kurahisisha biashara | 5 mikoa | ≥20 mikoa | Mikoa yote 31 |

**Chanzo:** Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji

#### 4.2.2.4.8 Sekta binafsi

Kwa kuzingatia mwelekeo wa Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Miatano wenye kaulimbiu ya *"Mageuzi ya Kukuza Uchumi Jumuishi na Uzalishaji AJira"*, Mwaka 2026/27, Serikali itaweka mkazo mahsusi katika kuifanya sekta binafsi

kuwa mhimili mkuu wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kichocheo cha mageuzi ya kiuchumi.

Katika kipindi hiki, Serikali itaendelea kuzihimiza na kuzitaka Taasisi za Umma kubuni na kutekeleza miradi mikubwa ya kimkakati kwa kushirikiana na sekta binafsi kupitia utaratibu wa Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP). Ushirikiano huu utalenga kuongeza kasi ya uwekezaji, kuimarisha ubora wa utekelezaji wa miradi, kupunguza mzigo wa kifedha kwa Serikali, na kuleta ubunifu na ufanisi katika utoaji wa huduma kwa wananchi.

#### 4.2.2.4.9 Uhusiano wa Kimataifa na Diplomasia ya Uchumi

Serikali kupitia sekta ya uhusiano wa kimataifa na diplomasia ya uchumi itaendelea kuimarisha na kuendeleza ushirikiano na nchi mbalimbali na mashirika ya kimataifa ili kukuza fursa za kidiplomasia na kiuchumi. Serikali italinda maslahi ya kiuchumi kupitia utekelezaji thabiti wa diplomasia ya uchumi katika balozi za Tanzania nje na kuongeza uwezo wa majadiliano na ushawishi wa Tanzania kwenye ushirikiano wake na mahusiano ya pande mbili, kikanda na kimataifa. Vilevile, itaimarisha nafasi ya Tanzania kuwa kitovu cha shughuli za kiuchumi hususan katika biashara za kimkakati na uwekezaji kwa kuitangaza kwenye majukwaa ya kikanda na kimataifa.

Utekelezaji wa malengo haya utakaofanyika kupitia utekelezaji thabiti wa diplomasia ya uchumi katika balozi za Tanzania nje katika kukuza uwekezaji nchini kwa asilimia 40; Tanzania kujumuishwa kikamilifu kwenye AfCFTA, EAC na SADC na kufikia angalau asilimia 70 ya utekelezaji wa itifaki za biashara za kikanda; kuifanya Tanzania kuwa lango kuu la biashara barani Afrika kupitia bandari za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara kwa kufikia Twenty - Foot Equivalent Units (TEUs) milioni 20 za makontena; na kuvutia uwekezaji kutoka nje (FDI's) katika sekta muhimu.

Utekelezaji huo utakuza diplomasia ya utamaduni ikiwa ni pamoja na kuongeza matumizi ya Lugha ya Kiswahili katika mashirika ya kimataifa na kuifanya kuwa Lugha ya kazi katika angalau taasisi moja ya kimataifa iliyoendelea na kuwezesha huduma za kukitafsiri kwa wakati halisi kupitia teknolojia ya akili mnemba (AI) kwenye mikutano na nyaraka muhimu za AU na UN. Vilevile, kupitia utekelezaji wa malengo hayo utawezesha ushirikiano wa taasisi za elimu ya juu 35 – 40 za Tanzania na za nchi nyingine. Aidha, viashiria na shabaha za sekta ya uhusiano wa kimataifa na diplomasia ya uchumi ni kama vilivyoainishwa katika **Jedwali Na. 4.18** na orodha ya miradi itakayotekelezwa kulingana na vipaumbele imeainishwa katika **Kiambatisho Na. 2**

**Jedwali Na. 4.18: Viashiria na Shabaha katika sekta ya Uhusiano wa Kimataifa na Diplomasia ya Uchumi**

| Na. | Kiashiria | Mwaka wa Kizio | Shabaha (2026/27) | Shabaha (2030/31) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Idadi ya mikutano ya uwili, kikanda na kimataifa ambayo Tanzania inashiriki | 110 (2024/25) | 115 | 595 |
| 2. | Idadi ya Hati za Makubaliano | 84 (2024/25) | 80 | 500 |

| Na. | Kiashiria | Mwaka wa Kizio | Shabaha (2026/27) | Shabaha (2030/31) |
|---|---|---|---|---|
| | zilizosainiwa kati ya Tanzania na nchi mbalimbali | | | |
| 3. | Idadi ya mikutano ya ujirani mwema iliyofanyika | 48 (2024/25) | 45 | 250 |
| 4. | Idadi ya taasisi za kitaifa na kikanda zinazofundisha rasmi Lugha ya Kiswahili | 100 (2024/25) | 100 | 240 |
| 5. | Idadi ya viwanja vya Serikali kwenye maeneo ya kimkakati nje vilivyoendelezwa | 1 (2024/25) | 3 | 15 |

***Chanzo:*** Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki

### 4.2.3 Kujenga Uwezo wa Watu na Maendeleo ya Jamii.

Eneo hili limetoa kipaumbele katika katika maeneo sita (6) ambayo ni: Jamii iliyoelimika, yenye Ujuzi na inayopenda kujifunza; nguvu kazi yenye ari na uwezo wa kufanya kazi; ajira na soko la ajira; jamii jumuishi na inayolindwa; afya bora kwa wote; na Upatikanaji na Uunganishwaji wa huduma za maji safi na Usafi wa Mazingira. Hivyo, mikakati, shabaha, afua, viashiria muhimu vya upimaji wa utendaji, miradi na programu za maendeleo katika maeneo hayo ni kama ifuatavyo:

#### 4.2.3.1 Jamii Iliyoelimika, yenye Ujuzi na inayopenda Kujifunza

Sekta ya Elimu itaendelea kujenga rasilimali watu yenye maarifa, ujuzi, stadi, motisha na maadili ili kuchochea maendeleo endelevu ya Taifa, sambamba na kuimarisha mfumo wa utafiti, ubunifu pamoja na kuongeza matumizi ya TEHAMA na teknolojia za kidijitali katika ufundishaji na ujifunzaji. Katika kutekeleza azma hii, sekta itaendelea kusimamia utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 (Toleo la 2023) kwa kukamilisha na kuimarisha Mfumo wa Taifa wa Mitaala na Mfumo wa Taifa wa Upimaji na Tathmini, kuboresha ubora katika ngazi zote za elimu, na kuimarisha utekelezaji wa Elimu ya Amali, elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi (TVET), pamoja na elimu ya juu yenye mwelekeo wa ujuzi unaoendana na mahitaji ya ajira na soko la kazi.

Aidha, sekta itaongeza upatikanaji w a fursa ya elimu kwa kuendelea na uboreshaji wa miundombinu ya kielimu, kuhakikisha upatikanaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa uwiano unaofaa na kuimarisha mafunzo kazini na tarajali kwa walimu na wakufunzi. Vilevile, Sekta ya elimu itaendelea kuongeza fursa za mikopo na ufadhili kwa wanafunzi, kuimarisha programu za Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati (STEM), pamoja na kukuza taaluma za Akili Unde (AI) na Sayansi ya Takwimu. Halikadhalika, sekta itaendelea na uendelezaji wa masuala ya utafiti, ubunifu na ushirikiano wa kimataifa ili kuongeza ushindani wa Taifa na kuchochea ukuaji wa uchumi jumuishi unaotegemea maarifa na teknolojia.

Kupitia utekelezaji wa malengo yaliyowekwa, sekta ya elimu itachangia kuimarika kwa uwezo wa watu na maendeleo ya jamii kwa kuongeza upatikanaji na ukamilishaji wa

elimu bora na jumuishi katika ngazi zote, pamoja na kuimarisha usawa wa kijinsia. Maboresho ya mitaala, mafunzo ya walimu na matumizi ya TEHAMA yataongeza ubora wa ujifunzaji na mwendelezo wa wanafunzi kwenda elimu ya juu, huku yakikuza nguvu kazi yenye ujuzi wa kidijitali, kiteknolojia na kitaalamu. Kuimarishwa kwa elimu ya ufundi na uhusiano wake na sekta za uzalishaji kutasaidia kukuza ujuzi wa viwandani, ubunifu na ajira zenye staha kwa vijana. Aidha, uendelezaji wa utafiti na ubunifu utaimarisha matumizi ya tafiti katika maamuzi ya kimkakati, kukuza vituo vya ubunifu na ushirikiano wa kimataifa, na kuweka mazingira wezeshi kwa *startups* na maendeleo ya teknolojia za hali ya juu. Viashiria na shabaha za sekta kwa mwaka wa fedha 2026/27 zimeainishwa katika **Jedwali Na. 4.19**, na orodha ya miradi itakayotekelezwa imeoneshwa katika **Kiambatisho Na. 2**.

**Jedwali Na. 4.19: Viashiria na Shabaha katika Sekta ya Elimu**

| Na. | Kiashiria | Mwaka wa Kizio | Shabaha (2026/27) | Shabaha (2030/31) |
|---|---|---|---|---|
| **Elimu ya Awali** | | | | |
| 1. | Kiwango cha Uandikishaji rika lengwa (Asilimia ya Watoto wa Miaka 5 Walioandikishwa Elimu ya Awali) | 51.2 (2024) | 60.96 | 100.00% |
| **Elimu ya Msingi** | | | | |
| 2. | Kiwango cha Uandikishaji Jumla (%) | 89.5 (2024) | 91.6 | 100.00 |
| 3. | Kiwango cha Uandikishaji Jumla Shuleni (%) | 98.2 (2023) | 98.56 | 100.00 |
| 4. | Kiwango cha uandikishaji rika lengwa (% ya wanaostahili) | 81.7 (2022) | 85.36 | 100.00 |
| 5. | Kiwango cha wanafunzi wanaomaliza Elimu msingi (%) | 80 (2024) | 83 | 95.00 |
| 6. | Kiwango cha wanafunzi wanaoacha Shule (%) | 6.2 (2024) | 5.22 | 1.30 |
| 7. | Kiwango cha wanafunzi wanaoijunga na Kidato cha Kwanza (%) | 73.3 (2024) | 78.64 | 100.00 |
| 8. | Uwiano wa Mwanafunzi kwa Mwalimu Mwenye Sifa (PTR) | 105:1 (2024) | | 40:01 |
| 9. | Uwiano wa Mwanafunzi kwa Mwalimu (PTR) | 61:1 (2024) | | 53:01 |
| 10. | Uwiano wa Mwanafunzi kwa Kitabu (PBR) | 3:1 (2024) | | 1:01 |
| 11. | Uwiano wa Wanafunzi kwa Darasa (PCR) | 63:1 (2024) | | 50:01 |
| 12. | Uwiano wa Wavulana kwa Tundu la Choo (PLR) | 42:1 (2023/24) | | 25:01 |
| 13. | Uwiano wa Wasichana kwa Tundu la Choo (PLR) | 39:1 (2023/24) | | 20:01 |
| 14. | Uwiano wa Wanafunzi kwa Dawati | 4:1 (2023/24) | | 2:01 |
| 15. | Asilimia ya Shule Zenye Umeme (%) | 48 (2023/24) | 51.6 | 66.00 |
| 16. | Uwiano wa Watoto Wenye Ulemavu | 78.6 (2022) | 82.48 | 98.00 |

| Na. | Kiashiria | Mwaka wa Kizio | Shabaha (2026/27) | Shabaha (2030/31) |
|---|---|---|---|---|
| | Wanaohudhuria Shule ya Msingi (%) | | | |
| 17. | Uwiano wa Wanafunzi kwa Mwalimu kwa Somo | 26:1 (2024) | | 23:01 |
| 18. | Uwiano wa Wanafunzi kwa Darasa | 63:1 (2024) | | 40:01 |
| 19. | Uwiano wa Wanafunzi kwa Tundu la Choo | 28:1 (2023/24) | | 20:01 |
| 20. | Uwiano wa Mwanafunzi kwa Mwalimu Mwenye Sifa (PTR) | 105:1 (2024) | | 40:01 |
| 21. | Uwiano wa Mwanafunzi kwa Mwalimu (PTR) | 61:1 (2024) | | 53:01 |
| 22. | Uwiano wa Mwanafunzi kwa Kitabu (PBR) | 3:1 (2024) | | 1:01 |
| 23. | Uwiano wa Wanafunzi kwa Darasa (PCR) | 63:1 (2024) | | 50:01 |
| 24. | Asilimia ya Shule za msingi zenye Maji Safi (%) | 54 (2023/24) | 56.4 | 66.00% |
| **Elimu ya Sekondari ya Chini (I – IV)** | | | | |
| 25. | Kiwango cha Uandikishaji Jumla (%) | 51.7 (2024) | 57.18 | 79.10 |
| 26. | Kiwango cha uandikishaji rika lengwa (% ya wanaostahili) | 43.2 (2022) | 44.56 | 50.00 |
| 27. | Kiwango cha ufaulu Mtihani wa Kidato cha Nne (%) | 92.37 (2024) | 93.9 | 100.00 |
| 28. | Kiwango cha wanafunzi wanaojiunga na Kidato cha Tano kutoka Kidato cha Nne (%) | 24.4 (2024) | 25.32 | 29.00 |
| 29. | Asilimia ya Shule za Sekondari Zenye Umeme | 69 (2023/24) | 75.2 | 100.00 |
| 30. | Kuongeza Ufaulu wa somo la Hisabati (%) | 25.4 (2024) | 26.72 | 32.00 |
| 31. | Kuongeza Ufaulu wa Masomo ya Sayansi (%) | 79.37 (2024) | 80.5 | 85.00 |
| 32. | Asilimia ya Shule za sekondari zenye Maji Safi (%) | 85 (2023/24) | 88 | 100.00% |
| **Elimu ya Sekondari ya Juu (V – VI)** | | | | |
| 33. | Kiwango cha Uandikishaji Jumla (%) | 9.1 (2024) | 9.88 | 13.00 |
| 34. | Kiwango cha uandikishaji rika lengwa (% ya wanaostahili) | 7.7 (2022) | 9.76 | 18.00 |
| 35. | Kiwango cha ufaulu Mtihani wa Kidato cha tano (%) | 7.2 (2022) | 25.76 | 100.00 |
| **Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi** | | | | |
| 36. | Kiwango cha umahiri wa Kusoma na Kuandika kwa Vijana (Miaka 15–35) | 87.5 (2022) | 90 | 100 |
| 37. | Uwiano wa Nguvu Kazi yenye Ujuzi wa Juu (%) | 3.0 (2011) | 4.8 | 12.00 |
| 38. | Uwiano wa Nguvu Kazi Yenye Ujuzi | 13.0 (2011) | 17 | 33.00 |

| Na. | Kiashiria | Mwaka wa Kizio | Shabaha (2026/27) | Shabaha (2030/31) |
|---|---|---|---|---|
| | wa Kati (%) | | | |
| 39. | Uwiano wa Nguvu Kazi Yenye Ujuzi wa Chini (%) | 84.0 (2011) | 78.2 | 55.00 |
| 40. | Wastani wa Idadi ya wanafunzi kwa mwaka walioandikishwa katika Vituo vya Mafunzo ya Ufundi Stadi | 415,131 (2023/24) | 591,446 | 1,296,705 |
| 41. | Asilimia ya Wanafunzi wa Kike walioandikishwa katika Vituo vya Mafunzo ya Ufundi Stadi (%) | 56.80 (2023/24) | 57.44 | 60.00 |
| 42. | Asilimia ya Wanafunzi Wenye Ulemavu walioandikishwa katika Vituo vya Mafunzo ya Ufundi Stadi (%) | 0.2 (2023/24) | 0.23 | 0.33 |
| 43. | Idadi ya Wanafunzi Waliodahiliwa katika Taasisi za Elimu ya Ufundi | 217,204 (2024) | 231,684 | 289,605 |
| 44. | Uwiano wa Wanafunzi wa Kike waliodahiliwa katika Taasisi za Ufundi (%) | 49 (2024) | 49.2 | 50.00 |
| 45. | Uwiano wa Wanafunzi Wenye Ulemavu Walioandikishwa katika Taasisi za Ufundi (%) | 0.04 (2023/24) | 0.05 | 0.10 |
| 46. | Asilimia ya Wanafunzi wanaosoma kozi za Sayansi na Uhandisi (%) | 17.2 (2023/24) | 19.36 | 28.00 |
| 47. | Asilimia ya Wanafunzi wa kike wanaosoma kozi za Sayansi na Uhandisi (%) | 35.7 (2023/24) | 36.56 | 40.00 |
| 48. | Idadi ya Walimu/Wakufunzi katika vyuo vya elimu ya ufundi | 10,948 (2023) | 11,870 | 15,559 |
| 49. | Asilimia ya Walimu/Wakufunzi wa Kike katika vyuo vya elimu ya ufundi (%) | 39.5 (2023/24) | 41.6 | 50.00 |
| 50. | Kiwango cha Uandikishaji Jumla katika vyuo vya elimu ya Ufundi (%) | 5.8 (2023/24) | 6.04 | 7.00% |
| 51. | Idadi ya Wahitimu wa Elimu ya Ufundi kwa Mwaka | 89,967 (2023/24) | 110,531 | 192,786 |
| 52. | Asilimia ya Wanafunzi waliodahiliwa Elimu ya Ufundi Waliopata Mikopo ya Masomo | 1.3 (2024) | 1.44 | 2.00% |
| 53. | Idadi ya Wakufunzi katika vyuo vya ufundi stadi | 2,723 (2023) | 2,842 | 3,318 |
| 54. | Asilimia ya Wakufunzi wa Kike katika vyuo vya ufundi stadi (%) | 34.0 (2023/24) | 36 | 44.00 |
| 55. | Idadi ya Watu Waliopata Mafunzo Kazini (Internship) | 30,000 (2021) | 54,000 | 150,000 |
| 56. | Idadi ya Waliohudhuria Programu za Mafunzo ya Uanagenzi | 46,200 (2021) | 83,160 | 231,000 |

| Na. | Kiashiria | Mwaka wa Kizio | Shabaha (2026/27) | Shabaha (2030/31) |
|---|---|---|---|---|
| | (Apprenticeship) | | | |
| **Elimu ya Juu** | | | | |
| 57. | Kiwango cha udahili katika Elimu ya Juu (%) | 5.8 (2023/24) | 6.04 | 7.00% |
| 58. | Upatikanaji wa fursa ya Elimu ya Juu (%) | 91.7 (2024) | 91.9 | 92.70% |
| 59. | Idadi ya Wanafunzi Waliopatiwa Mikopo ya Elimu ya Juu | 229,652 (2024) | 246,169 | 312,235 |
| 60. | Kiwango cha wahitimu wa kozi za Sayansi na Hisabati miongoni mwa Wahitimu wote wa Vyuo Vikuu (%) | 19.6 (2024) | 19.88 | 21.00 |
| 61. | Idadi ya Wanafunzi Wenye Ulemavu katika Taasisi za Elimu ya Juu | 1,498 (2023) | 2,420 | 6,108 |
| 62. | Asilimia ya Mikopo/Ruzuku inayotolewa kwa wanafunzi wanaosoma masomo ya Sayansi | 64 (2021) | 65.2 | 70.00 |
| 63. | Idadi ya Wahadhiri | 6,009 (2023) | 7,178 | 11,854 |
| 64. | Asilimia ya wahadhiri wa Kike (%) | 30 (2024) | 34 | 50.00 |
| 65. | Idadi ya Wahitimu | 56,520 (2024) | 58,216 | 64,998 |
| 66. | Idadi ya Wahitimu wa Kiume | 27,574 (2024) | 28,401 | 31,710 |
| 67. | Idadi ya Wahitimu wa Kike | 28,946 (2024) | 32,949 | 48,961 |

***Chanzo:*** Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

#### 4.2.3.2 Nguvu Kazi yenye Ari na Uwezo wa Kufanya Kazi

Serikali itaendelea kutekeleza programu na miradi inayolenga kuwawezesha Vijana katika nyanja za kiuchumi na kijami pamoja na kuwajengea uwezo katika nyanja mbalimbali. Utekelezaji wa azma hii utahakikisha vijana wananufaika na fursa za ndani na nje ya nchi. Mpango wa mwaka 2026/27 unalenga kukuza mifumo ya ubunifu kwa vijana ili kuongeza ushirikishwaji na kujenga uwezo wa uvumbuzi kuanzia ngazi ya chini hadi juu; kuandaa na kuendesha vituo vya maarifa ya kidigitali ili kuongeza uwezo wa kidigitali, ujuzi na ubunifu kwa vijana, wanawake na makundi maalumu; kuwawezesha vijana wanaomiliki biashara ndogo kupata elimu ya biashara na kuweza kujisajili katika Mfumo wa Kielektroniki wa Manunuzi ya Serikali (NeST); kuanzisha Mfuko wa Uwezeshaji wa Taifa na kuanzisha na kuimarisha vituo vya ubunifu na ukuaji wa biashara za vijana; kuanzisha mpango wa kitaifa wa dhamana ya mikopo ili kufungua upatikanaji wa ufadhili wa benki za biashara kwa wakulima vijana na wanawake; kukuza ujasiriamali na ubunifu kwa vijana; kuwawezesha vijana kuwa na ujuzi wa kujitangaza mtandaoni, kusimamia bajeti ya kazi za kujitegemea, na kujenga chapa binafsi; na kuanzisha vituo vya kitaifa vya ubunifu kwa ajili ya vijana vinavyotoa malezi, ufadhili na maeneo ya kufanyia kazi

Utekelezaji wa malengo yaliyowekwa kutapelekea kuongezeka kwa ushiriki wa vijana katika shughuli za kiuchumi ikiwemo uchimbaji mkubwa wa madini; kupunguza tatizo la ukosefu wa ajira kwa vijana; kuwa na vijana wenye tija na ubunifu; na kuongezeka

kwa fursa za upatikanaji wa mikopo kwa vijana. Viashiria na shabaha za sekta kwa mwaka wa fedha 2026/27 zimeainishwa katika **Jedwali Na. 4.20**, na orodha ya miradi itakayotekelezwa imeoneshwa katika **Kiambatisho Na. 2**

**Jedwali Na. 4.20: Viashiria na Shabaha katika Sekta ya Maendeleo ya Vijana**

| Na. | Kiashiria | Mwaka wa Kizio | Shabaha (2026/27) | Shabaha (2030/31) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Asilimia ya vijana wanaojua kusoma na kuandika (miaka 15-35) | 87.5 (2022) | 90 | 100 |
| 2. | Asilimia ya vijana wasiokuwa na ajira (15–35) | 8.3 (2024) | 7.84 | 6.00 |
| 3. | Asilimia ya vijana waliopo kwenye ajira hatarishi (%) | 42.4 (2023/24) | 39.68 | 28.80 |
| 4. | Idadi ya Vijana waliopatiwa mafunzo ya stadi za maisha, afya ya uzazi na elimu ya familia | 123,500 (2023/24) | | |
| 5. | Idadi ya Miradi ya Vikundi/Makampuni ya Vijana vilivyopata mikopo kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana kila mwaka | 56 (2024/25) | 84 | 200 |
| 6. | Idadi ya vituo vya Maendeleo ya Vijana vilivyoanzishwa/endelezwa | 3 (2024/25) | 3 | 5 |
| 7. | Idadi ya Majukwaa ya Vijana yaliyoanzishwa/endelezwa | 184 (2024/25) | 250 | 500 |

***Chanzo:*** Ofisi ya Rais, Maendeleo ya Vijana

### 4.2.3.3 Ajira na Soko la Ajira

Sekta ya Kazi, Ajira na Mahusiano inalenga kuimarisha huduma za kinga ya jamii, kuhamasisha ukuaji wa fursa za ajira na kazi, pamoja na kukuza ujuzi wa nguvu kazi iliyopo katika soko la ajira, huku ikitekeleza sera, sheria, mikakati, mipango na programu mbalimbali zinazolenga kujenga nguvu kazi yenye uwezo ili kuongeza tija, ubunifu na ushindani wa taifa katika uchumi wa kisasa. Mkazo utawekwa katika kuongeza nguvu kazi yenye ujuzi kupitia utekelezaji wa Programu ya Ukuzaji inayolenga utambuzi na urasimishaji wa ujuzi uliopatikana nje ya mfumo rasmi wa mafunzo (RPL), mafunzo ya utarajali (internship), mafunzo ya uanagenzi (apprenticeship) kwa kushirikiana na waajiri ili kuoanisha mafunzo na mahitaji ya soko la ajira: kuboresha soko la ajira ili kuwezesha kufikia ajira 1,700,000 mwaka 2026/27 na kuimarisha hifadhi ya jamii na uchumi jumuishi; kuongeza wigo wa jamii jumuishi iliyolindwa kwa kujumuisha sekta isiyo rasmi katika mifumo ya hifadhi ya jamii; na kujenga jamii iliyoshikamana, yenye uwajibikaji na inayochangia umoja wa kitaifa, uzalendo na mshikamano wa kijamii.

Utekelezaji wa malengo haya kupitia miradi na programu za maendeleo utaongeza idadi na ubora wa nguvu kazi yenye ujuzi ili kukidhi mahitaji ya soko la ajira la ndani na kimataifa. Kuimarika kwa mifumo ya mafunzo ya utarajali na uanagenzi kutaongeza ulinganifu kati ya mafunzo na mahitaji halisi ya waajiri, hivyo kuongeza ajira kwa wahitimu na kupunguza pengo la ujuzi katika sekta za uzalishaji na huduma;

na kuongezeka kwa utambuzi na urasimishaji wa ujuzi uliopatikana nje ya mfumo rasmi (RPL) kutawawezesha wafanyakazi wengi zaidi kutambuliwa kitaaluma, kuongeza tija mahali pa kazi na kuboresha kipato chao; kuchochea ukuaji wa ajira kupitia uwekezaji na ubunifu; kupanua wigo wa hifadhi ya jamii, hususan kwa sekta isiyo rasmi, kutaongeza usalama wa kipato na ustawi wa kaya, na mifumo ya usajili wa kidijitali ikiimarisha upatikanaji wa huduma za kinga ya jamii, na matokeo yake ni kujengwa kwa jamii jumuishi, yenye uwajibikaji na mshikamano wa kitaifa. Viashiria na shabaha za sekta kwa mwaka wa fedha 2026/27 zimeainishwa katika **Jedwali 4.21**, na orodha ya miradi itakayotekelezwa imeoneshwa katika **Kiambatisho Na. 2.**

**Jedwali Na. 4.21: Viashiria na Shabaha katika Sekta ya Ajira**

| Na. | Kiashiria | Mwaka wa Kizio | Shabaha (2026/27) | Shabaha( 2030/31) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Kiwango cha ushiriki wa Nguvu Kazi | 73.2 (2024) | 73.48 | 74.60 |
| 2. | Uwiano wa Watu wenye Ulemavu walioajiriwa | 32.5 (2024) | 34 | 40.00 |
| 3. | Wigo wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii (asilimia) | 10.1 (2023/24) | 11.7 | 18.12 |
| 4. | Kiasi cha Uwekezaji wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii katika (Tsh trillioni) | 10.63 (2024) | 11.46 | 14.76 |
| 5. | Ongezeko la Wigo wa Kinga ya Jamii | 28.4 (2023/24) | 31.24 | 42.60% |
| 6. | Vijana walio katika ajira hatarishi(%) | 42.4 (2023/24) | 39.68 | 28.80% |
| 7. | Asilimia ya ajira kwenye Sekta isiyo Rasmi | 94.2 (2024) | 91.56 | 81 |
| 8. | Uwiano wa Watu walioajiriwa kulinganisha na Idadi ya Watu (Asilimia) | 68.7 (2024) | 69.22 | 71.30 |
| 9. | Kiwango cha Ukosefu wa ajira (15+) | 6.2 (2024) | 5.84 | 4.40% |
| 10. | Kiwango cha ukosefu wa ajira kwa vijana (15–35) | 8.3 (2024) | 7.84 | 6.00% |
| 11. | Ajira zilizozalishwa | 981,000 (2024) | 1,700,000 | 8,500,000 |

***Chanzo:*** Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Mahusiano

Mchango wa sekta katika ajira zinazotarajiwa kuzalishwa mwaka 2026/27 unaonesha kuwa sekta ya kilimo inatarajiwa kuongoza kwa kuzalisha ajira 661,332; huduma na utalii 317,045; viwanda 230,105; biashara na matengenezo 103,908; usafiri na usafirishaji 103,908; na ujenzi 58,401 **(Kielelezo Na. 4.1).** Kwa ujumla, malengo haya yanaakisi mabadiliko ya kimuundo yanayolenga kukuza ajira kupitia sekta za uzalishaji na huduma zenye matokeo chanya katika uchumi.

**Kielelezo Na 4.1: Maoteo ya Mchango wa Sekta katika Ajira zinazotarajiwa kuzalishwa Mwaka 2026/27.**




***Chanzo:*** Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2026/27

### 4.2.3.4 Jamii Jumuishi na inayolindwa

Sekta ya ustawi na maendeleo ya jamii itaendelea kutekeleza miradi ya kipaumbele ya kuhakikisha kuwa Tanzania inanufaika na fursa ya kidemografia kupitia maendeleo ya rasilimali watu, ajira zenye staha, ujasiriamali na uwezeshaji kiuchumi ili kuwa na ukuaji wa uchumi jumuishi na kuboresha maisha; kuongeza wigo wa kuwa na jamii jumuishi iliyolindwa kwa kuongeza wigo wa hifadhi ya jamii ili kupunguza hatari na kuhakikisha usawa wa fursa kwa makundi yote; jamii iliyoshikamana na yenye uwajibikaji, inayochangia umoja wa Kitaifa na mshikamano wa kijamii; na kurasimisha sekta isiyo rasmi ili kuwa kichocheo cha ukuaji wa uchumi.

Utekelezaji wa malengo haya utafanyika kupitia miradi ya maendeleo itakayopelekea kuwa na mpango kamili wa hifadhi ya jamii kwa wazee (miaka 60+); ulinzi wa angalau asilimia 40 ya watu walio katika mazingira hatarishi; kufikia angalau asilimia 35 ya wanawake katika nafasi za uongozi kwenye biashara, serikali na elimu; na kupunguza mchango wa sekta isiyo rasmi katika Pato la Taifa kutoka asilimia 55 kufikia asilimia 29.

Viashiria na shabaha za sekta ya ustawi na maendeleo ya jamii kwa mwaka 2026/27 ni kama vilivyoainishwa katika **Jedwali 4.22** na orodha ya miradi itakayotekelezwa kulingana na vipaumbele imeainishwa katika **Kiambatisho Na 2**

**Jedwali Na. 4.22: Viashiria na Shabaha katika Sekta ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii**

| Na. | Kiashiria | Mwaka wa Kizio | Shabaha (2026/27) | Shabaha (2030/31) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Idadi ya watoto wanaolelewa baada ya mapatano | 48,051 (2024/25) | 71,955 | 163,905 |
| 2. | Idadi ya vituo vya malezi ya watoto vilivyosajiliwa | 4,178 (2024/25) | 6,903 | 11,263 |
| 3. | Idadi ya wazee wasiojiweza wanaopata huduma za bima ya afya bure | 1,256,544 (2024/25) | 3,116,008 | 4,975,473 |
| 4. | Wanawake katika nafasi za uongozi (%) | 27 **(**2024/25) | 30 | 35 |
| 5. | Idadi ya wafanyabiashara ndogondogo waliotambuliwa na kusajiliwa | 84,318(2024/25) | 200,000 | 1,000,000 |
| 6. | Hali ya Ukatili wa kijinsia | 38.9 (2022) | 35.12 | ≤20 |
| 7. | Ukatili wa wa kingono dhidi ya watoto wa kike (%) | 11 (2024) | 9.9 | ≤5.50 |
| 8. | Ukatili wa kimwili dhidi ya watoto wa kike (%) | 24 (2024) | 22 | ≤14.00 |
| 9. | Ukatili wa kihisia dhidi ya watoto wa kike (%) | 22 (2024) | 20.24 | ≤13.20 |
| 10. | Ukatili wa wa kingono dhidi ya watoto wa kiume (%) | 5 (2024) | 4.54 | ≤2.69 |
| 11. | Ukatili wa kimwili dhidi ya watoto wa kiume (%) | 21 (2024) | 19.2 | ≤12.00 |
| 12. | Ukatili wa kihisia dhidi ya watoto wa kiume (%) | 16 (2024) | 14.4 | ≤8.00 |

***Chanzo:*** Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makandi Maluum

#### 4.2.3.5 Afya Bora kwa Wote

Sekta ya Afya itaendelea kutekeleza sera, sheria, mikakati, mipango, miongozo, programu na miradi mbalimbali ili kufanikisha lengo la kuboresha afya ya wananchi. Katika kutekeleza lengo hilo, kwa mwaka wa fedha 2026/27 wizara imeweka vipambele vifuatavyo: Kuimarisha upatikanaji wa huduma za dawa kwa kuwekeza katika Viwanda vya dawa ili kuongeza uzalishaji; Kuimarisha mifumo ya ugharamiaji wa huduma za afya nchini ikiwa ni pamoja na kuendelea na utekelezaji wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote Sura 16; Kuimarisha huduma za kinga dhidi ya magonjwa ya kuambukiza yakiwemo magonjwa ya milipuko, Lishe, magonjwa yaliyokuwa hayapewi kipaumbele na magonjwa yasiyoambukiza; Kuimarisha upatikanaji na ubora wa huduma za afya zinazotolewa katika ngazi zote kuanzia Zahanati hadi Taifa, zikiwemo, kuimarisha matumizi ya TEHAMA ili kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma ikiwemo matumizi ya akili mnemba; Kuweka mazingira wezeshi ya viwanda vya ndani vya kuzalisha bidhaa za afya ili kuwezesha upatikanaji wa bidhaa hizo kwa urahisi na unafuu wakati wote; Kuimarisha Tafiti na matumizi ya matokeo ya tafiti mbalimbali za afya; Kuimarisha huduma za afya ya uzazi, mama na mtoto ili kupunguza vifo vya wajawazito na watoto wachanga; Kuimarisha upatikanaji na

uendelezaji wa wataalam katika Sekta ya Afya kwa fani za kati, ubingwa na ubingwa bobezi; Kuimarisha huduma za matibabu ya ubingwa na ubingwa bobezi pamoja na kuimarisha Tiba Utalii nchini; Kuendeleza na kusimamia afua za Tiba Asili na Tiba Mbadala; na Kuimarisha upatikanaji wa huduma za tiba dhidi ya magonjwa ya kuambukiza, magonjwa yasiyoambukiza na magonjwa ya mlipuko; Kuimarisha huduma za afya ya akili, huduma za utengamao hususan kwa watoto, wazee na watu wenye ulemavu.

Matokeo ya utekelezaji wa vipaumbele hivyo utapelekea kufikiwa kwa viashiria na shabaha ikiwemo: Kupunguza vifo vya watoto wachanga; Kuongeza wigo wa Bima ya Afya; Kupungua kwa idadi ya vifo vya akina mama wajawazito kwa kila vizazi hai 100,000; Kuongezeka kwa Umri wa kuishi; Kupunguza ueneaji wa magonjwa Makuu ya kuambukiza ikiwemo VVU, Malaria, na Kifua Kikuu; Kufikiwa kwa asilimia 58.0 ya jumla ya idadi ya watu wanaopata huduma za afya zinazofikika, zinazopatikana kwa ubora na gharama nafuu; Kujumuishwa kwa usimamizi wa afya na takwimu za kidijitali ili kutoa huduma za afya kwa ufanisi; Kupunguza uagizaji wa bidhaa muhimu za afya; na Tanzania kuwa moja ya vituo vikuu viwili (2) vya utalii wa matibabu katika ukanda wa Afrika mashariki na kati. Aidha, viashiria na shabaha za sekta ya Afya kwa mwaka 2026/27 ni kama vilivyoainishwa katika **Jedwali Na. 4.23** na orodha ya miradi itakayotekelezwa kulingana na vipaumbele imeainishwa katika **Kiambatisho Na. 2**

**Jedwali Na. 4.23: Viashiria na Shabaha katika Sekta ya Afya**

| Na. | Kiashiria | Mwaka wa kizio | Shabaha (2026/27) | Shabaha (2030/31) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Asilimia ya watoto wenye umri wa miezi 0–24 katika kaya wanaohudhuria katika vituo vya afya (%) | 95.0 (2023/24) | 95.2 | 96.00% |
| 2. | Idadi ya vifo vya watoto wachanga kwa kila vizazi hai 1000 | 33 (2022) | 31.8 | 27 |
| 3. | Idadi ya vifo vya watoto wenye umri chini ya miaka mitano kwa kila vizazi hai 1000 | 43 (2022) | 41.2 | 34 |
| 4. | Kiwango cha uzazi-idadi ya wastani wa watoto anaotarajiwa kuzaa mwanamke katika kipindi chote cha umri wake wa kuzaa (Total Fertility rate) | 4.8 (2022) | 4.66 | 4.1 |
| 5. | Uzazi uliohudumiwa na mfanyakazi wa afya mwenye ujuzi | 84 (2023/04) | 85.06 | 89.30% |
| 6. | Idadi ya vifo vitokanavyo na uzazi kwa kila vizazi hai 100,000 | 104 (2022) | 100.2 | 85 |
| 7. | Matumizi ya Serikali katika huduma za afya (%) | 11.6 (2023/24) | 12.12 | 14.20% |
| 8. | Kiwango cha udumavu kwa watoto wenye umri wa miezi 0–59 | 26.5 (2023/24) | 25.2 | 20.00% |
| 9. | Kiwango cha ukondefu kwa watoto | 2.6 (2023/24) | 2.6 | 2.60 |

| Na. | Kiashiria | Mwaka wa kizio | Shabaha (2026/27) | Shabaha (2030/31) |
|---|---|---|---|---|
| | wenye umri kuanzia miezi 0-59 | | | |
| 10. | Wananchi wenye bima ya afya (%) | 15.3 (2023) | 23.84 | 58.00% |
| 11. | Asilimia ya watoto wenye umri wa miezi 0–24 katika kaya wanaohudhuria katika vituo vya afya (%) | 95.0 (2023/24) | 95.2 | 96.00% |

***Chanzo:*** Wizara ya Afya

#### 4.2.3.6 Upatikanaji na Uunganishwaji wa huduma za maji safi na Usafi wa Mazingira

Maji ni kichocheo muhimu cha maendeleo katika sekta mbalimbali za uchumi hapa nchini ikiwepo kilimo, biashara, utalii na viwanda. Kutokana na umhimu huo, Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Miaka Mitano (FYDP IV) umelenga kuendelea kuimarisha usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji kwa kuzingatia ustahimilivu wa mabadiliko ya tabianchi na kuboresha upatikanaji wa huduma ya maji nchini. Katika mwaka 2026/27 sekta ya Maji itaendelea kuimarisha usimamizi na uendelezaji wa rasiimali za maji; kutekeleza miradi ya maji ili kuboresha upatikanaji wa huduma ya maji kwa wananchi katika maeneo ya mijini na vijijini; kuboresha huduma ya usafi wa mazingira; na kujenga mabwawa madogo, ya ukubwa wa kati na ya mkakati kwa ajili ya kuvuna maji ya mvua.

Katika kufikia azma hiyo, Serikali itaendelea na utekelezaji wa Mtandao wa Taifa wa Kusambaza Maji (National Water Grid) unaohusisha kutoa maji kwenye vyanzo vya uhakika kama vile maziwa na mito na kuyapeleka kwenye maeneo yenye uhaba wa maji. Baadhi ya miradi hiyo ni pamoja na: mradi wa kutoa maji kutoka Ziwa *Victoria* kwenda Dodoma kupitia Singida (Lake Victoria Dodoma Water Project - LVD); kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa miradi ya kutoa maji Ziwa Tanganyika kuyapeleka kwenye mikoa ya Kigoma, Katavi, Songwe na Rukwa;na mradi wa kutoa maji Ziwa Nyasa hadi mikoa ya Njombe na Ruvuma. Vilevile, Serikali itakamilisha usanifu wa miradi ya maji kwa kutumia mito mikubwa ikiwemo Mto Rufiji kupeleka Jiji la Dar es Salaam na mkoa wa Pwani na Lindi; mradi wa kutoa maji Mto Ruvuma kupeleka Manispaa ya Mtwara-Mikindani, Nanyumbu, Masasi na Lindi; Mto Momba kupeleka maji katika miji ya Momba, Tunduma, Vwawa, Mlowo hadi Mbalizi;na mradi unaoendeleawa Mto Kiwira kwa ajili ya jiji la Mbeya hadi Mbalizi na Rujewa. Aidha, Serikali itaendelea na ujenzi wa mabwawa ya kimkakati ya Kidunda na Farkwa ili kuwa na uhakika wa upatikanaji wa maji.

Utekelezaji wa malengo hayo kupitia ujenzi wa miradi ya maji na mabwawa utawezesha upatikanaji wa huduma ya maji endelevu na kuwafikia wananchi waliowengi nchini. Aidha, Serikali itaendelea na usimamizi wa rasilimali za maji ili ziweze kutumika kwa vizazi vya sasa na vijavyo. Hali hiyo itawezesha kuchochea ukuaji wa sekta za mageuzi kuongeza uzalishaji wa mazao ya kilimo, viwanda, ujenzi na kuongeza thamani pamoja na kupunguza magonjwa yatokanayo na maji. Viashiria

na shabaha za sekta ya maji kwa mwaka 2026/27 ni kama vilivyoainishwa katika **Jedwali Na. 4.24**.

**Jedwali Na. 4.24: Viashiria na Shabaha katika Sekta ya Maji**

| Na. | Kiashiria | Mwaka wa Kizio | Shabaha (2026/27) | Shabaha (2030/31) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Asilimia ya idadi ya watu wa vijijini wanaopata maji ya bomba au maji yalivyolindwa kama chanzo kikuu | 79.6 (2023/24) | 85.2 | 90 |
| 2. | Asilimia ya watu katika makao makuu ya mikoa wanaopata maji ya bomba au maji yaliyolindwa | 91,60 (2023/24) | 92.5 | 98 |
| 3. | Wastani wa masaa ya Upatikanaji wa Huduma ya Maji katika maeneo ya mijini | 14 (2023/24) | 16 | 20 |
| 4. | Uwiano wa kaya za vijijini zenye miundombinu iliyoboreshwa ya usafi wa mazingira | 72.0 (2023/24) | 77.5 | 100.00 |
| 5. | Kiwango ya upotevu wa maji (NRW) katika makao makuu ya mikoa (%) | 36.8 (2023/24) | 35 | 20 |
| 6. | Asilimia ya watu katika makao makuu ya wilaya na miji midogo wanaopata huduma ya maji ya bomba au maji yaliyolindwa kama chanzo kikuu | 74.5 (2023/24) | 80 | 90 |
| 7. | Asilimia ya watu katika jiji la Dar es Salaam wanaopata huduma ya maji ya bomba au maji salama kama chanzo chao kikuu | 92.5 (2023/24) | 94.5 | 98 |
| 8. | Kiwango cha upotevu wa maji (NRW) katika jiji la Dar es Salaam (%) | 40.0 (2023/24) | 35.6 | 20 |
| 9. | Idadi ya vyanzo vya maji vilivyowekwa mipaka na kutangazwa katika Gazeti la Serikali kwa ajili ya ulinzi na uhifadhi | 80 (2023/24) | 105 | 200 |

***Chanzo:*** Wizara ya Maji

### 4.2.4 Uhifadhi wa mazingira na ustahimilivu wa mabadiliko ya tabianchi

Eneo hili limetoa kipaumbele katika katika maeneo mawili (2) ambayo ni: Ustahimilivu wa mazingira; na ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Lengo la eneo hili ni kuimarisha uhifadhi wa mazingira na kuongeza ustahimilivu dhidi ya athari za mabadiliko ya tabianchi, kwa kuzingatia matumizi endelevu ya rasilimali na maendeleo ya makazi yaliyo salama na jumuishi. Hivyo, mikakati, shabaha, afua, viashiria muhimu vya upimaji wa utendaji, miradi na programu za maendeleo katika eneo hili ni kama ifuatavyo:

#### 4.2.4.1 Ustahimilivu wa Mazingira

Sekta ya uhifadhi na usimamizi wa Mazingira na Maliasili itaendelea kutekeleza sera, sheria, mikakati, mipango, miongozo, programu na miradi mbalimbali ya hifadhi ya mazingira ili kupunguza athari zinazosababishwa na uharibifu wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi. Kuimarisha uhifadhi wa bioanuai na mifumo-ikolojia kwa maendeleo endelevu kwa lengo la kuifanya Tanzania kuwa kinara wa matumizi endelevu ya ardhi, rasilimali za misitu, maji, ardhi oevu kwa ajili ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Kuimarisha uwezo wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na kutumia kikamilifu fursa za biashara ya kaboni ili kuongeza kipato cha jamii na taifa ili kuifanya Tanzania kuwa kinara katika uhimilivu wa mabadiliko ya tabianchi, uimarishaji wa biashara ya kaboni na kujenga uwezo wa sekta na taasisi katika kuratibu na kutekeleza hatua mbalimbali za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na kuimarisha uwezo wa usimamizi wa uchafuzi wa mazingira unaochangiwa na maji taka, taka hatarishi, taka ngumu ikiwemo plastiki, na kutumia fursa za uwekezaji katika sekta ya usimamizi wa taka.

Utekelezaji wa malengo haya utakaofanyika kupitia miradi ya maendeleo utapelekea: Kuongezeka kwa eneo lenye uoto wa asili kwa eneo lililoharibiwa ili kunusuru kuenea kwa hali ya jangwa na ukame; kuimarika kwa mifumo-ikolojia (ardhi ya kilimo; nyanda za malisho na ardhi-oevu) na ongezeko la uzalishaji kwa baadhi ya sekta za kiuchumi ikiwemo kilimo, mifugo, uvuvi, maji, nishati, misitu na utalii; na kuongezeka kwa matumizi ya nishati safi ya kupikia katika taasisi zinazolisha watu zaidi ya 100 na kupunguza uharibifu wa misitu. Vilevile, kutapelekea kuongezeka kwa mapato ya kupitia Biashara ya Kaboni katika sekta za misitu, nishati, uchukuzi na usimamizi wa taka; kuongezeka kwa fursa za ajira kwa wanawake na vijana katika shughuli za uanzishaji wa vitalu vya miche, urejelezaji wa taka ngumu, biashara ya kaboni na nishati safi ya kupikia na kuongezeka kwa ushiriki wa jamii ikiwemo wanawake na vijana katika shughuli za hifadhi ya mazingira hususan upandaji na utunzaji wa miti na uanzishaji wa bustani za kijani. Aidha, viashiria na shabaha za sekta ya uhifadhi wa mazingira kwa mwaka 2026/27 ni kama vilivyoainishwa katika **Jedwali Na. 4.25** na orodha ya miradi itakayotekelezwa kulingana na vipaumbele imeainishwa katika **Kiambatisho Na. 2.**

**Jedwali Na. 4.25: Viashiria na Shabaha katika Sekta ya Mazingira**

| No. | Kiashiria | Mwaka wa kizio | Shabaha (2026/27) | Shabaha (2030/31) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Miradi Mikubwa ambayo imepata Vibali vya Tathmini na Kaguzi za Mazingira | 128 (2023/24) | 136.53 | 170.67 |
| 2. | Kupungua kwa kiwango cha ukataji miti (ha/mwaka) | 469,420 (2023/24) | 422,478 | 234,710.00 |
| 3. | Kupungua kwa upotevu wa bionuai (%) | 0.3 (2023/24) | 28 | 20 |
| 4. | Kiwango cha Uhimilivu wa Mabadiliko ya Tabianchi (Kwa Afrika) | 18th (2022) | 17.4 | Top 15 |

| No. | Kiashiria | Mwaka wa kizio | Shabaha (2026/27) | Shabaha (2030/31) |
|---|---|---|---|---|
| 5. | Kupungua kwa gharama zitokanazo na athari kwa mabadiliko ya tabianchi (%) | 0.01 (2023/24) | 0.98 | 0.9 |
| 6. | Ushiriki wa jamii na wawekezaji wa ndani katika utekelezaji wa miradi ya Kaboni (%) | <5 (2025) | | ≥10–15 |
| 7. | Mapato ya kila mwaka yatokanayo na mauzo ya nje ya viwango vya kaboni (USD Billion Vs >USD 20 trillion global market) | 1 (2024) | | dola za Marekani bilioni 3 kila mwaka |

***Chanzo:*** Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira

#### 4.2.4.2 Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

Sekta ya ardhi na Maendeleo ya Makazi itaendelea kutekeleza miradi ya kipaumbele inayolenga kuimarisha mifumo ya usimamizi na usalama wa milki za ardhi na kukuza makazi endelevu ili kuchangia ukuaji wa uchumi, maendeleo ya viwanda na ustawi endelevu wa Jamii. Kuendelea kutekeleza programu ya kupanga, kupima na kumilikisha ardhi nchini kutawezesha kuwa na miji na majiji yaliyopangwa, kuongeza usajili wa hatimiliki na kupunguza migogoro ya ardhi nchini. Pia, uboreshaji wa miundombinu ya upimaji na ramani ni muhimu kwa kuwa unahusisha uandaaji wa ramani za msingi, usimikaji wa vituo vya upimaji vya kielectroniki (CORs) pamoja na kujenga kanzidata ya taarifa za kijiografia kwa lengo la kuongeza kasi ya kupanga na kupima na kupunguza gharama za upimaji ardhi. Vilevile, kuendelea na uboreshaji wa milki za ardhi kunaimarisha usimamizi na utunzaji wa taarifa za ardhi kupitia Mfumo wa kieletroniki wa ardhi (e-Ardhi). Vilevile, uwekezaji katikia Vyuo vya Ardhi Tabora na Morogogo utawezesha kupata wataalam wenye ujuzi na ustadi wa kitaalamu kwa ajili maendeleo ya sekta. Aidha, upimaji wa mipaka ya kitaifa na kimataifa kutaimarisha ulinzi na usalama wa maeneo ya mipakani.

Utekelezaji wa miradi ya maendeleo utakaofanyika utapelekea kufanya mageuzi ya kisera na kisheria ili kuhakikisha uwazi katika umiliki na matumizi ya ardhi, usimamizi wa haki za ardhi kwa wananchi wote ikiwemo wanawake, vijana, na makundi maalumu; kuimarisha mifumo ya utatuzi wa migogoro ya ardhi; kushirikisha sekta binafsi katika upimaji, usimamizi wa takwimu, na matumizi ya TEHAMA kwa ajili ya kuharakisha utoaji wa huduma; kuimarisha utekelezaji wa sheria za upangaji miji na matumizi ya ardhi ili kudhibiti ukuaji holela wa makazi yasiyo rasmi; kuanzisha benki ya kitaifa ya ardhi kwa ajili ya kusimamia na kutenga ardhi kwa matumizi ya kongani za viwanda, SEZs na shoroba kubwa za usafirishaji; kuimarisha mifumo ya udhibiti inayohusiana na maendeleo ya ardhi na miji ili kuchochea maendeleo ya soko la mali isiyohamishika; na utoaji wa mafunzo kwa maafisa ardhi katika ngazi ya Serikali za Mitaa kuhusu matumizi ya mifumo ya kidijitali, GIS, usuluhishi wa migogoro na usimamizi wa ardhi. Aidha, viashiria na shabaha za sekta ya Ardhi kwa mwaka 2026/27 ni kama vilivyoainishwa katika **Jedwali Na. 4.26** na orodha ya miradi itakayotekelezwa kulingana na vipaumbele imeainishwa katika **Kiambatisho Na. 2**.

**Jedwali Na. 4.26: Viashiria na Shabaha katika Sekta ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi**

| Na | Kiashiria | Mwaka wa Kizio | Shabaha (2026/27) | Shabaha (2030/31) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Asilimia ya Ardhi iliyopimwa | 26 (2025/26) | 31 | 51 |
| 2. | Idadi ya mali zilizorasimishwa katika makazi yasiyopangwa | 2,942,661 (2025/26) | 3,142,661 | 3,942,661 |
| 3. | Idadi ya leseni za makazi zilizotolewa kwa wamiliki wa mali katika makazi yasiyopangwa | 29,478 (2025/26) | 32,478 | 41,478 |
| 4. | Asilimia ya eneo la ardhi ya jumla yenye makazi yasiyo rasmi | 60.1 (2025/26) | 59 | 55 |
| 5. | Eneo la ardhi lililotengwa na kulindwa kwa matumizi ya umma (ekari) | 875,360 (2025/26) | 885,360 | 925,360 |
| 6. | Uwiano wa vijiji vyenye mipango ya matumizi bora ya ardhi (%) | 38.97 (2025/26) | 46.55 | 77.19 |
| 7. | Idadi ya Miji yenye Mipango ya jumla (mfano Mipango Kabambe) | 28 (2025/26) | 31 | 43 |
| 8. | Idadi ya ramani za msingi zilizohuishwa kwa eneo (mkoa) | 88 (2025/26) | 100 | 2,400 |
| 9. | Idadi ya Viwanja vilivyopimwa | 3,510,545 (2025/26) | 4,010,545 | 6,010,545 |
| 10. | Ukubwa wa ardhi uliotengwa kwa ajili ya uwekezaji (Hekta) | 220,433.27 (2025/26) | 225,433.27 | 245,433.27 |
| 11. | Idadi ya Hatimiliki milki (CROs) zilizosajiliwa | 1,288,133 (2025/26) | 1,488,133 | 2,288,133 |
| 12. | Idadi ya Hati za Hakimiliki za kimila (CCROs) zilizosajiliwa | 1,296,295 (2025/26) | 1,496,295 | 2,296,295 |

***Chanzo:*** Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

### 4.2.5 Vichocheo vya Maendeleo

Eneo hili limetoa kipaumbele katika katika maeneo tatu (3) ambayo ni: Nishati kwa mageuzi na ukuaji wa haraka; upanuzi na upatikanaji wa miundombinu na huduma za TEHAMA; na uchukuzi. Mikakati, shabaha, afua, viashiria muhimu vya upimaji wa utendaji, miradi na programu za maendeleo katika eneo hili ni kama ifuatavyo:

#### 4.2.5.1 Nishati

Sekta ya Nishati itaendelea kutekeleza miradi ya kipaumbele kwa kusimamiwa na taasisi za kisasa, zenye uwazi na ufanisi, zikisaidiwa na nguvu kazi yenye ujuzi. Mageuzi yataijengea sekta mfumo wa ushindani, uwazi na uendelevu wa kifedha, ikiwemo kubadilisha TANESCO kuwa shirika la kibiashara lenye vitengo vinavyojitegemea na kuendeshwa kwa mfumo wa udhibiti unaozingatia utendaji, ili kuruhusu ushiriki wa sekta binafsi na huduma za umeme za uhakika. Tanzania itaimarisha miundombinu ya nishati imara na unganishi, tayari kwa uwekezaji na upatikanaji wa nishati ndani na mipakani kupitia sekta binafsi na green capital. Uzalishaji wa umeme utaongezeka kufikia MW 70,000 ili kukidhi mahitaji ya baadaye, kuendeleza viwanda na kuhakikisha nishati kwa wote. Ujumuishaji wa nishati jadidifu utaongezeka hadi asilimia 50, kupunguza hewa ukaa na kuimarisha ustahimilivu wa

tabianchi. Mifumo ya usafirishaji na usambazaji itaboreshwa kupunguza hasara hadi chini ya asilimia 5 na kuimarisha gridi. Kaya zote nchini zitapata umeme wa uhakika na nafuu kwa asilimia 100. Usalama wa nishati utaimarishwa kupitia vyanzo mchanganyiko, ikiwemo akiba ya makaa ya mawe yenye teknolojia safi na ujumuishaji wa nishati jadidifu.

Kuongeza utafiti na uchimbaji wa mafuta na gesi ili kufungua kikamilifu fursa za rasilimali za nishati za taifa na kukuza uchumi; Kuimarisha uzalishaji na matumizi ya ndani ya gesi asilia kuhakikisha upatikanaji endelevu wa nishati kwa viwanda na ukuaji wa uchumi; Kubadili Tanzania kuwa muuzaji mkuu wa gesi barani Afrika kwa kupanua ushawishi katika masoko ya kikanda na kimataifa na kuchochea ukuaji endelevu wa uchumi wa taifa.

Utekelezaji wa malengo haya kupitia miradi ya maendeleo utapelekea kuimarika kwa nguvu kazi ya taifa yenye wataalamu 10,000 katika sekta ya nishati, kuwepo kwa usimamizi wa uwazi, ufanisi na uwajibikaji, pamoja na kubadilishwa kwa TANESCO kuwa shirika la kibiashara lililogawanywa kikamilifu katika idara za uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme. Aidha, kuanzishwa na kugharamiwa kwa Usimamizi Huru wa Mfumo na Soko la Umeme (ISMO) kutahakikisha upangaji wa uzalishaji, upatikanaji wa mfumo na uratibu wa soko shindani la umeme, huku kiunganishi cha kikanda cha kV 400 na maboresho ya mtandao wa usafirishaji vikihakikisha upatikanaji wa umeme wa uhakika na biashara ya kikanda. Sekta ya nishati itakusanya dola za Marekani bilioni 7 kutoka mikopo nafuu kufadhili uzalishaji wa nishati safi na usafirishaji wa umeme, kuongeza matumizi ya nishati kwa mtu mmoja kufikia 600 kWh, na kuongeza uwezo wa uzalishaji wa nishati safi hadi MW 8,000, ikiwemo MW 1,700 za jotoardhi, MW 500 za upepo na MW 715 za jua. Hatua hizi zitapunguza upotevu wa umeme kutoka asilimia 14.2 hadi 12.4, kujenga vituo vidogo 100 vijijini na mifumo ya gridi mahiri, kuongeza uunganishaji wa umeme kwa kaya kutoka asilimia 49 hadi 55.2 na vijijini kutoka asilimia 36 hadi 42.8, na kuimarisha upatikanaji wa umeme kwa kaya hadi asilimia 80. Vilevile, mitambo yenye uwezo wa MW 1,000 kupitia makaa ya mawe itasimikwa kwa kuzingatia vigezo vya kimazingira, huku taifa likihakikisha akiba ya ziada ya asilimia 20 (reserve margin).

Utekelezaji wa mpango wa motisha mahsusi kwa ajili ya kuvutia uwekezaji katika utafiti wa mafuta na gesi utalenga kufikia angalau asilimia 50 ya mabonde ya mashapo ya Tanzania, huku Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) likibadilishwa kuwa Kampuni ya Kibiashara inayokidhi viwango vya kimataifa. Hatua hizi zitaongeza uzalishaji wa gesi asilia ya nchi kavu kutoka MMSCFD 320 hadi MMSCFD 1,000 na matumizi ya gesi asilia nchini kutoka futi za ujazo 290,000 kwa siku hadi 800,000. Aidha, usambazaji wa gesi katika Kituo cha Biashara ya Gesi cha Kikanda utaongezeka kutoka milioni 290 za futi za ujazo kwa siku hadi milioni 3,500, huku uzalishaji wa gesi baharini ukiruhusu biashara ya LNG kufikia tani milioni 15 kwa mwaka (MTPA). Aidha, viashiria na shabaha za sekta ya Nishati kwa mwaka 2026/27 ni kama vilivyoainishwa katika **Jedwali Na. 4.27** na orodha ya miradi itakayotekelezwa kulingana na vipaumbele imeainishwa katika **Kiambatisho Na. 2.**

**Jedwali Na. 4.27: Viashiria na Shabaha katika Sekta ya Nishati**

| Na. | Kiashiria | Mwaka wa Kizio | Shabaha (2026/27) | Shabaha (2030/31) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Uzalishaji wa Gesi Asilia (katika milioni za futi za ujazo) | 69,538.30 (2024) | 73,630.64 | 90,000 |
| 2. | Sehemu ya gesi asilia katika jumla ya mchanganyiko wa usambazaji wa umeme (%) | 63 (2024) | 59.4 | 45 |
| 3. | Uenezi wa Mtandao wa Usambazaji wa Gesi Asilia (Kilomita) | 177.82 (2024) | 195.66 | 267 |
| 4. | Uwezo wa umeme uliowekwa | 4,504.54 MW (2025) | 4,654.54 | 8,000 MW |
| 5. | Kiwango cha matumizi kwa kila mtu | 243 kWh (2025) | 256 | 528 kWh |
| 6. | Upotevu wa umeme | 14.2 (2025) | 13.84 | 12.40% |
| 7. | Asilimia ya uunganishaji | 52.1% (2025) | 59% | 75% |
| 8. | Asilimia ya uunganishaji wa umeme kwa kaya | 52.1% (2025) | 59% | 75% |
| 9. | Wastani wa matukio ya kukatika kwa umeme (SAIFI) | Matukio yasiyozidi 26 kwa mwaka | Matukio yasiyozidi 26 kwa mwaka | Matukio yasiyozidi 26 kwa mwaka |
| 10. | Wastani wa muda ambao umeme haukuwepo (SAIDI) | Muda usiozidi dakika 1,536 kwa mwaka | Muda usiozidi dakika 1,536 kwa mwaka | Muda usiozidi dakika 1,536 kwa mwaka |
| 11. | Wastani wa muda ambao mteja amekosa umeme (CAIDI) | Muda usiozidi dakika 59 kwa mwaka | Muda usiozidi dakika 59 kwa mwaka | Muda usiozidi dakika 59 kwa mwaka |

***Chanzo:*** Wizara ya Nishati

### 4.2.5.2 TEHAMA

Sekta ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari itaendelea kutekeleza miradi ya kipaumbele inayolenga kujenga jamii jumuishi, iliyounganishwa na yenye ujuzi wa kidijitali kupitia upanuzi na uboreshaji wa miundombinu ya mawasiliano nchini. Kuimarisha miundombinu ya kitaifa ya usalama wa mtandao, utawala wa kidijitali na matumizi ya kimkakati ya teknolojia zinazoibukia ili kulinda mageuzi ya kidijitali na kuongeza ushindani wa kimataifa. Kuweka mazingira wezeshi ili kukuza ubunifu na ujasiriamali wa kidijitali, na maendeleo ya kampuni changa (startups) kwa kuhamasisha utafiti na maendeleo (R&D), uwekezaji wa ndani na wa nje, pamoja na ushirikiano wa Sekta Binafsi na Umma. Kuboresha mfumo wa utoaji data na takwimu za uzalishaji, uongezaji thamani pamoja na ajira katika majukwaa ya kidigitali kupitia maandalizi ya Akaunti Maalum ya Kupita shughuli za kidigitali (Digital Economy Satellite Account – DESA) ili kupima mchango wa shughuli hizo kwenye uchumi jumla. Kuimarisha uwezo wa kitaasisi wa kusimamia mageuzi ya kidijitali katika sekta zote,

kupanua upatikanaji wa huduma za mawasiliano zenye kuaminika, nafuu na kasi katika maeneo ya mijini na vijijini, na kukuza ujuzi wa kidijitali kwa makundi yote ya jamii. Aidha, utekelezaji huu utachochea ukuaji wa uchumi kidijitali na kuboresha maisha ya wananchi na kuiweka Tanzania katika nafasi imara ya uchumi wa kidijitali ifikapo mwaka 2050.

Utekelezaji wa malengo haya utakaofanyika kupitia miradi ya maendeleo utapelekea kuongezeka kwa mchango wa TEHAMA katika Pato la Taifa; kuongezeka kwa matumizi ya intaneti yenye kasi, simu janja, na ueneaji wa mtandao wa 4G/5G; kuboreshwa kwa utoaji wa huduma za kijamii na kiuchumi kupitia huduma za serikali mtandaoni, biashara mtandaoni, elimu na afya; kuongezeka kwa uelewa wa masuala ya kidijitali; kupungua kwa mashambulizi ya uhalifu mtandaoni; kupanda kwa nafasi ya nchi katika viwango vya usalama mtandaoni na ubunifu; kuongezeka kwa matumizi ya teknolojia zinazoibukia katika sekta muhimu; kuboreshwa kwa utoaji wa huduma za posta; kupunguza pengo la kidijitali kati ya mijini na vijijini; na kuongeza ujumuishaji wa wananchi kwa maendeleo endelevu ya kijamii na kiuchumi. Aidha, viashiria na shabaha za Sekta ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa Mwaka 2026/27 ni kama ilivyoainishwa katika **Jedwali Na. 4.28** na orodha ya miradi itakayotekelezwa kulingana na vipaumbele imeainishwa katika **Kiambatisho Na. 2**

**Jedwali Na. 4.28: Viashiria na Shabaha katika Sekta ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari**

| Na. | Kiashiria | Mwaka Kizio | Shabaha (2026/27) | Shabaha (2030/31) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Asilimia ya watumiaji wa intaneti yenye kasi nchini. | 40 (2025) | 46 | >70% |
| 2. | Mchango wa TEHAMA katika Pato la Taifa. | 1.6 (2024) | 2 | 3% |
| 3. | Ueneaji wa matumizi ya simu janja (% ya watu wanaotumia simu janja). | 37 (2025) | 43.6 | >70% |
| 4. | Asilimia ya sekta muhimu zinazotumia teknolojia zinazoibukia (AI, IoT, blockchain, green ICT). | <15 (2024) | 17 | > 25% |
| 5. | Matukio ya mashambulizi makubwa ya uhalifu mtandaoni (Incidence of Major Cyber-Attacks). | 1,200 (2024) | 1,010.00 | <250 |
| 6. | Nafasi ya nchi katika Kielezo cha Ubunifu Duniani (Global Innovation Index Rank). | 120/133 (2024) | | 60th |
| 7. | Kiwango cha uelewa wa masuala ya kidijitali kitaifa (%). | 30 (2024) | 36 | >60% |
| 8. | Nafasi ya nchi katika Kielezo cha Usalama wa Mtandao Afrika (Global Cybersecurity Index ranking in Africa). | 5th (2024) | 4.6 | 3rd |
| 9. | Kiwango cha ueneaji wa intaneti (Internet penetration rate) | 79.3 (2025) | 83.04 | 98% |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 10. | Uwiano wa watu wanaoishi vijijini wanaopata mtandao wa intaneti (%). | <25 (2024) | 33 | ≥65% |
| 11. | Gharama ya wastani ya 1GB ya intaneti (mobile data) kama asilimia ya kipato cha mwezi. | 3.5 (2024) | 3 | ≤1% |
| 12. | Asilimia ya watu wanaopata huduma za posta ndani ya km 5. | 75 (2023) | 79 | ≥95% |
| 13. | Thamani ya miamala ya biashara mtandaoni (% ya GDP). Value of e-commerce transactions as % of GDP | 1.5 (2022) | 2.2 | ≥5% |
| 14. | Asilimia ya watu wanaofikiwa na mtandao wa 4G (%). | 90 (2024) | 91.6 | 98% |
| 15. | Asilimia ya watu wanaofikiwa na mtandao wa 5G (%). | 26 (2024) | 34.8 | 70% |
| 16. | Alama ya Kielezo cha Ushindani wa Kidijitali Kitaifa (0–100 scale) %. | 32 (2023) | 35.6 | ≥50% |
| 17. | Asilimia ya huduma kuu za Serikali zinazopatikana mtandaoni. | 45 (2025) | 55 | 95% |

***Chanzo:*** Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari

#### 4.2.5.3 Uchukuzi

Sekta ya Uchukuzi itaendelea kutekeleza miradi ya kielelezo na kimkakati inayolenga kumairisha ufanisi na uunganishaji wa miundombinu ya usafiri na usafirishaji kwa kuboresha usafirishaji wa watu, bidhaa na rasilimali ndani ya miji na mikoa ili kuchochea ukuaji endelevu wa uchumi, maendeleo ya viwanda, na kuboresha upatikanaji wa masoko ya kimataifa na kuleta mageuzi ya kisekta katika usafiri na usafirishaji.

Utekelezaji wa malengo hayo kupitia miradi iliyoainishwa utawezesha kuongezeka kwa uunganishwaji wa usafiri wa anga; kuongezeka kwa wigo wa mtandao wa reli nchini; kujijenga kama kitovu cha ugavi katika Afrika Mashariki na Kati, hali itakayoboresha utoaji wa huduma za usafiri na usafirishaji na kuongeza mapato, ajira na ustawi wa wananchi; kupungua kwa msongamano wa abiria mijini hasa katika majiji makubwa; pamoja na kuongezeka kwa wigo wa miundombinu ya usafiri kwa njia ya maji. Aidha, viashiria na shabaha za sekta ya uchukuzi kwa mwaka 2026/27 ni kama vilivyoainishwa katika **Jedwali Na. 4.29** na orodha ya miradi itakayotekelezwa kulingana na vipaumbele imeainishwa katika **Kiambatisho Na. 2.**

**Jedwali Na. 4.29: Viashiria na Shabaha katika Sekta ya Uchukuzi**

| No. | Kiashiria | Mwaka wa Kizio | Shabaha (2026/27) | Shabaha (2030/31) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Uchangiaji wa Sekta ya Uchukuzi na Uhifadhi katika Pato la Taifa kwa bei za soko (%) | 7.5 (2024) | 7.54 | 7.70% |
| 2. | Ukuaji halisi wa Sekta ya Uchukuzi na Uhifadhi (%) | 4.2 (2024) | 5.08 | 8.60% |

| No. | Kiashiria | Mwaka wa Kizio | Shabaha (2026/27) | Shabaha (2030/31) |
|---|---|---|---|---|
| 3. | Muda wa meli kurejea kituoni kwake (Wastani wa siku) | 13.7 (Des, 2025) | 3 days | 3 days |
| 4. | Kiasi cha shehena iliyohudumiwa kupitia Bandari kwa mwaka (tani) | 32,753,618 (2024/25) | 42,372,709 | 62,029,618 |
| 5. | Urefu wa Reli ya SGR iliyojengwa (km) | 747 (Dis, 2025) | 1,219 | 1,721 |
| 6. | Kiasi cha shehena iliyosafirishwa kwa reli (tani) kwa mwaka | 531,359 (2024/25) | 2,334,000 | 8,347,989 |
| 7. | Idadi ya ndege za ATCL zinazofanya kazi | 16 (Des, 2025) | 18 | 28 |
| 8. | Idadi ya abiria waliosafirishwa kwa ndege za ATCL kwa mwaka | 1,178,025 (2024/25) | 1,750,056 | 3,125,463 |

***Chanzo:*** Wizara ya Uchukuzi

### 4.3 Programu za Kielelezo

Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2026/27 unatoa kipaumbele katika utekelezaji wa miradi iliyokuwa ya kielelezo katika Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka mitano (FYDP III) ambao utekelezaji wake unafika ukingoni. Aidha, Mpango huu utaweka msingi wa maandalizi ya utekelezaji wa miradi shikizi iliyoainishwa katika programu za kielelezo ambayo utekelezaji wake bado haujaanza. Maelekezo ya kina ya miradi shikizi ni kama ilivyoanishwa katika **Jedwali Na.4.30.**

**Jedwali Na. 4.30: Programu za Kielelezo na Miradi Shikizi**

| Na. | Mradi Shikizi | Gharama za utekelezaji kwa mwaka |
|---|---|---|
| **A** | **Mji wa Uwekezaji wa Bahari Bagamoyo na Usafiri fungamanishi** | |
| 1. | Ujenzi wa Bandari ya Mbegani | 3,000,000,000 |
| 2. | Ujenzi wa Reli ya Kati kwa kiwango cha Kimataifa cha SGR kipande cha 3–7. | 2,520,199,299,173 |
| 3. | Barabara - Pangani – Bagamoyo, Kigamboni – Chanika – Kibaha – Mbweni (77.5 km), | 2,000,000,000 |
| 4. | Kibaha–Morogoro–Dodoma Expressway (465 km) | 200,000,000 |
| 5. | Uendelezaji wa Viwanja 14 vya Ndege | 335,154,279,076 |
| 6. | Mkongo wa Taifa wa mawasiliano | 80,700,000,000 |
| 7. | Ujenzi wa Kituo Kikuu na Vituo vidogo vya kuendeleza ubunifu katika TEHAMA (ICT Parks) | 24,850,000,000 |
| 8. | Mradi fungamanishi wa biashara na usafirishaji | 100,000,000,000 |
| 9. | Mradi wa kuboresha wa bandari ya Dar es Salaam | 125,449,686,540 |
| 10 | Eneo maalumu la uwekezaji Bagamoyo | 294,984,477,689 |
| **B** | **Kitovu Changamani cha makaa ya mawe Mchuchuma na Chuma Liganga** | |
| 11 | Mradi wa Chuma cha pua Maganga Matitu - Ludewa | 125,000,000 |
| 12 | Mradi wa ujenzi wa barabara - Mawengi – Manda (110 km) | 10,000,000,000 |
| 13 | Barabara ya Mkiu – Mavanga – Madaba (112 km) | 1,200,000,000 |
| 14 | Barabara ya Nkomang'ombe – Liganga (70 km) | 18,000,000,000 |
| 15 | Barabara ya Nkomang'ombe – Mchuchuma (7 km) | 3,500,000,000 |
| 16 | Barabara ya Igawa –Tunduma ikiwemo barabara ya mchepuo (Bypass) Uyole (266.9 km) | 35,830,000,000 |

| Na. | Mradi Shikizi | Gharama za utekelezaji kwa mwaka |
|---|---|---|
| 17 | Ujenzi wa Miundombinu ya Mawasiliano Vijijini | 131,077,860,000 |
| 18 | Mradi wa makaa ya mawe Mchuchuma na Chuma Liganga | 826,230,000 |
| **C** | **Programu ya Kitaifa ya Umwagiliaji na Mageuzi ya Viwanda vya Kilimo** | |
| 19 | Miradi ya Umwagiliaji ya Rufiji, Songwe, Mara, Bugwema, Lumpungu, Kamsamba na Membe | 209,090,000,000 |
| 20 | Barabara ya Rufiji - Kilwa - Morogoro | 10,000,000,000 |
| 21 | Barabara ya Handeni–Kiberashi- Kibaya–Singida (km 424.24) | 7,150,000,000 |
| **D** | **Kitovu cha Teknolojia na Uchakataji wa Madini Adimu – Dodoma** | |
| 22 | Barabara ya Nyakahura –Kamubuga-Rulenge- Kabanga Nickel (141 km) | 23,300,000,000 |
| 23 | Barabara ya Kidatu – Ifakara – Lupilo – Malinyi – Londo - Lumecha/Songea (499 km) | 5,000,000,000 |
| 24 | Mradi wa Tanzania ya Kidigitali | 15,000,000,000 |
| 25 | Mradi wa Magadi soda – Engaruka | 2,000,000,000 |
| 26 | Mradi wa Utafiti wa Kina wa Jiofizikia kwa kutumia Ndege | 53,097,080,000 |
| 27 | Eneo maalum la uwekezaji Dodoma | 1,000,000,000 |
| **E** | **Kiwanda cha Kuchakata Gesi Asilia ya kimiminika (LNG) – Lindi** | |
| 28 | Mradi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Ghafi kutoka Uganda hadi Tanzania | 100,000,000,000 |
| 29 | Ujenzi wa Bomba la Kusafirishia Gesi kutoka Ntorya hadi Madimba | 23,200,000,000 |
| 30 | Mradi wa LNG - Lindi | 20,000,000,000 |
| **F** | **Kitovu cha Viwanda na Uchumi wa Buluu Katika kanda ya ziwa** | |
| 31 | Uimarishaji wa shirika la ndege - ATCL | 220,029,600,000 |
| 32 | Mradi wa maji wa ziwa Victoria - Dodoma | 100,000,000,000.00 |
| 33 | Ujenzi wa Meli ya Mizigo yenye Reli Iliyopachikwa | 200,000,000,000 |
| 34 | Eneo maalum la uwekezaji Mwanza | 1,000,000,000 |
| **G** | **Programu Shirikishi ya Uendelezaji wa Miji nchini** | |
| 35 | Mradi wa Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi | 9952810000 |
| 36 | Uboreshaji wa Milki za Ardhi | 36,380,531,647.58 |
| 37 | Miradi ya kuzalisha umeme kwa kutumia Nishati Mpya na Mbadala | 123,993,578,000 |
| 38 | Uimarishaji wa Hospitali za Rufaa | 152,300,000,000 |
| | **Jumla Kuu** | **4,799,590,432,126** |

***Chanzo:*** Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano

Vigezo vilivyotumika katika kuandaa miradi na programu za maendeleo kwa mwaka 2026/27 ili kutekeleza maeneo ya vipaumbele ni kama ifuatavyo: Uwezo wa kuleta mabadiliko ya kimfumo; utayari wa kuanza utekelezaji; kuchochea ukuaji wa sekta nyingine; uwezo wa kuzalisha ajira kwa wingi; uwezo wa kuleta mageuzi katika uchumi; uhifadhi wa mazingira na uhimilivu wa mabadiliko ya tabianchi. Aidha, programu zimechaguliwa kwa kuzingatia ulinganifu wa kimkakati na Dira 2050, LTPP na FYDP IV; faida ya kijamii na kiuchumi; uwezo na nafasi yake katika kuongeza kasi ya uzalishaji viwandani; kupanua na kuboresha huduma; kuongeza mauzo ya nje; na uwezo na nafasi yake katika kutengeneza ajira kwa wingi.

### 4.4. Mwelekeo wa Kimkakati na Mageuzi kwa mwaka 2026/27

Katika mwaka 2026/27, jitihada zitajikita katika maeneo yafuatayo:

i. Kufanya mageuzi ya mifumo na utawala bora ili kujenga msingi wa utawala bora, uwazi na ufanisi.
ii. Kufanya mageuzi ya kiuchumi yanayolenga usimamizi wa uchumi ili kuongeza wigo wa ukuaji wa sekta za uzalishaji zikiwemo kilimo, viwanda, huduma na uchumi wa kidijitali.
iii. Kufanya mageuzi ya sekta ya nishati katika sera na mifumo ili kukidhi mahitaji ya umeme nchini.
iv. Kuimarisha maandalizi ya miradi (Project Preparation): Serikali itaongeza uwekezaji katika hatua za awali za miradi ili kuhakikisha inakidhi vigezo vya kifedha, kiuchumi na kisheria vinavyohitajika kuvutia wawekezaji. Hii itahusisha:
    i. Kuandaa upembuzi yakinifu wa kina (feasibility studies);
    ii. Kufanya tathmini za athari za kiuchumi, kijamii na kimazingira;
    iii. Kuandaa miundo ya kifedha (financial structuring) na uchambuzi wa vihatarishi (risk allocation).
    iv. Kutengwa kwa rasilimali mahsusi kwa ajili ya wataalam wa kiufundi (transaction advisory), kifedha na kisheria watakaosaidia kuandaa miradi inayoweza kufadhiliwa (bankable projects). Lengo ni kuhakikisha miradi inakuwa na mvuto kwa wawekezaji wa ndani na nje, pamoja na taasisi za fedha.
v. Kuendeleza Mkakati wa Miradi ya PPP (PPP Pipeline): Kuandaa na kusimamia orodha ya miradi ya kimkakati inayoweza kutekelezwa kwa PPP katika sekta za kipaumbele kama nishati, usafiri na usafshaji, miundombinu ya maji, TEHAMA, viwanda na maendeleo ya miji.
vi. Kuimarisha mazingira ya biashara na uwekezaji: Mageuzi ya kisheria na kiutawala yataendelea ili kupunguza urasimu, kuongeza uwazi na kuimarisha utabirikaji wa kisera, hatua ambazo ni muhimu kwa kuongeza imani ya wawekezaji.
vii. Kutumia mwongozo wa kitaifa wa upangaji: Mwongozo huu unahakikisha sekta zinaandaa mipango mikakati yake kwa kuzingatia vipaumbele vya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2026/27 – 2030/31 pamoja na Dira 2050.
viii. Kufanya mageuzi ya mashirika ya umma ili kuongeza mchango wake katika uwekezaji na kuunganisha baadhi ya mashirika ili kuongeza ufanisi.

# SURA YA TANO

# UGHARAMIAJI WA MPANGO

## 5.1 Utangulizi

Sura hii inaeleza mwelekeo na mkakati wa ugharamiaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2026/27. Mpango huu ni wa kwanza katika utekelezaji wa FYDP IV na ni hatua ya awali ya utekelezaji wa Dira 2050 ambayo inalenga kujenga taifa lenye uchumi imara, unaotegemea rasilimali za ndani na ushirikiano wa sekta binafsi.

Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2026/27 ni mpango wa kimkakati, ambao unaweka msingi wa mageuzi makubwa ya muda mrefu katika matumizi ya rasilimali za taifa. Katika muktadha huu, Serikali inahama kutoka mfumo uliozoeleka wa kutumia bajeti ya umma na mikopo, na kuelekea mfumo wa ugharamiaji shirikishi unaolenga: Ushirikiano mkubwa wa sekta binafsi, ikilenga zaidi ya asilimia 70 ya jumla ya rasilimali za Mpango; Serikali kuwa mwezeshaji, msimamizi, na kichocheo *(catalyst)* cha uwekezaji, kwa kuhimiza mazingira endelevu ya kibiashara; Matumizi ya vyanzo bunifu vya ugharamiaji *(innovative finance)* ili kuvutia uwekezaji na kupanua vyanzo vya rasilimali; na nidhamu madhubuti ya fedha, ikijumuisha usimamizi makini wa madeni, uwazi katika mapato na matumizi, na utendaji unaofungwa na matokeo.

## 5.2 Mahitaji ya fedha kwa mwaka 2026/27

Mahitaji ya fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2026/27 yanakadiriwa kufikia kiasi cha shilingi trilioni 20.7 kutoka kwenye bajeti ya Serikali sawa na asilimia 33.3 ya Bajeti Kuu ya Serikali ya shiling trilioni 62.3.

### 5.2.1 Vyanzo vya Mapato kwa Mwaka 2026/27

Vyanzo vya mapato vinavyotarajia kuchangia katika utekelezaji wa Mpango 2026/27 vitatokana na vyanzo vinne vikuu kama ifuatavyo:

i. Mapato ya ndani: kodi, mapato yasiyo ya kodi, gawio kutoka kwa mashirika ya umma na mapato ya halmashauri;
ii. Rasilimali fedha za nje: mikopo nafuu, misaada, na mikopo isiyo nafuu kwa miradi ya kibiashara;
iii. Mitaji ya Sekta Binafsi: ushiriki wa sekta binafsi katika ufadhili wa miradi; na
iv. Mbinu bunifu za ufadhili na masoko ya hati fungani: kama vile hati fungani za za Serikali; Hati Fungani; Mfumo wa Uuzaji wa Hisa za Kaboni (Soko la Kaboni Tanzania) (Carbon Credit Trading Framework) (Tanzania Carbon Exchange); Vyanzo Mseto vya Ufadhili katika sekta za nishati, kilimo na uwezeshaji wa mikopo kwa wafanyabiashara wa kati na wadogo; na Sera ya Ugeuzaji Takwimu kuwa Chanzo cha Mapato (Data Monetization Policy).

### 5.2.2 Mwelekeo wa Sera ya Fedha na Bajeti kwa 2026/27

Katika mwaka 2026/27, Serikali itatekeleza sera za fedha na bajeti zinazolenga kulinda uthabiti wa uchumi, kuongeza uwezo wa ndani wa ugharamiaji, na kuweka misingi ya ushiriki mkubwa wa sekta binafsi katika kufadhili maendeleo. Mwelekeo huu unalenga:

i. Kuongeza uwiano wa mapato ya ndani kwa Pato la Taifa kwa kuimarisha mifumo ya kodi, kuongeza wigo wa kodi, na kuongeza ufanisi wa TRA;
ii. Kudhibiti nakisi ya bajeti ili kuhakikisha uhimilivu wa deni la Taifa sambamba na viwango vya kimataifa;
iii. Kuhamisha matumizi kutoka kwenye gharama zisizo za uzalishaji na kuelekeza kwenye miradi ya kimkakati yenye tija na matokeo ya kitaifa;
iv. Kuongeza matumizi katika sekta zinazochochea ukuaji kama vile nishati, viwanda, TEHAMA, kilimo, miundombinu na ujuzi; na
v. Kuongeza matumizi ya mifumo ya fedha ya kijani, kidigitali na mseto (blended finance) kama msingi wa fedha za miaka ijayo ya Dira 2050.

Ili kufikia lengo la kukusanya na kutumia shilingi trillioni 20.7 kwa ajili ya shughuli za maendeleo. Serikali itachukua hatua zifuatazo:

i. Kudhibiti nakisi ya bajeti isizidi asilimia 3.0 ya Pato la Taifa;
ii. Kuhakikisha mapato ya ndani yanafikia asilimia 17.1 ya Pato la Taifa;
iii. Kuimarisha nidhamu ya matumizi kupitia usimamizi makini na ufanisi katika matumizi ya rasilimali za umma;
iv. Kuhakikisha miradi inayofadhiliwa kwa mikopo inaleta matokeo ya muda mrefu yenye manufaa kwa vizazi vijavyo; na
v. Kuimarisha mifumo ya ufuatiliaji wa fedha kupitia Results-Based Monitoring, Evaluation, Accountability and Learning (RBMEAL) ili kuhakikisha uwajibikaji na ufanisi

### 5.2.3 Uboreshaji wa Matumizi na Nidhamu ya Kifedha

Ili kuhakikisha rasilimali za umma zinatumika kwa ufanisi na kuleta matokeo makubwa ya maendeleo, Serikali italenga kufanya mageuzi ya bajeti na ya mashirika ya umma. Lengo ni kuongeza thamani ya fedha (value for money) kwa kila shilingi ya umma kwa kupunguza matumizi yasiyo ya lazima, kuongeza utaratibu wa bajeti inayozingatia utendaji (Performance-Based Budgeting), kuhamisha rasilimali kwenye miradi ya kimkakati, na kuimarisha udhibiti wa malimbikizo ya madai.

## 5.3 Ushiriki wa Mashirika ya Umma (PSCs)

Mashirika ya Umma yanayojiendesha kibiashara yanatarajiwa kuongeza uwekezaji hadi shilingi trilioni 5.5 mwaka 2026/27 kwa kufanya yafuatayo: kupunguza ruzuku kwa angalau asilimia 10; kupunguza hasara kwa angalau asilimia 15; kuanzisha *corporate bonds* na mpango wa *Asset Monetisation*; kuunganisha baadhi ya mashirika ya umma ili kuongeza ufanisi; kuwezesha mashirika ya umma kuingia kwenye masoko ya mitaji (IPO) ili kuongeza ushiriki wa wananchi katika kukuza mitaji. Uwekezaji huo utatokana na faida ya utekelezaji wa shughuli zao katika sekta za nishati; usafiri na usafirishaji; kilimo; ulinzi na usalama; afya; milki; utalii; mawasiliano; madini; huduma za fedha; na viwanda na uzalishaji kama unavyoonekana kwenye **Kielezo Na 5.1.**

**Kielelezo Na. 5.1 : Mchango wa Uwekezaji wa Mashirika ya Umma kwa Shughuli za Kiuchumi kwa mwaka 2026/27**




***Chanzo:*** Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano

### 5.4 Uwekezaji wa Sekta Binafsi

Sekta binafsi inatarajiwa kuwekeza shilingi trilioni 60.1 sawa na asilimia 70 ya rasilimali. Uwekezaji huu utatokana na uwekezaji wa ndani *(Domestic Direct Investment – DDI)*; uwekezaji wa moja kwa moja wa nje *(Foreign Direct Investment – FDI)*; ubia kati ya sekta ya umma na binafsi; na masoko ya mitaji na fedha mseto *(blended finance)*.

Mchango wa sekta binafsi katika shughuli za uchumi hupimwa kupitia uwekezaji wake katika ukuzaji wa mtaji, hususan katika mali za kudumu kama viwanda, mitambo, mashine, miundombinu ya uzalishaji, teknolojia, na miradi ya kibiashara. Upimaji rasmi wa mchango huu hufanyika kupitia kipimo cha *Gross Fixed Capital Formation (GFCF)*. Kipimo hiki huonesha kiwango cha uwekezaji katika shughuli za uchumi baina ya sekta ya umma na sekta binafsi.

Takwimu zinaonesha kuwa katika kipindi cha mwaka 2018 hadi 2024, Sekta binafsi imechangia wastani wa takribani asilimia 70 ya jumla ya uwekezaji katika shughuli za uchumi za kila mwaka. Uwekezaji wa sekta binafsi umeongezeka kutoka shilingi trilioni 28.7 mwaka 2018 hadi shilingi trilioni 54.0 mwaka 2024. Sekta ya umma imeendelea kuchangia wastani wa takribani asilimia 30 ya jumla ya uwekezaji.

Uwiano huu wa takribani 70:30 umeendelea kuwa thabiti kwa kipindi chote, kama inavyooneshwa katika **Jedwali 5.1** hapo chini.

**Jedwali 5.1: Mwenendo wa uwekezaji wa Sekta ya umma na binafsi katika shughuli za kiuchumi (Tsh. milioni)**

| Mwaka | Mchango wa Uwekezaji kutoka Sekta ya Umma (Public GFCF) | Mchango wa Uwekezaji kutoka Sekta binafsi (Private GFCF) | Asilimia ya Uwekezaji kutoka Sekta binafsi | Asilimia ya Uwekezaji kutoka Sekta ya Umma |
|---|---|---|---|---|
| 2018 | 12,482,193 | 28,659,770 | 69.7% | 30.3% |
| 2019 | 14,853,202 | 35,157,613 | 70.3% | 29.7% |
| 2020 | 18,576,783 | 41,542,256 | 69.1% | 30.9% |
| 2021 | 20,334,802 | 46,887,021 | 69.7% | 30.3% |
| 2022 | 20,231,100 | 48,016,360 | 70.4% | 29.6% |
| 2023 | 20,944,360 | 50,538,097 | 70.7% | 29.3% |
| 2024 | 23,134,621 | 53,992,156 | 70.0% | 30.0% |

***Chanzo:*** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

Ili kufikia malengo na shabaha za Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2026/27, Sekta binafsi inatarajiwa kuwekeza katika sekta za kimageuzi na vichocheo ikiwemo usafiri na usafirishaji, nishati, madini, biashara, viwanda na uzalishaji, kilimo, milki, utalii na huduma za fedha. Mgawanyo huu ni kama unavyoonekana kwenye **Kielelezo Na. 5.2.**

**Kielelezo Na. 5.2. Mwelekeo wa Uwekezaji wa Sekta Binafsi kwa Shughuli za Kiuchumi kwa mwaka 2026/27**




***Chanzo:*** Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano

Mikakati ya ushirikishwaji wa Sekta binafsi kuwekeza shilingi trilioni 60.1 ni kama ifuatavyo:

i. Kupanua fursa za upatikanaji wa mikopo na rasilimali fedha katika kuwezesha ushirikishwaji wa sekta binafsi na benki za maendeleo, taasisi za fedha na wawezeshaji wa mitaji;
ii. Kupunguza vikwazo vya kibiashara ili kuweka mazingira rafiki ya ukuaji na ufanyaji wa biashara ndani na nje ya nchi kupitia utekelezaji wa MKUMBI II;
iii. Kuhamasisha urasimishaji wa biashara ndogo na za kati kupitia taasisi za usimamizi wa biashara;
iv. Kuhamasisha uwekezaji katika uboreshaji wa mifumo ya biashara, teknolojia, na ubunifu kwa biashara ndogo na za kati ili kuongeza tija na ushindani;
v. Kuongeza wigo wa ushirikiano wa kimataifa ili kuvutia na kuimarisha uwekezaji wa nje katika sekta za kimageuzi; kuboresha miundombinu ya mipakani kwa lengo la kuimarisha barabara, reli, na vituo vya forodha ili kurahisisha biashara na usafiri kati ya Tanzania na nchi jirani; na
vi. Kuimarisha ushirikishwaji wa vyama vya wafanyabiashara wakubwa ili kuchochea uwekezaji wa ndani kama CTI, TPSF, TNCC n.k.

# SURA YA SITA

# UFUATILIAJI NA TATHMINI

## 6.1 Utangulizi

Sura hii inaeleza mfumo wa ufuatiliaji, tathmini na utoaji taarifa katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2026/27. Mfumo huu umejengwa katika misingi ya usimamizi unaozingatia matokeo na unaolenga kuhakikisha kuwa utekelezaji wa mpango unafuatiliwa kwa kuzingatia mnyororo wa matokeo, hususan katika ngazi ya matokeo ya muda mfupi (outputs) na matokeo ya muda wa kati (outcomes).

Katika kufikia malengo ya mpango, ufuatiliaji, tathmini na utoaji taarifa ni nyenzo muhimu za usimamizi na uwajibikaji. Mfumo huu utawezesha ukusanyaji na uchambuzi wa taarifa sahihi kwa wakati ili kupima hatua zilizofikiwa katika utekelezaji, kubaini changamoto mapema, na kuchukua hatua stahiki za maboresho. Aidha, mfumo wa ufuatiliaji utachangia kuongeza uwazi na uwajibikaji, thamani ya fedha, kuwezesha matumizi ya uchambuzi unaozingatia takwimu sahihi katika kufanya maamuzi, na kutoa mrejesho kwa wananchi na wadau wengine wa maendeleo.

Kwa ujumla, mfumo wa ufuatiliaji na tathmini utahakikisha utekelezaji wa mpango unakuwa wenye tija, na unaolenga matokeo yaliyopangwa. Uwajibikaji na uwazi vitajengwa katika mnyororo wa matokeo unaoonesha uhusiano kati ya rasilimali zilizotumika, shughuli zilizotekelezwa, matokeo ya kijamii na kiuchumi yaliyopatikana katika kipindi cha muda mfupi, wa kati, na muda mrefu. Mfumo huu utawezesha kufuatilia hatua zilizofikiwa kwa uwazi na kuchukua hatua za maboresho pale inapobidi.

## 6.2 Malengo ya Mfumo wa Ufuatiliaji, Tathmini na Utoaji wa Taarifa

Malengo ya mfumo huu ni:

i. Kufuatilia utekelezaji wa shughuli na matumizi ya rasilimali dhidi ya malengo ya mwaka;
ii. Kupima maendeleo ya utekelezaji wa viashiria vya muda mfupi, wa kati, na muda mrefu;
iii. Kubaini changamoto na kupendekeza hatua za kuzitatua;
iv. Kuandaa na kuwasilisha taarifa sahihi za utekelezaji ambazo zitakuwa msingi wa kufanya maamuzi ya kisera na kiutendaji; na
v. Kuwa kigezo kikuu cha uwajibikaji kwa Wakuu wa Taasisi za Umma.

## 6.3 Mfumo wa Matokeo

Mfumo wa matokeo utaunganisha malengo ya mpango na viashiria vya utekelezaji katika ngazi zifuatazo:

| Ngazi | Maelezo |
|---|---|
| **Athari** | Mabadiliko ya muda mrefu katika ustawi wa |

| | |
|---|---|
| | jamii na ukuaji wa uchumi yanayotokana na utekelezaji wa mpango. |
| **Matokeo ya muda wa kati** | Mabadiliko katika upatikanaji, ubora au matumizi ya huduma kwa walengwa, kama vile kuimarika kwa masoko, huduma za afya au elimu. |
| **Matokeo ya muda mfupi** | Bidhaa au huduma zilizokamilika kutokana na utekelezaji wa shughuli, mfano: jengo la hospitali, barabara iliyokamilika, visima vilivyochimbwa. |
| **Shughuli** | Hatua mahsusi zinazotekelezwa ili kuzalisha matokeo ya moja kwa moja, mfano: ujenzi wa barabara za lami, ujenzi wa ofisi, uchimbaji wa visima virefu. |
| **Rasilimali** | Fedha, watumishi, vifaa, muda na rasilimali nyingine zinazotumika kutekeleza shughuli za mpango. |

## 6.4 Mfumo wa Ufuatiliaji

Mfumo huu unaainisha viashiria vya kupima matokeo ya moja kwa moja na matokeo ya muda wa kati; utaratibu wa ukusanyaji, uchambuzi, na utoaji wa taarifa; muundo wa kitaasisi; pamoja na utaratibu wa utoaji mrejesho.

### 6.4.1 Njia za Ufuatiliaji

i. Ziara za ukaguzi wa miradi.
ii. Taarifa za utekelezaji robo mwaka wa miradi na viashiria vya mpango.
iii. Mfumo wa Taifa wa Usimamizi wa Miradi ya maendeleo - NPMIS.
iv. Vikao vya mapitio ya utekelezaji kila robo mwaka.

### 6.4.2 Ngazi za Ufuatiliaji

Ufuatiliaji utafanyika katika ngazi zifuatazo:

i. **Ngazi ya shughuli:** watekelezaji wa miradi na afua zote za mpango wanapaswa kufanya ufuatiliaji wa moja kwa moja wa utekelezaji na kutoa taarifa.
ii. **Ngazi ya matokeo muda mfupi:** Utekelezaji wa shughuli utazalisha matokeo ya muda mfupi ambayo yatafanyiwa ufuatiliaji na watekelezaji, waratibu wa mipango katika ngazi ya wizara, pamoja na ngazi ya kitaifa ikiwemo Tume ya Taifa ya Mipango, kwa msingi wa mwezi au robo mwaka kulingana na ratiba ya ufuatiliaji.
iii. **Ngazi ya matokeo ya muda wa kati:** Ufuatiliaji utafanyika ili kupima mabadiliko katika upatikanaji, ubora na matumizi ya huduma kwa walengwa yanayotokana na matokeo ya moja kwa moja. Ufuatiliaji huu utafanywa na wizara, taasisi na mamlaka husika kwa kushirikiana na Tume ya Taifa ya Mipango, kwa kutumia tafiti, takwimu za kiutawala na mapitio ya utekelezaji wa mara kwa mara. Taarifa zitakazopatikana zitatumika kupima mafanikio ya mpango na kufanya maboresho ya kisera na kiutendaji.

## 6.5 Mfumo wa Tathmini

Tathmini itafanyika ili kupima ufanisi, tija, uendelevu na matokeo ya mpango.

### 6.5.1 Aina za Tathmini

i. Tathmini ya utekelezaji wa mpango kwa robo mwaka, nusu mwaka, na mwisho wa mwaka kupitia viashiria vya matokeo ya moja kwa moja na matokeo ya muda wa kati.
ii. Tathmini maalum kulingana na mahitaji.

## 6.6 Mfumo wa Utoaji Taarifa

Mfumo wa utoaji taarifa utawezesha mawasiliano ya matokeo kwa wadau mbalimbali. Taarifa za utekelezaji wa miradi zitawasilishwa kulingana na Mwongozo wa Usimamizi wa Uwekezaji wa Umma (Public Investment Management Guideline – PIMG) pamoja na **Kiambatisho Na. 1** kwa ajili ya utekelezaji wa viashiria vya mpango. Aidha, taarifa zote za utekelezaji wa miradi pamoja na viashiria vya mpango zitaandaliwa na kuwasilishwa kupitia mfumo wa Mfumo wa Kitaifa wa Usimamizi wa Miradi ya Maendeleo. Aina za taarifa za utekelezaji wa miradi ya maendeleo na viashiria vya Mpango ni kama ifuatavyo:

i. Taarifa ya robo mwaka kwa viashiria vya matokeo ya moja kwa moja na viashiria vya matokeo ya muda wa wakati;
ii. Taarifa ya nusu mwaka;
iii. Taarifa ya mwaka; na
iv. Taarifa maalum.

## 6.7 Ratiba ya Ufuatiliaji na Tathmini

Ratiba ya ufuatiliaji na tathmini inalenga kuhakikisha utekelezaji wa mpango na miradi unafanyika kwa ufanisi, kwa wakati, na kwa kuzingatia malengo yaliyowekwa. Idara na Vitengo vya Ufuatiliaji na Tathmini vinapaswa kuandaa mpango wa ufuatiliaji na tathmini wa utekelezaji wa mpango kwa ujumla pamoja na mipango mahsusi ya ufuatiliaji na tathmini kwa kila mradi.

**i. Ufuatiliaji wa Kila Robo Mwaka:** Idara na Vitengo vya Ufuatiliaji na Tathmini vya Wizara, Taasisi, na Idara zinazojitegemea vitafanya ufuatiliaji na tathmini ya robo mwaka kwa miradi yote ya maendeleo pamoja na viashiria vya mpango, hususan viashiria vya matokeo ya muda mfupi, kulingana na shabaha za robo mwaka. Taarifa za robo mwaka zitaandaliwa na kuwasilishwa Tume ya Taifa ya Mipango kupitia wizara za kisekta, kwa kuzingatia mipango ya ufuatiliaji na tathmini ya kila mradi pamoja na miongozo iliyopo. Taarifa ziwasilishwe kupitia mfumo wa NPMIS.

**ii. Ufuatiliaji na Tathmini ya Nusu Mwaka:** Idara na Vitengo vya Ufuatiliaji na Tathmini vitafanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa miradi kwa nusu mwaka, kwa kuzingatia mipango ya ufuatiliaji na tathmini ya miradi husika. Aidha, tathmini ya utekelezaji wa mpango itafanyika kupitia viashiria vya matokeo ya muda mfupi na muda wa kati, kulingana na shabaha za nusu mwaka zilizowekwa katika mpango wa maendeleo. Taarifa zitawasilishwa kupitia mfumo wa NPMIS.

**iii. Ufuatiliaji na Tathmini ya Mwaka:** Idara na Vitengo vya Ufuatiliaji na Tathmini vitafanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa miradi kwa mwaka, kwa kuzingatia mpango kazi wa mwaka husika. Vile vile, tathmini ya viashiria vya muda mfupi na muda wa kati vya mpango wa maendeleo itafanyika kulingana na shabaha za mwaka, ili kupima kiwango cha utekelezaji, mafanikio

yaliyopatikana, changamoto, na hatua za kuboresha utekelezaji katika kipindi kinachofuata. Taarifa zitawasilishwa kupitia mfumo wa NPMIS.

### 6.8 Taarifa za utekelezaji wa miradi, ufuatiliaji, na tathmini

Taarifa zote za utekelezaji wa miradi ya maendeleo pamoja na taarifa za ufuatiliaji na tathmini ya viashiria vya mpango wa muda mfupi na muda wa kati zitaandaliwa na kuwasilishwa Tume ya Taifa ya Mipango kupitia mfumo wa NPMIS. Kwa kuzingatia umuhimu wa taarifa hizi katika kufanya maamuzi ya maendeleo, Wakuu wa Taasisi za Umma wanapaswa kuzingatia masuala yafuatayo:

i. **Taarifa za ufuatiliaji na tathmini zitakuwa kigezo kikuu cha kupima utendaji** wa taasisi pamoja na wakuu wa taasisi husika. Taasisi ambazo hazitaandaa na kuwasilisha taarifa kwa mujibu wa ratiba iliyowekwa zitachukuliwa hatua za kiutendaji na kinidhamu kulingana na taratibu za utumishi wa umma.

ii. **Tume itaandaa taarifa za jumla za ufuatiliaji na tathmini** na kuziwasilisha katika vikao vya kimaamuzi, ikiwemo IMT, BLM, pamoja na vikao kazi vingine vya Serikali, kwa lengo la kuwezesha maamuzi sahihi na ya wakati.

iii. **Taarifa za ufuatiliaji na tathmini zitatumika kama msingi wa kuidhinisha utoaji wa fedha** kwa miradi na afua mbalimbali. Hivyo, Tume itaishauri Wizara ya Fedha kusitisha utoaji wa fedha kwa miradi au taasisi ambazo hazijawasilisha taarifa za utekelezaji na ufuatiliaji kwa wakati. Lengo ni kuhakikisha kuwa matumizi ya rasilimali yanaendana na matokeo halisi ya utekelezaji.

iv. **Tume haitapokea wala kufanyia kazi taarifa zitakazowasilishwa nje ya mfumo wa NPMIS.** Hatua hii inalenga kuhakikisha ufanisi katika uchakataji wa taarifa, kuongeza uwazi na uwajibikaji, pamoja na kupunguza matumizi ya karatasi na gharama zisizo za lazima.

v. **Maamuzi yote yanayohusu miradi na mipango ya maendeleo yatazingatia taarifa za ufuatiliaji na tathmini.** Tume itatoa ushauri kwa Serikali kwa kuzingatia ushahidi na takwimu zilizowasilishwa kupitia mfumo, ili kuhakikisha maamuzi yanayofanyika yanaendana na hali halisi ya utekelezaji.

### 6.9 Mgawanyo wa Majukumu

| Mdau | Wajibu wa Msingi | Muda wa Kutoa taarifa |
|---|---|---|
| **Tume ya Taifa ya Mipango** | Kusimamia NPMIS, kupokea na kufanya mapitio ya taarifa za utekelezaji kitaifa za kila wiki kwa miradi ya kielelezo, robo mwaka, na kufanya ufuatiliaji na tathmini | Kila robo mwaka, nusu mwaka, na mwaka |
| **Wizara / Idara Zinazojitegemea** | Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya kila mara na kutoa taarifa kulingana na mpango wa mwaka wa ufuatiliaji na tathmini; kuandaa na kuingiza taarifa za utekelezaji na ufuatiliaji na tathmini kwenye NPMIS. | Kulingana na mwongozo wa PIMG pamoja na mpango wa mwaka wa ufuatiliaji na tathmini. |
| **Sekretarieti za Mikoa** | Kusimamia utekelezaji wa mipango ya ufuatiliaji na tathmini za halmashauri; | Kulingana na mwongozo wa PIMG |

| Mdau | Wajibu wa Msingi | Muda wa Kutoa taarifa |
|---|---|---|
| | kufuatilia utekelezaji wa mpango wa maendeleo katika ngazi ya mkoa na halmashauri; kuandaa taarifa na kuwasilisha OR TAMISEMI. | pamoja na mpango wa mwaka wa ufuatiliaji na tathmini |
| **Mamlaka za Serikali za Mitaa** | Kusimamia utekelezaji wa mipango ya ufuatiliaji na tathmini; kufanya ufuatiliaji na tathmini; Kutoa taarifa za utekelezaji wa mpango pamoja na miradi katika ngazi ya halmashauri kwenye mfumo wa NPMIS. | Kulingana na mwongozo wa PIMG pamoja na mpango wa mwaka wa ufuatiliaji na tathmini. |
| **Wakala na Mashirika ya Umma** | Kusimamia utekelezaji wa mipango ya ufuatiliaji na tathmini; kufanya ufuatiliaji na tathmini; Kutoa taarifa za utekelezaji wa mpango pamoja na miradi katika ngazi ya taasisi kwenye mfumo wa NPMIS. | Kulingana na mwongozo wa PIMG pamoja na mpango wa mwaka wa ufuatiliaji na tathmini. |
| **Sekta Binafsi na Asasi za Kiraia** | Kushirikiana na Serikali katika kusimamia na kutoa taarifa sahihi wakati wa ufuatiliaji na tathmini; kuwasilisha maoni na ushauri wao moja kwa moja Tume ya Taifa ya Mipango ili kusaidia kuboresha utekelezaji wa mpango wa maendeleo | Inapohitajika. |

# SURA YA SABA

# VIHATARISHI VYA MPANGO KWA MWAKA 2026/27

## 7.1 Utangulizi

Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2026/27 umebainisha vihatarishi vinavyoweza kuathiri utekelezaji wake, pamoja na kuainisha mikakati madhubuti ya kupunguza au kudhibiti vihatarishi hivyo. Lengo kuu ni kuhakikisha ustahimilivu, ufanisi, na uendelevu katika utekelezaji wa malengo na matokeo yaliyopangwa. Aidha, zoezi la utambuzi wa vihatarishi limezingatia Mwongozo wa Usimamizi wa Vihatarishi katika Sekta ya Umma, 2023.

## 7.2 Maeneo ya Vihatarishi na Mikakati ya Kudhibiti

Mpango utatekelezwa katika sera changamano na mazingira ya kiuchumi yanayobainisha fursa zinazoibuka pamoja na vihatarishi vya aina mbalimbali.Vihatarishi hivi ni vya Kitaasisi, Kifedha, Kisiasa, Kimazingira, Kiteknolojia ambavyo kila kimoja kina uwezo wa kuathiri kasi na ufanisi wa utekelezaji wa Mpango iwapo havitadhibitiwa ipasavyo. **Jedwali la 7.1** linaelezea maeneo ya vihatarishi pamoja na hatua za kukabiliana navyo ili kusimamia utekelezaji wa Mpango.

**Jedwali la 7.1: Mikakati ya Kukabiliana Vihatarishi**

| Na. | Eneo la Kihatarishi | Maelezo na Muktadha | Mikakati ya kukabiliana na vihatarishi |
|---|---|---|---|
| 1. | Uwezo Hafifu wa Utekelezaji na Uratibu | Hatari ya mipango iliyogawanyika, kuchelewa kuanza kwa miradi, na uratibu hafifu baina ya Wizara, Idara na Wakala wa Serikali, Mamlaka za Serikali ya Mitaa na Taasisi za Umma, jambo linalosababisha kupungua kasi ya utekelezaji wa miradi shikizi ya Programu za kielelezo. | Kuanza kwa mfumo wa ufuatiliaji na tathmini (Result-Based Monitoring, Evaluation Accountability and Learning Framework) utatumika ili kuwa na usimamizi madhubuti wa mipango, programu za kielelezo na miradi shikizi. Mfumo huu utafuatilia na kutathmini viashiria muhimu vya utendaji; vihatarishi na gharama za utekelezaji wa miradi na programu. |
| 2. | Uwezo wa Kifedha wa kugharamia Mpango | Kasi ndogo ya ukusanyaji wa rasilimali na utegemezi wa bajeti za Serikali vinaweza kuchelewesha utekelezaji wa miradi. Vilevile, endapo sekta binafsi haitawekeza kama | Kuwa na vyanzo mbadala vya ugharamiaji kupitia sekta binafs, mfumo wa ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi, diaspora na hatifungani, na masoko ya mitaji; kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani na nidhamu ya |

| Na. | Eneo la Kihatarishi | Maelezo na Muktadha | Mikakati ya kukabiliana na vihatarishi |
|---|---|---|---|
| | | inavotarajiwa itakwamisha utekelezaji wa shughuli za kiuchumi na Mpango. | kifedha; kuimarisha mazingira ya biashara na uwekezaji na kutekeleza Mfumo wa Kitaifa wa Tathmini na Uwekaji Vipaumbele vya Miradi ili kulinganisha miradi na rasilimali zilizopo. |
| 3. | Mtikisiko na mdororo wa Kiuchumi duniani | Mitikisiko ya Kiuchumi kutoka Nje ikiwemo mfumuko wa bei, mabadiliko ya viwango vya kubadilisha fedha, mdororo wa uchumi wa dunia na mabadiliko ya bei za bidhaa vinaweza kupunguza mapato, kuongeza gharama za kukopa, kuvuruga minyororo ya ugavi na kudhoofisha uwekezaji | Kuimarisha akiba za fedha na za fedha za kigeni; kuongeza mauzo nje ya bidhaa na huduma mbalimbali na uongezaji thamani katika sekta ya kilimo, madini na viwanda; na kuimarisha ufuatiliaji wa mwenendo wa uchumi unaozingatia takwimu na matumizi ya modeli |
| 4. | Ushiriki usioridhisha wa sekta binafsi katika utekelezaji wa Mpango. | i. Utekelezaji mdogo wa maboresho kwenye uwekezaji, kodi na mifumo ya ubia kati ya sekta ya umma na binafsi unaweza kudhoofisha ushiriki wa sekta binafsi.<br>ii. Kutowekeza kwa kiwango kilichokusudiwa na hivyo kushindwa kufikia asilimia 70 kama ilivyoainishwa katika Mpango | i. Kuharakisha mageuzi ya biashara na kodi kupitia Mpango wa kuboresha udhibiti wa biashara (MKUMBI); kuimarisha mfumo wa kituo jumuishi cha uwekezaji; na kuhakikisha utabirikaji wa sera kupitia majadiliano ya kila robo mwaka kati ya sekta ya umma na binafsi<br>ii. Kuboreshwa kwa upatikanaji wa mitaji kwa kuimarisha mifumo ya dhamana za mikopo, kukuza masoko ya mitaji na kuvutia uwekezaji wa moja kwa moja sambamba na uwekezaji wa miundombinu ya misingi hususan nishati ya uhakika,barabara,reli, bandari na miundombinu ya kidijitali utaongeza ushindani |

| Na. | Eneo la Kihatarishi | Maelezo na Muktadha | Mikakati ya kukabiliana na vihatarishi |
|---|---|---|---|
| | | | na biashara na kupunguza gharama za uzalishaji . |
| 5. | Kutokushabiana kati ya rasilimali watu na ujuzi na unaotakiwa kwenye soko ya ajira | Kutoshabihiana kwa ujuzi wa nguvukazi na mahitaji halisi ya soko la ajira na matokeo ya elimu vinakwamisha ubiasharishaji na ubunifu | Kuoanisha mitaala ya elimu na mafunzo na sekta za kipaumbele za Mpango; kupanua wigo wa Elimu ya Ufundi na Ufundi Stadi (TVET) na mifumo ya mafunzo ya uanagenzi (apprenticeship); na kuimarisha masomo ya Sayansi, Teknolojia, Uhandisi, Hisabati, ujuzi wa kidijitali na mifumo ya ubunifu. |
| 6. | Mageuzi ya Kidijitali na Usalama wa kimtandao | Kuongeza wigo wa mifumo ya kidijitali huongeza hatari za mashambulizi ya kimtandao, uvujaji wa taarifa, mwingiliano hafifu wa mifumo na uelewa mdogo wa kidijitali hutishia utawala wa kimtandao na jitihada za uchumi wa kidigitali | Kutekeleza Mfumo wa Kitaifa wa Usalama wa kimtandao na usimamizi wa Takwimu; kuimarisha TZ-CERT na kuhakikisha ulinzi wa taarifa; kujenga uelewa wa kitaifa kuhusu masuala ya kidijitali; na kuunganisha na kulinda majukwaa ya Serikali kupitia usanifu shirikishi wa Mpango kwa njia ya kimtandao |
| 7. | Migogoro ya Kisiasa na mabadiliko ya kidiplomasia ya kikanda na kimataifa | i. Kutokutabirika kwa matamko ya kisera ya kikandana kimataifa yanasababisha kuvurugika kwa uendeshaji wa biashara yanayoweza kuathiri uwekezaji, usafirishaji na usalama wa rasilimali.<br>ii. Uwepo wa athari ya kiuchumi zitokanazo na migogoro katika maeneo ya mashariki ya kati ambayo yanategemewa na kwa uzalishaji wa mafuta na kuunganisha usafiri na usafirishaji abiria na | i. Kuimarisha diplomasia ya kikanda na ushirikiano wa kiusalama kulingana na miongozo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC) na Umoja wa Afrika; kuongeza wigo wa biashara na njia za usafirishaji; kuandaa mifumo ya tahadhari za awali; kuimarisha mawasiliano ya kimkakati na uratibu wa sera kwa miradi ya mipakani.<br>ii. Kuwekeza katika uzalishaji na usambazaji wa gesi asilia kama nishati mbadala, pamoja na kuimarisha akiba |

| Na. | Eneo la Kihatarishi | Maelezo na Muktadha | Mikakati ya kukabiliana na vihatarishi |
|---|---|---|---|
| | | mizigo. | ya kimkakati ya hifadhi ya mafuta ili kuongeza uwezo wa nchi kujilinda dhidi ya misukosuko ya Kimataifa na nishati ikiwemo mabadiliko ya bei katika soko la dunia. Vilevile kuongeza mauzo nje kupitia uzalishaji wa ndani ili kupata fedha za kigeni zilizokuwa zinategemewa kwa kiasi kikubwa kutoka katika sekta ya utalii. |

### 7.3 Usimamizi wa Vihatarishi

Usimamizi madhubuti wa vihatarishi hivi utahitaji pia ushirikiano imara wa wadau, matumizi ya takwimu na ushahidi katika kufanya maamuzi, mrejesho wa wananchi, pamoja na uratibu na uwiano wa sera katika sekta zote ili kuhakikisha malengo ya Mpango yanafikiwa. Kwa kuingiza misingi ya ustahimilivu, uendelevu, usawa na ubunifu katika mifumo yote, Mpango utaimarisha uwezo wake wa kupunguza athari za changamoto zinazoweza kujitokeza na kutafsiri vipaumbele vya kitaifa kuwa matokeo halisi ya kijamii na kiuchumi.

Ili kuhakikisha usimamizi endelevu na ufuatiliaji wa vihatarishi, Mpango utaimarisha Mfumo wa Usimamizi wa Vihatarishi kwa kuchukua hatua zifuatazo:

i. Kufanya mapitio ya vihatarishi kila robo mwaka kupitia Mfumo wa Kitaifa wa Usimamizi wa Miradi (NPMIS);

ii. Kuandaa dashibodi za ufuatiliaji kwa wakati ili kuwezesha maamuzi sahihi na ya haraka; na

iii. Kutoa mafunzo ya usimamizi wa vihatarishi kwa watendaji wa Wizara, Idara na Wakala za Serikali, Sekretarieti za Mikoa, na Mamlaka za Serikali za Mitaa, ambao ni watekelezaji wakuu wa miradi ya maendeleo.

**Kiambatisho Na. 1: Mwenendo wa Viashiria vilivyotumika katika Upimaji wa Utekelezaji Wa Mpango kwa kipindi cha Miaka Mitano.**

| Na. | Sekta | Kiashiria | Mwkaa wa Kizio | Utekelezaji wa Shabaha | | | | | Shabaha | Utekelezaji wa Shabaha (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 | |
| 1. | **Ujenzi** | Miundombinu (Nafasi katika mpangilio, kati ya nchi 189 kimataifa | 0 | | | 60 | 55 | 50 | 45 | 111 |
| 2. | | Kiwango cha wastani wa ukuaji (%) | 9 | 9.1 | 4.3 | 4.4 | 3.9 | 4.1 | 9.9 | 100 |
| 3. | | Mchango katika Pato la Taifa (%) | 13.9 | 14 | 13.8 | 14 | 14.1 | 12.8 | 16.7 | 100 |
| 4. | | Mchango wa Kampuni za Ndani katika Soko la Ujenzi (%) | | 35 | 35 | 35 | 35 | 40 | 60 | 20 |
| 5. | | Idadi ya Ajira zilizozalishwa katika Miradi ya Maendeleo | 23,585 (Des 2019) | 11,862 (Des 2020) | 24,007 (Des 2021) | 47,617 (Des 2022) | 26,367 (Des 2023) | 21,527 (Des 2024) | 18,988 (Des 2025) | -21 |
| 6. | | Nafasi ya barabara katika mpangilio wa kimataifa | 86 | | | 42 | 39 | 27 | 26 | 98 |
| 7. | | Ongezeko la Mtandao wa Barabara za Kitaifa (km) | 36,258 (Des 2019) | 36,362 (Des 2020) | 36,760 (Des 2021) | 37,226 (Des 2022) | 37,435 (Des 2023) | 37,435 (Des 2024) | 37,734.41 (Des 2025) | 80 |
| 8. | **Uchukuzi** | Nafasi ya reli katika mpangilio wa kidunia | 83 | 83 | 83 | 78 | 58 | 58 | 70 | 192.3 |
| 9. | | Urefu wa reli ya kati kwa kiwango cha Standard Gauge (SGR) kwa kilometa | 395.20 | 451.43 | 487.9 | 553.03 | 625.84 | 747 | 1,219 | 42.7 |
| 10. | | Kiasi cha shehena kinachosafirishwa na reli (tani) | 614,134 | 762,987 | 607,687 | 683,329 | 484,673 | 531,359 | 5,162,258 | 0.0 |
| 11. | | Idadi ya abiria wanaosafirishwa na reli | 972,000 | 1,250,373 | 1,143,787 | 1,394,058 | 1,213,225 | 7,851,127 | 2,272,682 | 528.9 |
| 12. | | Muda wa makasha kukaa bandarini (siku) | 7 | 7 | 9.0 | 9.2 | 6.7 | 5.2 | 5 | 90.0 |
| 13. | | Muda wa meli kukaa bandarini (siku) | 3.7 | 3.7 | 4.6 | 4.4 | 4.1 | 3 | 2 | 41.2 |
| 14. | | Idadi ya bandari kavu | 2 | 2 | 2 | 2 | 2 | 2 | 3 | 0 |
| 15. | | Idadi ya meli zinazohudumiwa | 3,704 | 4,241 | 4,686 | 5,675 | 4,487 | 4,888 | 4,000 | 400 |
| 16. | | Mizigo inayotoka nje kuelekea nchi za jirani (tani milioni) | 4.6 | 4.6 | 5.7 | 6.1 | 6.2 | 7.6 | 18 | 15.1 |
| 17. | | Mizigo ya kwenda nje toka kwa nchi jirani (tani milioni) | 0.9 | 0.9 | 2.7 | 2.9 | 3.0 | 3.4 | 10 | 6.3 |
| 18. | | Idadi ya ndege zilizonunuliwa | 11 | 11 | 11 | 13 | 15 | 15 | 19 | 50 |
| 19. | | Idadi ya ndege za mizigo zilizonunuliwa | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 1 | 1 | 100 |
| 20. | | Idadi ya ndege za abiria za masafa marefu zilizonunuliwa | 2 | 2 | 2 | 2 | 2 | 3 | 3 | 100 |
| 21. | | Idadi ya ndege za abiria za masafa ya kati (kanda) zilizonunuliwa | 2 | 2 | 4 | 4 | 6 | 6 | 8 | 67 |
| 22. | | Idadi ya ndege za ATCL zinazofanya kazi | 10 | 10 | 12 | 13 | 14 | 16 | 19 | 67 |
| 23. | | Idadi ya wanaanga waliofunzwa | 61 | 99 | 279 | 320 | 567 | 1,123 | 1,359 | 82 |
| 24. | | Idadi ya Viwanja vya ndege vyenye mifumo ya usimamizi wa taarifa za viwanja vya ndege (AMIS) | 1 | 1 | 1 | 1 | 2 | 9 | 14 | 61 |

| Na. | Sekta | Kiashiria | Mwkaa wa Kizio | Utekelezaji wa Shabaha | | | | | Shabaha | Utekelezaji wa Shabaha (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 | |
| 25. | | Idadi ya mitambo ya ulinzi kwenye viwanja vya ndege (X-ray machines) | 46 | 80 | 83 | 83 | 85 | 103 | 71 | 228 |
| 26. | | Viwanja vya ndege vyenye uzio kuzunguka kiwanja | 9 | 9 | 11 | 16 | 16 | 26 | 27 | 94 |
| 27. | | Idadi ya rada za hali ya hewa zilizonunuliwa | 3 | 3 | 5 | 5 | 5 | 5 | 7 | 40 |
| 28. | Nishati | Uzalishaji wa Umeme (MW) | 1,602.30 | 1,605.86 | 1,694.55 | 1,872.05 | 2,138 | 4,437.53 | 4,915 | 73 |
| 29. | | Idadi ya Mikoa Iliyounganishwa na Gridi | 23 | 23 | 23 | 24 | 24 | 24 | 26 | 33 |
| 30. | | Urefu wa Gridi ya Taifa (km) | 5,896.30 | 6,423.53 | 6,423.53 | 6,363.27 | 7,745 | 8,500.38 | 9,351 | 79 |
| 31. | | Kupungua kwa Upotevu wa Umeme (%) | 16.19 | 15.16 | 14.71 | 14.62 | 14.56 | 13.86 | 7.9 | 47 |
| 32. | Mawasiliano na Teknolojia ya Habari | Uwiano wa watumiaji wa intaneti nchini (%) | 47 | 49 | 48 | 54 | 59.3 | 74.3 | 85 | 80 |
| 33. | | Idadi ya Majengo yenye Anwani za Makazi | 450,980 | - | - | 18,000,000 | 18,000,000 | 18,186,000 | 18,558,268 | 97 |
| 34. | Kilimo | Hekta za Umwagiliaji | 694,715 | 695,005 | 695,005 | 727,280.6 | 727,280.6 | 983,466.6 | 1,200,000 | 57 |
| 35. | | Mbegu zilizoidhinishwa na zilizozalishwa | 76,285.56 | 44,581.08 | 50,747 | 58,807.61 | 71,356 | 79,700.62 | 1,040,000 | 0 |
| 36. | | Akiba ya taifa ya chakula (tani) | 52,724.73 | 107,384.06 | 141,575.902 | 46,893.983 | 785,003.02 | 727,280.60 | 1,140,000 | 62 |
| 37. | | Kiasi cha mazao ya bustani yaliyozalishwa (tani) | 6,597,863 | 7,304,723 | 7,304,723 | 7,723,116 | 7,518,560.84 | 7,518,560.83 | 14,600,000 | 12 |
| 38. | | Kiasi cha uzalishaji wa mazao ya biashara ya asili (traditional)(tani). | 1,144,631 | 898,967 | 898,967 | 973,436 | 1,201,832.65 | 1,451,694.11 | 1,583,200 | 70 |
| 39. | | Idadi ya viwanda vinavyomilikiwa na vyama vya ushirika | 113 | 183 | 267 | 267 | 267 | 329 | 338 | 96 |
| 40. | | Idadi ya vyama vya ushirika vinavotumia mfumo wa soko rasmi | 1202 | 1302 | 1402 | 1573 | 2,231 | 4,060 | 2,782 | 181 |
| 41. | | Idadi ya wanachama wa vyama vya ushirika (milioni) | 4.2 | 4.5 | 5.1 | 6.2 | 6.9 | 8.4 | 14.5 | 41 |
| 42. | Mifugo | Kiwango cha Wastani wa Ukuaji (%) | 4.9 | 5 | 5 | 5 | 5 | 5.5 | 6.5 | 38 |
| 43. | | Mchango katika Pato la Taifa (bei za sasa) (%) | 6.4 | 7.1 | 7.2 | 6.7 | 6.2 | 6.2 | 7 | -33 |
| 44. | | Kiwango cha Vifo vya Mifugo (%) | 27 | 24 | 21 | 18 | 16 | 16 | 12 | 73 |
| 45. | | Kiwango cha Magonjwa ya Mifugo (%) | 6 | 5 | 4.5 | 3.5 | 2.5 | 2.5 | 3 | 117 |
| 46. | | Kiwango cha Uogeshaji Mifugo katika josho (%) | 70 | 72 | 74 | 75 | 78 | 82 | 85 | 80 |
| 47. | | Kiwango cha Chanjo ya Mifugo (%) | 25 | 37 | 39.5 | 40 | 42 | 42 | 50 | 68 |
| 48. | | Wastani wa uzalishaji maziwa, Ng'ombe wa Asili (Lita) | 2 | 0.5 | 0.5 | 0.5 | 0.8 | 0.85 | 4 | -58 |
| 49. | | Ngozi bora iliyochakatwa (%) | 10 | 15 | 20 | 25 | 30 | 40 | 50 | 75 |
| 50. | | Uzalishaji wa Nyama (Tani) | 702,000 | 738,165.99 | 769,966.65 | 803,264.30 | 963,856.55 | 1,124,449 | 951,700 | 169 |
| 51. | | Uzalishaji wa Maziwa katika (Lita bilioni) | 3.01 | 3.1 | 3.4 | 3.6 | 3.97 | 4.1 | 4.3 | 84 |
| 52. | | Asilimia ya Maziwa yaliyochakatwa | 1.5 | 2 | 2 | 2 | 2.2 | 2.2 | 14 | 6 |

| a. | Sekta | Kiashiria | Mwkaa wa Kizio | Utekelezaji wa Shabaha | | | | | Shabaha | Utekelezaji wa Shabaha (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 | |
| . | | Ngozi na ngozi Zilizochakatwa (Tani) | 1,190 | 143 | 146 | 2,250 | 2,385 | 2,900 | 9,210.60 | 21 |
| . | | Mauzo ya nyama nje ya nchi (Tani) | 692 | 1,774.00 | 10,415.00 | 12,243.79 | 14,701.10 | 14,900 | 7,200 | 218 |
| . | | Usafirishaji wa Ngozi (Tani) | 6,747 | 7,951 | 7,371 | 4,491 | 5,778 | 7,243 | 8,000 | 39 |
| . | | Kiasi cha Ardhi kilichotengwa kwa ajili ya malisho (Hekta) | | | Hekta 3,189,456.94 | Hekta 3,384,485.5 | Hekta 3,466,111.43 | Hekta 3,489,701.13 | Hekta 3,509,701.1 | 54 |
| . | | Kiasi cha Ardhi kilichotangazwa kwenye gazeli la serikali (Hekta) | | | 143,754.02 | 1,138,581.3 1 | 1,138,581.31 | 1,349,486.29 | 1,500,000 | 89 |
| . | | Idadi ya Mabwawa ya Mifugo | | | 1,384 | 1,386 | 1,389 | 1,397 | 1,400 | 81 |
| . | | Idadi ya Visima Virefu (Idadi) | | | 103 | 104 | 104 | 124 | 130 | 78 |
| . | | Kiwango cha Wastani wa Ukuaji (%) | 6.3 | 6.7 | 2.6 | 1.9 | 1.4 | 2.3 | 8.4 | -86 |
| . | **Uvuvi** | Asilimia katika Pato la Taifa (Bei za sasa) | 1.8 | 1.7 | 1.8 | 1.8 | 1.7 | 1.9 | 1.9 | 100 |
| . | | Asilimia katika Mapato yatokanayo na Mauzo Nje | 3 | 3.4 | 3.2 | 3.3 | 3.4 | 3 | 4.5 | 0 |
| . | | Ulaji kwa kila Mtu | | 7.8 | 8.22 | 7.8 | 7.9 | 8.5 | 10.5 | 26 |
| . | | Mchango katika Ulaji wa Protini ya Wanyama Kitaifa | 30 | 30 | 30 | 30 | 30 | 33 | 35 | 60 |
| . | | Uzalishaji wa samaki (tani) | 497,567.28 | 493,850.24 | 502,305.34 | 513,218.90 | 530,379.66 | 575,000 | 600,000 | 76 |
| . | | Idadi ya viwanda vya kusindika samaki | 12 | 15 | 17 | 20 | 21 | 21 | 17 | 180 |
| . | | Idadi ya vituo vya Ukuzaji Viumbe Maji (Aquaculture Development Centres - ADC) | 9 | 9 | 9 | 9 | 9 | 12 | 12 | 100 |
| . | | Uzalishaji wa chakula cha samaki (tani) | 276.7 | 472.47 | 1,615.50 | 3,012.70 | 3,455.40 | 5,000 | 8,000 | 61 |
| . | | Uzalishaji wa vifaranga vya Samaki | | | 31,134,993 | 53,176,800 | 64,984,806 | 140,018,196 | 154,846,692 | 88 |
| . | | Idadi ya Vizimba vilivyopo | | | 780 | 993 | 1,215 | 1,636 | 2,057 | 67 |
| . | | Uzalishaji wa mwani (Tani) | | | 39,537.90 | 46,778.00 | 87,227.50 | 94,977.20 | 102,727 | 88 |
| . | | Idadi ya Maafisa Ugani wa Mifugo na Uvuvi | 657 | 657 | 657 | 657 | 657 | 700 | 1,850 | 4 |
| . | **Viwanda na Biashara** | Mchango katika Pato la Taifa (%) | 8.2 | 8.4 | 7.8 | 7.1 | 7 | 8.5 | 8.5 | 100 |
| . | | Kiwango cha ukuaji halisi wa Pato la Taifa (%) | 5.2 | 4.7 | 4.5 | 4.2 | 4.3 | 6.8 | 6.8 | 100 |
| . | | Mchango katika Ajira Zote (%) | 7.4 | 8.5 | 8 | 8 | 8.1 | 12.8 | 12.8 | 100 |
| . | | Mchango katika Mapato ya Mauzo Nje (%) | 17.1 | 17.7 | 22.9 | 26.9 | 17.7 | 19 | 19 | 100 |
| . | | Mchango wa bidhaa zilizozalishwa viwandani kwa teknolojia ya kati katika mauzo nje (%) | 28 | 29.2 | 21.1 | 0 | 25 | 36 | 39 | 72.7 |
| . | | Mchango wa bidhaa zilizozalishwa viwandani kwa teknolojia ya juu katika mauzo nje (%) | 8 | 8.8 | 8.9 | 0 | 25 | 42 | 10 | 1700 |
| . | | Mchango katika Mauzo yote nje (%) | 16.9 | 17.7 | 22.9 | 26.9 | 21.6 | 39 | 24 | 311.3 |
| . | **Madini** | Wastani wa Ukuaji (%) | 17.7 | 7.3 | 9.4 | 10.8 | 11.3 | 8.3 | 7.7 | 94 |
| . | | Mchango kwenye Pato la Taifa (%) | 5.3 | 6.8 | 7.3 | 9.0 | 9.1 | 10.1 | 10 | 102 |
| . | | Jumla ya Mapato ya Fedha za Nje (Dola za Marekani milioni) | 2,326.7 | 3,375 | 3,116.4 | 3,395.30 | 3,551.40 | 4,119.9 | 5,505 | 56 |
| . | | Mauzo ghafi nje (%) | 15 | 15 | 1.6 | 0.45 | 9 | 9 | 5 | 60 |

| Na. | Sekta | Kiashiria | Mwkaa wa Kizio | Utekelezaji wa Shabaha | | | | | Shabaha | Utekelezaji wa Shabaha (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 | |
| 84. | Utalii | Mchango katika Pato la Taifa (bei za sasa) (%) | 17.2 | 17.2 | 17.2 | 17.2 | 17.2 | 17.2 | 18.9 | 0 |
| 85. | | Idadi ya Watalii kutoka nje ya nchi | 1,527,230 | 620,867 | 922,692 | 1,454,920 | 1,808,205 | 2,294,495 | 5,000,000 | 136 |
| 86. | | Idadi ya Watalii ndani ya nchi | 959,831 | 788,933 | 2,363,260 | 1,084,737 | 1,985,707 | 3,610,960 | | |
| 87. | | Wastani wa idadi ya siku za kulala mtalii. | 13 | 10 | 10 | 9 | 10 | 10 | 14 | -300 |
| 88. | | Wastani wa Matumizi ya Mtalii kwa Siku (USD) | 0 | 321 | 364 | 367 | 419 | 416 | 479 | 160 |
| 89. | | Mchango katika Mapato ya Fedha za Kigeni (%) | 25 | 5.3 | 21 | 25 | 25 | 26 | 26 | 100 |
| 90. | | Mapato yatokanayo na Watalii (Dola za Marekani bilioni) | 2.6 | 0.7 | 1.3 | 3.9 | 3.9 | 4.4 | 3.9 | 115 |
| 91. | Michezo | Idadi ya miundombinu ya michezo na iliyoboreshwa nchini kote | 63 | 64 | 64 | 66 | 68 | 174 | 72 | 1233 |
| 92. | | Idadi ya miundombinu iliyojengwa/kukarabatiwa katika Chuo cha Kuendeleza Michezo Malya na Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamaoyo (TaSUBa). | 35 | 48 | 50 | 52 | 53 | 78 | 88 | 460 |
| 93. | | Idadi ya filamu na muziki zilizoidhinishwa, kusambazwa na kutumika (TFB) | 15,303 | 2,962 | 3,763 | 3,201 | 4,070 | 3806 | 5500 | -105 |
| 94. | | Idadi ya wasanii waliosajiliwa katika tasnia ya ubunifu (BASATA, COSOTA) | 3,462 | 3,931 | 4,299 | 5,254 | 6,473 | 7310<br>4950 (basata) | 8,666<br>8,000 (basata) | 74 |
| 95. | | Idadi ya wataalamu katika tasnia ya ubunifu waliopata mafunzo (COSOTA NA BASATA) | 2,852 | 450 | 442 | 500 | 10,837 | 11,500<br>1200(basata) | 4,297<br>3600 (basata) | 598 |
| 96. | | Idadi ya michezo na mashindano ya kimataifa yaliyoandaliwa na Tanzania kushiriki (BMT) | 178 | 0 | 98 | 135 | 157 | 110 | 150 | -40 |
| 97. | | Idadi ya vibali vilivyotolewa kwa vyama vya michezo na wanamichezo binafsi (BMT) | 178 | 0 | 57 | 45 | 194 | 110 | 350 | -31 |
| 98. | | Idadi ya wanariadha wanaocheza nje ya nchi (BMT) | 54 | - | 21 | 31 | 17 | 62 | 40 | 8 |
| 99. | | Idadi ya wageni wanaoendesha shughuli za kuzalisha filamu nchini Tanzania. (TFB) | 359 | 60 | 87 | 100 | 64 | 220 | 250 | -41 |
| 100. | | Idadi ya wasanii/wataalamu katika tasnia ya ubunifu/makundi yanayofanya maonesho yao nje ya nchi (TFB,BASATA, COSOTA) | 1,620 | 330 | 430 | 461 | 467 | 220 | 1,755 | -1155 |
| 101. | | Idadi ya wasanii wa nje/wataalamu katika tasnia ya ubunifu wanaofanya maonesho yao nchini Tanzania (TFB, COSOTA BASATA) | 720 | 142 | 153 | 162 | 167 | 242 | 300 | -45 |
| 102. | | Idadi ya wataalamu wa Kiswahili wanaofanya kazi nje ya Tanzania - BAKITA | 56 | 64 | 71 | 95 | 111 | 537 | 656 | 55 |
| 103. | | Idadi ya machapisho ya Kiswahili yaliyouzwa nje ya nchi - BAKITA | 200 | 252 | 2189 | 1640 | 242 | 672 | 700 | 60 |

| Na. | Sekta | Kiashiria | Mwkaa wa Kizio | Utekelezaji wa Shabaha | | | | | Shabaha | Utekelezaji wa Shabaha (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 | |
| 104. | | Idadi ya tuzo za kimataifa zilizoandaliwa na kutolewa kwenye utamaduni, sanaa na tasnia ya ubunifu (BASATA, TFB, BAKITA NA COSOTA) | 47 | 38 | 41 | 188 | 62 | 44 | 55 | 25 |
| 105. | | Idadi ya vikundi vya utamaduni na sanaa kutoka nje ya nchi vilivyoshiriki katika matamasha ya Kimataifa yanayoandaliwa kila mwaka na TaSUBa. | 5 | 4 | 4 | 6 | 23 | 11 | 20 | 40 |
| 106. | | Idadi ya wanafunzi waliodahiliwa katika Chuo cha Kuendeleza Michezo Malya | 300 | 439 | 533 | 684 | 758 | 358 | 500 | 20 |
| 107. | | Idadi ya wanafunzi waliodahiliwa TaSUBa | 350 | 439 | 533 | 684 | 758 | 947 | 1100 | 70 |
| | | Idadi ya wilaya zinazofikiwa na matangazo ya TBC (TBC FM na BONGO FM) | 102 | 119 | 121 | 134 | 137 | 138 | 139 | 97 |
| 108. | **Uwekezaji** | Idadi ya Miradi ya Uwekezaji iliyosajiliwa na TISEZA | 230 | 249 | 305 | 378 | 737 | 969 | 600 | 199.7 |
| 109. | | Thamani ya Miradi ya Uwekezaji (Dola za Marekani) | 1760.2 | 3404.6 | 2351.34 | 5497.61 | 6663.87 | 8,813 | 8,500 | 104.6 |
| 110. | | Idadi ya Ajira kutokana na Miradi ya Uwekezaji | 33509 | 39170 | 46246 | 56192 | 228906 | 280,000 | 250,000 | 113.9 |
| 111. | | Idadi ya Miongozo ya Uwekezaji ya Mikoa (Kila mkoa) | 13 | 7 | 0 | 2 | 0 | 26 | 26 | 100 |
| 112. | | Idadi ya Ofisi za Utoaji Huduma Mahala Pamoja | 11 | 13 | 13 | 13 | 14 | 15 | 18 | 57.1 |
| 113. | | Kiasi cha Ardhi ya Uwekezaji iliyotengwa (ekari) | 90,990 | 98,861 | 99,735 | 159,813 | 214,972.94 | 391,030.94 | 528,917 | 68.5 |
| 114. | | Idadi ya Makongamano ya Uwekezaji Kimataifa | 21 | 49 | 63 | 89 | 204 | 180 | 150 | 123.3 |
| 115. | | Idadi ya Maboresho ya sheria na kanuni za kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji yaliyofanywa | 35 | 42 | 55 | 66 | 86 | 106 | 88 | 71.7 |
| 116. | | Idadi ya maboresho ya kufuta au kupunguza tozo, ada na ushuru katika kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji yaliyofanywa | 218 | 232 | 307 | 374 | 413 | 452 | 388 | 48.9 |
| 117. | **Mambo ya nje** | Idadi ya mikutano ya uwili, kikanda na kimataifa ambayo Tanzania inashiriki | 50 | 32 | 80 | 90 | 101 | 110 | 250 | 30 |
| 118. | | Idadi ya Hati za Makubaliano zilizosainiwa kati ya Tanzania na nchi mbalimbali | 15 | 32 | 33 | 66 | 78 | 84 | 80 | 106.15 |
| 119. | | Idadi ya mikutano ya ujirani mwema iliyofanyika | 5 | 12 | 35 | 32 | 53 | 48 | 40 | 122.8 |
| 120. | | Idadi ya taasisi za kitaifa na kikanda zinazofundisha rasmi Lugha ya Kiswahili | 5 | 30 | 42 | 40 | 100 | 100 | 120 | 82.6 |
| 121. | | Idadi ya viwanja vya Serikali kwenye maeneo ya kimkakati nje vilivyoendelezwa | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 11 | 0 |
| 122. | **Elimu** | Kiwango cha uandikishaji rika lengwa (% ya wanaostahili) | 38.7 | 35.9 | 34.2 | 37.4 | 40.5 | 51.2 | 51 | 102 |

| Na. | Sekta | Kiashiria | Mwkaa wa Kizio | Utekelezaji wa Shabaha | | | | | Shabaha | Utekelezaji wa Shabaha (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 | |
| 123. | | Uwiano wa idadi ya wanafunzi kwa mwalimu mwenye sifa | 1:149 | 1:130 | 1:123 | 1:117 | 1:127 | 1:105 | 1:50 | 44 |
| 124. | | Kiwango cha uandikishaji jumla (% ya wanaostahili) | 110.6 | 110.6 | 109.7 | 108.5 | 98.2 | 84.2 | 80.6 | 88 |
| 125. | | Kiwango cha uandikishaji wa rika lengwa | 95.7 | 95.7 | 95.3 | 94.4 | 86 | 79.6 | 76.8 | 85 |
| 126. | | Uwiano wa Idadi ya Wanafunzi wa Elimu ya msingi kwa Mwalimu | 1:54 | 1:51 | 1:57 | 1:57 | 1:55 | 1:50 | 1:55 | -400 |
| 127. | | Uwiano wa Idadi ya Wanafunzi kwa Kitabu | 1:4 | 1:3 | 1:2 | 1:2 | 1:2 | 1:3 | 1:1 | 33 |
| 128. | | Uwiano wa Idadi ya Wanafunzi kwa Darasa | 1:75 | 1:75 | 1:74 | 1:70 | 1:68 | 1:63 | 1:60 | 80 |
| 129. | | Uwiano wa Idadi ya Wanafunzi wa Kiume kwa Tundu la Choo | 1:54 | 1:54 | 1:51 | 1:52 | 1:46 | 1:47 | 1:40 | 50 |
| 130. | | Uwiano wa Idadi ya Wanafunzi wa Kike kwa Tundu la Choo | 1:51 | 1:51 | 1:48 | 1:48 | 1:43 | 1:43 | 1:39 | 67 |
| 131. | | Uwiano wa Idadi ya wanafunzi kwa Dawati | 1:4 | 1:4 | 1:4 | 1:4 | 1:4 | 1:4 | 1:4 | 100 |
| 132. | | Asilimia ya Shule za msingi zenye umeme | 43.5 | 42.2 | 48.8 | 56 | 61.9 | 68 | 73.5 | 82 |
| 133. | | Kiwango cha uandikishaji jumla (% ya wanaostahili) | 46 | 46 | 47.4 | 48.2 | 52.7 | 51.7 | 53.1 | 80 |
| 134. | | Asilimia ya Uandikishaji wa Watoto Wenye Umri wa Rika lengwa Ikilinganishwa na idadi ya watoto wote wenye umri wa kwenda shule | 36 | 36 | 37 | 38.3 | 41.8 | 40.6 | 40 | 115 |
| 135. | | Uwiano wa Idadi ya Wanafunzi wa Elimu ya Sekondari kwa Mwalimu | 1:23 | 1:23 | 1:24 | 1:25 | 1:26 | 1:26 | 1:20 | -100 |
| 136. | | Uwiano wa Idadi ya Wanafunzi wa Elimu ya Sekondari kwa Darasa | 1:41 | 1:40 | 1:42 | 1:36 | 1:37 | 1:34 | 1:34 | 100 |
| 137. | | Uwiano wa Idadi ya Wanafunzi wa Sekondari kwa Tundu la Choo | 1:27 | 1:20 | 1:27 | 1:28 | 1:34 | 1:28 | 1:26 | -100 |
| 138. | | Asilimia ya Shule za Sekondari Zenye Umeme | 69.8 | 69.8 | 73.9 | 77.2 | 77.5 | 81.4 | 97.8 | 41 |
| 139. | | Asilimia ya kundirika la wanafunzi waliofaulu mtihani wa Elimu ya Sekondari ya Chini | 80.65 | 85.84 | 87.3 | 87.79 | 89.37 | NA | 90 | 93 |
| 140. | | Kiwango cha uandikishaji jumla (% ya Wanaostahili) | 6.9 | 6.9 | 6.7 | 7.6 | 7.7 | 9.1 | 9.8 | 76 |
| 141. | | Kiwango cha uandikishaji rika lengwa (% ya wanaostahili) | 3.3 | 3.3 | 3.4 | 4 | 4.1 | 5.2 | 6.7 | 56 |
| 142. | | Uandikishaji halisi wa wanafunzi wa kiume (%) | 3.3 | 3.3 | 3.4 | 3.9 | 4.1 | 5 | 6.3 | 57 |
| 143. | | Uandikishaji halisi wa wanafunzi wa kike (%) | 3.2 | 3.2 | 3.4 | 4.1 | 4.1 | 5.4 | 7.1 | 56 |
| 144. | | Asilimia ya wanafunzi wanaofaulu mtihani wa kidato cha VI | 99.51 | 99.5 | 99.6 | 99.9 | 99.9 | 99.9 | n/a | 100 |
| 145. | | Idadi ya wanafunzi waliopata mikopo ya elimu ya juu | 132,392 | 149,472 | 177,893 | 198,105 | 227,998 | na | 248,331 | 82 |
| 146. | | Idadi ya wahitimu wa vyuo vikuu | 60,940 | 48,621 | 54,810 | 57,742 | 56,520 | 62,570 | 70,081 | 17 |

| Na. | Sekta | Kiashiria | Mwkaa wa Kizio | Utekelezaji wa Shabaha | | | | | Shabaha | Utekelezaji wa Shabaha (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 | |
| 147. | | Kiwango cha udahili jumla (%) | 4.5 | 5.8 | 7.4 | 6.9 | 8 | 9.2 | 6 | 313 |
| 148. | | Idadi ya wanafunzi wanaohitimu kwa mwaka | 86,547 | 146,671 | 154,800 | 140,014 | 89,967 | 98,492 | 120,000 | 36 |
| 149. | **Afya** | Idadi ya vifo vya watoto wachanga kwa kila vizazi hai 1000 | 26 | 25 | 24 | 24 | 24 | 24 | 15 | 18 |
| 150. | | Idadi ya vifo vya watoto wenye umri chini ya miaka mitano kwa kila vizazi hai 1000 | 81 | 67 | 43 | 43 | 43 | 43 | 40 | 92.6 |
| 151. | | Uzazi uliohudumiwa na mfanyakazi wa afya mwenye ujuzi | 80 | 92.3 | 93.6 | 94.4 | 94.6 | 93 | 85 | 260 |
| 152. | | Wastani wa umri wa kuishi (miaka) | 66.1 | 66.7 | 65.4 | 67.6 | 67.8 | 68 | 68 | 100 |
| 153. | | Kiwango cha maambukizi ya VVU kitaifa (%) | 4.7 | 4.9 | 4.9 | 4.9 | 4.4 | 4.4 | 3.1 | 18 |
| 154. | **Maji** | Asilimia ya idadi ya watu wa vijijini wanaopata maji ya bomba au maji yalivyolindwa kama chanzo kikuu | 70 | 72.3 | 74.5 | 77 | 79.6 | 85.2 | 83 | 116.9 |
| 155. | | Uwiano wa kaya za vijijini zenye miundombinu iliyoboreshwa ya usafi wa mazingira | 36 | 47.3 | 60.4 | 73.5 | 77.5 | 77.5 | 78.5 | 97.6 |
| 156. | | Asilimia ya watu katika makao makuu ya mikoa wanaopata maji ya bomba au maji yaliyolindwa | 84 | 85 | 86.5 | 88 | 90 | 92.5 | 91.6 | 111.6 |
| 157. | | Asilimia ya kaya katika makao makuu ya mikoa iliyounganishwa kwenye mfumo rasmi wa maji-taka | 13 | 11 | 13 | 13 | 14 | 10.7 | 13 | -230.0 |
| 158. | | Asilimia ya upotevu wa maji (NRW) katika makao makuu ya mikoa | 30 | 36.8 | 35.7 | 35.3 | 35.3 | 32 | 33.4 | 58.8 |
| 159. | | Asilimia ya watu katika makao makuu ya wilaya na miji midogo wanaopata huduma ya maji ya bomba au maji yaliyolindwa kama chanzo kikuu | 70 | 67 | 72 | 73.4 | 74.5 | 80 | 74.5 | 222.2 |
| 160. | | Asilimia ya watu katika jiji la Dar es Salaam wanaopata huduma ya maji ya bomba au maji salama kama chanzo chao kikuu | 85 | 87 | 89 | 90 | 92.5 | 94.6 | 93 | 120 |
| 161. | | Asilimia ya kaya katika jiji la Dar es Salaam waliounganishwa kwenye mfumo rasmi wa maji-taka | 13 | 13 | 11 | 13 | 12.4 | 13 | 13 | 100 |
| 162. | | Kiwango cha upotevu wa maji (NRW) katika jiji la Dar es Salaam | 35 | 38.3 | 39.2 | 41.5 | 39.5 | 40 | 43.2 | 60 |
| 163. | | Idadi ya vyanzo vya maji vilivyotengwa na kutangazwa kwa ajili ya ulinzi na uhifadhi | 18 | 18 | 34 | 34 | 59 | 80 | 68 | 124 |
| 164. | **Ardhi nyumba na maendeleo ya makazi** | Idadi ya mali zilizorasimishwa katika makazi yasiyo rasmi | 1,496,357 | 1,754,822 | 2,207,627 | 2,469,686 | 2,576,355 | 2,820,150 | 2,942,661 | 91.5 |
| 165. | | Asilimia ya eneo la ardhi yenye makazi yasiyo rasmi | 70 | 70 | 69 | 67.3 | 67.3 | 60.1 | 60.1 | 100.0 |
| 166. | | Eneo la ardhi lililotengwa na kulindwa kwa matumizi ya umma (ekari) | 858,665 | 858,665 | 858,665 | 865,337 | 870,437 | 874,937 | 875,360 | 97.5 |

| Na. | Sekta | Kiashiria | Mwkaa wa Kizio | Utekelezaji wa Shabaha | | | | | Shabaha | Utekelezaji wa Shabaha (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 | |
| 167. | | Idadi ya miji yenye mipango kabambe ya upimaji iliyohuishwa | 24 | 25 | 27 | 28 | 28 | 28 | 28 | 100.0 |
| 168. | | Idadi ya viwanja vilivyotengwa | 1,551,716 | 2,015,532 | 2,391,366 | 2,706,343 | 3,146,541 | 3,401,896 | 3,544,338 | 92.9 |
| 169. | | Idadi ya ramani za msingi zilizohuishwa kwa eneo | 1 | 19 | 62 | 84 | 86 | 88 | 88 | 100.0 |
| 170. | | Uwiano wa vijiji vyenye mipango ya matumizi bora ya ardhi (%) | 19.3 | 19.3 | 20.9 | 23.2 | 33.5 | 34.5 | 38.97 | 77.3 |
| 171. | | Idadi ya mabaraza ya ardhi yanayofanya kazi | 57 | 68 | 81 | 93 | 105 | 112 | 117 | 91.7 |
| 172. | | Asilimia ya ardhi iliyopimwa | 25 | 25 | 25 | 25 | 26 | 26 | 26 | 100.0 |
| 173. | | Idadi ya leseni za makazi zilizotolewa katika makazi yasiyo rasmi | 1,738 | 1,738 | 23,862 (2021/22) | 23,862 (2021/22) | 23,862 (2021/22) | 23,862 (2021/22) | 29,478 | 79.8 |
| 174. | **Maendeleo ya jamii** | Idadi ya vituo vya malezi ya watoto vilivyosajiliwa | 1,543 | 1,543 | 2,714 | 3,233 | 4,068 | 4,723 (*Des,2025*) | 7,500 | 62 |
| 175. | | Idadi ya wazee wasiojiweza wanaopata huduma za bima ya afya bure | 166,866 | 166,866 | 201,509 | 262,513 | 365,284 | 1,256,544 | 574,321 | 219 |
| 176. | | Idadi ya watoto wanaolelewa baada ya mapatano | 12,068 | 12,068 | 26,903 | 32,905 | 46,473 | 48,051 | 50,000 | 95 |
| 177. | | Idadi ya watu wenye mafunzo ya uanagenzi | 46,200 | 14,440 | 22,200 | 11,973 | 6,300 | 8,250 | 46,300 | -37950 |
| 178. | | Idadi ya watu walioshiriki mafunzo ya utarajali (Internship) | 30,000 | 4,118 | 2,490 | 1,888 | 3,085 | 1,861 | 31,000 | -2814 |
| 179. | **Utumishi** | Idadi ya Watumishi waliopatiwa mafunzo ya maadili ya utendaji katika Utumishi wa Umma | 3,124 | 7,372 | 11,890 | 27,262 | 42,272 | 69,047 | 61,500 | 112.93 |
| 180. | | Idadi ya taasisi zilizofundishwa matumizi ya Mfumo wa e-Mrejesho (ili kuongeza uwajibikaji na mapambano dhidi ya rushwa katika utumishi wa umma na nchi kwa ujumla) | 0 | 0 | 148 | 248 | 368 | 450 | 508 | 88.58 |
| 181. | | Kupungua kwa malalamiko yatokanayo na utawala bora na masuala ya utawala bora | 123 | 156 | 158 | 152 | 147 | 138 | 100 | -65 |
| 182. | **Katiba na sheria** | Asilimia ya raia wanaoishi katika mikoa yenye Mahakama Kuu inayofanya kazi | 69 | 77 | 77 | 83 | 83 | 83 | 100 | 45 |
| 183. | | Asilimia ya kesi zilizohudumiwa na watoa msaada wa huduma za kisheria | 0.13 | 8.2 | 11.4 | 13.97 | 13.97 | 15 | 20 | 75 |
| 184. | | Idadi ya IJCs zilizojengwa na zinazofanya kazi katika maeneo yaliyo chaguliwa | 10 | 16 | 19 | 19 | 28 | 28 | 28 | 100 |
| 185. | | Idadi ya majengo ya mahakama ya wilaya yaliyojengwa | 64 | 82 | 94 | 101 | 107 | 114 | 139 | 67 |
| 186. | | Idadi ya majengo ya mahakama ya mwanzo yaliyojengwa | 649 | 656 | 663 | 667 | 668 | 740 | 791 | 64 |
| 187. | | Idadi ya ofisi za Mwanasheria Mkuu wa Serikali | 0 | 0 | 1 | 2 | 5 | 8 | 10 | 80 |

| Na. | Sekta | Kiashiria | Mwkaa wa Kizio | Utekelezaji wa Shabaha | | | | | Shabaha | Utekelezaji wa Shabaha (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 | |
| | | zilizojengwa mikoani | | | | | | | | |
| 188. | | Idadi ya ofisi za NPS zilizojengwa mikoani | 1 | 1 | 1 | 5 | 11 | 15 | 7 | 233 |
| 189. | | Idadi ya ofisi za NPS zilizojengwa wilayani | 1 | 1 | 1 | 1 | 2 | 5 | 11 | 40 |
| 190. | | Idadi ya wilaya zenye watoa msaada wa huduma za kisheria waliosajiliwa | | | | | | 116 | 138 | 84 |
| 191. | | Wastani wa idadi ya siku tangu kufunguliwa kwa kesi na kutolewa hukumu | 390 | 312 | 166 | 239 | 242 | 78 | 350 | 780 |
| 192. | | Asilimia ya watu walioridhishwa na huduma za mahakama | 78 | 78 | 78 | 88 | 88 | 88 | 80 | 500 |
| 193. | | Wastani wa idadi ya siku tangu kufunguliwa kwa kesi na kutolewa hukumu katika Mahakama ya Biashara | 480 | 390 | 365 | 324 | 231 | 231 | 350 | 192 |
| 194. | | Asilimia ya mlundikano wa kesi, kwa jumla ya kesi zote zinazosubiri maamuzi | 5 | 13 | 9 | 3 | 5 | 4 | 2 | 33 |
| 195. | **Mambo ya Ndani** | Kiwango cha kupungua kwa uhalifu nchini (%) | 5.2 | -7.5 | -1.9 | 4.3 | 3.2 | 3.5 | 3.5 | 100 |
